HILI SOCIAL CUSTOMS
C. Velten

Duquesne University Library
African Collection

esturi za Wasuaheli

von

Dr. C. Velten

Desturi za Wasuaḥeli

na

khabari za desturi za sheri'a za Wasuaḥeli

von

Dr. C. Velten,
Lehrer des Suaheli
am Seminar für Orientalische Sprachen.

Duquesne University Library
African Collection

Göttingen.
Vandenhoeck & Ruprecht.
1903.

G1658
V419x

572.9676
V445d
Afr. Coll.

Eine deutsche Uebersetzung erscheint gleichzeitig.

Vorwort.

Die vorliegenden „Desturi za Wasuaheli“ (Sitten und Gebräuche der Suaheli) bildeten ursprünglich eine Sammlung von Berichten, die Eingeborene während meines Aufenthaltes in Ostafrika auf meine Veranlassung in arabischer Schrift aufgezeichnet hatten. Ich habe diese Berichte mit dem derzeitigen Lektor am Orientalischen Seminar Mtoro bin Mwenyi Bakari aus Bagamoyo durchgesehen und dabei von ihm noch manches darin nicht Erwähnte, bisher Unbekannte erfahren. Einmal auf den richtigen Weg hingewiesen, hat Mtoro bei der weiteren Ausarbeitung dieses Werkes durch eigene Aufzeichnungen sehr dazu beigetragen, daß es das Wesentlichste von den Sitten und Gebräuchen der Suaheli birgt, was für uns von Interesse und Nutzen ist.

Bei der Auswahl meiner Gewährsmänner, deren Namen hier alle zu erwähnen zu weit führen würde, bin ich stets darauf bedacht gewesen, mich nur an reine Suaheli-Leute zu wenden. Man kommt, wie es wahrscheinlich schon geschehen ist, sehr leicht in Versuchung, sich an den intelligenteren, eher zugänglichen, weniger mißtrauischen und mitteilsameren Araber zu halten, um über die Sitten der Suaheli Aufklärung zu erhalten, das ist jedoch falsch. Man wird dabei mehr einen Einblick in die Gebräuche der mit der ostafrikanischen Küstenbevölkerung in enger Verbindung stehenden Araber erhalten als in die der Suaheli. Wenn auch letztere Vieles im Laufe der Zeit von diesen angenommen haben, so kommt es uns doch in der Hauptsache auf ihre ureigensten Gebräuche an.

APR 12 1971

Die im Anhang gegebenen „khabari za desturi za sheri'a za Wasuaheli“ (Rechtsanschauungen der Suaheli) stammen sämtlich von dem verstorbenen Mw'allim Baraka bin Shomari aus Kondutschi bei Daressalam, die derselbe im Jahre 1895 in meinem Auftrage niederschrieb. Sie geben uns ein getreues Bild von den juristischen Kenntnissen eines gebildeten Suaheli und zeigen uns, soweit dies vom Standpunkt eines Eingeborenen und Laien möglich ist, aufs eingehendste die Vereinigung des muhammedanischen Rechts mit dem Gewohnheitsrecht der Suaheli, wie es im Lande der Suaheli unter den früheren Machthabern ausgeübt wurde.

Ich hoffe mit dieser Veröffentlichung folgende Zwecke zu erreichen: Die vorliegende Suaheli-Ausgabe soll eine weitere Bereicherung der noch in den Kinderschuhen steckenden Suaheli-Literatur werden. Ferner ist es mein Wunsch, daß die des Suaheli Kundigen, sogenannten „alten Afrikaner,“ wie die am Orientalischen Seminar sich auf den Kolonialdienst vorbereitenden jungen Kolonialleute darin eine angenehme und zugleich belehrende Lektüre finden mögen. Schliesslich soll die deutsche Ausgabe dieses Buches vor allem den zum ersten Mal, auch ohne Sprachkenntnisse, in die Kolonie Kommenden ein Mittel an die Hand geben, unsere schwarzen Schutzbefohlenen von vornherein richtig verstehen und sie auch danach richtig behandeln zu können.

Die Transkription des Suaheli ist die allgemein eingeführte englische, welche auch in unseren Schulen in Ostafrika in Gebrauch ist. Ich habe außerdem noch in meinen bisher erschienenen Arbeiten und auch hier, mit Rücksicht auf die arabische Schreibweise des Suaheli, die aus dem Arabischen ins Suaheli übernommenen Wörter in ihrer suahelisierten Form mit den in der arabischen Transkription üblichen unterscheidenden Merkmalen versehen, die es dem Studierenden auf diese Weise leicht ermöglichen, auch das in einem arabisch geschriebenen Suaheli-Text stehende arabische Wort sofort zu erkennen. Man mag diese Einführung für überflüssig halten,

wie jede mit zu vielen unterscheidenden Zeichen versehene Schreibweise für den praktischen Gebrauch kaum Anwendung finden kann; ich habe es jedoch in diesem Punkte bei meiner praktischen Erfahrung in Ostafrika und bei meinem siebenjährigen Unterricht am Orientalischen Seminar als eine Notwendigkeit empfunden, die, solange wir es mit einer arabischen Schrift des Suaheli zu tun haben, auch beizubehalten ist. Ich habe dies ausführlicher in der Einleitung zu meinen „Märchen und Erzählungen der Suaheli," Band XVIII der Lehrbücher des Orientalischen Seminars besprochen.

Das Nähere in betreff der Schreibweise ist aus meiner „Praktischen Anleitung zur Erlernung der Schrift der Suaheli" (Vandenhoeck & Ruprecht, Göttingen 1901) zu ersehen.

Die Erklärungen in den Fußnoten sind zuweilen in Wiederholung der im Kapitel vorher gegebenen Anmerkungen gemacht, und zwar deshalb, damit der Leser jedes beliebige Kapitel zu seinem Studium herausgreifen kann.

Die Interpunktion des Suaheli-Textes habe ich derart gestaltet, dass jeder Leser sich sofort in der Konstruktion der Sätze zurechtfinden kann.

Berlin, im April 1903.

Dr. C. Velten.

Orḍa ya khabari zilizomo zote.

	Seite
mwanzo wa maneno	1
desturi za Wasuaḥeli qabla ya kuzaliwa mtoto	3
kuzaliwa kwake mtoto na desturi ba'ada ya kuzaliwa kwake	8
michezo ya watoto	27
khabari ya chuo	39
khabari ya mw'allimu	49
desturi za adabu	52
khabari ya kuamkiana kwa Wasuaḥeli	62
khabari ya kumtia mtoto kumbini	67
desturi za wari	81

khabari ya ḥirizi 88
khabari ya kuoa 93
khabari ya ngoma za furaḥa 122
khabari ya pepo 144
ngoma za pepo 149
kazi ya waanawake 168
kazi ya waanaume 177
desturi katika kazi ya kulima 187
khabari ya ṭalâqa 193
khabari ya maraḍi na dawa zao 198
khabari ya mtu kuzikwa 213
khabari za majumbe 222
khabari ya ʻushuru 230
kusafiri kwao Wasuaḥeli 236
khabari ya usare kwa Wasuaḥeli 251
khabari ya utumwa 253
khabari ya ukarimu 266
khabari ya náẓiri 271
khabari ya vyapo 273
mifano ya Wasuaḥeli wanavoṯhanni mambo aliyoumba muungu . 278
khabari ya siku kuu 285
maneno ya fumbo 289

khabari za desturi za sheriʻa za Wasuaḥeli.

vifungo vyetu vya zamani 297
desturi ya sheriʻa ya uwizi 302
khabari ya mwenyi kumpiga ao kumwua mwenziwe. 305
desturi ya sheriʻa ya deni 310
desturi ya sheriʻa ya kuḍámini 313
khabari ya desturi ya beʻi 315
khabari ya kuweka rahani 318
khabari ya kuokota kitu njiani 321
desturi ya sheriʻa ya amâna 324
khabari ya shirka 326
desturi ya sheriʻa ya shâhidi na ya yamîni. 327
desturi ya sheriʻa ya kuoa 331
desturi ya sheriʻa ya ṭalâqa 335
desturi ya sheriʻa ya kuzini 339
khabari ya mali ya mtoto yatima 342
khabari ya desturi ya waṣiya 344
khabari ya urithi 354

mwanzo wa maneno.

desturi[1]) za Wasuaḥeli, ma'ana watu wa mrima, jumla[2]) ya desturi zao ni moja toka Amu[3]) ḥatta Mvita[4]), na mwanzo wa mrima wa kideutschi tangu bandari ya Tanga ḥatta mgau[5]) Lindi. lakini mna tafauti[6]) kidogo za mila[7]) kama mfano wa h'arusi[8]) na kuzikana na kulea watoto — hufanyiziwa labda desturi nyingine kidogo, lakini mno huwa sawa, kama dini[9]) yao ni moja vilevile tangu Amu ḥatta mgau Lindi. na desturi ya majirani[10]) zao kidogo wametafautiana katika mila. na hao majirani zao watu wa Tanga majirani zao Wadigo na Wasegeju, na watu wa Pangani jirani zao Wazigua na Wabondei, watu wa Sa'adani jirani zao Wadoe, na watu wa Bagamoyo jirani zao Wazaramu, watu wa Kilwa jirani zao Wangindo, na watu wa Lindi jirani zao Wahiyao. na desturi za watu hao jumla zimefanana na desturi za Wasuaḥeli, illa mna tafauti kidogo ndani yake. na mtu anayejua desturi za Wasuaḥeli, humwelea na desturi hizo, na desturi nyingi za watu wa barra vilevile.

amma mtu kutaka kujua desturi za Wasuaḥeli, ni kumpata mzee mwanamume ao mwanamke kumwuliza khabari, sababu wao ndio wanaojua khabari zote, nao

---

1) Sitten u. Gebräuche. — 2) Summe. — 3) Lamu. — 4) Mombasa. — 5) Bezirk, Gebiet. — 6) Unterschied. — 7) Sitten. — 8) Hochzeit. — 9) Religion. — 10) Nachbar.

hufuata desturi za kizamani, záyidi ya hawa vijana wa sasa. desturi za kizamani wengi wameziwacha, na haba wanazifuata. na wao vijana, killa ikiingia desturi, iliyo mpya, ikiwapendeza, huifuata. kama zamani walifuata desturi ya Waʿarabu, na maneno yao kati walikuwa wakitia kiʿarabu. tenna wakatazama desturi za Wahindi, na wengine, waliwozipenda, wakazishika. wa amma sasa, tangu imekuja desturi ya Wazungu, desturi za kiʿarabu na za kihindi nyingi wameziwacha, wanapenda kushika hii desturi mpya. wakiona desturi ya Wazungu, ikiwapendeza, huifuata, na ḥatta katika maneno, wakisema, hutia neno la kizungu ndani yake. lakini hao vijana — desturi hizo wanazishika zamani za ujana wao, wakipata fahamu[1]), wanarejeʿa katika desturi za wahenga[2]) wao, kama walivoonyeshwa na wazee wao.

---

1) Verständnis. — 2) Vorfahren.

desturi za Wasuaḥeli qabla ya kuzaliwa mtoto.

khabari ya kumhota [1]) mwanamke iwapo si mzazi.

Msuaḥeli iwapo hakupata mtoto, hutafuta mganga kumhota yule mwanamke, apate kuzaa. na maʿana mwanamke kukosa kuzaa — huwa na mwemimba [2]), ndio anáyemkosesha kuzaa. bassi mwanamume atakwenda kwa mganga, akampe khabari: „nataka ukamhote mke wangu.“ wakesha patana, atakwenda mwituni, akachimbe mizizi yake ya dawa, ampelekee yule mwanamke. marra atataka kuku, na unga wa mtama, na chooko, na kunde, na mchele. mchele hupikwa na dawa namna nyingine, na unga wa mtama hupikwa na dawa namna nyingine. zikesha wiva zile dawa, atakuja mume na mkewe, wale pamoja, na yule mganga naye hula. wakesha kula, yule mwanamke huzibambika [3]) zile dawa katika maji, ikawa ndio maji yake ya kunywa mudda wa siku sabaʿ. nayo hufanyiziwa zamani anapokuwa katika ḥêḍi [4]). ḥatta ḥêḍi ikesha, na siku sabaʿ zimekwisha — marra mwanamume humwendea mkewe, muungu anapopenda — yule mwanamke marra hushika mimba [5]).

1) dawa machen. — 2) Fehler, Krankheit, auch shango genannt. — 3) verbinden, hineinlegen. — 4) Menstruation. — 5) Schwangerschaft.

khabari ya kutezamia dalili [1]) za mimba.

na mwanamke iwapo siku zimekwisha, na damu [2]) hakuiona, moyo wake huwa na khofu, kama anachukua mimba, huenenda kwa waʿallimu kutezamia. naye mwʿallim humwandikia kombe la zaʿafrani [3]) ao la wino wa mchele sura ya „araaita,“ [4]) ao „inna aʿaṭeinaka,“ [5]) kisha huosha lile kombe zile sura zilizoandikwa, akampa kunywa. naye lâzima kunywa siku sabaʿ. na baʿad ya zile siku sabaʿ kama ḥêḍi haikuja, huandikiwa jingine. ao huenda kwa waanawake wazee ao waganga, wapungao [6]) pepo. humwambia: „pepo wako ndiye aliyekuzuia damu.“ hupewa mizizi ya kunywa na mafusho kujifukiza. baʿada ya hapo hujulikana kuwa ana pepo ao ni mimba.

khabari ya uchungu [7]) wa uzazi.

mwanamke usiku anaposhikwa na uchungu wa uzazi, naye kijana, anazaa mtoto wa kwanza, hajui kizazi, hupelekwa nyumbani kwa wazee wake, huwa yeye pamoja na wazee waanawake, mama zake na bibi zake, kaẓâlika na kungwi [8]) lake wa kumzalisha. na huyu kungwi huwa na mwanamke mwingine wa kumpokea yule mtoto anapozaliwa, na jina lake mpokezi ao mpokeaji. iwapo anakawia kuzaa, marra hutuma mtu kwenda kwitwa mumewe. anapokuja humwambia: „tumekwita umwage mchele,“ maʿana kuomba muungu apate kujifungua upesi. yule mume marra hupewa mchele, naye husema: „mimi namwaga mchele, iwapo mtoto huyu

1) Anzeichen. — 2) Blut. — 3) mit Safran einen Teller beschreiben. — 4) Sure 107, 1. — 5) Sure 108, 1. — 6) punga pepo Teufel austreiben. — 7) Wehen. — 8) Lehrmeisterin, die bei den Suaheli-Mädchen sehr oft eine grössere Rolle im Leben des Mädchens spielt als die eigene Mutter.

wangu, mke wangu ajifungue mavi na mikojo[1]), na kama mtoto si wangu — na akae, aje baba yake mwingine, amwage mchele.“ wa każàlika mume husema: „iwapo tumegomba mimi na mke wangu — kitumbe cha kumgongo[2]), mimi namwaga mchele, na moyo wangu u radi[3]), mke wangu ajifungue.“ bassi iwapo muungu amempokea maneno yake, marra yule mwanamke hujifungua kabisa kondo[4]) zote, maʿana mtoto kutoka, na damu ya uzazi kumwaika.

khabari ya kukawia uzazi.

iwapo mwanamke anakawia kuzaa, huitwa mwʿallimu kuandikiwa kombe[5]) yule mwanamke, apate kujifungua. na kombe lake hutwaa ṣaḥani[6]) nyeupe na wino wa mchele. na huo wino wa mchele hutwaliwa mchele mkavu, ukakaangwa ḥatta ukaungua, tenna husagwa, makaa yake huchujwa, ukachanganywa na manimani[7]) na gundi[8]) kidogo, tenna huanikwa juani ḥatta ugande, tenna hutiwa katika chupa, umekuwa wino.

bassi na wino huu mwʿallimu huandika aya za qorani[9]), maʿana „ayati el-kursi,“[10]) na „wa qul jaa el-ḥaqqu wa za haqa al-bâṭilu inna el-bâṭilu kana za hûqa,“[11]) na mwisho wake huandika „wala ḥaula wala quwwata illa billahi el-ʿaliyyi el-ʿathîm.“[12]) na kati ya ṣaḥani huandika waqfu[13]) kama huu:

---

1) Excremente und Urin, d. h. dass sie von allem entbunden werde. — 2) Die Kleinigkeit wollen wir auf den Rücken (über die Schulter) werfen, d. h. vergessen. — 3) zufrieden. — 4) Streit, Kampf, d. h. aus allen Wehen. — 5) Teller. — 6) Teller. — 7) schwarze Erd-Frucht aus Indien. — 8) Leim. — 9) Sprüche aus dem Koran. — 10) Sure 2,256. — 11) Sure 17,83. — 12) und es giebt keine Kraft und keine Macht ausser in Gott. — 13) Aufstellung, Figur.



maʿana haya maneno ni majina ya mitume[1]) na malaika[2]). husoma:

kyaf ha ya ʿain ṣad
ha mim ʿain sin qaf
ṭaha
yasin
muzammil
jebrîl
isrâfîl
mikaîl
ʿizrâîl[3]).

majina mawili ya kwanza maʿana yake kiapo, alichoapa muungu, na majina matatu yanayokuja — majina ya mitume, na majina manne ya mwisho malaika makubwa. baʿada ya kwisha kuandikwa kombe hili, huoshwa kwa maji, likatiwa ndani ya chupa kupelekewa yule mwanamke kunywa. naye hunywa marra akipewa chupa, hunywa kidogo, na lililosalia hunywa waqati[4]) mwingine, akitaka maji — ḥatta ajifungue.

1) Propheten. — 2) Engel. — 3) Bei einem geschriebenen waqfu laufen die Striche auf der rechten und linken Seite durch die Buchstaben. Im Druck ist dies hier nur angedeutet. — 4) Zeit.

kama hakujifungua, hufanyiziwa kombe jengine ya aya nyingine na waqfu mwingine, kama zilizoandikwa ndani ya vitabu vyenyi maneno ya uzazi wa mwanamke, máthali kama kitabu cha „majárabadi eddéribi.“

ao mwʿallimu humwandikia na ḥírizi [1]) iliyo yote. na ḥírizi hufungwa juu ya mkono, ḥatta ajifungue, khalafu hufunguliwa ile ḥírizi, sababu shughli [2]) yake imekwisha. lakini mwanamke atakapo kuivaa — anaweza — ḥírizi haimḍuru [3]), na akitaka kuivua — khiyari [4]) yake mwanamke.

ao iwapo mwanamke amekawia kuzaa na kujifungua kabisa, maʿana kutokwa na vitu vilivobaqi [5]) kama chupa [6]) — bassi huandikiwa ḥírizi na mwʿallim „sura ya tabâraka“ [7]) mwanzo ḥatta mwisho, hufungwa ile ḥírizi tumboni. iwapo bakhti [8]) — hujifungua, na ile ḥírizi hufunguliwa. lakini atakapo kuivaa, aweza kuivaa, lakini haifungwi tumboni, hujifunga paḥali pengine atakapo.

ao iwapo hakujifungua kwa ile ḥírizi, hufanyiziwa ḥírizi nyingine kwa sura nyingine, mfano „wa 'l-mursalati ʿorfan.“ [9]) ao huyu mwʿallim huandika ḥírizi pamoja na waqfu wa abjed [10]).

ao iwapo hawakwenda kwa mwʿallimu, huitwa waanawake makungwi wengine, waliwo wazee, sababu wale wa kwanza wameshindwa, kumtezama ḥali [11]) yake na kumfanzia dawa [12]) ya miti shamba. hupikwa ile mizizi kwa kuku na kunde, akanywa maji ile yule mzazi.

---

1) Amulett. — 2) Geschäft, Wirkung. — 3) schaden. — 4) Wunsch. — 5) übrig bleiben. — 6) Nachgeburt. — 7) Sure 25 oder 67. — 8) Glück. — 9) Sure 77. — 10) wie sie in dem kitabu cha abjed stehen. — 11) Zustand. — 12) Arznei.

kuzaliwa kwake mtoto na desturi ba'ada ya kuzaliwa kwake.

marra kama mzazi amejifungua, hupelekewa khabari [1]) mume — ya kama: „mkeo amejifungua.“ naye atakuja, watampa rukhṣa [2]) ya kuingia ndani, atauliza „baba ao mama“ ma'ana mtoto mwanamume ao mwanamke? watamjibu. atasema: „nipeni mwanangu nimwone.“ makungwi watataka 'ada [3]) zao, ndipo wampe mtoto wake. akiwa mtoto mwanamke — atatoa rupia mbili awape, na akiwa mtoto mwanamume — atatoa rupia nne. jina lake hizo „kipokeo.“ marra mume atakwenda dukani, akanunue kanda la mtama, na debe la asali ya miwa, na manni moja pilipili mtama [4]) na tangawizi [5]), kama ana fedda [6]), na kama hana — atakopa dukani. na huko kukopa ndio desturi yetu, kitu ajapokuwa nacho — hupenda kukopa. akesha nunua vitu, tulivovitaja, mtama hutwangwa, mchele [7]) wake hupikiwa uji wa fuga mgonjwa, uliwo mkali, pilipili nyingi na asali, killa aṣ-ṣubuḥi. na mchele wa mtama hupikwa chakula ubwabwa, kitoweo chake kuku ao papa

1) Nachricht. — 2) Erlaubnis. — 3) übliche Geschenk. — 4) pilipili mtama genannt, weil die Pfefferkörner wie mtama-Körner aussehen. — 5) Ingwer. — 6) Geld. — 7) jede enthülste Kornfrucht wird mchele genannt, meist versteht man aber unter mchele enthülsten Reis.

mbichi mchanga mudda wa siku sabaʿ. na unga ndiwo uji wake mtoto hupikwa na sukari [8]).

turejee kunako khabari ya wale wazee. makungwi baʿada ya kumpokea yule mtoto, humvua nguo zile, alizotoka nazo katika tumbo la mama yake, huitwa „nguo“ ao „kunga ya uzazi.“ [2]) tenna hukatwa na kitovu, na khalafu hufungwa kile kitovu na uzi, na ule uzi hufungwa yule mtoto shingoni, ḥatta kitovu kikauke. baʿada ya siku sabaʿ labda huanguka kile kipande cha kitovu.

baʿada ya kuanguka kile kitovu, huletwa bua kukuu la mtama, lililopata mwaka, huchomwa lile bua ḥatta likaungua. tenna husagwa, yale makaa yake hupakazwa yule mtoto juu ya kitovu. ndio dawa yake.

na vitu hivo nguo ya mtoto na kipande cha kitovu huvizika uani, wakaweka ʿalama [3]). na baʿad ya siku sabaʿ mtoto akisha nyolewa, nywele zake na kucha zake huzikwa pamoja. kisha hupandwa mnazi. na mnazi hupewa yule mtoto. na akikua, huonyesha wenziwe — ya kama: „mnazi huu ndio kitovu changu.“ na wanapoupanda ule mnazi husema: „huu mnazi tunaoupanda — muungu amkuze mwanetu [4]), aje aunywe maji mnazi huu.“

khabari ya kuażżiniwa [5]) mtoto.

mtoto akizaliwa, ikiwa usiku, aṣ-ṣubuḥi huenda aketwa mwʿallim kuja mważżinia yule mtoto. na kumważżinia kwake humshika shikio la kuume, husema: „allâhu [6]) akbar, allâhu akbar, allâhu akbar, allâhu akbar. ashhadu an lâ ilâha illâ 'llâhu, ashhadu anna Muḥammadan rasûlu 'llâhi. ḥaiya ʿalâ 'ṣ-ṣalâti, ḥaiya

1) Zucker. — 2) Nachgeburt. — 3) Zeichen. — 4) mwana wetu. — 5) zum Gebet rufen, d. h. Aufnahme in den Islam. — 6) siehe Uebersetzung.

ʿalâ ʾṣ-ṣalâti, ḥaiya ʿalâ el-falâḥi, ḥaiya ʿalâ el-falâḥi. allâhu akbaru, allâhu akbaru, lâ ilâha illâ ʾllâhu.“

na maʿana mtoto kuażżiniwa, kujulishwa, ya kwamba huyu mtoto wa kiislamu, ya kama ameshika sasa mila[1]) ya kiislamu.

khabari ya kumweua[2]) mzazi.

na baʿada ya siku arbaʿini atakuja tenna mwʿallimu, amweue mzazi, maʿana kumwosha na kumṭabarisha[3]) na aya za qorani[4]) na duʿa[5]). marra hunyolewa yule mzazi, akavaa nguo nyingine mpya. zile nguo, alizotoka nazo uzazini, huwapa makungwi. naye hawamqubalishi[6]) kutembea mwanamke, atokaye ndani ya uzazi, qabla kutimia siku arbaʿini.

khabari ya kumwonyesha jua na mvua mtoto.

baʿada ya siku sabaʿ yule mtoto wanapotaka kumtoa nje kumwonyesha jua, mkubwa wa makungwi humpa khabari baba yake — ya kama: „kesho tafuta jogoo na mchele, tupike „kisingizi.“ [7]) maʿana ya kwitwa kisingizi — wale makungwi hawakulala usiku kucha kumlinda yule mwanamke siku aliyozaa. na mtu akiwa mweza[8]), huchinsha mbuzi, ukapikwa wali, watu wakala. mume na mke hupewa pekeyao wakala.

na katika khabari ya kuonyeshwa jua siku ya sabaʿ, hutandika nguo chini ya kizingiti[9]), ao humpakata mtu, akaja mwanamke mzee, akashika mchi, husema na yule mtoto: „muungu amekuleta juu ya ulimwengu, shindia moyo wako, na vitu vya watu usiwe

---

1) Sitten u. Gebräuche. — 2) religiöse Waschung ausführen, reinigen. — 3) rein machen. — 4) Vers, Abschnitt des Koran. — 5) Anrufung. — 6) erlauben. — 7) Einschläferungs-Essen. — 8) vermögend. — 9) Türschwelle.

mtamaʿni[1]). umekuja juu ya ulimwengu, ziba mashikio yako, usisikilize maneno ya watu. umekuja juu ya ulimwengu, ukapewa kitu chema — kikae tumboni, kibaya — kitoke. umekuja juu ya ulimwengu, usiwe mgomvi, ukagombanisha watu, sababu wahenga wamesema:

„lifaʿalo kueleza lieleze,
lisilofaʿa limeze.“

umekuja juu ya ulimwengu, usipite nyumba zenyi wake wa watu, utapoteza roho yako. muungu amekuleta juu ya ulimwengu, shindia moyo wako na amana za watu. muungu amekuleta katika dunya, ukae kwa heshma na watu, sababu wahenga wamesema:

„mwiza mwiza[2])
si utumwa.“

na maʿana ya kushika ule mchi, kuwekwa juu ya kifua cha mtoto, ni ʿalama ya kuonyeshwa moyo wake uwe mzito kama ule mchi, sababu achelee mali za watu na mambo mengine tuliyotangulia kuyasema.

na baʿada ya maneno haya kuambiwa mtoto, hutolewa uanjani, akadakwa marra sabaʿ, hambiwa „tezama jua.“ khalafu hurejeshwa ndani.

tenna walipomtoa nje mtoto, mtu mmoja humpakata, na mmoja akatia maji katika ungo, kisha humwitia kwa mkono, husema „mvua mvua mvua“ maʿana jua ameliona, na hii ndio mvua.

wakesha, yule mume atataka rukhsa kwenda zake, watamjibu: „kamwage mkweo.“[3]) na mkwewe atamjibu: „sasa nimequbali, kama wewe mkwe[4]) wangu, na sasa umenipatia mchumba.“ maʿana kama amezaliwa

---

1) Begehrer. — 2) d. h. zu Befehl, zu Befehl zu sagen ist keine Sklaverei, damit ist man noch kein Sklave. mwiza = he wallah. — 3) Schwiegervater. — 4) Schwiegersohn.

mtoto mwanamke. marra atamgonga konzi[1]) katika kichwa, maʿana furaḥa. na kama amezaliwa mtoto mwanamume, humwita „mume mwenzangu,“ maʿana mke wao ni moja, humwita wote wawili „bibi.“[2])

baʿada ya kumwonyesha mtoto jua na mvua, mwanamume atakwenda zake, na jioni watampelekea mkewe. maʿana yule mzazi amepelekwa kwa wazee wake, akishikwa na uzazi.

iko desturi nyingine iliyolâzima kutajwa: katika nyumba nyingine, anapokaa mzazi, iko desturi siku atakáyozaliwa yule mtoto — huzima moto, wakawasha mwingine mpya. ule moto mpya hautoki nje. wala wa nje hauingii mwingine ndani, ḥatta kutoka mtoto marra ya kwanza baʿada ya siku sabaʿ.

khabari ya mke na mume baʿada ya kuzaliwa mtoto.

mamie[3]) mtoto mama zake na makungwi zake humkataza — ya kama: „mumeo akitaka kulala nawe — kataa, sababu mtoto wako ataugua.“ na kulea mtoto wake mudda wa mwaka — hajui mwanamume. na sababu ya mwanamke kukatazwa kulala na mumewe — huchelea mtoto asivunjike. na kuvunjika kwake huugua maraḍi[4]) ya nyogea[5]), hawezi kusimama wala hawezi kwenda, ajapokuwa mtoto wa miaka miwili. naye amekonda, mwili wake mafupa na mishipa bassi. na watu wakimwona, hujua husema: „huyu mtoto amevunjwa na mama yake na baba yake.“ na watu mji mzima huwasema, ya kama wana nyege[6]) sana.

---

1) Knuff geben. — 2) bibi, Frau und Grossmutter. — 3) mama yake. — 4) Krankheit. — 5) Rachitis. — 6) Kitzel.

khabari ya siku ya kuzaliwa.

mtoto akizaliwa siku ya el-jumaᶜ [1]), huambiwa mtoto huyu amezaliwa siku ya kheri [2]), sababu siku el-jumaᶜ ni kama siku kuu. akiwa mwanamume, hupewa jina la Jumaᶜ, akiwa mwanamke huitwa Maajumaᶜ, maᶜana mwana jumaᶜ. na akizaliwa mtoto jumaᶜ ya nne, husema: „amezaliwa siku mbaya mtoto huyu,“ maᶜana ni siku nzito, nuhsi [3]) huitwa.

khabari ya maulidi [4]).

mtu akijiweza, akipata mtoto, akitaka kumnyoa baᶜada ya siku sabaᶜ ao baᶜada ya siku arbaᶜini, humnyoa kwa maulidi. na kama maskini humnyoa pasipo maulidi.

na anapotaka kuyasoma hayo maulidi, huenda kwa mwᶜallim mkubwa wa mji, naye anawᶜarrifu waᶜallimu wenziwe, ao yeye mwenyi maulidi huenda, akawaᶜarrifu waᶜallim kama awatakao. huᶜarrifu na jamaᶜa zake na marafiqi zake na majirani zake, waje kuitikia maulidi. na hao waᶜallim wanapokuja, huja na waanafunzi wao na vitabu vya maulidi na maṭari [5]) ya kutikilia [6]) vipokeo [7]). na hao waᶜallimu hukaa chumba kimoja na hawa watu waanaume walioalikwa, waᶜallimu hukaa juu mikeka na mito, na watu wengine katika majamvi. na katika chumba cha pili hukaa waanawake na mtoto, hunyamaza wote kimya kusikiliza. na mbele yao wale waᶜallimu zimewekwa sinia [8]). juu ya sinia pana chupa za mirashi [9]) na viṣaḥani vya sukari ya mawe [10]) na ya mchanga [11]) na tangawizi [12]) na vyetezo [13]) vya ᶜûdi [14])

---

1) Freitag. — 2) Glückstag. — 3) Unglückstag. — 4) Taufest. — 5) kleine Handtrommel. — 6) relat. Form von itikia. — 7) Refrain. — 8) Tablett. — 9) Rosenwasser. — 10) Würfelzucker. — 11) Streuzucker. — 12) Ingwer. — 13) Räucherschale. — 14) Aloe.

na ubani[1]). maʿana sukari na tangawizi, mtu anayesinzia hutwaa kidonge cha sukari, akala na tangawizi.

tenna huanzwa maulidi mwanzo wa saʿa ya nne ya usiku ḥatta al-fajiri[2]). nao katika waʿallim hutoa moja kipokeo mudda wa roboʿ saʿa, khalafu hutoa mwʿallimu mwingine kipokeo. kikesha kipokeo wanafunzi na watu wengine waliopo huitikia kwa umoja, na hao wanafunzi hupiga maṭari, kufuata kile kipokeo, huimba „hê allâh hê allâh.“

ḥatta waqati wa al-fajiri husema waʿallimu: „tunataka kuyaṣalisha maulidi, fanyeni ṭayyari.“ huletwa yule mtoto, wakatia ṭibu[3]) katika bakuli, tenna husimama watu wote pia, hutolewa kipokeo cha uzazi: „yâ nabîyu salâmun ʿaleika, yâ rasûlu salâmun ʿaleika, yâ ḥabîbî salâmun ʿaleika, ṣalawâtu ʾllâhi ʿaleika.“[4]) na watu huitikia vilevile. na mtoto ameshikwa mkononi na baba yake ao na mwʿallimu. hupakwa ṭibu juu ya kichwa na shingoni yule mtoto. na waqati huu babiye mtoto na jamaʿa zake huja wakawatunza mapesa waʿallimu toka pesa kumi na tano ḥatta rupia. na ṭibu iliyobaqi killa mtu hushika kidogo mkononi, hupakaa mikono. na marashi humwagiwa wale watu waliopo waanaume na waanawake, na ʿûdi hufukizwa.

ḥatta kipokeo kikesha, watu hukaa kitako, humalizwa maulidi, na mwisho wake ndio fâṭiḥa[5]). watu huenenda mskitini kuṣali, na waanawake hutengeneza vyakula, hupikwa wali wa pilau[6]) ao wa nazi. wakirudi mskitini, huandikiwa vyakula, wakala, kisha huagana na mwenyi maulidi, humwombea: „muungu amkuze mtoto wako, nawe akupe fáḍila[7]) nyingi.“ naye huitikia „amîn.“[8]) bassi watu huenenda zao.

1) Weihrauch. — 2) Morgengrauen. — 3) Wohlgerüche. — 4) vergl. Uebersetzung. — 5) erste Sure. — 6) gewürztes Reisgericht. — 7) Güte. — 8) Amen.

na maulidi haya yanasomwa mwezi mfunguo sitta siku ya mwezi kumi na moja jioni kuamkia kumi na mbili — killa mwaka. na maʿana kusomwa mfunguo sitta haya maulidi — ndio siku aliyozaliwa mtume Muḥammadi mwezi kumi na mbili na jumaʿ ya tatu waqati wa al-fajiri, ndio maʿana kufuata ṭabiʿa[1]) hii. ao husomwa siku ya hʿarusi kuingia ndani, ao husomwa watoto wakitoka kumbini[2]), maʿana ni furaha.

na namna za maulidi hayo mbili: kuna maulidi ya barzanji[3]), mno husoma Waʿarabu, kuna na maulidi ya shárafa el-anâmi[4]), hayo husoma Wasuaḥeli.

khabari ya ʿaqîqa[5]).

khabari hii ya ʿaqîqa áṣili[6]) yake inatoka kwa Waʿarabu, zamani Wasuaḥeli hawakuwa nayo, lakini sasa wengine wanafanyiza. mtoto akipata siku sabaʿ, hufanyiziwa ʿaqîqa. na hiyo ʿaqîqa huja mwʿallim kusoma maulidi ao duʿa nyingine. huchinshwa mbuzi wawili, iwapo mtoto mwanamume. mbuzi mmoja hukaangwa, ikafanywa kitoweo cha wali, na mbuzi wa pili huchomwa mishikaki[7]), ikanunuliwa asali ya nyuki, ndio kitoweo chake. tenna hualikwa watu wakala. na mafupa yake hayavunjwi, huchimbwa shimo yakazikwa, maʿana yake katika ḥadithi[8]) zimeandikwa — siku ya qiyama[9]) yale mafupa mwenyeʿzimgu[10]) humfanyia ngamia yule mtoto kupanda katika pepo[11]).

na ikiwa mtoto mwanamke, huchinshwa mbuzi mmoja, ikafanyizwa karamu[12]) vilevile.

1) Charakter, doch wird ṭabiʿa oft im Sinne von „Sitte“ gebraucht. — 2) aus dem Versteck, d. i. Beschneidung. — 3) Geburtstag des Heiligen aus der Stadt Barzanj — 4) Geburtstag des Fürsten der Menschheit. — 5) Sühnopfer, auch Fest der ersten Haarschur genannt. — 6) Ursprung. — 7) am Spiess. — 8) Geschichte. — 9) Tag der Auferstehung. — 10) mwenyi ʿezi muungu, Gott der Allmächtige. — 11) Paradies. — 12) Fest.

na hiyo ʿaqîqa, mtoto iwapo ni mdogo, lâzima juu ya wazee wake kumfanyia. akipata miaka kumi na mitano, naye ni mweza, analâzima kujifanyia mwenyewe.

ao mtoto akifa hufanyiziwa ʿaqîqa, shurṭi [1]) zake vilevile kama tulizotangulia kuzisema, maʿana mtoto hasomewi khítima [2]), ndio sababu hufanyiwa ʿaqîqa.

1) Bedingung. — 2) Koranlesung.

khabari ya chakula cha mtoto.

mtoto hulishwa mtama, na mtama hutwangwa unga, hukatiwa katika mitungi, usipate vumbi na mchanga. na kulla aṣ-ṣubuḥi huteka qadri ya chakula cha mtoto, ukapikwa na sukari, akalishwa mtoto. na kulisha kwao hutia uji katika kikungu kidogo, ukapozwa ḥatta ukapoa, tenna hutiwa katika kiṣaḥani. mama yake akampakata mtoto, hutia uji katika kiganja, akamlisha mtoto na kidole. na mtoto humeza. akisha kula humpa maji, ao humnyonyesha ziwa. tenna hulala yule mtoto.

na kama mtoto hataki kulala, humchuchia katika kitanda, ao humbeba mongoni, akamwimbia mwimbo. na mamaye humwimbia:

„silie [1]) mama [2]) silie,
silie wangu mtoto,
mtoto mtotototo [3]),
mla ubwabwa wa moto,
kitumbo kifuke moto.“

1) usilie. — 2) mama — als Kosename für mtoto. — 3) ganz kleines Kindchen.

ao huimba:

ôâ [1]) mtoto
nyamaa [2]) mwanangu mtoto,

1) Ausdruck der Liebkosung. — 2) sei still, ruhig.

mwana nionee [1]) uchungu
pekeyangu na muungu [2])
mimi na mkunga [3]) wangu,
nyamaa kulia mtoto,
nyamaa
ôâ mtoto.“

1) du Kindchen, das mir Schmerz bereitet hat. — 2) weiss es. — 3) Hebamme.

ao huimba:

„maji yakanza kujaa, hujaa kinyelenyele [1]),
yakafika mwambani, kofi na vigelegele.
humtumaje mtoto, tonge [2]) usimwegee?“ [3])

1) langsam. — 2) Bissen. — 3) gönnen. Der Sinn ist folgender: Wenn Mann und Weib freien, geben sie bedächtig vor (geben sich nicht wie sie sind), sind sie verheiratet, dann gibts Zank und Schläge. Warum zankst du mit der Frau und liebkost nicht mit ihr?

ao huimba:

„silie [1]) mama silie,
ukalia waniliza,
wanikumbusha makiwa [2]),
makiwa ya baba na mama.
baba na mama watende [3]),
wanioza dume kongwe [4]),
halisafiri [5]) halendi,
kazi kumega matonge.“ [6])

1) usilie. — 2) Trauer. — 3) wollten (Gutes) thun. — 4) mume mzee. — 5) auf dume bezüglich. — 6) Bissen zurechtmachen.

ao huimba:

„kile nini kile nini, kilicho ñgambo ya mto? [1])
nikakita hakitiki, kazi kunipa majuto.“

1) eine Frau sehnt sich nach einem Mann, der auf dem andern Ufer des Flusses steht, sie ruft ihn, aber er hört nicht.

ao huimba:

„nalikwenda matembezi
upande wa Mangapwani [1]),
hakuta papa upanga [2]),
hamwuliza „wenda wapi?“
„nenda kuhani matanga.“
„aliyekufa ni nani?“
„mkuu wetu Kipanga [3]).
tambuu mwatafunaje [4]),
popoo zingali changa?“

1) Ortsname. — 2) Haifischsorte; gemeint ist ein hübsches junges Mädchen. — 3) kipanga, eigentlich Name eines Vogels, hier ein Mann gemeint. — 4) Das Mädchen sagt zu dem Mann, der ihr begegnet ist und ihr nun nachstellt: „Wie wollt ihr den Betel kauen, wenn die Nuss noch nicht reif ist, d. h. ich bin noch viel zu jung, als dass ein Mann mir nachstellen könnte.

ao huimba:

„ukenda nisallimie [1]), kwa jina usinitaje.
mlangoni pana watu [2]), kidege kitapitaje?
ukenda nikonyezee [3]), jioni mwambie aje.“

1) eine Frau schickt einem Mann eine Liebesbotschaft durch ein Sklavenmädchen. — 2) nachdem der Mann ihr hat sagen lassen zu kommen, antwortet sie dem Boten: „an der Thür stehen immer Leute, wie soll da das Vögelchen vorbei.“ — 3) Wink geben.

baʿada ya kuamka mtoto, huoshwa uso wake, hupakazwa wanja [1]) usoni. tenna husagwa muru [2]), na huo muru akapewa kunywa, na mwingine wakampaka maungo mazima, maʿana dawa ya watoto kwa vichango [3]). nao huuza Wahindi na Washihiri. na iwapo mtoto hapati choo, killa marra humpikia mamungunye [4])

1) Antimonpulver. — 2) ein indisches Gewürz, ähnlich wie Pfeilwurz. — 3) chango Bandwurm, kichango kleine Würmer, die Kinder häufig haben. — 4) Flaschenkürbis.

ya maji, yasiyo sukari wala asali, ao hutia nazi. na kama hakupata choo, humramba mkundu yule mtoto, hupata choo. na desturi yao mtoto akenda choo, humpangusa kwa makumbi ya mnazi, tenna humwosha na maji.

na akilala humwekea kisu chini ya mchago[1]) na mikono yake na miguu kufungwa mvuje[2]) kuchelea na kuinamiwa na dege[3]); na nyumba yenyi mtoto mdogo juu ya paa hutundikwa kaa[4]) juu ya mti katikati ya mwamba kuchelea yule mtoto asipatikane na dege. maʿana dege juu ya mtoto maraḍi mabaya. ásili yake ndege mkubwa, hupita usiku killa nyumba yenyi mtoto, hukunjua mabawa yake, akakuñguta[5]). nyumba yenyi mtoto — akasikia mabawa ya dege, ajapokuwa amelala, atasituka[6]), aṣ-ṣubuḥi atashikwa na ḥoma. sherṭi apatikane mtu, ajuaye dawa ya babu[7]). kama hakupatikana, mtoto atakufa. na ikawa bakhti[8]), yule mtoto kama hakufa, ataugua siku nyingi, na mwisho wake macho yake yatakuwa na makengeza[9]).

na huyu[10]), ajaye na dawa ya babu, hupatana kumzindika[11]), maʿana kumfunga dawa yule mtoto, maʿana yake kuchelea, yule mtoto asivunjike mwili wake kwa wale watu, waliwolala nje na waanawake, na watu kumtazama kwa macho maovu yule mtoto. tenna huleta jimbo[12]) likatiwa katika jungu, maji yake ndiyo anayokoshewa mtoto aṣ-ṣubuḥi na jioni. wasipofanyiza hivo, mtoto, watu waliwolala vibaya, wakimshika, huwa na nyogea[13]).

1) Kissen. — 2) Teufelsdreck. — 3) grosser Vogel d. h. sheṭani. — 4) Krabbe. — 5) sich schütteln. — 6) erschreckt werden. — 7) Grossvater, gemeint ist der Vogel oder Teufel. — 8) Glück. — 9) schielen. — 10) mganga. — 11) Zauber legen, der bösen Zauber unschädlich macht. — 12) Kräutermedizin. — 13) Kinderkrankheit, Rachitis.

khabari ya nguo za mtoto.

nguo za ʿmtoto mdogo hutungwa ushanga mweupe na mwekundu na mweusi pamoja. mapana yake nyanda[1]) nne, jina lake shegele. humfunga kiunoni, hutunga pamoja na ushanga wa utunda, wakamvika kiunoni. akipata ʿomri[2]) wa miaka miwili, havai shegele, humvua, wakamvika kanzu na suruali[3]), kichwani kilotia[4]). miguuni humvika vikuku vya feḍḍa, na mikononi kazalika. na shingoni humvika mkufu utanda[5]) moja.

na mtoto mwanamume mavazi yake kanzu na suruali na kilotia, lakini namna mbali mavazi ya kiume na ya kike. mashikioni mwa mtoto mwanamume hutiwa pete za feḍḍa.

majina ya watoto.

watoto wakiwa wadogo, hawana majina, hupewa majina ya mchezo, huitwa „panya,“[6]) ao „buku,“[7]) mashavu[8]), sanura[9]). kifimbo, kinyenyere[10]), kidagaa[11]), mapengo[12]), tukwa[13]), kibarrabarra[14]), babu[15]). haya majina, wanayopewa watoto waanaume na watoto waanawake.

na wengine huwapa watoto wao majina yao ya killa siku baʿada ya siku sabaʿ kuzaliwa, wengine baʿada ya siku arbaʿini, na wengine baʿada ya mwaka. na majina hayo yanatoka katika majina ya wajomba zao, na wakiwa waanawake majina ya mashangazi zao.

wako watu wengine, wanaoweka náziri[16]), qabla ya mwanamke kupata mimba, husema: „mimi nikipata

1) Fingerdicke. — 2) Alter. — 3) Hose. — 4) Kindermütze. — 5) Schnur. — 6) Maus. — 7) Ratte. — 8) Backe. — 9) Katze. — 10) kleine Ameise. — 11) kleiner Fisch. — 12) Zahnlücke. — 13) Ichneumon. — 14) kleiner Schelm. — 15) Grossvater. — 16) Gelübde.

mtoto mwanamke ao mwanamume, ntampa jina każa wa każa[1]). akizaliwa yule mtoto — lâzima kupewa lile jina alilonaẓiriwa.

na wengine mno huitwa „mtoro“ baʿad ya siku sabaʿ ya kuzaliwa. na maʿana yake mama yake akipata watoto wawili — wamekufa — mtoto wa tatu huitwa mtoro. na kwitwa kwake jina hilo hufungwa kamba shingoni ḥatta kiunoni, ndio ʿalama[2]) ya mtoro, naye asitoroke kama walivotoroka nduguze[3]).

ao „mtoro“ — iwapo mtoto hutoroka chuoni, ao mtumwa hutoroka, naye huambiwa „mtoro,“ lakini si jina lake mtoro.

na jina hili la baʿada ya siku sabaʿ ao arbaʿini ao la mwaka hukaa nalo, ḥatta akenda kumbini[4]). akitoka kumbini, hupewa jina jingine. naye hukaa na jina hilo ḥatta kufa kwake, lakini iwapo anataka kutawalli[5]) kama jumbe, hutwaa lile jina, alilotawalli baba yake.

watu wengine hujigeuza majina nafsi[6]) zao. iwapo, mji aliwokaa, amefanya qiṣṣa[7]) kiovu, amekwenda mji mwingine — hujita jina jingine. ao mtumwa ametoroka kwao, amekwenda mji wa ugeni, hubadili jina jingine, watu wasimjue. ao wengine hujigeuza jina jingine, sababu lile jina halipendi.

khabari ya kuota meno.

aiḍa[8]) mtoto akiwa qaribu ya kuota meno, hufanyiwa „dawa za fungo,“ maʿana ya kufunga meno, yasiote vibaya, yasitangulie meno ya juu. na dawa hiyo hufanya wazee waanaume ao waanawake, huchimba mizizi ya ndago, akatungiwa ḥirizi kuvaa shingoni, ḥatta meno yamwote.

1) soundso. — 2) Zeichen. — 3) ndugu zake. — 4) Beschneidung. — 5) Amt antreten. — 6) Seele. — 7) Sache. — 8) ferner.

na meno yakikawia kuota, huhotwa[1]) yule mtoto na waganga, maʿana hufanyiziwa dawa, hupewa majimbo[2]) ya koga na ya kupakaa. tenna huchumwa hoza[3]), maʿana majani mengine ya mwitu, akapakwa yule mtoto. baʿada ya siku chache hutoka meno yule mtoto.

na iwapo mtoto ameota meno ya juu, zamani hawamlei mtoto, na ḥatta sasa wengine hawapendi. wengine husema: „siwezi kuitupa damu yangu, nitailea.“ na wengine wanalea, lakini hawana furaḥa naye mtoto. na mtoto huyu huitwa kibi[4]), maʿana yake „mbaya,“ lakini khalafu hupewa jina kama desturi ya watoto wengine. na watu wengine hufanyiza khofu[5]) kumpa mkono mtoto huyu, sababu huchelea kufa ao kuugua.

ao mtoto akizaliwa, akitanguliza kutoa miguu mbele, huitwa vilevile kibi. hawamlei, watamwua, ao humpeleka mskitini, wakamwacha ndani ya mskiti. watu, wanaokuja kuṣali al-fajiri, wakimwona — hujua, ya kama mtoto huyu amezaliwa vibaya. hutokea mtu, akachukua kumlea, humfanya mwanawe, sababu ya kukataa kumlea huogopa kufa. desturi hiyo kwa Waṣuaḥeli imeshikana na Wazaramu.

khabari ya mtoto iwapo akiugua na kuzinguliwa[6]) kwake.

mtoto akiugua, wazee wake huenda kwa mwʿallimu kutazamia. mwʿallimu hutoa vitabu vyake na ubao wa ramli[7]), husema yule mwʿallimu „amepatikana[8]) huyu mtoto,“ ao „hawezi tu.“ humwuliza yule mwʿal-

---

1) mit Zauber behandelt werden. — 2) Kräutermedizin. — 3) Medizin. — 4) -bi oder -wi als adjectiv im früheren Suaheli „schlecht, böse.“ — 5) Angst. — 6) zingua von einer Krankheit befreien. — 7) Zauberbrett. — 8) na uchawi.

limu: „tufanyize nini sasa?“ hujibu: „mzingueni.“ „zinguo lake linataka nini?“ hujibu: „kwanza mkate, na nazi, na kuku wa mawaa[1]) mawili, na kombe[2]) saba‘, na mbegu saba‘, na komwe[3]) moja, na żira‘a[4]) saba‘ bafta[5]) ao doti ya mrekani[6]).“ huenda wakavitafuta vitu hivo.

marra humwita mw‘allimu, naye huja na waanafunzi wake, killa mtu ana mṣaḥafu[7]). mw‘allimu husema: „wewe soma sura hii, nawe soma sura hii.“ na watu wawili hushika ungo wenye vile vitu. huzungusha ule ungo. na kombe huwashwa, ma‘ana hutiwa mafuta ya uto na utambi wake pamba. wanapokwisha kusoma mw‘allim na waanafunzi wake, kombe zote zimezimika. na chini pana jungu la maji, hutoa kombe, akatia ndani ya jungu la maji, ḥatta kombe saba‘ zishe. kisha hutoa nazi, akaizibua maji, akamwosha yule mtoto kichwani, kisha huivunja kizingitini. yule mtu aliyeshika mtoto huondoka, watoto huokota vipande vya nazi wakasikua[8]), wakawacha vifuu[9]). hutiwa katika lile jungu la maji, husema: „aṣ-ṣubuḥi lipelekeni njia panda[10]) mkaliwache.“ naye mw‘allimu humpa kitu kama watakacho. mkate na bissi na nazi hupewa wale watoto wa chuoni wakala.

kazâlika mkubwa akiugua, huzinguliwa kama hivi tulivosema.

khabari ya chale za malole[11]).

ba‘ada ya mwaka moja yule mtoto huchanshwa kichwani pembe ya mashikio chale mbili za malole, ndio

1) zweifarbig. — 2) Muschel. — 3) eine Frucht. — 4) Ellen. — 5) weisser Baumwollstoff. — 6) amerikani roher Baumwollstoff. — 7) geschriebener Koran. — 8) Fleisch aus der Kokosnuss holen. — 9) Schale. — 10) Kreuzweg. — 11) Narben des Erkennens = Stammesabzeichen, lala sehen.

desturi yao Wasuaḥeli, ajulikane huyu ni mwana wa kiungwana.

zamani za kwanza mtoto akitaka kuchanshwa, sherṭi kwa siwa[1]) na zumari[2]) na ngoma kuu kama mfano wa hʿarusi. hii khabari ya kizamani imekwisha.

khabari ya mtoto wa mazeru[3]).

áṣili[4]) yake mrima kuna watoto, hutokea weupe sana, wazee wao weusi. nao wanaṣadiqi[5]), ya kama mtoto huyu amebadiliwa na mtoto wa sheṭani[6]). mama yake katika siku sabaʿ za kwanza aliondoka usiku kwenda chooni, akamwacha pekeyake, chini ya mto hakuweka koja[7]) ao kisu, ao mkononi hakufungwa mvuje[8]) — sheṭani ameona mtoto pekeyake — amembadili, amewacha mtoto wa sheṭani, amechukua wa bin Adam[9]).

ao wengine husema: mama yake alipokuwa na mimba, amenamiwa[10]) na sheṭani, ndipo akazaa mtoto mweupe. ndio maʿana Wasuaḥeli, watoto wao wakiwa wadogo, wanawafunga mvuje mikononi. na mvuje ʿarufu[11]) mbaya, maʿana sheṭani mvuje hapatani nao.

na watoto hao, Wasuaḥeli wakiwaona, husituka[12]) sana, wala hawawapendi. wengine huwapenda kuwaua. na wakiwalea, wakiwa wakubwa, hawapeani mikono na watu, kama mfano wa mwenyi mabaranga[13]) ao ukoma[14]). hii khabari ya watoto wa kimazeru.

khabari ya kulea mtoto aliyefiwa na mamake[15]).

mtu iwapo ameoa mke, amepata mtoto, mkewe amekufa, na mtoto mchanga[16]), akiwa na wazee wake

1) Horn aus einem hohlen Baumstamm gefertigt. — 2) Flöte. — 3) Albino, zeru = eupe. — 4) Ursprung. — 5) glauben. — 6) Teufel. — 7) Halskette. — 8) Teufelsdreck. — 9) Menschenkind. — 10) ameinamiwa. — 11) Geruch. — 12) erschreckt werden. — 13) Hautkrankheit. — 14) Krebs. — 15) mama yake. — 16) Säugling.

yule mume ao mke, watamtwaa mtoto wamlee. na ikiwa hao hawapo, na tenna akiwa hana ndugu, atapatana na mwanamke mwinginc kulea mtoto wake. na gharama [1]) yake zamani ilikuwa si nyingi. kulea mtoto hatta kunyanyua miguu [2]) — mlezi hupewa riale tatu, lakini sasa riale kumi na mbili; ao beina yao mapatano.

akiwa na mtoto mwanamke yule mwanamke mlezi, na yule anayemlea mwanamume — hawaoani, wala wakikutana njiani hawazini. beina yao udugu kwa siku zote. wala yule mwanamke aliyemnyonyesha hamwoi, ni mama yake. juu yake ḥarâm [3]) kumwoa.

na iwapo watoto hao wamelelewa katika mji moja, khalafu wakasafiri miji mingine, wakakutana, wakaoana, maʿana hawakujuana, huwachishwa, maʿana beina yao ni udugu, ni ndugu wa ziwa [4]) jina lake.

khabari ya mwanamke mwenyi kisukumi [5]).

wa kazâlika mwanamke iwapo mzazi, anapata watoto, lâkin hawakui, marra wanakufa, ao anaolewa na mume, mume hana maʿisha [6]) mengi, anakufa, mwanamke huyu waanaume humwogopa, huitwa mwanamke mwenyi kisukumi. iwapo kisukumi chake cha kuua watoto, hutafutwa wazee waanawake waganga. na yule mume huwapa mashauri wazee wa yule mwanamke — ya kama: „mke wangu mgonjwa, nataka kumfanyizia dawa.“ wazee wake hujibu: „sisi tu radi.“ [7]) bassi wale wazee waganga humtwaa yule mwanamke, wakampeleka uani, marra humvua nguo, wakamfunua mago [8]). na áṣili ya yule mwanamke huzaa watoto wasikue — huwa na kinyama kimeota chini ya pembe ya kisimi [9]). kinyama hicho ndicho kinachoua watoto, jina lake kigwaru cha

1) Kosten. — 2) Beine strecken. — 3) verboten. — 4) Milchbruder. — 5) von sukuma zurückstossen. — 6) Leben. — 7) zufrieden. — 8) die Schenkel auseinanderspreizen. — 9) Kitzler.

kuma. bassi wale waanawake wazee hukitafuta killa pembe, ḥatta wakakipata, marra hukikata, lakini huona uchungu yule mwanamke. waanawake waliwooga, hukataa kukatwa. wakesha mkata, marra humtia dawa, naye hawi na donda, uchungu wake wa marra moja. siku ya pili mumewe akimtaka, huweza kulala naye. bassi akesha katwa kinyama hicho, muungu iwapo amewapa mtoto kwa baraka[1]) zake, atakua mtoto. yamekwisha maneno haya.

khabari ya mrima watu kukosa kizazi kingi.

ma'ana yake Wasuaḥeli kukosa uzazi mwingi, sababu wanaanza ujana kutwaana. ḥatta wakaoa, shaḥawa[2]) katika mwili imewakauka. iwapo ni mzazi, hupata mtoto mmoja ao wawili, hana shaḥawa tenna illa povu[3]). lakini zamani walikuwa na kizazi, sababu wazee wa zamani walikuwa wakiwakataza watoto wao kuolewa mapema na kutwaa waanawake mapema.

alikuwa jumbe mmoja Ukami jina lake Shenekambi, amezaa watoto mitêni, lakini si kwa mwanamke mmoja, alikuwa na wake wengi na masuria wengi, killa mwanamke moja amezaa watoto kumi ao záyidi.

na katika barra sasa hupatikana mtu mwenyi watoto watano ao sitta, lakini katika mji wa mrima hapana.

na ma'ana nyingine ya mrima kuto' kuwa[4]) na kizazi kingi — wao waanawake, wakishika mimba, huḥaribu[5]), ma'ana ya kuḥaribu hukataa kizazi, husema: „nikizaa mtoto ntachakaa[6])", sitatakwa na mwanamume tenna, afaḍali[7]), nikae kama ujane[8]).

---

1) Segen. — 2) Same. — 3) Schaum. — 4) kutoa kuwa nicht zu sein. — 5) zerstören. — 6) altern. — 7) es ist besser. — 8) unverheiratet, Witwenschaft.

michezo ya watoto.

mchezo wa geli.

geli kipande cha mti[1]), huchimba kishimo, wakaweka kile kijiti. mkononi hushika fimbo, marra hurusha kile kipande, akakipiga na fimbo, nacho huruka, kikenda mbali. na kule chendako, kuna watoto wanakingoja, kikafika — hukidaka kwa mikono, ao hukipiga na fimbo. yule aliyecheza mudda wake umekwisha, atacheza mwingine. na mchezo huu hugawana, wakiwa watano — wawili huku na watatu huku. hufanya na mkubwa wao, jina lake mwingizaji[2]), huanza watoto kucheza, mwisho hucheza yeye. akikosa, huja wale wengine, wanaokuwa upande mwingine. na wanapokirusha, husema „hiyo," ma'ana kinakuja kipande, na wengine huitikia „na ije."

nao hufanya ulalamishi[3]) katika kuḥesabu[4]). ḥesabu yake tangu moja ḥatta kumi, lakini huḥesabu vingine — moja, mbili, tatu, pumbu la mazeru ligeuka[5]), nane, kenda, kumi — marra watagomba. watatukana wakitaka kwenda zao:

„tumecheza na wazoga[6])
wamekimbia, wamekimbia kwa oga."

---

1) 20 cm. langes fingerdickes Hölzchen. — 2) Einführer, Lehrmeister des Spiels. — 3) Streit. — 4) zählen. — 5) die Hoden des Albino werden umgewandelt. — 6) Cadaver, Aas.

mchezo wa ṭiyyara[1]).

ṭiyyara qarṭasi[2]). mwanzo wake wanafunga mabapa[3]) ya miwale[4]) kwa uzi, kisha wanapika uwanga[5]), hubandika juu ya mwale, kesha huweka juu ya qarṭasi ḥatta ikauke. kesha hufunga na kinanda[6]), hutia na mkia. marra huifunga uzi, huenenda pwani, wakairusha. na ikiwa juu — huvuma. na zikiwa mbili, hupiganisha, moja hushika yake, na moja akashika yake.

ao hufanya kishadda[7]). kishadda kama ṭiyyara, lakini mwale mmoja kati. ao hufanyiza mwewe[8]). mwewe kana kishadda, lakini hana mkia.

mchezo wa nyama mlindi.

nyama mlindi mchezo wake wanasuka kambaa la nguo, kisha humlaza mtoto chini, akasimama mtu mmoja kumlinda, naye hushika kambaa. tenna huamru watoto kumpiga yule aliyelala, naye huwavizia wale watoto wampigao. akimpata mmoja — humpiga na kambaa, lâzima yeye aliyopigwa atalala. na akiwa mlalamishi — humfukuza.

mchezo wa kitangayangaya.

hujikusanya watoto, husema: „nani tumtangaize?“ moja atasema: „mimi.“ na kumtangaiza humshika juu ya kichwa — husema:

---

1) Drache. — 2) Papier. — 3) schmale Streifen. — 4) Raphiapalme. — 5) Stärkemehl. — 6) eigentlich Musikinstrument. Hier — schmaler Papierstreifen, einmal der Länge nach gefaltet, der beim Durchschneiden der Luft einen summenden Ton gibt. — 7) Strauss von zusammengebundenen Papierstreifen. — 8) Habicht.

„kitangayangaya [1]),
babiye Mgaya [2]),
mwenyi ndevu mbili,
kitumbo baridi [3]),
mwenyi pembe [4])
ndiye mkaidi [5]), siye.“

tenna humwambia: „ukasikia »kuru kuru« njoo.“

wakesha, watoto wote hukimbia kwenda kujificha. wakesha, humwita „kuru,“ naye huenda kuwatafuta. atakayempata, humfunya [6]) ukucha, yeye atatangaizwa.

mchezo wa bui [7]).

bui mchezo wake kama kitangayangaya, lakin humshika mtoto mmoja, akafungwa kitambaa machoni, kisha humwuliza: „bui?“ huitikia: „naʿam.“ [8]) „watoka wapi?“ hujibu: „natoka Maskati.“ „umekula nini?“ hujibu: „nimekula tende.“ „kitoweo nini?“ hujibu: „nazi mbovu.“ humwambia: „umpataye — mfunye kucha.“ hukimbia watoto, naye huwatafuta. atakayempata, atafungwa yeye kitambaa.

mchezo wa kibafute.

kibafute — watoto hunuuna mhindi mbichi wakachoma. mwingine wanatafuna, na mwingine wanachezea kibafute. na kucheza kwake — hupukucha punje [9]), akatia mkononi máthalan [10]) mbili, kisha hufumba kiganja [11]), humwambia mwenziwe: „kibafute.“ naye akijibu „mbili fute,“ zikiwa mbili, humpa. zikiwa záyidi,

---

1) Du bist der Sucher. — 2) Du bist in Nöthen wie der baba Mgaya. — 3) d. h. hungrig. — 4) Name für den Sucher. — 5) ungezogen, widerspenstig. — 6) zwicken. — 7) Spinne. — 8) ja. — 9) Körner herausnehmen. — 10) z. B. — 11) Handfläche.

atamwambia nne, atalipa yule aliyosema mbili — atalipa mbili.

mchezo wa lalalalalalá.

huchezwa vilevile kwa muhindi. mtoto humwambia mwenziwe, wakitaka kula muhindi pamoja: „sema lalalalalá, na mimi ntasema gumgumgum.“ ma'ana yule, asemaye lalalala, hawezi kutafuna muhindi, na huyu, asemaye gumgum, anaweza kutafuna.

na mchezo huu huchezewa mtoto na wazee wake, anapokuwa na choyo [1]). máthali baba yake, ameshika muhindi yule mtoto, ao kitu kingine kinacholiwa, humwambia „baba [2]) nigawie nami,“ na yule mtoto hampi, bassi humtaka kwa ujanja [3]), humwambia: „tucheze mchezo wa lalalala.“

1) Geiz. — 2) Kosename für das Kind. — 3) Schelmerei, List.

mchezo wa pembea [1]).

pembea watoto hufunga kamba katika nguzo za nyumba. kesha mtu hukaa juu ya ile kamba, mtoto mwingine humsukuma, naye huimba mwimbo:

„pembea, iyô [2]), pembea,
pembea, iyô, pembea,
wewe Maasiti [3]), pembea,
kalaga hasi [4]), pembea.
mtama ukigwa [5]), pembea
tule tuta [6]), pembea,
tuta kaya [7]), pembea,
ya mgambo [8]), pembea.“

1) Schaukel. — 2) Ausruf der Freude. — 3) Name eines Mädchens, welches der auf der Schaukel stehende Junge einladet zu ihm auf die Schaukel zu steigen. — 4) Altsuaheli = kaa kitako. — 5) gwa fallen; wenn die Hirse geerntet wird, d. h. wenn das Mädchen herangereift ist, wollen wir heiraten. — 6) kaum gereiftes mtama. — 7) Ort, Stadt. — 8) Freude.

mwimbo huu wa pembea huimba katika pembea ya kamba, ao hujikusanya watoto waanaume na waanawake pamoja, husimama wima, nao hushikana mikono, akemba mmoja, na wote huitikia. anapotaja jina la mwanamke, yule kijana hukaa kitako chini, ao anayekwimba kijana mwanamke, akitaja jina la mwanamume, yule kijana mwanamume hukaa chini naye.

ao huimba:

„watoto mnara [1]), mnara ~~wa njia,~~
baba akija, naja kumwambia
»kitanda chako kitabangiwa [2]).«
likavuma na livume [3]) — shindo likaingia [4]),
mwambani tega.“ [5])

1) gemeint ist „ein Mann.“ — 2) kimeharibiwa d. h. dein Bett ist missbraucht worden. — 3) auf shindo bezüglich. — 4) ich bin des Gerüchtes sicher. — 5) an der Klippe (d. h. von dem Kinde selbst) ist es gefangen.

Wie mir mein Gewährsmann mitteilte, haben die Kinder diese Lieder von den Alten gehört, ohne jedoch ihren eigentlichen Sinn zu verstehen.

ao hucheza:

„mama kanambia »winga [1]) kuku,«
nami siwezi kuwinga kuku,
nimejikalia kiwetewete [2]),
mpunga wa mama waliwa na ndege,
ish ish.“

na wakisema „ish ish,“ hao wasio katika pembea, huruka.

---

1) fortjagen. — 2) ohne Füsse.

ao huimba:

nalialia ôyi!
namlilila kitoto changu,
kitoto changu katwaliwa

na watu wa Makonde.
„watoto ni wangapi?“
„saba‘ hê,
Kitunguja [1])
katwaliwa
na watu wa Makonde.“ [2])

1) Name des Kindes. — 2) eine Frau beweint ihren Mann, der von einer Frau der Makonde entführt worden. Eine andere Frau fragt sie, wieviel Männer sie noch habe, darauf antwortet sie „sieben,“ aber der Kitunguja fehlt mir.

mchezo wa kutega ndege.

kwanza hugonga urimbo [1]) wa mchongoma [2]), wakaupika kwa mafuta. ukawiva — huupaka juu ya vijiti. tenna huenda mashamba, wakatezama tua linalo ndege wengi, wakaweka vijiti vya urimbo. ndege wakafika juu ya vijiti — wananasa. na akinasa ndege, husema „kibawa,“ [3]) hukimbia mbio kwenda kumtoa yule ndege.

na wengine wanatega kwa tanzi [4]), huweka nyenze [5]) chini ya tanzi, nyenze akilia — kwamba wakiona nyenze — hushuka chini ya tanzi — marra amenasa.

wengine wanatega kwa matundu [6]), hutia ndege ndani ya tundu, anayelia sana — chiriku [7]). hutia na mawele [8]) ndani ya tundu, wakaliweka lile tundu juu ya mti. na mitego [9]) wameiwacha wazi. yule chiriku hulia, na chiriku aliye nje, akisikia mwenziwe analia, hukaa juu ya mtego, na ule mtego hufiatuka [10]), amenasa ndege. khabari ya wale watoto: ndege wakiwapata — wanawachinsha, huwachoma kwa chumvi,

1) Vogelleim. — 2) Baum. — 3) Flügelchen. — 4) Schlinge. — 5) ein Insekt. — 6) Käfig. — 7) Vogel. — 8) Hirseart. — 9) Fallen, das sind kleine Seitenbehälter am Käfig. — 10) zuklappen.

wakala. na wakipata ndege wakubwa — wanawauza. na hao chiriku — hawaliwi, hufugwa tu ndani ya matundu. huu mchezo wa kutega ndege.

mchezo wa kueleza[1]) mashua.

mashua zao huunda miwale[2]), ao wanaangua makarara[3]) ya mnazi. kisha hufanya matanga na mlingoti. maji yakapwa[4]), huenda pwani kueleza mashua zao. nao hushindana, mashua ya nani inakwenda mbio. hukaa pwani ḥatta maji yakajaa. maji kujaa wanavua nguo, wanakoga na kuogelea. na koga kwao hupigana mikambi[5]), hujigawa, watano huku na watano huku. na huo mkambi mtu huzama, kisha hunyanyua mguu juu, marra hupiga mkambi, hufikia juu ya kichwa ao mongoni. ao hushindana mbizi[6]), humwambia mtoto: „sisi tutazama, nawe ututafute, utakáyempata mfunye[7]) ukucha, yeye ndiye atakáyetutafuta.“ wakesha cheza mchezo wao, wakitoka nje, wengine nguo zao zimeibiwa, wanakwenda uchi majumbani, nao hulia kwa kuogopa wazee wao. wakifika nyumbani, hutukanwa, sababu wanakatazwa koga pwani, maʿana kuna khaṭari[8]) — chunusi[9]). ao marra nyingine maji hujaa, na watoto wamekaa juu ya fungu[10]), wanacheza, hawana khabari, kama maji yanajaa, wakikumbuka kwenda ufukoni, maji yamejaa, asiyejua kogelea atakufa. ndio sababu wazee wao huwakataza koga pwani.

mchezo wa kibuzi.

kibuzi hujikusanya watoto, hunyosha miguu katika ṣafu[11]) moja, na moja hukaa kitako, ndiye anayeanza kwimba mwimbo:

---

1) schwimmen lassen. — 2) Palmrippen. — 3) holzige Blütenscheide. — 4) pwa ebben. — 5) Rad schlagen. — 6) tauchen. — 7) zwicken. — 8) Gefahr. — 9) Seeungeheuer, das Leute tötet. — 10) Sandbank. — 11) Reihe.

„kibuzi [1]) kibuzi“
wototo huitikia:
„memême memême“ [2])
yeye huimba:
„mwana mbuzi kajamba“ [3])
watoto huitikia:
„kajambile [4]) mchunga“
yeye huimba:
„dekedeke [5]) malenga [6])
mkono shindika
uende [7]) Manga
ukatwae fumo [8]) na upanga“
wote huitikia: „kuku,“ ao „tutu.“

---

yeye huimba:
„simba kalegea“ [9])
watoto huitikia:
„kalegea kôngwe [10])
kôngwe la mwana mzee“
yeye huimba:
„tate [11]) haligonile [12])
ligona [13]) kwa mke mbuya [14])
na matikiti na matango [15])
kumi na mbili.“

---

1) er ist wie eine kleine Ziege. — 2) ruft mä mä mä. — 3) kajiamba. — 4) kajiambile = amemjambia. — 5) ich habe bereut. — 6) Wasser. — 7) auf mkono bezüglich. — 8) Speer. — 9) regea. — 10) alt. — 11) Vater. — 12) gona schlafen; haligonile er hat nicht geschlafen. — 13) er schlief. — 14) Geliebte. — 15) mit Wassermelonen und Gurken; mein Gewährsmann teilte mir mit, es bedeute „Nacht und Tag“ und zwar 12 im Ganzen.

Der Sinn soll folgender sein: Ein Mann hat sich um eine zweite Frau beworben und viel darüber geredet, ist aber abgewiesen und nun klein und reumütig zu seiner ersten Frau zurückgekehrt.

ao watoto wakinyosha miguu hivo, huimba moja:
„hiki [1]) cha nani?“
mwingine hujibu:
„cha baba“
huimba tenna yule wa kwanza:
„hiki cha nani?“
mwingine hujibu:
„cha mama.“

1) nämlich kiguu, indem der eine auf des anderen Bein zeigt.

mchezo wa kongoti [1]).

kongoti watoto hufunga mabua yakawa marefu, kisha huyavika kanzu, wakafanyiza mkia na mikono, kisha huingia mtu ndani, akenda na lile kongoti huenda. nalo huwa refu sana, ndio ma'ana ya kwitwa kongoti. mtu akiona hujituka [2]). khaṣṣa [3]) watoto wadogo. watoto walio watundu [4]), likipita kongoti, huambiwa: „na wewe ukiwa mtundu, kongoti litakuchukua. wale watoto, waliwo nyuma ya kongoti, wote ni watoto watundu, kongoti hupita likiwachukua.“

na mwimbo wao, wanapozungusha kongoti, moja husema:

„kongoti hê leo [5]),
kongoti“

na wengine huitikia:

„na mkia wake
nyumbani mwenu
hamna mwanamke
mwenyi kibiongo?“

1) Storch. — 2) erschreckt werden. — 3) besonders. — 4) unartig. — 5) das kongoti kommt.

mchezo wa kônya[1]).

watoto wakitakana urafiqi, hupingana[2]) na kônya, ma'ana ya hiyo kônya hupingana vidole vya mwisho, huja na mtoto shâhidi[3]) kukata vile vidole, humwambia: „shuhudia mimi, napigana na fulani kônya.“ na yule shâhidi hukata vidole vyao. kônya hupinga urafiqi.

urafiqi huo wakesha pingana, mmoja wapo akiwa na kitu — kofia mpya ao kitu kingine, wakikutana njiani, mmoja husema „kônya — kofia yako,“ bassi marra avue ampe. na akiwa rafiqi mwema — humrudishia kofia yake, huchelea wazee wake wasimgombeze, illa kitu kidogo huchukua. ao ukimwona rafiqi anakuja, marra useme: „mbémbémbé kofia yangu“ — hawezi kuchukua.

1) Freundschaft. — 2) mit dem kleinen Finger in einander haken. — 3) Zeuge.

mchezo wa kinyuri.

watoto huweka mikono juu, kisha hufunyana[1]) makucha, kesha huimba mwimbo:

„kinyuri[2]) nyurika
kavaa nguo mbili[3])
na milango miwili[4])
mkakasi[5]) na urembo wake,
aliye juu na aruke.“

ukesha mwimbo, ule mkono ulio juu, huondoa mtoto.

1) zupfen, mit zwei Fingerspitzen die obere Handfläche der Hand des Mitspielenden. — 2) dessen Hand oben ist. — 3) kikoi na kanzu oder shiti mbili. — 4) von zwei verschiedenen Farben. — 5) Dose mit Wohlgerüchen.

mchezo wa kilipembe ao kitikiti.

ma'ana ya kilipembe husimama watoto wawili, wakashikana mabega, kisha huja mtoto wa tatu, akakaa juu ya mikono ya mwenziwe, nao humnyanyua juu, tenna huimba mwimbo:

„kitikiti cha mfaume
mwana wa nani? mwana wa jumbe
akipatapo akikalia,
tumchukue kijuujuu
tumchukue kijuujuu."

mchezo wa nyoka.

nyoka — hufanyiza dimba[1]) katika mchanga. tenna katikati hukaa kitako watoto. na mtoto mmoja husimama nje ya dimba, naye husema maneno „nyoka huyô nyoka," na wale watoto huitikia „na apite." tenna husema „yuko Gongoni," huitikia vilevile „na apite." „yuko Mengesani," huitikia „na apite." tenna husema „hûyó nyoka yupo miguuni," marra watoto wote husimama wakakimbia. anayekawia husimama, humzomea[2]), husema wakapiga makofi:

„fulani kaliwa na nyoka
fulani kaliwa na nyoka."

---

1) Kreis. — 2) auslachen.

michezo ya watu wazima na watoto.

na watu wazima hufanyiza michezo mingi na watoto, máthalan huwambia maneno yaliyo magumu, mfano wa:

„kikuku kike, kaka[1]), kwako kiko?"

---

1) Bruder.

na maneno hayo mtu hawezi kuyataja kwa upesi, huyachanganya pamoja.

ao husema:

„jana sili[1]) mananasi
sivo nikopokagavyo.“[2])

1) kinyume für nimekula. — 2) kopoka wund machen.

ao husema:

„wauawo[1]) wawe wao[2])
waua wewe — wauawa.“

1) wanaoua. — 2) wafalme.

ao husema:

„nanena[1]) nane ngapi?

mtoto hujibu kumi na sitta, si kumi na sitta, ásili yake nane.

1) Wortspiel zwischen nanena und nane na.

khabari ya chuo[1]).

khabari ya mtoto kwenda chuoni.

mwʿallimu[2]) anapoanza chuo kusomesha, huja mtu na mtoto wake, humwambia mwʿallimu: „nataka unisomeshee mwanangu.“ humwuliza: „ijara[3]) yako qiâsi[4]) gani?“ atajibu: „reale kumi ao kumi na tano.“ wakesha patana, atamwambia: „kesho kaanga bisi na nazi, umlete mtoto chuoni.“

as-ṣubuḥi atampeleka, atachukua na rupia mbili, rupia hizo jina lake „ufito“ ao „ubati.“ na mwanzo wa kusoma mtoto kwanza huandikiwa juu ya ubao. yule mtoto akishika ubao, akikumbuka mchezo wa geli[5]) na ṭiyyâra[6]) — umempita — marra hulia. kulla akimwona mwʿallimu mbele yake, ajiona kama yu pamoja na ʿIzraîli[7]).

kwanza huandikiwa: „aʿûżu bi'llâhi mina 'esh-sheiṭâni 'r-rajimi. rabbi yassir walâ tuʿassir ʿaunaka. yâ rabbi yâ muʿînu yâ laṭîfu yà allâh.“[8]) akijua, huandika alif, be[9]) ḥatta mwisho. na anapoandikiwa sura[10])

---

1) Schule. — 2) Lehrer. — 3) Lohn. — 4) Maß d. h. wie teuer? — 5) u. 6) Kinderspiele. — 7) der nach Ansicht der Suaheli auf Befehl Gottes den Menschen von der Erde abruft und die Seele an sich nimmt. — 8) Ich nehme meine Zuflucht zu Allah vor dem verfluchten Satan. O mein Herr, laß deine Hilfe eintreten und versage sie nicht. O mein Herr, o Helfer o Huldreicher, o Gott. — 9) Alphabet. — 10) Suren des Korans.

nyingine, akasoma ḥatta akajua. aṣ-ṣubuḥi huenda mbele ya mwʿallim, hushika ubao wake, husoma sura aliyoandika kwa moyo billa kutezama. ḥatta akijua, mwʿallimu humpa rukhṣa kwenda pwani kufuta ubao wake. akisha futa ule ubao, hutia jasi[1]). na hilo jasi udongo mweupe mfano wake kama chaki. maʿana yake kutiwa jasi — wino waqti wa kufuta ule ubao marra utoke. nao hukatazwa waanafunzi kufuta mbao kwa miguu, maʿana ḥaramu[2]). na asiyejua ubao wake kuṣafisha[3]), hapewi rukhṣa kwenda kwao.

kaẓâlika watoto wakifika pwani kufuta hizo mbao, huvua nguo wakoga na kupigana. na wengine hupigana kwa mbao, wakenda chuoni — hawana mbao, zimevunjika. hukimbia, huogopa kupigwa na mwʿallimu.

na wale wenyi mbao, zilizo nzima, wakifika chuoni, mwʿallimu huwaandikisha. na kuwaandikisha kwake hushika msaḥafu[4]) mwʿallimu, akasoma aya[5]) ya qorani, humwambia yule mwanafunzi, naye huandika. na anapotamka yule mwʿallimu, mwanafunzi sherṭi[6]) atamke vilevile. nao huogopa watoto kuandikishwa na mwʿallimu. pakiwa na mtoto, aliyekhitimu[7]), yeye hupata rukhṣa kwa mwʿallimu kuandikisha wenziwe, lakini yule mtoto wenziwe humpa kao yake, maʿana pesa moja ao mbili, kama hawakumpa — hawaandikishi.

desturi ya watoto kwenda chuoni killa aṣ-ṣubuḥi, saʿa kumi na mbili lâzima watoto wawekwe chuoni, atakáyekawilia akifika chuoni, hupigwa. na desturi yao wanafunzi wakafika chuoni aṣ-ṣubuḥi, humwamkia mwʿallimu. na kumwamkia kwake humpa mkono, wakambusu[8]). na waqati wa jioni kaẓâlika wakipewa

---

1) Bimstein. — 2) verboten. — 3) reinigen. — 4) geschriebenes Exemplar des Korans. — 5) Verse des Korans. — 6) Bedingung. — 7) Schulzeit beendigt haben. — 8) küssen.

rukhṣa. na jioni wanapopewa rukhṣa, humwombea muungu mwʿallimu wao, husema mtu moja „żikru 'llâh,“ [1]) na waanafunzi huitikia: „lâ ilâha illâ 'llâhu wa Muḥammadun rasûlu 'llâh. mwʿallimna, mwʿallimna, jazâka 'llâh kheiran wa baʿadu 'l-kheiri wa baʿadu 'l-kheiri jennatan naʿîma.“ [2]) humpa mkono, tenna huenda zao.

ʿada [3]) za chuoni.

killa al-khamisi [4]) ʿada pesa mbili kulla mtoto hupeleka kwa mwʿallimu, ḥatta mtoto akhitimu. na kulla ramaḍani ikiandama, hupewa mfungo wake mwʿallimu pesa nane, kumi, ao sittaʿshara. na kulla siku kuu [5]) mwʿallimu hupewa siku kuu yake vilevile kama katika ramaḍani. na wanafunzi hupewa rukhṣa siku tatu kucheza. na mtoto akaingia sura, inayoḥitaji [6]) ʿada kutolewa, kwanza mtoto akifika „qul huwa 'llâhu“ [7]) — hutoa kuku kupeleka kwa mwʿallimu ao mapesa. sura ya pili „lam yakuni“ [8]) akifika — hutoa mzigo wa kuni ao mapesa. sura ya tatu „wa 's-samâi żâti 'l-burûji“ [9]) hupikwa uji na maandazi, mwʿallimu na waanafunzi wake na watu wengine huja wakanywa, ao hutoa mapesa kumpa mwʿallimu. sura ya nne akafika „juzu ya ʿama“ hupikwa mkate, huletewa na reale, akapewa mwʿallimu. maʿana yake afikapo ʿama, huambiwa amefungua ḥija [10]), maʿana anajua kusoma pekeyake na kuandika pekeyake. na akafika „yâ sîn,“ [11]) hupelekewa ʿada yake rupia ao roboʿ. na ʿada ya mwisho

1) Lobpreis Gottes. — 2) Es gibt keinen Gott außer dem einen Gott und Muhammed ist der Sendbote Gottes. Unser Lehrer, unser Lehrer, möge Gott dir Gutes vergelten und nach dem Guten und nach dem Guten ein wonniges Paradies. — 3) übliches Geschenk. — 4) Donnerstag. — 5) Feiertag. — 6) wünschen, fordern. — 7) Sure 112. — 8) S. 98. — 9) S. 85. — 10) Alphabet. — 11) S. 36.

ni ile siku ya kwanza endayo chuoni mwanafunzi kupelekwa rupia mbili na mkate na nazi na bisi. na akakhitimu, hupewa ijara yake mwʿallimu kama walivopatana.

na desturi hizi, na ʿada tulizozitaja, zimepita kwa waanafunzi wa zamani na waʿallimu wa zamani. waʿallimu wa sasa shidda[1]) kupatikana mambo haya yote, sababu huwarusha wale waʿallimu, huwambia „kesho, kesho kutwa.“

adabu[2]) ya mwʿallim na mwanafunzi wake.

kwanza: ukiwa kwa mwʿallim wako, sherṭi uwe kama mtumwa. kama kazi, atakáyokutuma mwʿallim wako, lâzima uiqubali[3]).

adabu ya pili: mwanafunzi aṣ-ṣubuḥi na jioni kwenda kwa mwʿallim wake kuamza[4]) na kutwesha[5]).

adabu ya tatu: mke wa mwʿallim wako umfanye kama mama yako, ajapokuwa ni kijana.

adabu ya nne: ukamwona mwʿallimu wako katika njia amechukua kitu, lâzima umpokee.

adabu ya tano: kama unefuatana na mwʿallim wako, wewe usiwe mbele, mwʿallim akawa nyuma.

ya sitta: mwʿallimu iwapo amesafiri, akirudi katika mji, marra uende ukamwamkie.

ya sabaʿ: ikiwa anazungumza na watu, usimkate maneno yake mbele za watu.

adabu ya nane: mtu aliye mwʿallimu, asiyekuwa mwʿallimu wako, sherṭi umḥeshimu[6]).

adabu ya tisaʿ: rafiqi wa mwʿallim wako, umpe ḥéshima[7]) kama mwʿallim wako.

adabu ya kumi: kikao anachokaa mwʿallim wako,

---

1) selten. — 2) Anstand. — 3) einwilligen. — 4) guten Morgen wünschen. — 5) gute Nacht wünschen. — 6) ehren. — 7) Respekt.

usikikalie, illa iwapo hayupo, amekuachia chuo kusomesha.

adabu ya ḥedʿashara: mwʿallimu wako akipita, panapo watu, akitoa salâm, uitikie kwa ḥéshima na kusimama.

adabu ya thenʿashara: usikae katika barza, ukamteta mwʿallim wako.

fimbo na ʿażabu[1]) nyingine wanazopigiwa wanafunzi.

mwʿallimu husuka kambaa, na hilo kambaa ncha za miyaa[2]), husukwa ncha mbili ao ncha tatu, ao huambiwa wanafunzi kwenda mwituni kukata fito za mwafu[3]). na fito hizo leini[4]), nazo ndefu kama kambaa. ao mwʿallimu hununua khenzerani[5]) dukani. ndizo wanazorudiwa waanafunzi chuoni.

na mwʿallimu akisahau ufito wake ao kambaa lake, waanafunzi wakiona huiba, wakachoma moto. aṣ-ṣubuḥi wakiulizwa, killa mtu huapa kiapo „mimi sikuona, mimi sikuona.“

na ʿażabu wanayotiwa watoto chuoni, iwapo mtoto mtundu[6]), anakawia kuja chuoni, mwʿallimu humnyima rukhṣa[7]) kwenda kwao. na chakula huletewa chuoni na wazee wake. na siku ya el-jumaʿ hapati rukhṣa, hukaa chuoni.

na akendelea utundu — hupigwa, ao hukaa kitako, akanyosha miguu, akafungwa kamba, na mikono vilevile hufungwa kamba katika nguzo ya nyumba. lakini watu wakiondoka, yeye mwenyewe hufungua na meno — akakimbia.

na iwapo ni mtundu sana, hutiwa gogo[8]) mguuni

---

1) Strafe. — 2) Dumpalme. — 3) wilder Jasmin. — 4) geschmeidig, biegsam. — 5) spanisches Rohr. — 6) unartig. — 7) Urlaub verweigern. — 8) Holzklotz.

na kipande cha mnyoo[1]). akakaa chuoni, kisha kusoma, na watoto wengine wameondoka, hushika gogo lake, akenda zake. hukaa na gogo siku mbili ao siku tatu, kisha huja rafiqi ya yule mwʿallim kumwombea yule mtoto.

mwʿallim akialikwa karamu[2]) shamba pamoja na waanafunzi, hufuraḥi sana wale waanafunzi, sababu hucheza njiani na kuangua matunda, embe, mapera, hukata mananasi, na wengine hupigana. ḥatta wakafika shamba, waliloalikwa, mwʿallimu huletewa mashitaka[3]), mambo waliyotenda waanafunzi wake, hupewa ʿażabu yao.

desturi ya waanafunzi wakifanya vitendo, visivo adabu, maneno hupelekewa mwʿallimu wao. naye huwarudi[4]) kuwapiga. asipowarudi, watu humtukana yule mwʿallimu kwa siri[5]), husema: „mwʿallimu fulani waanafunzi wake hawana adabu.“ na maʿana ya kuto' kuwa[6]) na adabu — yeye hana adabu. na waanafunzi watundu sana, hawaogopi mtu illa mwʿallimu wao.

na mwʿallimu wao, akiwa mkali, humpa jina „kiparamoto,“[7]) ao akiwa mfupi, humwita „nyundo,“[8]) na akiwa mrefu, humwita „kongoti“[9]) ao „korongo,“[10]) na akiwa na ndevu ndefu, humwita „kibeberu.“[11])

nao wanafunzi huwa marra nyingi watundu mno. na mwʿallimu akikaa barazani, kama hataki kuondoka, nao wanataka kucheza — hawapati, mwanafunzi mmoja humwambia mwʿallimu: „amekuja mtu fulani kukuuliza, ataka uende kwake.“ nayo si kweli — uwongo. ataondoka mwʿallim, wakapata kucheza.

haifai kucheza na watoto wa chuoni kama iliyoandikwa katika khabari ya zamani:

---

1) Kette. — 2) Fest. — 3) Klagen. — 4) eigentl. ruddi zurechtweisen. — 5) im Geheimen. — 6) verneinter Infinitiv. — 7) von paa; Feuergeber. — 8) Hammer. — 9) Kranich. — 10) Storch. — 11) Ziegenbart.

ḥadithi[1]) **ya watoto wa chuoni na sheṭâni**[2]).

sheṭâni alizaa watoto saba', mtoto wa saba' jina lake Wasiwasi. mama yao akawauṣia[3]) watoto wake — ya kama: „wanangu[4]), mkitaka raḍi yangu, umsicheze na watoto wa chuoni, sababu watundu sana.“ watoto sitta wakasikia waṣia[5]) wa mama yao, yule wa saba' asiushike.

siku moja yule sheṭani, jina lake Wasiwasi, amejigeuza punda, akenda njia panda, akalala, ḥatta watoto walipolikizwa chuoni. walipofika pale njia panda[6]), wakamwona punda amelala, wakafuraḥi watoto wote, wasende majumbani kwao kula. killa mtu akatafuta ufito, wakampiga yule punda. na yule punda asisimame. watoto wakatafuta pilipili hoho[7]), wakasaga, wakamtia ukunduni[8]). akaondoka kwa ile pilipili kumwasha ukunduni, akenda mbio. nao wanamfuata, na huko wanampiga. naye huwapiga mateke[9]), nao wanamfuata, wakamta'abisha[10]) punda mchana kutwa. ḥatta jioni watoto wakamwacha punda.

alipofika kwao, yule punda akatoa qiṣṣa[11]) kilichompata. mama yake akamwambia: „nimekwambia mwanangu, usicheze na watoto wa chuoni, leo wametaka kukuua.“

khabari ya mtoto mwanamke.

mtoto mwanamke huitwa kigori mwanzo wa miaka saba', ḥatta akipata miaka kumi na mitano huitwa mwari. qa'ida ya watoto hao hukaa nyumbani. kwanza hutogwa[12]) mashikio kwa miba. na siku ya kutoga hufanya furaḥa[13]) naye kama h'arusi[14]). naye mtoto

1) Geschichte. — 2) Teufel. — 3) vermachen, ans Herz legen. — 4) waana wangu. — 5) Testament, Ermahnung. — 6) Kreuzweg. — 7) roter Pfeffer. — 8) After. — 9) Fußtritte. — 10) quälen. — 11) Sache. — 12) Ohrlöcher stechen. — 13) Freude. — 14) Hochzeit.

hufundishwa killa adabu ya nyumba, huosha vyombo, ṣaḥani na mabakuli. na akesha, hupewa chanzo cha ukili [1]) kusuka [2]). killa siku kazi yake kusuka mikeka na kufundishwa kupika.

naye hana rukhṣa ya kutoka nje, illa usiku kwenda kumtazama watu waliomkhuṣṣi [3]), naye hendi [4]) pekeyake, hufuatana na kijakazi ao mwanamke mzee. na iwapo mtembezi, killa paḥali huenda, hupigwa na wazee wake. naye shidda [5]) kupata mume mwema, maʿana watu husema: „mtoto wa fulani mtembezi, anajua killa paḥali.“

kaẓâlika iwapo yumo katika nyumba, na mlangoni anakuja mgeni, mwanamke ao mwanamme, nao hawajui — lâzima ajifiche katika chumba kingine, asizungumze nao. wazee wake wakimsikia, humgomba sana, humwambia: „ukisikia hodi, unachungulia uso wako, watu wote wakuone?“ na watu wakisikia, ya kama uso wake hajifichi, humsema katika mji: „mtoto wa fulani uso wake umemkauka — hana ḥaya [6]), si mwanamke wa kuolewa.“ hupata labda mume, lakini hukawia.

na mtoto mwanamke akipata miaka kumi, huja mwanamke moja, ndio kungwi [7]) lake, akamvika utunda [8]) kiunoni. huyu ndio somo [9]) yake ya siku zote, na maʿana ya huo utunda ni pendo, ili kumtia hamu [10]) mwanamume kumtaka mwanamke. mwanamke asiyekuwa na utunda, watu husema kiuno chake kimepooza.

khabari ya waanafunzi wasomayo ʿilmu [11]).

waanafunzi hao — wakubwa, ʿomri [12]) wao tangu miaka ʿesherini ḥatta khamsoʿesherini. watu hao

1) Mattenstreifen. — 2) flechten. — 3) nahestehen. — 4) hendi. — 5) selten. — 6) Scham. — 7) Lehrmeisterin; von kunga verhehlen, verheimlichen. — 8) Hüftschnur aus weißen Perlen, die von allen Suaheli-Frauen und Mädchen auf dem bloßen Leib getragen wird. — 9) Freundin. — 10) Verlangen. — 11) Wissenschaft, Auslegung des Korans. — 12) Alter.

baʿada ya kujua qorâni, huenda kwa shekhe[1]), kusoma ʿilmu, kujifundisha sherṭi[2]) zinazowâjibu[3]) juu ya ṣala[4]), na sherṭi za mke kuoa na kuacha, na ḥokumu[5]) za kuuza na kununua, na jamiʿei[6]) ya sheriʿa[7]). lakini watu hao mbele ya shekhe wao hawafanyizi upuuzi kama waanafunzi wadogo, humḥeshimu[8]) sana shekhe wao.

na desturi ya watu, wendao katika darsa[9]), wakafika, iwapo shekhe bado kuanza kusomesha, humwamkia „ṣubalkhêri“[10]) ao humpa mkono wakambusu[11]). na iwapo anasomesha, si adabu kumwamkia, illa baʿada ya kusomesha. na watu walio katika darsa ya ʿilmu, waanafunzi na watu wengine, wanaosikiliza, si adabu kuzungumza maneno mengine, illa humsikiliza yule shekhe fasiri[12]) atoayo. na kulla mtu huchukua kitabu, endapo katika darsa. na killa kitabu namna mbali, wengine huchukua „naḥau,“[13]) wengine „min ḥajji,“[14]) wengine „tefsiri ya qorâni,“[15]) vitabu vya ʿilmu namna nyingi. na desturi ya yule shekhe akesha somesha, hupiga fâṭiḥa[16]), na watu walio barazani huitikia amîn[17]). kulla mtu huomba duʿa[18]) atakayo. wengine huomba: „muungu anipe ʿafya[19]), aniondolee maraḍi,“[20]) wengine huomba „muungu anipe fahamu[21]), nijue ʿilmu,“ wengine huomba „muungu aniṣameḥe[22]) żambi[23]) zangu, anistiri[24]) ʿaîbu[25]) yangu,“ huomba mtu kama atakavo.

na hiyo darsa husomeshwa aṣ-ṣubuḥi na jioni. wengine husomesha aṣ-ṣubuḥi tu. mashekhe, wengine

---

1) Gelehrter, Alter. — 2) Bedingung. — 3) sich beziehen (verpflichten). — 4) Gebet. — 5) Gesetz. — 6) Gesamtheit. — 7) Gesetz. — 8) ehren. — 9) Schule. — 10) ṣubḥ al-khêr guten Morgen. — 11) küssen. — 12) Erklärung. — 13) Grammatik. — 14) Pilgerreise. — 15) Erläuterung des Korans. — 16) erste Sure. — 17) Amen. — 18) Anrufung. — 19) Gesundheit. — 20) Krankheit. — 21) Verstand. — 22) verzeihen. — 23) Sünde. — 24) bedecken. — 25) Schande.

husomeshea majumbani kwao, na wengine husomeshea meskitini. desturi ya Wasuaḥeli mtu, ajuayo qorâni na ʿilmu, humpenda sana. iwapo mgeni, naye anataka kukaa katika mji, akitaka mke kuposa, marra hupewa, killa mwenyi mtoto wake hufuraḥi yule mwana chuoni kumwoa, ajapokuwa maskini.

lakini ikiwa mtu anatoka mbali, akaja katika mji mwingine, kukaa kule kama mwʿallimu, akanena „mimi mwʿallimu, nimesoma qorâni na ʿilmu," na watu hawamjui, humwandikia soali[1]). anapozijibu zile soali, huqubaliwa[2]), ya kuwa ḥaqîqa[3]) yeye ndio mwʿallimu.

1) Frage. — 2) zustimmen. — 3) Wahrheit.

khabari ya mwʿallimu.

kuna mwʿallimu aliyechukuliwa na mkubwa wa mji. kama iliyokuwa zamani. naye hupewa mshahara[1]) kulla mwezi khamsoʿasherîn rupia. mwʿallimu huyu hukaa meskitini kuṣalisha na kuangalia khabari za meskiti. naye hupewa katika ṣádaqa[2]) zinazokwenda meskitini. na jumla[3]) ya watu katika mji hupigwa mbiu[4]), ya kama mtu, anayetaka kuoa, hana rukhṣa ya kuoa kwa mwʿallimu mwingine illa mwʿallimu huyu. naye hupata kwa killa mtu, anayetaka kuoa, ijara[5]) rupia mbili. naye mwʿallimu hupewa nyumba ya kukaa na watu wa mji.

kuna mwʿallimu mwingine, huajiriwa[6]) na watu, kusomesha watoto wao majumbani kwao, hupatana naye killa mwezi kumpa mshahara rupia kumi ao khamustʿashara. killa aṣ-ṣubuhi huenda marra moja akasomesha, na jioni vilevile, illa el-jumaʿa na siku za siku kuu. na kulla ʿada[7]) zinazoḥitajia[8]) — hupewa, mfano wa ramaḍani na siku kuu zake, lakini watoto wakikhitimu[9]), hana ijara tenna, illa hupewa kilemba. nao hawapatani kwa mwezi ao kwa miaka, hupatana watakâpokhitimu

---

1) Monatslohn. — 2) Almosen. — 3) Summe. — 4) Büffelhorn, eigentl. das Horn blasen d. i. bekanntmachen. — 5) Lohn, Zahlung. — 6) in Lohn nehmen. — 7) Geschenk. — 8) erforderlich sein. — 9) die Schule verlassen.

watoto, ikawa mwaka moja ao miaka miwili, ndio mapatano yao.

kazi ya hao waʿallimu kazi nyingi billa ya kusomesha. baʿada ya kurejeʿa meskitini kuṣali aṣ-ṣubuḥi, hushika mṣaḥafu, akasoma qorâni, ao huvuta auradi[1]), na huo auradi majina ya muungu, huyataja kwa wingi. akisha vuta auradi, huja mtu, akamwambia: „tafaḍḍali[2]), nataka unisomee khîtima[3]) za wazee wangu mbili ao tatu.“ ao huja mtu anataka kigwe[4]) cha mtoto, ao mtu anataka kujenga nyumba, mwanzo ataka asomewe „yâ sîni“[5]) juu ya kiwanja chake. bassi mwʿallimu huchukua mṣaḥafu, akenda pale kiwanjani. ao huja mtu anataka kuoza ao kuozwa. bassi hufanyiza khabari hiyo mwʿallimu, nao humpa kitu kama wanachojaʿaliwa[6]). kaẓâlika iwapo yeye ni imâmu[7]) katika mskiti, na ule mskiti una khêri[8]), shamba ao nyumba, dukhûli[9]) ipatika nayo katika shamba, sehemu[10]) kubwa huwekwa sababu ya mskiti, ukivunjika — feḍḍa yake hujengwa, na sehemu moja mwʿallimu na mwaẓẓini[11]) na mteka[12]) maji hugawiwa.

ao amekuja mtu, ametoka barra, anataka kuwa islâmu, huenda kwa mwʿallimu, husema — ya kama: „mimi nataka kuwa islâmu.“ humwambia: „nenda ukafue nguo zako, na nywele uzinyoe, ukesha oge, tenna njoo kwangu.“ kisha atakuja, atamfundisha yule mwʿallim, atasema: „sema — ashhadu an lâ ilâha illâ 'llâhu, wa ashhadu anna Muḥammed rasûlu 'llâhi.“[13]) maʿana ashhadu „nimepokea kwa moyo wangu, nimebaini[14]) kwa ulimi — hapana muungu mwingine illa yeye moja. nime-

1) Rosenkranz. — 2) bitte. — 3) Koranlesung. — 4) Amulettschnur. — 5) Sure 36. — 6) bestimmen. — 7) Vorbeter. — 8) Gut. 9) Einkommen. — 10) Anteil. — 11) Rufer zum Gebet. — 12) Wasserschöpfer. — 13) muhamedanisches Glaubensbekenntnis. — 14) aussprechen.

pokea tenna kwa moyo wangu, nimebaini kwa ulimi, ya kwamba Muḥammadi ni mjumbe wake muungu, si mtoto wake.“ yule mtu akisha sema maneno haya, naye ameqirri [1]) kwa moyo wake, amekuwa islâmu.

tenna hufundishwa kufunga ramaḍani [2]), na kuṣali [3]), kulla namna ya ṣala [4]) huonyeshwa, na kwenda mskitini killa waqti wa ṣala mchana kutwa marra tano, na kufundishwa kuelekea qibla [5]) zamani za kuṣali. naye huuliza neno gani la ḥalâli [6]). neno gani la harâmu [7]), atajibiwa kama lifaʿalo. huyo mtu, atokayo barra, hutaka mwenyewe kwa raḍi [8]) zake, haambiwi kwa nguvu. hutaka na kufundishwa kuchinsha nyama, mbuzi na ñgombe, mwanzo wake husema „bismillâhi.“ [9])

aiḍa [10]) na khabari ya watoto kusomesha — taʿabu [11]) kubwa, pato lake dogo, sababu watoto wakikhitimu, feḍḍa yake mwʿallimu hapati yote. wengi wanasoma burre sasa kuliko wanaotoa ijara, maʿana mwanzo hupatana kutoa feḍḍa, na mtoto akikhitimu, humzungusha mwʿallimu, hawampi kitu.

---

1) anerkennen. — 2) fasten im Ramasanmonat. — 3) beten. — 4) Gebet. — 5) Richtung nach Mekka — 6) erlaubt. — 7) verboten. — 8) Zufriedenheit. — 9) im Namen Gottes. — 10) ferner. — 11) Mühe.

desturi za adabu[1]).

adabu za watoto.

mtoto wanapomlea, khaṣṣa[2]) akipata ʿomri wa miaka sitta ao sabaʿ, humfundisha mno adabu. naye lâzima kusikiliza sana amri ya wazee wake. iwapo wamemkataza neno, lâzima asikilize. na kama akafanyiza kwa amri yake — hana adabu.

aiḍa humfundisha kuwaamkia watu, khaṣṣa akimwona mtu mkubwa, anajuana na wazee wake, amwamkie.

tenna hufundishwa kuwasogelea watu wakubwa kwa ḥéshima[3]) na adabu. na akiwa mjuvi, anatukana watu — humpiga.

ao akiwa killa mtu, apitaye njia, humwomba pesa — hupigwa.

aiḍa mtoto akikaa pamoja na watu wazima, asikae kitako qabla ya watu wakubwa hawajakaa kitako. akifanya — huambiwa mtoto huyu hana adabu.

kaẓâlika iwapo amekaa mbele za watu, si desturi kusema maneno haya na haya, humsema watu „mtoto wa fulani hana adabu.“

aiḍa kijana iwapo amekwenda na mzee wake katika ḥáḍara[4]) ya hʿarusi[5]) ao karamu[6]), naye amekaa pa-

1) Anstand. — 2) besonders. — 3) Achtung. — 4) Anwesenheit, Gesellschaft. — 5) Hochzeit. — 6) Fest.

moja nao wanazungumza — wâjibu[1]) wake kunyamaza kimya kusikiliza amri watakáyomwambia. si adabu marra kucheka na huyu, marra kucheka na huyu. watu watamwambia „kijana huyu hana adabu, wala haifai kumchukua katika vikao vya watu.“ illa iwapo yeye amekaa na vijana wenziwe tu, huweza kuzungumza na kucheka na kufanya kelele atakavyo.

tenna mtoto humfunza asiwe na kibri[2]) mbele ya watu.

na iwapo amefuatana na baba yake, si lâzima mtoto kutangulia mbele, illa baba huwa mbele. ao amefuatana na mwʿallimu wake, kaẓâlika atakuwa mbele. na asipofanya hivo, amemtukanisha mzee wake na mwʿallimu wake, naye mwenyewe amejitukana, sababu watu watamwuliza: „baba yako hakukufundisha adabu, wala mwʿallim wako hakukufundisha adabu, ndio maʿana usishike adabu?“

kaẓâlika mtoto si lâzima kutoa ʿaîbu[3]) za watu, mathal[4]) „fulani mkewe hupika chakula kibichi,“ ao „leo wamelala na njaa, hawana chakula, nyumba ya kiza, haina taa.“ mtoto akisema maneno kama haya, watu hujua, ya kama hana adabu.

wa kaẓâlika mtoto huambiwa marra nyingi na wazee wake: „kulla ukaambiwa maneno ya sirri[5]), lâzima uyafiche, si lâzima kumwambia huyu na huyu. ufanyapo kama hivo, hukwambia watu „kijana huyu hana adabu, wala usimpe neno la sirri.“

na iwapo wamekuja wageni katika nyumba, wanakula chakula pamoja, mtoto huambiwa, asitangulie kunawa mikono yake qabla wakubwa hawajanawa. na kama katika nyumba hapana mtu wa kuandikia, mtoto

---

1) Pflicht. — 2) Stolz. — 3) Schande. — 4) z. B. — 5) Geheimnis.

hushika birika[1]), akanawya watu. ijapokuwa wamekwenda katika ugeni, waliopo wote wakubwa, yeye ataandikia.

na iwapo wanakula, si adabu killa marra kutwaa nyama, illa wampe rukhṣa — kula nyama. na iwapo anakula, killa tonge[2]) ya chakula hutwaa chinyango[3]) ya nyama, watu wote humtezama, khalafu husema: „kijana huyu hana adabu, siku nyingine usimchukue katika háḍara, anatia feḍeha.“[4])

aiḍa na akala, si desturi mbele za watu kula chakula akatafuna kama mbwa, hukatazwa sana na wazee wake.

iwapo mtoto adabu, alizofundishwa na wazee wake, hakuzishika, amefanyiza neno katika mtaa, máthali ametukana mtu, ao amemwambia mtu mkubwa „wewe mwongo,“ yule aliyemtukana atakwenda kwa wazee wake, akawatukane, wakimwona killa siku mtundu — hufanya mashauri ya kumpeleka kumbini[5]), ma'ana huko endako kumbini hufundishwa sana adabu na makungwi[6]) zao.

kulla mtoto lâzima kusikiliza amri za watu watatu, iwapo anataka raḍi[7]) ya muungu: auwali[8]) amri ya mfalme, na ya pili ya wazee wake wawili, na ya tatu ya mw'allimu wake. amri hizo tatu lâzima azisikilize sana. na kama akaziżarau[9]) amri hizo, amekhálifu[10]) amri ya muungu.

khabari ya miayo[11]).

mtoto akenda miayo, killa marra huulizwa „una njaa ao umechoka?“ naye hukatazwa kufunua mdomo

1) Wassergefäß. — 2) Bissen. — 3) Stückchen. — 4) Schande. — 5) ins Versteck d. i. zur Beschneidung. — 6) Lehrmeister. — 7) Zufriedenheit. — 8) zuerst. — 9) mißachten. — 10) sich auflehnen. — 11) Gähnen.

zama za kwenda miayo. na akiwa mtoto hana fahamu[1]), akenda miayo, mama yake humfumba kinywa, sababu huchelea inzi kumwingia kinywani. na akiwa na fahamu, ni ʿaîbu[2]), humwambia: „ukiwa mbele za watu, ukenda miayo — kinywa kifumbe, usiwache wazi kama kinywa cha mamba.“ sababu mamba, akiwa na njaa, hukaa juu ya fungu ya mto, akacha kinywa wazi, inzi wakaingia ndani ya kinywa, kesha hufumba kinywa chake. ndio sababu humwambia: „nawe usiwe kama mamba.“

khabari ya kwenda chafya[3]).

kaẓâlika mtoto hufundishwa, akenda chafya baba yake ao mama yake, kumwambia kusema „shikamô.“[4]) na mzee wake huitikia „marḥaba.“[5]) ao husema „mwinyi,“ na mzee wake hujibu „mwinyi wangu sáyyidi.“[6]) na akiwa mtoto mwanamke, hujibu „mwana wangu sáyyidi.“

na ikiwa mtoto amekwenda chafya mbele ya wazee wake, humwambia:

kua, uwe tindi[1]),
utindi male[2]),
ukalie kiti
cha mkungo[3]), ulingane
na ulanga[4]).

1) uwe mrefu kama ncha ya mti. — 2) utindi uishe, maʿana ʿomri wako uwe mkubwa. — 3) kiti cha mkungo (eine Art Ebenholz) haben meist nur die pazi. — 4) = mbingu d. h. ulingane mulki wote uwe wako.

kisha humwambia: „shukuru[7]), sema al-ḥamdu lillâhi.“[8])

1) Verstand. — 2) Schande. — 3) Niesen. — 4) nashika miguu yako. — 5) willkommen, danke. — 6) mein Herr. — 7) danken. — 8) Lob sei Gott.

khabari ya mbweo [1]).

mtoto akenda mbweo, wengine huwakataza, husema: „usizoee mno kwenda mbweo.“ wengine hawawakatazi mbweo — illa chafya mbele ya chakula humwambia „unakwenda chafya kama mbuzi aliyefungwa juu ya kigwingwi?“ [2])

na kwenda mbweo, kwetu si ʿaîbu, ni kama kumwonyesha yule aliyo mkirimu [3]), ya kwamba chakula chake kizuri, naye ameshiba.

desturi za adabu za watu wazima.

mtu anapokwenda katika nyumba ya mwenziwe, atapiga „hodi.“ nao waliwo ndani, wataitikia „hodi,“ tenna watamwambia „qaribu.“ naye atakaa barazani, khalafu atatoka nje mwanamume yule mwenyi nyumba, atamwambia mkewe: „binti mwenyi lete jelba.“ [4]) akiwa mtafuni [5]), watatafuna tambuu [6]), na kuulizana hali [7]): „kina [8]) mwana hawajambo na kina mwinyi wote?“ atajibu: „hawajambo, watoto wanakushikamô, wakubwa wanakusallimu.“ [9]) iwapo mgeni wa kuzungumza, marra moja atakwenda zake, akiwa wa kulala, atahimiziwa [10]) chakula na paḥali pa kulala.

adabu ya pili — mtu akenda katika nyumba ya rafiqi yake ao ndugu yake, atapiga hodi, na wasipoitikia, husimama mudda [11]) kidogo, hapana mtu aliyemjibu, atakwenda zake.

kaẓâlika akaingia ndani ya nyumba, kama hakubisha hodi, ao kubisha hodi, marra akaingia ndani — si adabu. illa ukibisha hodi, usimame mlangoni kusi-

---

1) Rülpsen. — 2) Pfahl. — 3) Gastgeber. — 4) Beteldose. — 5) Betelkauer. — 6) Betel. — 7) Zustand. — 8) Geschlecht, Familie. — 9) grüßen. — 10) beeilen. — 11) Zeitraum.

kiliza majibu, sababu watu, wakiwa ndani, wana mambo mengi, hutokea nguo hawakuvaa vema, ndio ma'ana ya kusikiliza majibu ya hodi.

na wanapomjibu watamwambia „qaribu, pita ndani.“ waqati wa kungia ndani, akiwakuta wamekaa mtu na mkewe ukumbini — haiḍuru[1]), mtakaa pamoja mzungumze. na kama umewakuta wako chumbani wanaongea, nawe umepita ukumbini, umeona wako chumbani, si adabu kabisa kuingia chumbani.

ao umekwenda katika nyumba ya rafiqi yako. umepiga hodi, umemkuta mwanamke pekeyake, na mume hayuko. usikae ukaweka maongezi, rafiqi yako akija ataqaṣirika. illa iwapo yule mwanamke amepata rukhṣa „fulani akija mwache aningoje.“ ao iwapo umefuatana na rafiqi yako, msiwe mmekwenda pamoja, ukapata panapo nyumba ya mama yako ao yako, ukangia ndani, rafiqi ukamwacha nje pekeyake, si adabu.

adabu nyingine — nyumba ya jirani[2]) yako, naye ana mke, na mkewe ḥasherati[3]) — usiwe na ḥaja[4]) kwenda nyumbani kule. wakikupata khabari watu, ya kama unakwenda nyumba kwa fulani, husema anazini na mke wa jirani yako — si adabu.

iwapo umekwenda kwa rafiqi yako kumtezama, naye hukumkuta, illa yuko mkewe pekeyake, mwanamke si adabu kukuqaribisha[5]) ndani, wala wewe si adabu kuingia ndani. uende zako ao umngojee barazani, ḥatta aje rafiqi yako.

ao amekuta katika nyumba kijana mwana mwari, na watu wote wametoka, akipiga hodi, mwana mwari kuja mlangoni, yule mtu atauliza „baba yako yuko“ — atajibu kwa makofi[6]), hasemi naye kwa maneno.

---

1) schaden. — 2) Nachbar. — 3) Herumtreiberin. — 4) Wunsch. — 5) näher treten heißen. — 6) ~~in die Hände klatschen~~

akisema, mtoto mwana mwari humsema — hana adabu, mama yake atamtukana sana.

desturi ya Wasuaḥeli — ukawaona wamekaa paḥali watu watatu ao wanne, wanafanyiza mashauri yao, nawe ikawa unapita, hawakukwita — afaḍali uende zako, usikae kusikiliza maneno yao. na kama utasikiliza, watakuuliza: „unataka nini hapa?“ ao watasema: „nani aliyokwita katika maneno haya?“ watakufukuza, watakwambia „huna adabu.“ na kama wana mstaḥi, hawawezi kukufukuza — wataondoka wao, watafute paḥali pengine wakae.

adabu ya Wasuaḥeli — mwanamume akenda kwa rafiqi yake wakaletewa chakula, nacho kimefunikwa nakawa[1]), yule rafiqi mgeni si adabu kufunua, ajapompa rukhṣa ya kufunua,, lakini hafunui.

kaẓalika wakiletewa jelba, ndani mna tambuu, mgeni hafunui. killa kitu kilichofunikwa, mgeni si adabu kukifunua. afunuaye ni yule mume mwenyi nyumba yake, afanyapo hivi mgeni, kwa desturi ya kisuaḥeli — hana adabu.

kaẓalika waanawake hawafunuliani vyungu ao kitu kingine kilichofunikwa. mwanamke kama amekwenda kwa shoga yake, akaona chungu kimefunikwa, naye akakifunua — utakuwa ugomvi. maʿana humwambia: „wewe msungo[2]), kungwi[3]) lako hakukufunza mizungu[4]) miomboni[5]). na maʿana ya kuqaṣirika ni kama aliyemfunua nguo kumwacha uchi. ndio maʿana Wasuaḥeli hawafunuliani vitu.

Wasuaḥeli hawawachi kuambana, kama walivosema wahenga[6]) wetu:

---

1) tadellos, ordentlich. — 2) die nichts versteht. — 3) Lehrmeisterin. — 4) Verstand. — 5) unter dem mwombo-Baum. — 6) Vorfahren.

„watu — nyamba[1])
wasiposema[2]) — huamba.“ [3])

máthali ni kama mtu kupata feḍḍa, akasema „mwaka huu nimepata bi'ashara“ — watu humteta, husema „fulani akipata kitu kidogo, hujitangisha[4]) mji mzima.“ ao kama hana kitu, akasema „mwaka huu ni katika shidda[5]) na mashakka“ [6]) — watu humsema vilevile, husema „fulani ana moyo wa kibua, akikosa — huenda akajifeḍeḥi[7]) killa paḥali.“ na hiyo si adabu, mtu kujishitakia ḥali[8]) yake mbele za watu.

desturi nyingine za adabu: mtu akafanyiza chakula kumwita rafiqi yake, bassi mkewe iwapo siku moja amepika chakula kimetokea kibichi, ao nyama mbichi, yule mwanamke humwambia mumewe: „bana, leo chakula si kizuri, tafaḍḍali usimwite rafiqi yako.“ mume hujibu: „haiḍuru, wewe hukuquṣudia[9]) kupika kibichi. iwapo amekuja yule rafiqi, watakula, atamwuliza: „kimekupendeza chakula hiki?“ atajibu: „kizuri,“ ijapokuwa hakikumpendeza, sababu si adabu.

na akiondoka kwenda katika barza za watu, si adabu kusema — ya kama: nimekwitwa na fulani, nimekula chakula — chumvi nyingi, ao nyama mbichi.“ watu wakijua, fulani ndio ṭabi'a[10]) yake, anakashifu[11]) majumba ya watu, wakiwa na karamu, hawamwambii, wala marafiqi zake hawamwiti. kaẓâlika na akiposa mke, hupata, lakini kwa shidda[12]), illa apate mtu ma'arufu[13]) wa kumsemea uposa wake.

kaẓâlika rafiqi akiwa mgeni, mke wa rafiqi yake

---

1) nyamba vom Verb amba = mtesi oder mwambaji Schwätzer. — 2) sema offen reden. — 3) amba heimlich reden. — 4) sich breitmachen. — 5) Elend. — 6) Zweifel. — 7) sich beklagen. — 8) sich über seinen Zustand beklagen. — 9) beabsichtigen. — 10) Charakter. — 11) schlecht machen. — 12) selten. — 13) angesehen.

marra moja hamwoni, illa atamwonyesha mama yake na ndugu yake mwanamke, lakini akiwa kijana hamwonyeshi. wala nao hawaji, wakijua, ndugu yao anazungumza na mtu mgeni. humsema: „kijana fulani uso umemkauka.“

kaẓâlika urafiqi wa kisuaḥeli ajapo rafiqi kumtezama rafiqi yake, akikaa mwezi, khasara[1]) humlâzimu yule rafiqi mwenyeji. na siku ya kuondoka akimpa kitu — hapokei. illa iwapo ameondoka amefika katika mji wake, amletee zawadi[2]).

na rafiqi yake wakikopana, hawawiani, illa mwenyewe rafiqi hufanyiza náẓari[3]) — imenilâzimu kulipa. lakini mambo hayo hufanya wale waliwo wema, watu wabaya huleta daʿawa[4]) na kutukanana, na urafiqi uishe. na akikopa kwa mtu, asiyekuwa rafiqi, hulipa kwa taʿabu[5]), wazito wa kulipa, husema:

„kukopa hʿarusi
kulipa matanga.“

magomvi ya mtoto na wazee wake na mapatano yao.

mtoto akikosana na wazee wake, akikaa sikụ nyingi billa ya kusema nao, mji mzima humsema „kijana fulani hana adabu.“ iwapo maneno mengi katika mji, hutuma mtu humwambia: „tafaḍḍali, nataka ukaseme na wazee wangu, wawe raḍi.“ yule mtu atakwenda, aweleze khabari kama iliyotoka kwa mtoto wao. wakikataa, mshenga[6]) huwabembeleza: „msifanye machungu mengi, mtoto mbaya huwa naye, na mwema ukawa naye.“ tenna husema: „kiganja, alichonyia mwana, huoshwa — hakikatwi.“

bassi wakiwa raḍi wale wazee, mshenga atarudi

1) Schaden. — 2) Geschenk. — 3) Gelübde. — 4) Klage. — 5) Mühe. — 6) Bote.

kwa yule mtoto, atamwambia: „wazee wako wamekuwa raḍi, lakini kaa kwa adabu, usifanyize ujuvi. na sasa chukua changukia miguu tukawape.“ atachukua kitambi na kanzu ao kitu kingine. vitu hivo jina lake „takarraḍi,“ [1]) ao „changukia miguu,“ sababu desturi ya Wasuaḥeli, mtoto akigomba na wazee wake ao mkwewe, akipatana nao, hutoa kitu kuwapa.

turejee kwa yule mshenga. akisha chukua vitu hivo, atapeleka kwa wale wazee, atasema: „nimemleta mwanenu, mambo aliyoyatenda ataka mumsámeḥe [2]), ma'ana „vikombe vikawa pamoja — haviwachi kugongana.“ tenna yule mshenga atasema: „mwamkie baba yako, umpe na mkono.“ atamwamkia, babiye mtu atatikia, kisha amwombee muungu mwanawe: „yaliyopita — yamepita, yaliyosalia — kitumbe cha mongo.“ [3]) hayo ndio magomvi ya Wasuaḥeli na mapatano yao.

---

1) Zufriedenstellung. — 2) verzeihen. — 3) nyuma ya mgongo.

khabari ya kuamkiana kwa Wasuaheli.

zamani watu wakikutana aṣ-ṣubuḥi huamkiana. iwapo kijana amekutana na jumbe ao mtu mkubwa kuliko yeye — humwambia „chelewa," maʿana „umeamka vizuri kitandani?" naye huitikia „âye," maʿana yake „aḥsante" ao „vizuri." tenna humwambia „mwinyi," [1]) huitikia „mwinyi wangu sayyid." [2])

naye mwenyi kuamkia akimwamkia jumbe, husema maneno yaleyale, na kofia na vyatu huvua, akimkuta nje ao ndani. na iwapo waziri ao shaha [3]) ao mwinyi mkuu iwapo anamwamkia jumbe — vilevile kofia huvua. lakini mtu akimwamkia waziri ao shaha — havui kofia, iwapo ni mungwana, mtumwa huvua.

na vijana kuamkiana kwao ni namna moja, illa kofia hawavuliani.

na watu hao iwapo wanajuana, huulizana khabari za nyumbani. na kuulizana kwao: „mmelalaje nyumbani?" hujibu: „hatujambo al-ḥamdu lillâh." [4]) „kina [5]) mwana [6]) hawajambo na watoto?" hujibu: „hawajambo, illa mpwao ao mjukuúo mwanamke jana hakulala, alikuwa na ḥoma, lâkin leo hajambo." hujibu: „muungu amwondolee jambo." naye husema: „nanyi mu ḥali gani

1) eigentl. Besitzer, dann Herr. — 2) Herr. — 3) Nach dem jumben kommt dem Range nach als nächster der shaha, dann waziri, dann mwinyi mkuu. — 4) Lob sei Gott. — 5) Geschlecht, Familie. — 6) unter mwana wird häufig wie hier die Frau des Hauses gemeint.

nyumbani? kina mwana wote hawajambo?“ hujibu: „hawajambo.“ „ukenda nyumbani, nishikíemô [1]) kina mwana wakubwa, na watoto nisallimie.“ naye hujibu: „nawe nisallimie watoto wako, na kina mwana nishikíemô, na mwanao nishikie shikio.“ maʿana akifika nyumbani, humshika shikio yule mtoto, humwambia: „mjomba wako fulani akushika shikio.“

na iwapo mwanamke mzee ameona watu wamekaa barazani, naye anapita njiani, ao anataka kuingia ndani katika ile nyumba, waliyokaa watu — huvua ushungi, akawamkia watu barazani, naye husema: „mchewa kina mwinyi,“ maʿana „mmeamka vizuri kitandani?“ hujibu: „âye, tuchewa mwana, mwinyi mwana mwinyi mwana.“ huitikia: „mwinyi wangu sayyid, mwinyi wangu sayyid.“ ao humwamkia: „shikamô mwana.“ huitikia: „marḥaba [2]), marḥaba kina mwinyi.“

na akiingia ndani, husema: „kwetu?“ huitikia waanawake: „tuwamo.“ ao husema vilevile: „mwinyi mwinyi“ — waanawake huitikia: „tuwamo.“

na zamani mtu, akipiga „hodi“ katika nyumba ya kimrima, humkataza, humwambia: „si desturi ya kimrima „hodi,“ nyumba za „hodi“ ni nyumba za Waʿarabu.“

na mtoto kumwamkia baba ao mama ao mtu mzee aṣ-ṣubuḥi, humwambia: „kuchewa“ ao „chelewa?“ hujibu: „nichewa.“ humwuliza: „hujambo?“ naye hujibu: „sijambo.“ kisha humwamkia baba yake „shikamô,“ naye huitikia „marḥaba.“ ao humwambia „mwinyi,“ huitikia „mwinyi wangu sayyid.“ na kuamkiana kwa watoto sasa vilevile kama zamani.

na mtoto akimwamkia baba yake ao mama yake, iwapo mchana, humwambia: „za mtana?“ [3]) naye huitikia: „njema.“ tenna humwamkia.

---

1) nishikie miguu. — 2) willkommen, danke. — 3) khabari za mchana.

na iwapo jioni — humwambia „za jioni?“ [1]) hujibu „njema,“ tenna humwamkia.

na watu wazima vilevile kama wakikutana marra ya pili mchana ao jioni, husema: „za mtana?“ ao „za jioni?“

na mtoto, akitaka kulala, kwanza huenda kuwatwesha wazee wake, husema: „nakutwesha — shikamô.“ nao humwambia: „kalale unono, lala na nguvu zako, uamke na nguvu zako, lala uli [2]) simba, uamke uli ndovu.“

na watoto wadogo wakiamkiana, huwambiana zamani na sasa: „hujambo?“ „sijambo.“ tenna huulizana: „unakwenda wapi,“ ao „twende kucheza.“

na mtu akimwona mpenzi wake, humwambia: „hujambo?“ hujibu: „sijambo.“ „kama lulu?“ hujibu: „kama lulu.“

„kama marijani?“ [3]) hujibu: „kama marijani.“ „kama feḍḍaluku?“ [4]) hujibu: „kama feḍḍaluku.“ na kuamkiana huku kwa mpenzi wake ao kwa mtoto mdogo tu, maʿana ʿalama ya mapendano, lakini sasa shidda kuamkiana kama hivi.

kama mtu amekwenda mtazama rafiqi yake mgonjwa, humwuliza: „je rafiqi hujambo?“ hujibu: „sijambo.“ „umelalaje leo ugonjwa wako?“ humwambia: „ya leo si ya jana,“ maʿana magonjwa, niliyoyaona leo, siyo niliyoyaona jana. humwambia: „muungu atakondolea [5]) jambo.“ huitikia: „amîn.“ [6])

hio ndio desturi ya kuamkiana zamani katika mrima, na sasa wanaamkiana vilevile katika nyumba za watu wazima wazima, lakini kwa vijana wanapenda kuamkiana kwa kiʿarabu. kama mfano wa aṣ-ṣubuḥi wakikutana, huambiana: „ṣubal-khêri,“ [7]) na mwingine hujibu: „'llâh bi'l-khêri.“ [8]) „umelalaje?“ „sijambo al-

1) khabari za jioni. — 2) du bist. — 3) Korallen. — 4) rote Korallen. — 5) atakuondolea. — 6) Amen. — 7) ṣubḥ al-khêr Morgen des Guten. — 8) Allah mit dem Guten (gewähre Gutes).

ḥamdu lillâh.“ „nawe umelalaje?“ hujibu vilevile: „sijambo al-ḥamdu lillâh.“ na iwapo siku nyingi hawakuonana, humwuliza: „za [1]) siku nyingi?“ hujibu: „njema.“ „za siku nyingi nawe?“ hujibu vilevile: „njema.“

na wakikutana mchana na usiku, husema: „msa 'l-khêri,“ [2]) huitikia „'llâh bi'l-khêr.“

na watu wakikaa barazani, na mtu anapita njiani, huwambia wale waliwokaa kitako: „salâm ʿaleikum,“ nao huitikia „ʿaleikum salâm — qaribu.“ naye hujibu: „stareḥe,“ [3]) ao hujibu: „kaeni tafaḍḍalini katika makazi yenu,“ kama akija ao anakwenda zake.

khabari ya kuagana.

zamani baʿada ya kwisha kuzungumza, humtwesha humwambia: „nakutwesha.“ naye hujibu: „âye.“ tenna humwamkia „mwinyi“ akiwa mkubwa, akiwa ni kijana tu humwambia: „nakwenda nyumbani.“

illa sasa mno huagana „kwa ḥêri,“ naye hujibu: „kwa ḥêri ya kuonana.“ amma humzidishia maneno: „nenda ukaja, waliwokwenda wako wapi? nenda na njaa zako.“ hujibu: „âh, nimeshiba al-ḥamdu lillâh kule kuonana nawe.“

maamkiano ya makutano ya njiani.

mtu akisafiri, watu humwambia: „salâma uendako, urudi salimîni.“ naye hujibu: „amîna.“ ao huambiwa: „ndege njema, uenende ukale na vipofu.“ hujibu vilevile „amîna.“

na mtu akirudi katika safari, humwamkia: „pongezi“ ao „hongea,“ maʿana „umerudi salâma?“ naye hujibu „tumeuya,“ maʿana „nimerudi salâma.“

na iwapo mtu anapita, na watu wanafanya kazi,

1) khabari za. — 2) Abend des Guten. — 3) laß dich nicht stören.

kazi iliyoyote, huwambia: „kazi mafundi?“ huitikia: „auwali muungu,“ [1]) na khalafu huamkiana kama desturi.

na mtu akimkuta mwenziwe katika shamba kulima, humwambia: „fulani konde konde?“ naye mwenyi kulima huitikia: „ya kulima na mvua moja konde ndio mchawi.“

na mvuvi akirudi baḥarini, watu humwambia: „mavuvi?“ naye hujibu: „ya mshipi na samaki,“ ma'ana yake „mshipi umekamata samaki.“

na watu wengine katika mrima wakimwamkia mvuvi akirudi, humwambia: „fulani sayo?“ [2]) akitikia:

„zama gayogayo [3])
mvuvi huanga [4]) na payo.“ [5])

na mwinda akirudi porini, watu humwamkia: „nyama?“ naye hujibu „wa porini,“ tenna humwuliza khabari.

na watu wakipita njiani, akiona mtu anavuna, humwambia: „mavuno?“ naye hujibu: „ya mpunga“ ao „ya mtama.“

na mwanamke akitoka ndani ya uzazi, huja waanawake wenziwe kumhongeza [6]), nao humwambia: „hongea mwari,“ husema: „al-ḥamdu lillāh.“ tenna humwambia: „ndiwo ukubwa huo, umepata bibi ao babu? [7]) hujibu: „bibi.“

---

1) aliyeanza killa kazi d. h. er ist der größte Meister, der alles geschaffen, womit wir arbeiten. — 2) khabari ya baḥarini? — 3) ein länglicher Fisch, gewöhnlich gayogayo mchanga genannt. — 4) anga = hangaika. — 5) Unruhe. — 6) begrüßen, Glück wünschen. — 7) scherzweise für Mädchen oder Junge.

khabari ya kumtia mtoto kumbini [1]).

matengenezo.

wengine hupeleka watoto wao ᶜomri [2]) wa miaka mitano, wengine huwapeleka kwa ᶜomri wa miaka sabaᶜ, na wengine wakisha soma kwa ᶜomri wa miaka tisaᶜ.

na babaye mtoto, akitaka kumpeleka mtoto kumbini, hualika kwanza jamaᶜa [3]) zake usiku qabla ya kuṭahiriwa [4]) kucheza manyago [5]). na al-ᶜaṣiri [6]) wanakwenda baba na jamaᶜa zake maqaburini [7]) kufyagia [8]). na wakifika kule maqaburini, hufyagia yale maqaburi na kumwagia ṭibu na dalia. na huku wanasema: „tumekuja kwenu wazee wetu, mtoto wenu na mjukuu wenu tunampeleka kumbini leo, muungu amjaᶜalie [9]) salama. ninyi mmekufa, lakini vivuli vyenu vizima, asiugue huyu mtoto kumbini. na akipona, tutakuja wafyagilia tenna.“ bassi hufyagia lile qaburi, pakiwa na majani hun̄goa, pakiwa na taka huziondoa. nao huchukua ubani [10]) ndani ya chetezo [11]). wakesha fyagia, kile chetezo hukiweka chini ya kichwa cha qaburi. maᶜana kufukiza qaburi billa ya kutia ubani katika chetezo — haifai. na kulla marra mtu akitaka ku-

1) ins Versteck schicken d. i. Beschneidung. — 2) Alter. — 3) Verwandtschaft. — 4) ṭahiri beschneiden. — 5) Tanz. — 6) Nachmittag. — 7) zu den Gräbern. — 8) fegen, reinigen. — 9) bestimmen. — 10) Weihrauch. — 11) Räucherschale.

mwombea muungu, hutia ubani katika moto ndani ya chetezo.

na usiku huja jamaʿa zake tenna na watu wengine, hukusanyika kucheza manyago. na manyago ni jina la ngoma. na áṣili ya kwitwa manyago — waqati [1]) wa al-fajiri hufanyiza vituko [2]), mfano hufanyiza majani ao miti huyafungafunga, khalafu huingia mtu ndani akacheza. huwa labda kama ngamia, ao tembo, ao mbwa ao nyama mwingine, ndio sababu kwitwa vinyago [3]).

na desturi ya zamani hupikwa pombe, watu wakanywa usiku ule waqti wa kucheza manyago, sasa hutezama wale watu, walio wakubwa, tenna waliomkhuṣṣi [4]) yule mwenyi manyago, hufanyiziwa chakula. na huyu ngariba [5]) ao muwinzi [6]) huwapo katika manyago, hucheza pamoja na watu. huwalika wawinzi wenziwe katika manyago. huja nao wakacheza vilevile. na waʿana kualikwa wawinzi wenziwe ni ḥéshima [7]).

khabari ya kuṭahiriwa.

na al-fajiri manyago yakivunjika, ngariba huingia ndani ya banda, lililowekwa tangu usiku wale watoto, wanaotaka ṭahiriwa. maʿana wao hawana rukhṣa kutoka kwenda katika manyago. na hilo banda huitwa banda la „kumbi,“ maʿana banda la kujificha, nalo limejengwa ndani ya mwitu. hapana rukhṣa waanawake kwenda, ḥatta waanawaume, wasiwoṭahiriwa, hawendi.

tenna huingia ngariba, na wale wari [8]) wote huwa uchi. na ngariba huwa na kijembe, kinachokwitwa kirimbo. akifika, humwita mwari moja, jina lake huitwa

---

1) Zeit. — 2) Schreckgespenst. — 3) kinyago = sanamu Bild. — 4) nahesteben. — 5) Beschneider. — 6) Beschneider. — 7) Höflichkeit. — 8) mwari wird gewöhnlich das junge Mädchen genannt, das zum ersten Mal die Menstruation hat, aber auch die sich der Beschneidung unterziehenden Knaben werden wie hier so benannt. —

kiranja,[1]) naye ni mtumwa. naye kiranja huwekwa juu ya tego, maʿana kibao cha kukaa mtu moja tu. naye hushikwa na mtu. yule amshikaye huitwa jina lake shuwali. tenna huyu ngariba humpuna[2]) kidogo mboo[3]) yake, tenna humṭáhiri kwa kile kijembe. na wengine hushikwa ile mboo kwa mbano[4]) wa kijiti kidogo, khalafu humkata. wengine huvumilia[5]), wengine hawawezi kuvumilia, sababu inapokatwa ngozi ya ndani, mtu huona uchungu sana. na wengine wakimwona mwenzao analia, banda kama halikujengwa kwa nguvu, hulivunja akatoka akakimbia.

na yule ngariba iwapo wapo mangariba wenziwe, aliowaalika yeye, huwapa ḥéshima, killa mtu humpa wari wawili kuṭáhiri.

khabari ya dawa.

baʿada ya kwisha kukatwa, wale watoto hupikiwa uji, ao huletewa madafu kunywa, sababu wapate kujihongeza, maʿana yake wakojoe. tenna hutiwa dawa. na hiyo dawa ni unga wa mti, wengine husagiwa mkumbi[6]). wakapaka juu ya kile kidonda, hufunga na kitambaa. na wengine hawafanzi hivo, wao hutia kwanza kitambaa na mafuta[7]) ya kizungu, humwagia juu ya kile kitambaa. na desturi hiyo imekuja sasa záyidi kama ile ya zamani.

tenna killa aṣ-ṣubuḥi huja kungwi lake, ndio jina lake anayemwosha na kumtazama. naye hufungua kile kitambaa kilichofungwa siku ya kwanza, huosha kwa maji ya moto, ḥatta patakate pale palipokatwa. tenna hutiwa dawa marra ya pili, maʿana unga wa mti. hatiwi tenna mafuta ya ulaya illa siku ya kwanza.

---

1) Anfänger, von anza. — 2) hin- und herschieben. — 3) penis. — 4) Klammer. — 5) aushalten. — 6) Baum. — 7) Petroleum.

kisha hufungwa tenna kitambaa, hufanya desturi hiyo killa aṣ-ṣubuḥi mudda wa siku sitta.

siku ya sabaʿ huambiwa wazee wao: „siku sitta zimekwisha, kesho watoto wanakwenda mogo.“ [1]) na huo mogo, iwapo wamealikiwa mashamba ya mbali, hupelekwa katika mto wakoga. na iwapo mashamba ya qaribu, hupelekwa pwani koga. nao hutolewa alfajiri kupelekwa pwani. wanapokwenda huimbiwa mwimbo na kungwi lao:

„lawa [2]) lawa tugende“ [3])

nao huitikia vilevile:

„lawa lawa tugende.“

na kule pwani huenda, wakoga mwili wote, tenna hupakwa dawa nyingine, hurudi kumbini.

wazee wao wakijua, watoto wamerudi pwani, jioni husaga tui [4]) la nazi na pamba. hutia ndani ya tui, na lile tui hutiwa ndani ya kikombe, hupelekwa ḥatta kumbini. wale makungwi wakiwaona waanawake, huwapokea vile vikombe, huvipeleka kumbini, kama wanawopokea killa siku vyakula, wanavoleta wazee wao, kuwaletea watoto wao. na chakula kikija, kungwi, akipokea kuwapelekea wale wari, huimba:

„cha [5]) jumbé
chano cha jumbé.“ [6])

nao huitikia vilevile:

„cha jumbé
chano cha jumbé.“

bassi kungwi akisha peleka kile kikombe chenyi tui, huja shuwali na kungwi kuwapaka lile tui na kubandika pamba juu yake. na katika kazi ile huimba mwimbo:

---

1) von oga baden. — 2) herausgehen. — 3) twende laßt uns gehen. — 4) ölige Saft aus dem Fleisch der Kokosnuß. — 5) chano. — 6) kommt mit guten Speisen.

„nigemapo [1]) tembo [2])
moyo wanitetema
nigemapo tembo
moyo wanitetema."

1) gema zapfen. — 2) Palmwein.

wari huitikia vilevile:

„nigemapo tembo
moyo wanitetema."

ba'ada ya kwisha kupaka pamba na lile tui, huuguza wale wari madonda yao. na kulla aṣ-ṣubuḥi wakesha osha, hupakwa dawa, ma'ana gome [1]) la mti limesagwa, unga wake ndiwo wanaopakwa.

saba' ya pili [2]) hupelekwa tenna pwani koga. wanapokwenda pwani, hupakazwa mzimu [3]) katika nyuso zao. na huo mzimu udongo mweupe, watoka ndani ya inchi. na kupakwa kule ni 'alama [4]) kujulikana, ya kwamba' wale wanaokwenda pwani ni wari. na wakireje'a pwani hawapakwi tenna tui la nazi, sababu wengine wamepona, illa wasiwopona, hupakwa dawa zao zilezile za killa siku.

na kama mtoto moja mlalafi [5]), killa marra hujigonga akilala, kidonda chake hakiponi, hupikiwa mafuta ya kondoo yakawa moto. na hayo mafuta yanatoka ndani ya mkia wa kondoo. kupakwa kwake hupakwa kwa pamba, iliyofungwa juu ya kijiti. ba'ada ya haya hupona yule kijana. mno watoto hupona ba'ada ya saba' mbili, na wengine hupona kwa saba' ya tatu.

khabari zinazofundishwa wari kumbini na nyimbo zao.

na hao wari, wanapolala, kuamshwa kwao aṣ-subuḥi kungwi huwaimbia mwimbo:

1) Rinde. — 2) in der zweiten Woche. — 3) weißer Lehm. — 4) Zeichen. — 5) unruhiger Schläfer.

„kwére kwérekwéche [1])
kwére kwérekwéche
mramba kalia
kwére kwérekwéche.“

1) der mramba-Vogel zeigt durch seinen Gesang kwere kwere kweche = kule kule kumekucha den Sonnenaufgang an.

ao huimbiwa:
„wari ramka [1])
nyumba ya zimwi.“ [2])

1) amkeni. — 2) kumbi.

nao huitikia:
„wari ramka
nyumba ya zimwi.“

na kungwi na shuwali hukaa siku zote kumbini na wale wari, lakini huyu ngariba huja aṣ-ṣubuḥi marra moja kuwatezama madonda yao. na anapokuja, huwamkia watoto „wari mbukwa,“ [1]) nao hujibu „mbukwa ngariba.“ tenna wale wari huenenda uchi mbele ya ngariba kuwatezama madonda yao.

na wale watoto kule kumbini hufundishwa adabu [2]) na makungwi zao, mfano kuwatezama vema wazee wao, na kumchelea ḥakimu [3]), na kumcha mwᶜallim wao, na kuḥeshimu watu wapita njia, na kukaa na wake vema majumbani, na jamieᶜi [4]) ya adabu hufundishwa kule kumbini. na tenna hufundishwa nyimbo, na katika nyimbo hizo mna fumbo [5]). ukesha imbwa mwimbo, huulizwa mtoto maᶜana yake. asipojua hupigwa, tenna huambiwa maᶜana yake.

makungwi huimba:

1) wie geht's, guten Morgen. — 2) Anstand. — 3) Herrscher. — 4) all. — 5) versteckter Sinn.

1. „nende na mwamu [1])
shamba kulima.
shamba kulima?
namba [2]) tashinda.

2. shinde papano
tegé mgono [3])
tegé mgono
pugu [4]) kaingia [5]).

3) pugu kaingia,
nyama wa mwitu
nyama wa mwitu
nyoka kanduma [6]).

4. nyoka kanduma
sungu [7]) handika
sungu handika
henda hilia [8]).

5. henda hilia
kinjia njia,
nikuta na mke
masusi matombo [9]).

6. matombo mangne
msitu mkuu [10]) wa kisima manga [11]).
mali maliwa [12])
mali ya ngombe.“ [13])

---

1) Schwager. — 2) amba sprechen. — 3) Falle. — 4) Vogel. — 5) ich habe mich um ein hübsches Mädchen beworben, sie hat eingewilligt. — 6) ein anderer hat sie mir weggenommen. — 7) uchungu. — 8) nikaenda nikilia. — 9) maziwa yaliyojaa. — 10) kuma kubwa. — 11) wie ein arab. Brunnen. — 12) imeliwa. — 13) ich besitze nichts mehr, sonst würde ich der hübschen wieder nachgehen.

ao iwapo wanacheza kumbini, na kutukanana na kupigana, kungwi lao huimba mwimbo wa kuwataʿabisha:

„kwa mkono,
tuguye nyenzi [1])
kwa mkono.“

1) tukamate nyinzi.

tenna hukamata inzi kwa mkono na kwimba mwimbo huu.

ao iwapo wamecheka, na kungwi amewaona wamecheka, huimba mwimbo kungwi kwa kuqaṣirika, sababu husema „mnanicheka mimi?“ huimba:

„utete utete, chanda na pete,
chanda na pete, kinoo na wembe,
kinoo na wembe, ulimi na mate,
ulimi na mate, wanicheke wanicheke,
wanamba [1]) mlimo [2]) siumanyire.“ [3])

1) wanasema. — 2) Arbeit. — 3) manya nicht wissen.

ao kungwi huimba jua liwapo limekuchwa:

„shundi [1]) likalia zua liswa [2])
mwana ndege kalia kalegeza
shundi likalia zua liswa.“

1) Vogel, auch tipitipi oder dudumizi genannt, giebt durch seinen Gesang „tipitipi“ den Sonnenuntergang an. — 2) jua limekuchwa.

ao kungwi ao ngariba ao shuwali anataka kitu kwa mamaze wari huimba:

„hamna nyemi [1])
hamna nyemi?
mkanipa kido [2])
hemba [3]) nyimbo.“

1) Mitleid. — 2) kidogo. — 3) nikaimba.

ao huimba mwimbo:

„baba nipe mundu
hakate miaa
hakate miaa,
nisuke mabambo
nisuke mabambo,
nende mkumbi [1])
hauze kwarara [2])
nipone njaa ya masika.“

1) Hinterland von Mbueni. — 2) Früchte des Waldes, die zur Zeit der Hungersnot gegessen werden.

ao huimba:

„kantia kantia
ndani ya shimo [1])
nami simo [2])

1) gemeint ist kumbi. — 2) ich habe nicht hin gewollt.

ao huimba:

„kule lilawako [1]) jua
na kule lendako jua [2]),
balangulu [3]) kule lilawako
liswa [4]) lili jekundu.“

1) lawa = toka. — 2) von Sonnenaufgang bis Sonnenuntergang habe ich Hunger. — 3) Heuschrecken. — 4) Sonne.

ao huimba:

„baba nipe mshipi
havulie shemnungwi [1]),
shemnungwi nitende chambo
havulie kakaguu [2]),
kakaguu nilemea [3]) kulipaa [4])
nilipike na magamba.“ [5])

1) Fisch. — 2) Fisch. — 3) ich kann nicht. — 4) abschuppen. — 5) Der Sinn ist folgender: Vater gib mir Geld, damit ich mir eine suria kaufen kann. Wenn wir uns nicht vertragen, verkaufe ich sie, und heirate eine Frau. Vertragen auch wir uns nicht, so gebe ich der die Scheidung.

ao huimba:

„pweza [1]) mwana mataraza [2]),
akaapo hucharaza [3]),
kakaa chini ya jiwe
panapo mtanga [4]) na taza [5]).
mchokozi [6]) si mjinga,
mwerevu kamwegeleza.“ [7])

1) Fisch. — 2) mcheza. — 3) tanzen. — 4) mchanga. — 5) Muschel. — 6) Anfänger. — 7) dumm machen. — Sinn vergl. Uebersetzung.

ao huimba:

„ngara [1]) ngarumbwe [2]), ngarumbwe mnazi
ngarawa mbili, moja ifu [3]) maji
moja ikiri [4]), ipakie pamba
na mpilipili mlingote feḍḍa
nanga ya ẓahabu, pita mkunguni [5])
na kulolosa.“ [6])

1) ngalawa. — 2) Name des Bootes. — 3) imekufa. — 4) imefika. — 5) in den Hafen. — 6) kuotesha.

ao huimba:

„kisiki [1]) kimile [2]) pa [3]) mlango
nipe mundu [4]) sesengule.“ [5])

1) kisimi. — 2) alte Form für kimekaa. — 3) mbele ya. — 4) Sichel, hier mboo gemeint. — 5) sesengula = kata.

ao huimba:

msituni [1]) kuna mti
mashina manne pamoja,
tambi kumi na mbili,
tunda zake urembo urembo [2]).

1) mwituni. — 2) Sinn: Am Sternenhimmel sind 4 Sterne umgeben von 12 andern, die alle sehr leuchten. Das Sternbild kilimia gemeint.

ao huimba:
„kuanguka mti chini ya iwe [1])
tambi simile, sina lingoa [2])
mwenye kuuchimba, ndiye mwenyewe.“ [3])

1) jiwe. — 2) ngoa, lingoa Zweifel. — 3) Sinn: Ein König ist gestorben und begraben worden. Seine Kinder (die Aeste) sind zerstreut. Er der das Land geschaffen, war auch der Eigentümer.

ao huimba:
„naliona mataʿajjabu kuku [1]) kuvaa vyatu
kanyoosha shingo yake, ikapata żiraʿa tatu.
„unakwitwa Masikati kwa Rashidi [2]) mla watu.“

1) gemeint ist ein Sklave. — 2) der seine Sklaven sehr geschlagen haben soll.

na kama hao mamaze wari wakipika chakula kibichi, huimba mwimbo wale makungwi kumbini:
„mamiye mwari
kapika matebetebe [1])
kaleta,
anapopika — moyo
wamwaka moto.“ [2])

1) wässerige Speisen. — 2) brennt ihr das Herz wie Feuer (nämlich vor Verlangen spazieren zu gehen).

ngariba akija kuwatazama wari huimba:
„kidau [1]) changu cha mwale
kijile [2]) kikielea,
msukosuko [3]) wa wimbi
chegama [4]) pa ufuko,
nisikia mfu [5]) maji
nizile [6]) kuwalola.“ [7])

1) gemeint das kumbi. — 2) kimekuja. — 3) Schaukeln. — 4) kimcegama. — 5) kimekufa. — 6) nimekuja. — 7) kuwatazama.

na wari wakitaka kupumzika huimba:
„ngariba tu wanao
tuleke [1]) tutuletule.“ [2])

1) leka lassen. — 2) von tua niederlegen.

na wari wakiwa na njaa, na chakula kimekuja, hawajapata rukhṣa ya kukila, huimba:
„paku [1]), nya [2]) paku,
njoo utupakulie.“

1) Name des Kalfaktors im kumbi; von pakua auftragen. — 2) enyi besitzend.

wakesha kula, huulizwa na kungwi:
„kula mlile [1]) ndege,
mwenda wapi kunywa maji?“

1) mmekula.

nao hujibu:
„chura chalialia
mtanda [1]) hauna maji.“

1) Teich.

na wakitaka kushukuru, huimba:
„kula tulile [1])
ḥamdu, ḥamdu lillâh, ḥamdu.“

1) tumekula.

kurejeshwa kwa wari majumbani kwao.

ḥatta siku zinapokwisha kule kumbini, ngariba huwaletea khabari wazee wa wari — ya kama: „watoto wamekwisha pona.“ na wao wazee wao wamekuwa ṭayyari [1]) kuwanunulia mavazi watoto wao, sababu kulla mtoto, akitoka kumbini, hutoka na nguo mpya. na

1) bereit.

siku wanayolalia kutoka[1]) huchezwa manyago usiku kucha kama marra ya kwanza kule qaribu ya kumbini. ḥatta aṣ-ṣubuḥi hunyolewa wale watoto. na baba zao na ndugu zao wapo pale, lakini hawasemi nao. kunyolewa kwao hupigiwa siwa[2]) na zumari[3]), nao huwa wamekaa juu ya viti. wakesha nyolewa, hupelekwa vyooni kuoshwa. wakirudi, huvikwa mavazi mapya. na zile nguo kukuu, na mikeka, waliyolalia, hupewa makungwi, ndio ʿada[4]) yao. na wakesha vaa, hufungwa ukingo[5]), na wale watoto hutiwa ndani ya ukingo, wasionekane na watu. tenna hupelekwa mjini. na wanapopelekwa, huimbiwa mwimbo na ngariba:

„siwalile[1]) wana wenu
siwalile wana wenu
siwalile hâ wana wenu
siwalile.“

1) sikuwala.

na wata huitikia ule mwimbo, waanawake hupiga vigelegele[6]) na kumwaga mchele kuwafurahia watoto wao. wakifika majumbani, huwapa mikono mama zao na mashangazi zao, nao hutoa tunza kuwapa — tangu pesa kumi ḥatta pesa tano. na kama wasipowafichua mama zao, watoto hawana rukhṣa kusema nao, sababu makungwi wamewakataza, maʿana yale mapesa hugawana makungwi na ngariba na shuwali. tenna khalafu hufanziwa chakula cha watoto, ndio karamu yao. sababu iwapo ni watoto kumi — nyumba zote kumi hufanyizwa chakula, na nyumba zote kumi huzenda makungwi na wari wao wakala. mudda wa siku tatu

1) am Abend bevor sie das kumbi verlassen. — 2) großes Horn. — 3) Flöte. — 4) Geschenk. — 5) Art Baldachin, verhängtes Zelt. — 6) Freudengeschrei.

hutembezwa katika nyumba zile na nyumba nyingine za jamaʿa zao. nao popote katika zile nyumba hupewa mapesa kidogo kuwapa makungwi zao.

khabari ya vijana wa kisuaḥeli.

iwapo kijana mboo yake ndogo, huzungumza kwa mganga — ya kama: „mimi mboo yangu ndogo, vijana waanawake wananicheka.“ mganga hujibu: „nipe mchele wangu, nikufanyie dawa. itakuwa qiâsi [1]) utakacho.“ wakesha patana, hufuatana kwenda shamba kutafuta miegea [2]), ambao ndio kwanza unazaa. nayo miegea matunda yake marefu, nayo manene, wala hayaliwi. wakiupata, hukaa chini wote wawili. yule mganga hushika wembe kumchanja [3]), humwuliza: „unataka ukubwa upi, morta [4]) ao shubiri?“ [5]) husema: „nataka shubiri.“ atamchanja. kisha achanje na lile yegea [6]), atatwaa utomvu [7]) wa yegea, na damu ya mboo achanganye pamoja. kisha atamwambia: „litezame sana hili yegea, mudda wa siku sabaʿ uje ulikate hili yegea, sababu usipolikata — mboo yako utazidi kuwa ndefu mno.“ baʿada ya siku sabaʿ huenda akalikata.

---

1) Maß. — 2) Baum. — 3) ritzen. — 4) Spanne zwischen Daumen und Zeigefinger. — 5) Spanne zwischen Daumen und kleinem Finger. — 6) Frucht. — 7) Saft.

desturi za wari [1]).

khabari ya mtoto mwari kuvunja ungo.

mtoto wa miaka saba‘ mwanamke huitwa kigori [2]). ḥatta akipata miaka kumi na mitatu, watu husema, kigori fulani amekuwa mwari. na ma‘ana ya kwitwa mwari, ni kutokwa na damu [3]) marra ya kwanza. damu hiyo ikimtoka, yule kijana hulia, asiyoshe wala asipanguze pekeyake. wazee wake wakimwona ana damu yake, marra hupelekewa khabari kungwi [4]) lake, ya kama kigori leo amekuwa mwari. kungwi lake huja kule kwa wazee wake yule kijana. naye humbeba kumpeleka nyumbani kwake kwenda kumwalika [5]). na killa aṣ-ṣubuḥi humpeleka chooni kumwosha kwa maji ya baridi sana, na kumfundisha mambo ya ile damu, inapomtokea tenna

na ma‘ana ya kutokwa na ile damu wanasema „huu ndio uzima wa mwanamke,“ mwanamke asiyekuwa na damu — mgonjwa. na hiyo damu inawaanza watoto waanawake mwanzo wa miaka kumi na mitatu ḥatta kumi na minne. na ikikawia, hufanywa dawa yule mtoto. hubadiliwa miko [6]), ma‘ana kama zamani

1) mwari pl. wari wird jedes Mädchen von seiner ersten Menstruation gewöhnlich bis zu seiner Verheiratung genannt. — 2) bis zur ersten Menstruation. — 3) Blut. — 4) Lehrmeisterin. — 5) in Behandlung nehmen. — 6) es wird der Löffel gewechselt d. h. andere Diät vorschreiben.

amekatazwa asile kuku, huambiwa „sasa mwacheni ale kuku,“ tenna humpa miko mengine. kupikiwa na dawa ya mizizi na kuku mudda wa siku saba[ʿ] hupikwa, mchuzi akanywa. naye lâzima kuchukua mwana sesere[1]) wake killa endapo, akilala, akipika, akitwanga, akenda chooni — mwana sesere huwa mikononi mwake ao humbeba, ḥatta damu imtokee.

na yule kungwi mwari wake humpa kitambaa, jina lake kitambaa hicho sodo, kufunika ile damu inapokuja. nacho hufungwa juu ya utunda[2]). na mwanamke hamwonyeshi mtu kitambaa hicho, mama yake wala mumewe hamwonyeshi, illa kungwi lake pale anapokuwa kwa kungwi lake.

na tenna humpa jiwe la msio[3]). na maʿana ya msio ni vilevile kama msingo, maʿana kujisinga[4]). na hilo jiwe ni jiwe la tumbawe[5]), linalotoka pwani juu ya mwamba. huchongwa na fundi, ḥatta likawa leini[6]) na duwara[7]). waanawake hununua. themani[8]) yake rupia moja ao rupia u nuṣṣu. na katika kulla mji hutokea mtu, awezaye kuchonga mawe haya.

na matumizi ya jiwe hilo: kijana mwanamke akivunja ungo, hupewa na kungwi lake kusagia viungo[9]) kama ṭibu[10]), dalia, maua maulidi, na kulla manukato kujisinga yule mwari mwenyewe. na paḥali pa pili jiwe hili linatumika siku ya mtu kuolewa mwanamke. husagiwa viungo vilevile juu yake kama tulivotangulia kuyasema. na jiwe hilo likichukuliwa katika hʿarusi[11]), ao mwanamke amekwenda kwa shoga yake kuliazima[12]) — halichukuliwi wazi, hufunikwa nguo, watu wasilione.

---

1) Puppe. — 2) Perlschnur (weiß) um die Hüften auf dem bloßen Leib getragen, die nie abgelegt wird. — 3) Stein der Salbung. — 4) sich salben. — 5) Korallenfels. — 6) glatt. — 7) rund. — 8) Preis. — 9) Gewürze. — 10) Wohlgerüche. — 11) Hochzeit. — 12) leihen.

lakini iwapo limewekwa nyumbani ba'ada ya matumizi yake — halifunikwi, kulla mtu aweza kuliona.

na siku anazokuwa katika damu huvaa kaniki[1]), ma'ana yake kuficha ile damu, isionekane, inapomtoka kwa wingi. na tenna hana rukhṣa kusuka nywele zake, illa siku saba' kwisha. na desturi hiyo hushika vile-vile killa damu ikimjia.

naye huyo mwari haonekani na watu wengine, waliwo wageni, illa kungwi lake na jama'a[2]) zake. naye mwari hukaa kwa kungwi lake miezi sitta ao mwaka mzima. na wengine hukaa mwezi moja tu, khalafu hureje'a kwa wazee wake. na kule kwa kungwi lake hufundishwa kupika, na kusuka mikeka, na kukaa vema na watu kuwaḥeshimu[3]), na anapoolewa kukaa vema na mumewe.

khabari za wari katika kumbi lao.

ḥatta waqti ukesha wa kukaa kule kwa kungwi lake, huwambia wazee wake — ya kama: „huyu kijana twataka kumpeleka muyomboni.“[4]) na wazee wake hupika pombe na togwa. na huko muyomboni hukusanyika waanawake wengi, na wari wengine huja. marra nyingine huingia ndani ya nyumba yenyi nafasi[5]) kule shamba, marra nyingine hujenga banda. nao hao wari hupelekwa usiku, watu wasiwaone. tenna hubebwa na waanawake. ma'ana huyu kungwi ana wari wake, waliotangulia zamani, labda watu sitta — saba', huwaalika — ya kama: „kesho tunakwenda muyomboni, njooni mumchukue mwenzenu.“ nao lazima kabisa waje, sababu mwari hawachi amri ya kungwi lake. husikiliza sana amri ya kungwi lake kuliko ya mama yake.

---

1) dunkelblauer Baumwollstoff. — 2) Familie. — 3) ehren. — 4) unter den muyombo-Baum. — 5) Raum.

wakisha mpeleka yule mwari ḥatta kumbini, huchezewa ngoma jina lake unyago. na hapo panapo unyago, hupigwa ngoma, waanawake wengine wakatikitiza kuwaonyesha wale wari, na wao watikitize kama walivotikitiza wale wakubwa. na wasipojua huwafundisha. nao huimba:

„mkifichaficha vyuno vyenu,
njooni mwone changu mgeni.“ [1])

1) ich eure kungwi drehe meine Hüfte so, als ob sie nicht zu mir zu gehören scheint.

ao huimba:

„mwalilia kuti[1]) kuwa[2])
mwalilia.“[3])

1) kutikitiza. — 2) zugegen sein. — 3) Sinn: njooni sasa mtikitize.

ao huimba:

„kifidua[1]) — fidua mbele,
nyuma kwa wajinga.“

1) fidua = tikitiza.

ao huimba:

„kisaga cha msaga mea[1]),
nisage sembe[2]) unga
na wari wangu.“

1) Keim. — 2) = chembe Körnchen.

ao huimba:

„fagia uga[1]), mgeni aingie.“

1) der Hof d. h. kuma nach der Menstruation.

ao hutolewa mwimbo wa mzungu (Verstand):

„ngunguru[1]) katora[2])
katora
atorire[3]) na mromo.“[4])

1) das Begehrte. — 2) tora = twaa. — 3) ametwaa. — 4) = mdomo Mund, Lippe.

na huyu mwari huwekewa kitu nyuma ya mongo wake, akakitwaa kile kitu kwa mdomo kujiinamia nyuma. na huku anatikitiza, ikapigwa ngoma na kwimba mwimbo huo.

ao hutolewa mwimbo wa mzungu mwingine:

„sage sage,
nisagie mume,
gomberenga.“ [1])

1) Ort. Gemeint ist: der Mann, der noch in Gomberenga ist, den sie noch nicht besitzt.

ao huimba:

„kuki [1]) laṁbaṁba [2])
lanilemela.“ [3])

1) mkuki. — 2) layumbayumba schwankt hin und her. — 3) drückt zu schwer auf mich.

ao huimba:

„mwezi uzengwa [1]) mtala [2])
nalala [3]) si heza.“ [4])

1) umejengwa. — 2) auf allen Seiten. — 3) sagt der Mann. — 4) ich will keinen Beischlaf.

ao huimba:

„zoka [1]) kulu [2]) la mlali [3])
la pingapinga.“ [4])

1) nyoka. — 2) kubwa. — 3) ein Ort. — 4) sich hin und herdrehen.

na wakesha kwimba wale makungwi, naye mwari hawezi kutambua maʿana ya mwimbo, ao akiwekewa mzungu, hakuweza kuutwaa — hupigwa yule mwari, tenna huambiwa maʿana yake hivi. akijua ule mzungu, waanawake wote husema na ṣauti [1]) kubwa „cheréko

1) Stimme.

cheréko," ma'ana „kizazi kizazi kizazi changu kizuri." na wari wasipoweza mizungu kuitwaa — huimbiwa:

„kazongo hê leo
kazongo, kuna luhizo."

ma'ana yake: ta'abu[1]) leo ta'abu, kuna leo ta'abu. tenna huwapiga, wasiojua mzungu, na khalafu kuwaonyesha.

khabari ya wari kupelekwa muyomboni na kurudi kwao.

na siku ya saba' ba'ada ya kuingia kumbini na kwisha kucheza ngoma zao, hupelekwa wari wote muyomboni, na huo muyombo mti. hukaa wote makungwi na wari, wakapiga tenna ngoma na kucheza, na pakiwa na pombe hunywa pombe. nao hukaa mchana kutwa kwimba nyimbo, kama tulizotangulia kuzitaja. hatta jioni hunyolewa wale wari, wengine huchegwa sekini[2]) usoni. wakapakwa na wanja, na vichwani walivonyolewa hupakwa dalia. kisha huvikwa mavazi mapya, na kupambwa vyombo vya fedda. hatta jioni huletwa mjini, hawana nyimbo wanapoletwa. watoto wa kiungwana hufichuliwa nyumbani na jama'a zao, kulla kitu huwaletea nyumbani. wengine huwapa mkeka, wengine huwapa timbi[3]), wengine huwapa pete[4]), na wengine huwapa mapesa. na vijakazi hutembezwa katika mji. nao wamepambwa kama walivopambwa wari waungwana, hutembezwa na makungwi zao waanawake. wakiona mwanamume, wanayomjua, humpa mkono, naye hutoa mapesa kumpa fichuo[5]) lake. na wakiona mwanamke, wanayemjua, humwangukia miguu, ndio kuamkia kwake. naye hutoa kitu akawapa. nao hawana rukhsa ya ku-

1) Mühe. — 2) die Stirnhaare ausrasieren. — 3) Armband. — 4) Ring. — 5) Wiederentdeckung.

sema na watu, illa mtu aliyemfichua. hutembezwa mudda wa siku tatu. tenna yale mapambo huvuliwa, wakapewa mavazi ya killa siku kuvaa.

makosa[1]) ya kijana mwanamke.

kijana mwanamke kama hajaolewa, akapata mtu nje kumbikiri[2]), mji mzima humcheka. khassa[3]) akipata mimba[4]), humwambia watu: „ameuza bikira[5]) kwa uta-ma'ni[6]) mwingi.“ na akiwa na mimba humjua wazee wake kwa kutaka vitu hiki na hiki, hutaka sana ndimu na ndizi, ao mua, sukari, ao matunda yaliyo mazuri. wazee wake humjua marra, humwuliza: „kwa nini weye unataka hiki na hiki?“ hasemi. na katika nyumba pakiwa mtumwaname ao mwanamke — humchukia, na kifua chake maziwa humjaa, na kipanda uso huwa na nuru[7]), na neno la mwisho damu humwisha — wale wazee humvua nguo, wakamtazama, huona kitovu kimemtoka nje, hujua, ya kama huyu ameshika mimba.

watamwuliza: „nani aliyekufanya mambo haya?“ hawezi kuficha, atasema: „fulani amenibikiri.“ watatezama, wakiona mambo yanafa'a kutoka nje, watapeleka maneno kwa wazee wa yule mwanamume. wakipatana — ataoa, lakini, mtoto huyu akizaliwa, si mtoto wa ḥalâli[8]). lakini Wasuaḥeli wanasema: „ninaḥalalisha[9]) mimba.“

kaẓâlika akiwa aliyebikiri mtumwa, na 'aîbu[10]) yao hawataki waitoe nje, humpa dawa ya kuḥaribu[11]) mimba. hupewa baruti[12]), akanywa na maji pamoja, ao hupewa dawa za mwituni. mudda wa siku saba' kunywa, ḥatta mimba iḥaribike.

1) Fehltritt. — 2) entjungfern. — 3) besonders. — 4) Schwangerschaft. — 5) Jungfernschaft. — 6) Sehnsucht. — 7) Helligkeit d. h. helle Flecken. — 8) erlaubt. — 9) erlaubt machen. — 10) Schande. — 11) zerstören, dawa ya kuḥaribu Abtreibemittel. — 12) Pulver.

khabari ya ḥírizi[1]).

ḥírizi ya zamani.

zamani Wasuaḥeli hawakujua kusoma, wakitaka ḥírizi ya mtoto ao ya mkubwa, huenda kwa mganga, akawapa ḥírizi. naye mganga, iwapo anataka kufanya ḥírizi ya mtoto, huchimba mzizi mbali, na ḥírizi ya wakubwa mizizi mbali. ya mtoto — baʿada ya kuchimba mzizi, hukata vipande sabaʿ vya ule mzizi. kisha hutwaa tumba[2]). na hiyo tumba ni kibuyu kidogo cha muunye[3]). ndani yake mna mafutə ya nyonyo na asali ya nyuki. hutoa kipande cha qarṭâsi[4]), akapaka yale mafuta ya nyonyo, hutia na usira[5]). na usira ni ngozi ya nyoka aliyekufa, huichoma ḥatta ikaungua. makaa yake ndio usira. huchanganya pamoja na ile mizizi. tenna hutiwa kitambaa cheusi, akaishona. na juu ya kitambaa hushona kwa uzi mweupe, ḥatta kitambaa kisionekane. tenna huvikwa mtoto shingoni, maʿana yake asiugue marra kwa marra.

ao hufanyizwa kigwe[6]) cha mafundo sabaʿ, na

---

1) Amulett, das Suaheliwort ist kinga. — 2) kleine Kalabasse für allerlei dawa (Medizinmittel), Ricinusöl und Honig ist immer darin. — 3) muunye oder muñgunye Flaschenkürbis. — 4) Papier. — 5) zu Asche geröstete Schlangenhaut. — 6) Schnur mit Amulett darin.

katikati ya mafundo haya hutiwa vipande vya mizizi, kama tulivosema katika khabari ya ḥírizi.

kažâlika ḥírizi za wakubwa, mizizi yake namna mbali. sababu mtu, akenda kwa mganga, husema: „mimi nataka ḥírizi ya safari[1]), njiani simba asiniḍuru.“[2]) ao husema: „nataka ḥírizi ya biʿashara[3]), duka langu kutoka upesi.“ ao hutaka ḥírizi „waanawake wampende sana,“ ao „hutaka ḥírizi ya vita.“ mganga hujua mwenyewe namna ya mizizi ya kuchimba kwa ḥírizi aliyotaka. iwapo ḥírizi ya safari, asiḍurike na simba, hutwaa kitambaa cheusi na usira[4]) wa simba, maʿana uso wake simba huchomwa. mazizi yake hufanyizwa ḥírizi. nayo vilevile huchanganywa na mafuta ya nyonyo na asali ya nyuki, hupaka kitambaa, ndio kuandikwa kwake. na iwapo anataka ḥírizi ya neno jengine, hufanyizwa kama hivi, lakini miti ndio mbalimbali.

waganga wengine mno hushona kwa makucha ya simba ao ya chui, lakini ḥírizi hizo mno wanaziuza ghali, wengine hawawezi kuzinunua. na thamani yake tangu rupia moja ḥatta rupia tano. killa ḥírizi kwa thamani yake.

ḥírizi za sasa.

sasa wanatumia hírizi za „miti shamba“ na „za qorâni.“ watu wa mashamba wengine wanataka ḥírizi za qorâni, na watu wa mji wengine wanataka ḥírizi za miti shamba.

na hizo hírizi za qorâni, iwapo ḥírizi ya mtoto, akiwa mtoto wa siku sabaʿ, hufanyiziwa kigwe cha yâ sîni[5]). na hicho kigwe tamvua[6]) jeusi, hulisokota mwʿallimu.

---

1) Reise. — 2) schaden. — 3) Handel. — 4) zu Asche geröstete Stirnhaare eines Löwen. — 5) Sure 36. — 6) Schnur, Band.

kisha husoma yâ sîni, kulla yâ sîni kesha hupiga fundo, ḥatta mafundo saba' yeshe na yâ sîni saba' zimekwisha. hupewa mtoto kuvaa shingoni, ma'ana yake kumlea kile kigwe.

na akipata 'omri [1]) wa miezi sitta, hufanyiziwa ḥirizi ya jicho la watu. na ḥirizi yake huandikwa „yâ sîn," ao „qul huwa 'llâhu aḥadu," [2]) ao „qul a'ûżu bi-rabbi el-falaqi," [3]) ao „qul a'ûżu bi-rabbi en-nâsi," [4]) ao „âyat el-kursi." [5]) kisha hufukizwa kwa ubani [6]), ikashonwa kwa kitambaa cheusi ao cheupe, kuvikwa mtoto shingoni. ma'ana ya kwitwa ḥirizi ya jicho, watu ma'adui [7]) wakimtezama kwa jicho la uḥásidi [8]) — asiḍurike, ao asipatwe na magonjwa killa marra.

każalika ḥirizi za wakubwa huandikwa „yâ sîn," ao „tâhâ mâ anzelnâ," [9]) ao „sûra âla 'imrân." [10]) muradi [11]) hutazamwa yule mtu namna ya ḥirizi aliyotaka, ikiwa ya safari ao ya bi'ashara ao ya vita.

na katika ḥirizi kubwa sana huitwa „jauhari el-qorâni," [12]) ao „anthurûni," [13]) ao seifu 'llâhu el-qaṭe'i [14]). na jauhari el-qorâni na anthurûni na „seifu 'llâhi el-qaṭe'i" ni du'a za qorani. ma'ana ya kuwa ḥirizi hizi kubwa, watu wameziqubali, ya kwamba zina nguvu sana. mtu akichukua, moyo wake huingiwa na ṭama'a [15]) ya kuto' ḍurika [16]) na kitu, illa qudra [17]) ya muungu — haizuiliki. na ḥirizi hizi ni ghali sana. mwenyi mali, akitaka ḥirizi moja kama hii, lâzima atoe tangu rupia 'esherini ḥatta záyidi. na maskini za muungu hununua ḥirizi ya rupia moja ḥatta tano.

---

1) Alter. — 2) Sure 112, 1. — 3) Sure 113, 1. — 4) Sure 114, 1. — 5) Sure 2, 256. — 6) Weihrauch. — 7) Feinde. — 8) Feindschaft. — 9) Sure 20, 1. — 10) Sure 3. — 11) Wille. — 12) Juwel des Koraus. — 13) Schaut mich an. — 14) das Schwert Gottes das schneidige. — 15) Verlangen. — 16) verneinter Infinitiv. — 17) Wille.

na hizo ḥirizi tulizozitaja „jauhar el-qorâni,“ ao „anthurûni,“ ao „seifu 'llâhi el-qaṭe'i“ kuandikwa kwake zina sherṭi[1]) nyingi. yataka mtu awe ṭahara[2]) maungo yake, na waqti[3]) wa kuandika kwanza aṣali[4]) „raka'a-teini“[5]) kuomba muungu. na ikisha, hufukizwa ile ḥirizi na ubani[6]) na 'ûdi[7]) na uvumba[8]).

na mtu mathal[9]) akitaka kwenda safari ao vitani, inapokuwa amevaa ile ḥirizi, kwanza huifukiza kwa ubani na 'ûdi na uvumba, husema maneno kama atakayo. máthalan[9]) kama anakwenda katika bi'ashara, husema: „muungu anifungulie milango ya khêri[10]), nende marra, nirejee marra.“ ao anakwenda vitani husema: „mimi nnakwenda katika vita, nende salâma, nirudi salimîni, na ma'ádui zetu tuwashinde.“

na sherṭi zake kuivaa hiyo ḥirizi — mtu akenda chooni — huivua. na akilala na mwanamke — huivua. na iwapo mwanamke yumo katika damu — hana rukhṣa kuishika ḥirizi yo yote.

watu wengine hununua „kitabu cha ahl badrin,“[11]) hukitia kitambaa, akakishona, tenna huvaa shingoni, kitabu kikawa ubavuni. na namna ya ḥirizi hii watu huvaa zamani za safari ao panapo vita.

na ḥirizi iwapo mtoto amefungwa shingoni mwake, hufungwa sana, huchelea yule mtoto asiivue akaitupa, ao asije mtu mbaya kumvua, akenda kuiuza paḥali pengine, ao ampelekee mtoto wake. sababu wengine hawawezi kununua ḥirizi kuwapa watoto wao. na yule mtu aliyoiba, anaweza kuitumia ile ḥirizi, sababu nguvu za ile ḥirizi hazipotei.

---

1) Bedingung. — 2) religiös rein. — 3) Zeit. — 4) beten. — 5) Rumpfbeugen beim Gebet. — 6) Weihrauch. — 7) Aloe. — 8) wohlriechendes Harz. — 9) z. B. — 10) Glück. — 11) das Buch der Leute von Bedr.

na katika ḥíi izi nyingine mfano wa katika ḥírizi ya „yâ sîn“ huandikwa mwanzo wake ao mwisho wake waqfu[1]) kama hivi:



ma'ana yake:

„qul huwa 'llâhu aḥadu 'llâhu 's-ṣamadu lam yelid wa-lam yûlad wa-lam yakun lahu kufuwan aḥadu.“[2])

---

1) Figur. — 2) Sprich, er ist Gott, ein einziger; Gott ist der Ewige; nicht gebar er und nicht wurde er geboren und keiner war ihm gleich. Sure 112.

khabari ya kuoa.

khabari ya kuposa.

mtu akitaka kuoa, kwanza huposa, ndio maʿana mwenyi kuoa huitwa mposaji. na uposa wake hutuma mtu, jamaʿa wa yule mwanamke, kupeleka maneno kwa baba yake yule mchumba. naye mwenyi kupelekwa huitwa mshenga[1]) ao mjumbe. akisikia, atariḍi[2]) maneno yake, atasema: „nataka kiatu changu.“ atamwuliza: „qiasi gani kiatu chako?“ watapatana tangu riale ḥatta riale u nuṣṣu. na wengine hufanyiza kwa eḥsani[3]) tu. na wengine humpeleka mshenga kumsemea maneno babaye mchumba, na wengine huandika barua. wakisha patana mposaji na mshenga, hujibu mshenga: „nipe leso niandike barua.“ marra yule mchumba mume hutoa leso, na mshenga huandika barua — ya kama:

„mvele wangu fulani bin fulani — nakuʿarrifu[4]), amekuja mtoto wa fulani anataka binti[5]) wako kumwoa. na hayo ni mambo ya khêri[6]). na mtoto mwanamke biḍaʿa[7]) mbovu kama baruti na moto, ao kama pamba na moto, ao kama kitunguu. ṯafaḍḍali ukasoma barua — nataka majibu, nawe niwie raḍi[8]) sana.“

ikesha ile barua, bakhsha[9]) yake ile leso, maʿana ndio ḥéshima[10]) kubwa. na mshenga akapewa barua,

1) Bote. — 2) einwilligen. — 3) Güte, Gefälligkeit. — 4) mitteilen. — 5) Tochter. — 6) Gute. — 7) Ware. — 8) zufrieden. — 9) Kuvert. — 10) Achtung.

apeleke kunako uchumba. babiye mtu, akisha soma, ataweta jamaʿa zake, wake na waume, kuwapa shauri. wengine wataqubali[1]), wengine watakataa. wanaokataa — wanataka kitu kidogo wapewe na mchumba mume. yule mchumba mwanamume akisikia — ya kama „uposa wako una magomvi,“ atatoa kitu awape wale wenye ugomvi. watasema sasa „maneno yamekwisha, huyu ndiye mume.“

atajibu babiye mtu: „barua yako imefika fulani bin fulani kutaka binti wangu, tumeridi wote.“ naye mshenga atamwʿarrifu maneno, yaliyotoka kwa wakwewe. tenna yule mchumba killa tunu[2]) atanunua kumpelekea mchumbawe[3]) kama nguo nzuri ao matunda mema ya-nayowiva sasa, lakini hawaonani tangu siku ya kupeleka feḍḍa ḥatta siku ya kuoa, ikiwa mudda wa mwezi ao mwaka.

baʿada ya kurejeʿa mshenga na majibu, ya kama wamequbali, humtuma marra kuuliza: „qiasi gani kilemba[4]) chake,“ ao „vitu vyao qiasi gani?“ hurejeʿa tenna mshenga kuuliza: „qiasi gani kilemba chenu, na máhari[5]) yenu?“ babiye mtu hujibu: „kilemba changu ao vitu vyetu riale sabaʿini.“ maʿana wengine hutaka rupia settini, wengine themanini, wengine ḥatta mia. tenna husema: „na máhari yake mwanamke riale arbaʿini,“ sababu máhari ya mwanamke mungwana riale ʿesherini kama ameolewa marra ya kwanza, ameachwa, ao amefiwa, na reale arbaʿini mwanamke bikra.

akisha sikia maneno yale mshenga, hurudi kwake, akamwita mchumba, humpa khabari zile zinazotoka kwa wakweze[6]). naye akiqubali, na feḍḍa anazo — marra humḥasibia[7]) yule mshenga feḍḍa ya uposa

1) einwilligen. — 2) Kostbarkeit, Seltenheit. — 3) mchumba wake. — 4) Turban d. i. Ehrengeschenk. — 5) Heiratsgut, Morgengabe. — 6) wakwe zake oder wake. — 7) vorzählen.

kumpa kupeleka kwa mkwewe. na kama mkwewe amekufa, hupewa nduguye ao babu yake. na kama hawapo hao — hutazama watu waliomkhuṣṣi[1]) yule mwanamke katika nyumba yao, lakini aliye mwanamume. na kama hapana kabisa — hupewa mwenyewe mwanamke.

tureje'e kwa baba. akisha pewa feḍḍa, huweta jama'a zake wote kuwaonyesha feḍḍa. tenna hugawana. mama hupewa uweleko[2]) wake rupia kumi, na kondawi[3]) lake rupia tano. na iwapo yupo shangazi — hupewa kidogo, na akiwapo bibi — hupewa. na akiwapo babo mdogo — hupewa kidogo, kulla mtu wa jama'a hupewa kidogo kidogo, ma'ana ḥéshima. naye baba feḍḍa yote iliyobaqia huchukua yeye. nao feḍḍa hiyo hawaitumii, hununua vitu siku ya h'arusi kumletea mtoto wao.

na iwapo mwenyi kuposa hana feḍḍa yote ya kutoa, ametoa máthali[4]) rupia kumi tu katika rupia saba'ini, feḍḍa hiyo huambiwa „kifunga mlango“ ao „kifunga uchumba,“ sababu yule mchumba asiposwe na mtu mwingine. na kama ametoa nuṣṣu ya uposa — huambiwa „fulani ameposa, lakini ametoa feḍḍa nuṣṣu.“

na iwapo yametokea magomvi — mume hawamtaki, humrejeshea feḍḍa yake.

na ikisha toka feḍḍa ya uposa, maneno yamekwisha, ḥatta akitaja siku ya h'arusi „nataka kuoa,“ humwambia: „tumesikia maneno yako, lakini twataka máhari yake mwanamke.“ mume husema „sina máhari sasa hivi, khalafu ntampa, tupatane mudda, kama mudda wa mwaka ao záyidi.“ wao watasema: „tumequbali

1) nahestehen. — 2) Tuch, in welchem die kleinen Kinder auf dem Rücken getragen werden d. i. hier Ehrengeschenk. — 3) Binde der Wöchnerinnen um den Leib, gleichfalls hier Geschenk bedeutend. — 4) z. B.

mudda kama utakao, lakini tuandikie khaṭṭi[1]) tushike.“ naye mume ataandika katika hiyo khaṭṭi:

„mimi fulani bin fulani namwandikia fulani binti fulani, nna máhari yake riale settini kwa mudda wa mwaka kumpa ḥaqqi yake. nimeqirri[2]) kwa iqrari[3]) yangu. sháhidi[4]) fulani na wa pili fulani.“

ba'ada ya kwisha khabari hii, ba'ada ya siku chache mume hutaka mkewe, humwambia mshenga wake: „mwezi mwandamo nataka kuoa.“ mshenga hupeleka khabari kwa mkwewe. nao hujibu: „vema, sisi tu ṭayyari.“[5]) tenna babiye mke hu'arrifu kama watu waliomkhuṣṣi — ya kama: „siku fulani nna kikombe cha qahawa.“ neno hili lâzima juu ya babiye[6]) mke, na kama hawezi, kama maskini, hufanya mume, kama yeye mweza.

khabari ya kikombe cha qahawa[7]).

nayo haipikwi qahawa, ni jina tu, hufanyizwa maandazi[8]) na vyakula vingenevo. mume akaalika watu, walio rafiki zake, na watu wengineo, kwenda kwake. hula vile vyakula.

al-'aṣiri hupigwa ṭâri la njia[9]). vijana wote huvaa majambia na panga mikononi hucheza. na waanawake wamechukua maua na mashadda[10]), waliyonunua kwa mapesa yao. khaṣṣa hununua yasmini, wakazitunga ḥatta likawa shadda. tenna waanawake huwapa waanaume wanapocheza — husema:

„cheza bwana cheza.“

ao husema:

„ringa bwana ringa.“

---

1) Schuldschein. — 2) anerkennen. — 3) Anerkennung. — 4) Zeuge. — 5) bereit. — 6) baba yake. — 7) Kaffee. — 8) Kuchen. — 9) ngoma. — 10) Blumensträußchen.

na waanaume huimba kipokeo cha ṭâri:

„yâ rabbi ʿaunaka
lâ maula siwâ 'llâh.“ [1])

ao huimba:

„allâhu allâh rabbunâ
allâhu allâh ḥasbunâ
allâhu laṭîfun.“ [2])

nao hucheza polepole. wakiondoka al-ʿaṣiri — hufika nyumbani pa hʿarusi saʿa kumi na mbili, napo si mbali — mwendo wa robo ʿ saʿa. wakifika — waanawake hupiga kigelegele. moja husema:

„hiyo bwana, híyo bwana, hiyo bwána.“

na wengine huitikia:

„hiyōō bwana.“

wakifika nyumbani humwagiwa marashi [3]) wote waanawake na waanaume. hupewa tambuu [4]) kutafuna, na wengine wanavuta sigaretti. maʿana mshenga hupewa upatu [5]) wa tambuu, na hiyo tambuu imekwisha ungwa, maʿana ya kuungwa imetiwa popoo [6]) na tumbaku [7]) na chokaa [8]) na ʿiliki [9]) na mdalasini [10]) na mkungumanga [11]) — hufungwa pamoja, ikatiwa ndani ya upatu. mshenga huwapa watu walio barazani kutafuna.

tenna huambiwa watu „tafaḍḍalini siku fulani saʿa ya tatu tunataka mtutokee, maʿana ndio siku ya karamu, maʿana siku ya hʿarusi.“ na maneno haya anasema ndugu yake ao rafiqi yake mume wa hʿarusi.

ḥatta ile siku ikafika, huamrishwa kijumbe [12]) kupita majumbani kuwaʿarrifu watu hawa. na kuwaʿarrifu kwake huchukua ngoma yule kijumbe, inakwitwa mrun-

---

1) siehe Uebersetzung. — 2) siehe Uebersetzung. — 3) Rosenwasser. — 4) Betel. — 5) Tablett. — 6) Betelnuß. — 7) Tabak. — 8) Kalk. — 9) Kardamom. — 10) Zimt. — 11) Muskatnuß. — 12) Bote.

gura, huenda akapiga killa nyumba, tenna huwambia: „saʿa tatu mkutano hʿarusini.“

hawa watu walioalikwa kikombe cha qahawa, baʿada ya kucheza ṭâri la njia — hucheza usiku ṭâri la kudiriji [1]). nalo huchezwa kama ṭâri la njia, illa huchezewa paḥali pamoja. waanawake hukaa juu ya viti na waanaume hucheza. nao hucheza watu wawili kwa panga. na ratibu [2]) ndiye anayediriji [3]), hushika kitabu na ṭâri mkononi, akemba zile nyimbo, watu wakaitikia, na mkononi mwake ṭâri anapiga. na nyimbo zake namna moja na ṭâri la njia. mno huimba nyimbo za kiʿarabu, shidda kuimba nyimbo za kisuaḥeli katika ṭâri la njia ao ṭâri la kudiriji.

nao huimba [1]):

„mwana mamba [2]) alia mno,
mwana mamba alia mno,
nipeni mwanangu, nende hê,
nipeni mwanangu, nende hê,
kunako mayungi kule.“ [3])

1) Klage einer Mutter. — 2) ihr Kind. — 3) da wo es mayungi-Blumen gibt d. h. wo es Ruhe und Freude findet.

ao huimba:

„watoto jâha [1]), jâha hê
allâh watoto jâha, jâha hê.“

1) Freude.

ao huimba:

„usinitie wasiwasi [1]),
ibilisi [2]) nondokea!
ya rabbi mola mkwasi
apendalo mola bassi.“

1) Eine Freundin teilt einer Frau mit, daß ihr Mann zu einer andern geht, darauf gibt diese ihr obige Antwort. — 2) Teufel d. h. die Angeberin.

1) ngoma. — 2) Vorsänger. — 3) leiten.

ao huimba:

„rabbi nipo mlangoni, mja ḍa'ifu
nimile[1]) na babu[2]) mužinibu[3]) nimewaqifu[4])
kwa mikono, vidole nyanda kumi, zitile[5]) ṣafu[6]),
naomba kombo[7]) makomboyo[8]) kwa takhaffifu[9])
kwa baraka[10]) zako Aḥmadi[11]) mutaqaddamu.“[12])

1) alte Form für nimesimama. — 2) Tür. — 3) Sünder. — 4) stehen. — 5) altes Verb ita machen; zitile Perfekt-Form für zimeita = zimefanya. — 6) Reihe. — 7) Gabe d. h. Vergebung meiner Sünden. — 8) makombo yako. — 9) schnell. — 10) Sorgen. — 11) Muhammed. — 12) der vorausgegangen.

ao huimba:

„yâ khâliqa el-makhlûqi
jalla wa-'alâ fasubḥâna
'llâh rabbuna el-'aâlamîna.“[1])

ao huimba:

„yâ rabbi yâ 'llâh
hê yâ 'llâh hê yâ 'llâh
allâh yâ rabbi allâh
hê yâ 'llâh hê.“[2])

ao huimba:

aṣ-ṣalâtu wa's-salâmu
'ala shefi'ei
'alâ en-nabîyi
allâh allâh[3]).

1) siehe Uebersetzung. — 2) siehe Uebersetzung. — 3) siehe Uebersetzung.

na kama huyu mwenyi h'arusi ana kitu, huchezwa ṭâri hili siku nne ḥatta tano. kama hana kitu — siku moja tu, sababu gharama[1]) nyingi. aṣ-ṣubuḥi na jioni maandazi na vyakula na marashi na tambuu na siga-

1) Kosten.

retti, sababu hawaji watu kumi ao ʿesherini — huja watu thalatha mia ao záyidi.

khabari ya kutazamia[1]) nyumba.

siku za kuwa qaribu ya kuoa babiye mke humwambia mchumba mume kwenda kwa mwʿallimu kutazamia nyumba. naye huenda kwa mwʿallimu. mwʿallimu humwuliza: „jina lako nani, na mwanamke jina lake nani?“ kesha mwʿallim hutoa kibao, akayapima majina yao wote wawili mke na mume kwa ḥesabu[2]) kutezama nyumba kuwa njema. maʿana waʿallim wengine majina hayo huyapima kwa kitabu cha „abjed,“ na wengine hawana lâzima kitabu — hushika kibao, akaandika ḥesabu ya yale majina kwa ʿaqili yake. kwanza hutwaa kipande cha mpingo[3]) kimeandikwa „abjed“ kwa ḥarufu[4]) mbalimbali, maʿana alif mbali, na be mbali, na jim mbali, na dal mbali, kulla ḥarufu moja upande moja. hutupa kile kipande, na akiona ḥarufu juu ya kipande mnamo jina lake — hutazama katika „kitabu cha abjed“ chini ya ḥarufu, iliyosimama juu ya kipande, ataona ḥesabu ya ḥarufu ya jina lake. na kupatikana ḥesabu za ḥarufu nyingine za jina lake — hutupa vilevile kipande kile ḥatta jina lake lishe. na kama haoni marra ya kwanza, akitupa kipande, ḥarufu ya jina lake — hamna, hutazama katika kitabu chini ya ḥarufu ileile.

baʿada ya kujilikana ḥesabu zote za jina — hujumlisha. máthalan mwanamume jina lake Muḥammadi, mwanamke jina lake Faṭuma — mwʿallimu atafanya ḥesabu ya ḥarufu. jina la Muḥammadi „mim — nne, ḥe — tisaʿ, mim tenna — sabaʿ, dal — tano.

---

1) Prüfung des Hauses d. h. der Heirat. — 2) Zahl, Zahlenwert. — 3) Würfel aus Ebenholz. — 4) Buchstabe.

m	ḥ	m	d
4	9	7	5

imetokea jumla khamso wa ʿesherini. katika khamso ʿesherini zimeanguka thelitʿashara, baqi [1]) thenʿashara.

na jina la mwanamke Faṭuma: fe — sitta, ṭe — tatu, wau — moja, na mim — nane

f	ṭ	u	m
6	3	1	8

imetokea jumla themintʿashara, zimeanguka tisaʿ, baqi tisaʿ. hili jina la mwanamke liko chini, la mwanamme liko juu. huweza kumwoa mwanamke huyu, sababu nyota [2]) yao moja, mlango wao umetokea moja, na mapatano yao ni mamoja katika nyumba.

na ikatokea jina la mwanamke liko juu, na mwanamume chini — wengine hukataa kumwoa mwanamke huyu. ao wengine hubadili jina, maʿana huyu mwʿallim husema „tumḥasibu huyu mwanamke na jina jengine lenye mapatano nawe, máthalan kama jina la Faṭuma halikufaʿa — huitwa Mwana Ḥadija. likifaʿa jina hili — huenda zake yule mchumba.

naye humpa khabari babiye mke, kama iliyotoka kwa mwʿallim, ya kama jina hili halifai kumwolea. lakini huyu mtoto mwanamke haambiwi neno. na siku ya kuoa mbele ya mwʿallim huenda babiye mtu kwa mwʿallim na mashâhidi mawili na huyu mchumba mume. mwanamke hendi, huwa nyumbani. tenna babiye mtu hutoa amri kumpa mwʿallimu kumwoza mke, lakini huozwa kwa jina lile jipya. yule mtoto mwanamke hajui, kama amebadiliwa jina.

maʿana ya kutezamia majina, wasioane billa kutezamia, nyumba itokeapo mbaya — si nzuri kama maneno yaliyosemwa ndani ya shaʿiri [3]):

---

1) Rest. — 2) Stern des Glücks. — 3) Gedicht.

1. nanze [1]) jina la illâhi [2]),
auwali [3]) bismillâhi [4]),
peke [5]) asiye shabihi [6])
subhâna [7]) wa taʿâla [8]).
2. nanze ḥadithi [9]) katiti [10])
ina masemo baidi [11]),
penyi wino hatafiti [12])
na qarṭasi [13]) pamoja.
3. hafuta wino kuandika
nyote mpate pulika [14]),
nyoyo msitie shakka [15])
nimeṣafi [16]) tawambia.
4. kwani wametakallamu [17])
mashekhe [18]) na waʿallimu,
quṣudi [19]) myafahamu
mambo matatu sikia.
5. kwanza ni ufalume
una nguvu na tume [20])
na raʿia [21]) msikimwe
ifuateni sheriʿa [22]).
6. na la pili ni safari
yataka mtu baṣiri [23]),
atazame na qamari [24])
jumba aliyokukaa.
7. na la tatu ni zuaji [25]),
yataka mtu mbuji [26])

---

1) nianze. — 2) Name Gottes. — 3) zuerst. — 4) im Namen Gottes. — 5) pekeyake. — 6) Aehnlichkeit. — 7) Lobpreisung. — 8) Erhabene. — 9) Erzählung. — 10) klein. — 11) verschieden. — 12) des Reimes wegen für tafuta. — 13) Papier. — 14) hören. — 15) Zweifel. — 16) d. h. mein Herz ist rein. — 17) reden. — 18) Gelehrten. — 19) Absicht. — 20) Befehl. — 21) Untertan. — 22) Gesetz. — 23) Einsicht, Erkenntnis. — 24) Mond. — 25) Heirat. — 26) klug.

wa kupata faraji [1])
ḥatta ikatengenea.

8. na ṣifa [2]) zake zatoa
tazidi kupambanua,
kulla mtu atajua
ma'ana yatamwelea.

9. nyumba mlango wa kwanza,
roḥoni mwangu huwaza,
ina utesi [3]) na kiza,
hiyo si njema kuoa.

10. nyumba mlango wa pili
ya matanda [4]) na milele [5])
ndio beti [6]) el-mali
na watu kuyawandaa.

11. nyumba mlango wa tatu
hutunda [7]) hupata vitu,
illa mke hawi mtu
huwa baa akipoa [8]).

12. nyumba mlango wa nne
ndugu hawatangamani [9])
wazazi hawapatani,
hii si njema kuoa.

13. nyumba mlango wa tano
ya mke huzaa mno,
illa mmoja hapono [10])
hufa akatangulia.

14. nyumba mlango wa sitta
mume hendi [11]) vita,

---

1) Glück. — 2) Lob. — 3) Zank und Streit. — 4) Kleider. — 5) ewig. — 6) Haus. — 7) pflücken d. h. auf Verdienst ausgehen. — 8) wegnehmen. — 9) sich vertragen. — 10) haponi. — 11) haifai kwenda.

akenda — hurudi uta,
na maraḍi humwingia.

15. nyumba mlango wa saba[c]
wa makonde [1]) na maḥaba [2])
kulla kibaba kibaba [3])
kisua cha kuvutia.

16. nyumba mlango wa nane
ndiyo mbi [4]), usinene,
ya mke majongonene [5])
na mume kujipania [6]).

17. nyumba mlango wa kenda
wa kusafiri na kwenda,
kulla ambalo watenda
mola huwatukulia [7]).

18. nyumba mlango wa kumi
mke huwa na ulimi,
akauzwa [8]) haungami [9]),
husingizia [10]) wa [11]) mitaa.

19. mlango wa kumi na moja
ndiyo beti el-ḥaja [12]),
na kilicho mbali huja,
na mtima [13]) hutangaa [14]).

20. mlango wa kumi na mbili
mashakka [15]) nyote wawili
wazaa na tahalili [16])
na watu kuwazumia [17]).

---

1) Faust. — 2) Liebe. — 3) sie haben immer nur eine kibaba. — 4) schlecht. — 5) jongonene ist eigentlich eine grobgenähte Naht, d. h. die Frau hat geflickte Kleider. — 6) hochschürzen. — 7) chukulia. — 8) ulizwa. — 9) die Wahrheit sagen. — 10) verdächtigen. — 11) watu. — 12) Sehnsucht. — 13) Herz. — 14) sich freuen. — 15) Zweifel, Sorgen. — 16) Grabgesang. — 17) zumia = lia weinen; zumo = kelele.

khabari ya kupiga pamba.

siku nne ao tano ba'ada ya watu kunywa kikombe cha qahawa, hualikwa tenna waanawake na waanaume na mshenga kwenda kupiga pamba. wapigao pamba ni waanawake, na waanaume huwa barazani, hucheza bao [1]), karata [2]), ao mazungumzo mengine. na waanawake katika kazi yao ya kupiga pamba huimba nyimbo za h'arusi:

„nna usingizi [1]), wanienga [2]) mato [3]),
kanitandikie kitanda na mto,
tusowere nacho [5]) cha feruzi [6]) kito."

1) nämlich die Braut. — 2) enga = tazama; der mir in die Augen sieht d. h. der mir in die Augen sticht. — 3) macho. — 4) sowa = cheza. — 5) auf kito bezüglich. — 6) Kleinod.

ao huimba:

„kibarikinya [1]) cha moshi
kimekuja,
waanawake vaeni makoti,
tumwendee bana balozi [2]),
asimamishe mlingoti." [3])

1) Schiff, gemeint ist der Bräutigam. — 2) Konsul, d. h. hier der Bräutigam. Wir wollen uns so schmücken, daß er uns haben möchte. — 3) Mast d. i. penis.

ao huimba:

„sikununa [1]), najaribu pendo,
maneno matupu, wala si vitendo,
paŋgokapo jino, hapakosi pengo."

1) nuna sich ärgern.

na wakisha kupiga pamba yote, hupewa chakula ndizi kwa nyama na muhogo pamoja, na uji, khalafu huenda zao.

1) Brettspiel. — 2) Karten.

baʿada ya siku mbili ao tatu watu walewale huʿarrifiwa tenna na mshenga. naye huenda killa nyumba huwambia: „kina mwana na kina bwana mnakwitwa kwa babiye hʿarusi kushona godoro[1]) na mito.“ na hilo godoro hushona mafundi na mito vilevile, na watu husaʿidia[2]) kutia ile pamba katika mifuko. nao waanawake huimba nyimbo zao. wale mafundi hupewa ijara[3]) yao linapokwisha. tenna hupelekwa ndani, likatandikwa katika chumba cha hʿarusi mwanamke, na juu ya lile godoro hufunikwa nguo, tenna hupangwa mito, mito mitatu. ikisha watu huenda zao.

khabari ya matengenezo mengine kwa siku ya hʿarusi.

siku chache baʿada ya pamba kisha kupigwa na godoro na mito kushonwa, tenna mume anataka kuoa. watu walio mbali hupelekewa mshenga kuambiwa: „siku ya el-jumaʿa hʿarusi[4]) anaingia nyumbani.“ na waliwo qaribu hujua wenyewe, huja pekeyao katika hʿarusi.

na babiye mke atanunua mchele na unga wa ngano na samli, hufanyizia maandazi na vitumbua na kulla andazi la hʿarusi. anunue na mbuzi kitoweo cha karamu kulisha watu. hiyo jina lake „kombe la hʿarusi.“ na yale maandazi huliwa siku sabaʿ za fungate[5]), hula wale maʿarusi[6]) na watu wengine, wanaokuja waamkia maʿarusi.

na hʿarusi mno hufanyizwa katika nyumba ya wazee wa hʿarusi mwanamke, ḥatta siku sabaʿ zishe. na aṣ-ṣubuḥi ya hʿarusi hupambwa nyumba ya hʿarusi, huṣafidiwa kwa vikombe na viti na vyoo na kufukizwa kwa ʿûdi[7]) na chupa za mirashi[8]).

1) Matratze. — 2) helfen. — 3) Lohn. — 4) Bräutigam. — 5) sieben d. h. die sieben Tage nach der Hochzeit. — 6) Brautleute. — 7) Aloe. — 8) Rosenwasser.

khabari ya mwʿallimu anavooza.

siku ya mume anapotaka kuoa huenenda babiye mtu kwa mwʿallimu na mume na mashâhidi mawili, ao mashâhidi hupatikana katika barza aliyopo mwʿallim. akifika babiye mtu, humwambia mwʿallimu: „nimekupa amri, huyu mume umwoze mwanangu.“ tenna hukaa kitako wote. mwʿallimu huuliza: „máhari yake qiasi gani?“ husema kama walivopatana.

na katika ḥáḍara [1]) hiyo hununuliwa ḥalwa [2]) kula, waliopo katika ḥáḍara hiyo, baʿada kwisha kuoa.

na kuoza kwake mwʿallimu kwanza hupiga fâṭiḥa [3]), watu huitikia. tenna yule hʿarusi humqabili [4]) uso wake mwʿallimu, humpa mkono, na mwʿallim husoma khútuba [5]) ya nikaḥa [6]), kama aya zilizomo katika qorâni.

baʿada ya kwisha ile khútuba, mwʿallimu humwita yule hʿarusi kwa jina lake „ʿAbdallah,“ huitikia „labeka.“ „umequbali kumwoa Mwana ʿAsha binti Faqihi kwa máhari yake riale khamsini?“ naye hujibu: „naʿam, nimequbali.“ huitwa namna hii marra tatu. marra ya tatu huulizwa babiye mtu: „umemwoza ʿAbdallah binti wako kwa máhari yake riale khamsini?“ hujibu babiye mtu: „naʿam, nimemwoza.“ na mwʿallim husema: „na mimi nimekuoza.“ tenna mwʿallim hupiga fâṭiḥa, na watu huitikia, na kuwaombea muungu waliooana mke na mume. husema: „muungu awajaʿali [7]) unyumba wenu uwe wa khêri [8]), suʿudi [9]) na baraka [10]) na mapendano, mpate na kizazi kwa fáḍili [11]) zake muungu rabbi elʿaâlamîna.“ [12])

na ijara yake kuoza yule mwʿallim — yule hʿarusi hutoa rupia mbili kumpa mwʿallimu, iwapo mwanamke

---

1) Gesellschaft. — 2) süße Speise. — 3) erste Sure. — 4) nähern. — 5) Predigt. — 6) Ehe. — 7) bestimmen. — 8) Glück. — 9) Hülfe. — 10) Segen. — 11) Güte. — 12) Herr der Welten.

kijana. iwapo ameolewa chuo cha kwanza — ameachwa — ijara yake rupia. ba'ada ya kutoa zile rupia huenda zao.

khabari ya siku ya h'arusi.

mwanzo wa al-'aṣiri huja waanawake shoga zake na wengine wa h'arusi mwanamke kumṣafidi [1]). humpeleka chooni, wakamwosha na kuchanwa nywele, na kusingwa kwa ṭibu [2]) mwili wote, tenna hufukizwa, humsuka nywele na kumchega, ma'ana hukata zile nywele kidogo usoni, huitwa denge. akisha chegwa, hubadiliwa nguo nyingine kuvaa. tenna humtoja wanja [3]) machoni na uso kidogo. na huko wanakwimba waanawake:

„mwengeenge [4]) kama kioo [5]),
mume nduguyo,
mwengeenge kama kioo."

ao huimba:

„ukipamba mke, mume kujipamba ni sunna [1]),
usipojipamba, watu hukwambia mtumwa.
achimba ndago [2]), hè nana [3]).
achimba ndago kwa Silima?" [4])

1) arab. = vizuri. — 2) Unkraut. — 3) Einschiebsel — ohne Bedeutung des Reimes wegen, sog. kipokeo. — 4) männlicher Eigenname.

ao huimba:

„anatangatanga [1]) kwa killa kibanda kungia [2]),
ni kama nakhoża, aliyekosa baḥaria,
hilo ni juya [3]) hè nana
kwa killa samaki huingia."

1) umherlaufen. — 2) ein Mädchen will nicht heiraten, sondern treibt sich lieber in allen Hütten herum. — 3) Fischnetz.

1) putzen. — 2) Wohlgerüche. — 3) Antimonpulver. — 4) enga = tazama. — 5) kama unavotazama katika kioo.

baʿada ya uzuri huu kwisha mshuko wa ʿisha[1]) huletwa mwanamume nyumbani kwa mkewe na rafiqi zake kwa shangwe na furaḥa. wengine humpeleka mume kwa ṭâri ḥatta lifike nyumbani kwa hʿarusi. naye amejifanya uzuri mwenyewe kwa kanzu, na joḥo[2]), na kilemba, na vyatu, na jambia labda, na upanga, ao bakora mkononi.

ḥatta akifika nyumba ya hʿarusi, mume akitaka kuingia, waanawake humziwia mlangoni, hutaka kingia[3]) chao, humwambia: „tunataka kingia chetu.“ na mlango wameufunga waanawake. naye hutoa tangu rupia moja ḥatta rupia tano. ao yeye hutaka kuwadanganya hao waanawake, huwambia: „nipeni rukhṣa, nikamwone mke wangu, kisha ntawapa kingia chenu.“ waanawake hawaqubali.

akisha ingia ndani, wale makungwi humpa mkewe. naye humpa mkono, akamwamkia. na hapo ndipo wanapoonana marra ya kwanza. na mwanamke hasemi na mumewe, illa atoe kono[4]) na kipakasa[5]) na fichuo[6]). kono maʿana ni vile alivompa mkono, anataka ijara ya mkono wake kumshika mwanamke mpya. na kipakasa ni kule kupakatwa. na fichuo ni kule kusema naye, sababu zamani hakuona uso wake, wala ṣauti[7]) yake hakumsikia, ndio maʿana kutakwa ʿada[8]) hizi. na yule mume hutoa. máthalan kumpa pete kono lake, ao timbi kipakasa chake, na mkufu fichuo lake. ao humpa feḍḍa qádiri awezavyo — rupia tano kono lake, rupia tano kipakasa chake, na rupia tano fichuo lake. wengine hutoa záyidi, na wengine haba.

baʿada ya kwisha toa ʿada hizo, mume huenda ukumbini, na mkewe hukaa chumbani mwake. naye hʿarusi

1) Abendgebet. — 2) arabischer schwarzer Mantel. — 3) Eintritt. — 4) Handgeld, Erklärung folgt. — 5) Betastung, Erklärung folgt. — 6) Entdeckung, Erklärung folgt. — 7) Stimme. — 8) übliche Geschenke.

huenda kula kombe la hʿarusi, naye humega wali, hutia ndani ya ṣaḥani na nyama, hupelekewa mkewe kula, unakwitwa „wali wa ʿada.“

waqati huu vijana waanawake hupiga maṭâri yao na matuwazi, huimba na nyimbo zao za hʿarusi, máthalan mwanamke anamwambia mumewe:

„pendo la mashiti?“ [1]) nhalitakiani [2]),
nunua mtumwa, utie nyumbani [3]).
naona muhindi makanda makanda,
mtwanzi ni nani?“

mwanamume hujibu:

„mtwanzi ni wewe, uliye nyumbani [4]).
wataka mtumwa? safiri barrani [5]).
hutwangi muhindi makanda makanda?
kwa ubora gani?“

1) deine Liebe reicht nur für einen shiti-Stoff. — 2) silitaki mimi. — 3) damit ich sehe du liebst mich. — 4) der ich dich wie einen Sklaven in mein Haus gekauft habe. — 5) such dir selbst einen.

ao huimba:

„tazama waraqa [1]), niliokuletea,
na mola jalali, akinijaʿlia,
ni mgeni wako, takuwaṣilia.“

1) ein junger Mann an seine Geliebte.

ao huimba:

„naliona pendo [1]), likinidangana,
nikithanni wewe, mwingine hapana.
wewe mwana maji, wakimbia wimbi?
limekubandama.“

1) ein Mädchen klagt ihren ungetreuen Liebhaber an, der sie mit einem Kinde im Stich gelassen hat.

ao huimba [1]):

1) ein Mann, der eine schöne Frau hat und eifersüchtig ist, gibt der Sklavin Mwana Kombo den Auftrag, auf sie aufzupassen.

„kijakazi Mwana Kombo bibi nyumbani akwita,
uende ukateke maji, ḥatta ujaze birika.“ [1])
„kisimani maji tele [2]), wala si ya kulimbika [3]).
alindwani [4])? kilindo — hulindwa,
ndege — mḳe mzuri halindwa.“

1) bleibe so lange zu Hause und mach dir zu tun bis ich wieder zurückkehre. — 2) antwortet das Sklavenmädchen. — 3) = ngoja. — 4) alindwa nini.

ao huimba:
„mkanye [1]) mumeo, kwangu sikumwita,
sikutega tanzi, wala sikuvuta,
alipiga hodi usiku wa kiza,
hamqaribisha.“ [2])

1) kanya = kataza. — 2) sagt eine Frau zur andern, um sie zu ärgern.

ao huimba:
„kijaluba changu kimenipotea.“ [1])
„na nyumbani mwako, sina mazoea [2]),
ukilia wivu — utajikondea.“

1) eine Frau sagt zur andern „mein Mann ist mir verloren gegangen.“ — 2) erwidert die andere die sich getroffen fühlt.

ao huimba [1]):
„wataka nitinde [2]) — kwa kisu kikali [3]),
wala sinitinde kwa hili na hili [4]).
nambiwa napendwa, sioni dalili.“

1) eine Frau glaubt, daß ihr Mann eine andere liebt. — 2) tinda = chinsha. — 3) so sei es mit scharfem Messer d. h. sage es mir unumwunden. — 4) indem du mir dies und jenes vorlügst.

ao huimba:
„masikini bwana [1]) kajisafiria,
kajendea kwao, alikozaliwa,
ningekuwa ndege, ningemwandamia.“

1) der Liebhaber.

ao huimba[1]):
„nasikia shindo, ni khabari gani?
haya si vitendo vya kudanganyana!
nachie mwenyewe[2]), nikuonye ma'ana.“[3])

1) eine geschiedene Frau, deren Mann eine andere geheiratet hat. — 2) überlaß ihn mir wieder. — 3) denn ich kenne seine Angelegenheiten besser als du.

ao huimba:
„naona vishindo[1]) vya nakhoża kutweka[2]),
ukingia ndani[3]), hamna mkeka[4]).
chura[5]) mpumbavu, alinda kisima[6]),
na maji yatekwa.“[7])

1) eine Frau hat erfahren, daß ihr Mann eine zweite Frau ins Haus nehmen will. — 2) Du (der Mann) bist so unruhig, du bleibst ja kaum zu Hause. — 3) zum Hause der anderen. — 4) so arm ist sie. — 5) der Mann. — 6) die Frau. — 7) sie wird ihm seine Untreue durch Gleiches heimzahlen.

ao huimba:
„shadda la rehani[1]) lanisikitisha,
hingia[2]) nyumbani, matozi yanosha[3]),
chema hakidumu[4]), hakina ma'isha.“

1) gemeint sind die Reize einer schönen Frau. — 2) nikingia. — 3) machozi yaniosha. — 4) dumu lange währen.

ao huimba:
1. kinyunya[1]) cha sumu[2]), kina laża[3]) mno,
pale ukilapo, usikaze meno,
kalia demani[4]), sende joshi[5]) mno.
2. maji birikani, yameingia panya[6]),
hayafai tenna, illa kutawanywa[7]).
sijaona sumu kufanywa kinyunya.

1) Kuchenteig (gemeint ist der weibliche Geschlechtsteil). — 2) Gift. — 3) Geschmack. — 4) rechts. — 5) links. — 6) penis. — 7) ausgegossen werden.

ao huimba:

maji ya ziwa[1]) ya tamu, hayashindi ya kisima,
ukataka kuyateka, uyateke kwa ḥeshima.
jike lisilo maḥaba[2]) kama nguo kuazima[3]).

1) weibl. Geschlechtsteil. — 2) Liebe. — 3) ist nichts wert.

na watu wakesha kula „kombe la hʿarusi," watasoma fâṭiḥa. na khalafu waanaume na waanawake huwaombea muungu mke na mume, nao husema:

„muungu awajaʿali unyumba mwema kusema na kusikiliza, awazidie chumo jingi, awaondolee magonjwa katika nyumba yenu, awape kizazi kike na kiume. muungu awakingie[1]) maḥásidi[2]), ambaye siye yeye na muungu wake, kwa fáḍili[3]) zake muungu."

baʿada ya kwisha kula na kusoma fâṭiḥa, yule hʿarusi mavazi yake huyavua, huvaa visutu viwili, sababu anataka koshwa miguu. kisutu kimoja huvaa chini, na kimoja hujifunika. naye hukaa juu ya kiti, na miguu yake ndani ya sinia ao chanu. kungwi wa yule mkewe atamwosha miguu, na kijakazi kimeshika birika ya maji. marra kungwi atakwimba mwimbo, waanawake waitikie:

„tumwoshe mou[1]) bwana
kwa maji ya zâmzâm[2])
tumwoshe mou bwana
kwa maji ya zâmzâm."

1) miguu. — 2) maji inayotoka Makka.

ao huimba:

„upatu wa masogora[1])
nawingie mbilimbili
upatu wa masogora
nawingie mbilimbili."

1) werden die an der Waschung teilnehmenden Männer genannt. sogora = ḥodari.

1) beschützen vor jd. — 2) Feinde. — 3) Güte.

ao huimba:

„na utiwe marupia
upatu wa Wasuaḥeli.“

wale vijana wakasikia mwimbo huo, killa mtu hufanya shauri kitu cha kutia katika upatu. mwingine rupia amma rupia mbili amma tatu, killa mtu kwa uweza wake. na asiyo kitu — hendi panapo upatu, huona ḥaya[1]). watu wote wakesha pita, yule kungwi ataḥesabu[2]) feḍḍa iliyopatikana. kisha ataweta wazee wa yule mwanamke, wazigawe feḍḍa mafungu matatu. fungu moja la kungwi, la pili watapewa wazazi, la tatu watapewa maʿarusi, mke na mume, feḍḍa waliyochukua makungwi na wazazi hawaitumii, watanunua matumizi ya fungate, ḥatta ishe fungate.

baʿada ya kwisha kula kombe la hʿarusi na kosha miguu, mume atapanda kitandani. na kungwi ataleta kitambaa cha bafta, atakiweka chini ya matako ya yule mwanamke — jina lake kisarawanda. mume atalala naye mkewe, na ile damu ya kizinda[3]) itaingia katika kitambaa kile cheupe. akisha kazi yake mume, marra aondoke, atakuja kungwi, achukue kitambaa kumwonyesha mama yake ao bibi yake ao shangazi usiku uleule.

kaẓälika khabari ya makungwi: humpima yule kijana mwanamke qabla ya kuolewa, kama ana kizinda ao hana. na kumpima kwake humtia mkufu katika uchi wake, ukaingia mkufu — hana bikra, makungwi hujua sasa, ya kama hana bikra. akiolewa na mume, kungwi hukamata kuku mdogo, wakamchinsha, damu huitia katika kisarawanda, na kile kitambaa huweka chini yake.

ḥatta wakitaka kulala, kitakuja kijakazi na manukato — dalia na ṭibu na mkakasi waʿudi, yule mume atalala juu ya kitanda, na kijakazi kisinge kwa yale manukato maungo mazima, illa uchi hana rukhṣa kuushika.

1) Scham. — 2) zählen. — 3) = bikra Jungfernschaft.

marra kijakazi atapata rukhṣa, ende zake, kisha mke atamshika mumewe amsinge.

turejee khabari ya kile kisarawanda. damu iliyoonekana ya bikra — kungwi aṣ-ṣubuḥi tenna atawaonyesha waanawake jamaʿa wa yule mke, na baba hupewa khabari na mama. nao watafuraḥi sana, watajikusanya kundi zima, watembeze shangwe[1]) killa paḥali, wembe mwimbo wa shangwe:

„kiongoo[1]) ongoa[2]) njia,
babiye hʿarusi atembeza ukingo.“

1) kirongozi. — 2) zeigen.

sababu watu wasipoiona damu — hawaṣadiqi[2]), ya kama mtoto wa fulani ameonekana bikra. baba yake na mama yake, wakiwa na vitu, watampa jeuo[3]) lake, ikawa nyumba ao shamba, ao kitu cha feḍḍa mkufu ao mtali. kaẓàlika mume naye, akiwa na kitu, atampa jeuo mkewe kama kitu alichonacho. na kama hana bikra — hapati kitu kwa wazee wake wala kwa mume wake. kaẓàlika yule mume, iwapo khánithi[4]), hamwezi yule mwanamke kumvunja bikra — makungwi killa siku wanamwuliza mwari: „wamwonaje huyu mume? jissi gani? siku zimekuwa nyingi!“ na yule mume huulizwa naye, kama walivomwuliza mwari, na watani zake humfanyizia cheko, humwambia: „anapiga mateke? twambie.“ ao humwambia: „bwana mwari kaumbwa.“ na waanawake wengine huimba mwimbo:

„huyo mwanamume kamanya[1]) kula
na kugona[2]) hadodo[3]) hamlemela[4])
ôi![5]) hadodo hamlemela.“

1) manya = jua. — 2) gona = lala. — 3) kitu kidogo. — 4) lema = shinda. — 5) Ausdruck des Erstaunens.

1) Freude. — 2) glauben. — 3) Morgengabe, auch jezwa (arab.) genannt. — 4) impotent.

naye mume atajitahidi[1]) kwenda kwa waganga kutafuta dawa. ikiwa bakhti[2]) yake atapata mganga amṭibu[3]). kaẓâlika na hiyo dawa mzizi wa mwitu, hupikwa na kuku pamoja. na kama hafai, atakaa naye mwanamke miezi sitta, ikisha — naye hakumbikiri, sheri'a[4]) itamwachisha, na máhari nuṣṣu atatoa, mwanamke aolewe na mume mwingine. imekwisha khabari hii.

khabari ya fungate.

zile siku ba'ada ya siku ya h'arusi zile siku sitta zilizobaqi — zinakwitwa „fungate.“ na hiyo fungate haina karamu tenna, illa hufanywa maandazi tu. killa aṣ-ṣubuḥi huja watu waanaume na waanawake billa kualikwa, huwaamkia ma'arusi, ma'ana waanaume humwamkia h'arusi mwanamume na waanawake humwamkia h'arusi mwanamke, illa ndugu waanawaume huenda ndani kumwamkia dada yao h'arusi.

na kuamkia kwao watu hao humwambia 'arusi mwanamume „ṣubalkheri h'arusi,“ na yule h'arusi mwanamke huamkiwa „ḥali gani h'arusi?“ nayo huitikia kwa ndani „sijambo.“ khalafu humwuliza khabari „jinsi alivolala.“ na mwanamke hana rukhṣa ya kutoka illa kwa ḥaja[5]), lakini mumewe huweza kutoka ukumbini, wakija watu kumwamkia.

na watu vijana hucheza al-'aṣiri kiumbizi, ma'ana ngoma ya fimbo, na h'arusi huenda labda kucheza kiumbizi. na usiku vijana hucheza ṭari la diriji kama tuliyotangulia kusema katika khabari za ṭari.

khabari ya mwisho wa ha'rusi.

ba'ada ya fungate kwisha, ma'ana zile siku saba' walizokaa katika nyumba ya h'arusi, yule mke hupe-

1) sich bemühen. — 2) Glück. — 3) in Behandlung nehmen. — 4) Gesetz. — 5) Wunsch, Bedürfnis.

lekwa kwa mumewe. naye hufanyiwa ukingo, na huo ukingo ni msutu. hufanywa pazia, lililo kubwa, huingia ndani hʿarusi na waanawake wengine. na majakazi hushika matuwazi, na wengine wana mbiu, huenda wakemba nyimbo:

„bana ende [1]) kwao,
ende kwa wazee wake
wa mzaze [2]) yeo [3]).“

1) aende. — 2) waliomzaa. — 3) leo, bezüglich auf ende.

ao huimba:

„iyo iyo kaolewa,
ukitaka tembo utaletewa.“

wakampeleka mwanamke ḥatta nyumbani kwa mumewe. na maʿana ya kumficha huyu mwanamke — asionekane na watu.

akifika nyumbani, mwanamume hualika watu wazima waanawake, jamaʿa za yule mume ao za mke, kuonyeshwa jiko yule mwanamke. na kuonyeshwa kwake hufanyizwa chakula kingi, akaalika watu, kama awatakao, kula kile chakula, huitwa „mwonyo wa jiko.“

baʿada ya hilo haifanyizwi tenna karamu, ndio mwisho wa hʿarusi.

khabari ya mume na mkewe nyumbani.

kama mtu ana mkewe nyumbani, huyu mke hana rukhṣa kufanya neno lo lote — illa kwa ízini ya mumewe, iwapo amkataza neno każa — sitaki — bassi. iwapo amefanya, huambiwa ʿaîli [1]) mwanamke, sababu hakufuata ṭaʿa [2]) ya mumewe.

na mwanamke mungwana hana rukhṣa kutembea mchana billa ʿużuru [3]) — illa kwa ḥaja. naye lâzima kujifunika ushungi [4]). kama anataka kwenda kuzungumza

1) ungehorsam. — 2) Gehorsam. — 3) Erlaubnis. — 4) Kopftuch.

kwa rafiqi yake, lâzima kwenda usiku baʿada ya saʿa moja ḥatta saʿa ya tatu. tenna lâzima kijakazi chake afuatane naye pamoja.

na mke iwapo amekhálifu[1]) amri ya mumewe — radda[2]) juu ya mumewe, illa makosa makubwa humpeleka kwa ḥakim[3]) akarudiwa.

khabari ya kupata pendo kwa mume.

mwanamke asipopendwa na mumewe ao mwandani[4]) wake, huenenda kwa mganga, humpa khabari ya kwamba: „nataka dawa ya pendo.“ yule mganga hutoa tumba[5]) na wembe, humchansha chale ndogo sana juu ya uso wake, humpaka mafuta ya nyonyo[6]) yaliyo ndani ya tumba.

ao humpa mizizi ya dawa, humwambia: „ukipika chakula, mizizi hii tia ndani, umpe chakula ale, lakini asiione mizizi.“ hufanyiza yule mwanamke.

ao humchansha chale ya sirri[7]) mfano wa kinenani[8]), humwambia: leo mwambie mumeo akutwae, utapata pendo.“

wengine huandikiwa ḥirizi[8]) na waganga. mume akiiona, humwuliza „ḥirizi ya nini hii,“ hujibu „ya maraḍi[9]) tu.“

desturi ya mtu mwenyi wake wawili.

mwenyi wake wawili yu katika mashakka[10]). kwanza aweze kuapa maneno ya uwongo killa siku, wasigombe, sababu mwanamke na mke mwenziwe haweshi[11]) magomvi kwa uwivu. mwanamume akinunua kitu, akafika nyumbani, asingie katika nyumba na kile kitu. iwapo anataka kugawa — agawie nje, killa mtu ampelekee fungu lake. akigawia ndani, itakuwa ugomvi.

1) sich widersetzen. — 2) Zurechtweisung. — 3) Herrscher, Richter. — 4) Liebhaber. — 5) Medizintasche. — 6) Rizinusöl. — 7) Geheimnis. — 8) Schwätzerin, d. i. weibl. Geschlechtsteil. — 8) Amulett. — 9) Krankheit. — 10) Zweifel. — 11) hawaishi.

kažâlika chakula — killa nyumba haifai kula ḥattà ashibe. ukenda nyumba ya pili, kama hukula chakula — ugomvi.

kažâlika ngono[1]) — sherṭi agawe sawasawa — siku tatu huku na siku tatu huku. na kulla nyumba utakáyolala, sherṭi mwanamke ulale naye. ukimlala mwanamke mmoja — aṣ-ṣubuḥi ugomvi, atashitaki mwanamke kwa wazee wake, atasema: „huyu mwanamume hana ngono nami.“

kažâlika mume akitaka kuoa mke wa tatu, sherṭi wale wake wa kwanza awatake raḍi[2]), atoe kitu kuwapa, jina lake „mwago.“

na akanunua suria — asimgawie ngono sawa kama wake, kwa mke akilala siku tatu, kwa suria siku moja. kažâlika akinunua nguo kuwapa, suria asimpe namna ya wakewe, wataqaṣirika sana. lakini juu ya kufanyiza wema kama huo, ugomvi kwa mtu mwenyi wake wawili hawishi, sababu mmoja anataka hivi, na mmoja anataka hivi. na wakikaa nyumba moja — hawapatani. khaṣṣa usiku, mume anapotwesha, kwenda kulala kwa mke wa pili, na ngono si zake, tenna usiku awasikie mke na mume wanazungumza na kucheka — aṣ-ṣubuḥi ugomvi.

na wanapogomba, ni khaṭari[3]) kubwa mno, huumana kwa meno, ao hupigana kwa fimbo. wake wawili haifai kuweka nyumba moja. wengine wanapatana, lakini si kwa kweli. na desturi ya wake wawili — sherṭi yule mume afundishwe sana, ao asome katika vitabu — adabu ya wake wawili. asipojua, itakuwa killa siku magomvi.

khabari ya mwanamke mfiwa.

ba'ada ya kufa mume wake, hukaa 'eda[4]) miezi minne na siku kumi. ikesha 'eda kwa miezi ile, atokeapo

1) Beischlaf. — 2) zufrieden. — 3) Gefahr. — 4) Wartezeit.

mume kutaka kumwoa, haqubali, sababu ana masikitiko ya mumewe mudda mwaka uishe. na hiyo ʿeda mwanamke hukaa ndani ya nyumba, naye huvaa mavazi meupe ao meusi, lakini sherṭi yule mwanamke awe mweza ao mumewe awe mweza. asipokuwa, hakai ʿeda, maʿana miezi minne yataka matumizi. wengine ʿeda zao wanazikalia nje, wanasema: „mimi kuku, nachumia mdomo wangu.“

kaẓàlika mke mfiwa katika ʿeda hana rukhṣa kufanya urembo[1]), manukato, ao nguo zilizo nzuri, illa nguo zile, anazovaa katika ʿeda, zikiwa chafu hufuliwa, na maungo yake ana rukhṣa koga, lakini ngomani hendi.

na maʿana ya ʿeda ya mwanamke mfiwa — kujitezama nafsi[2]) yake kwamba hana mimba, hii ndio maʿana kukaa ʿeda kuto' kuolewa[3]). na tenna kwa mwanamke mfiwa ʿeda ndio sababu ya masikitiko ya mumewe.

na mwanamke mfiwa huweka ʿada[4]), killa al-khamisi hupeleka mafuta mskitini, ao hufanyiza chakula, akaweta watu kumreḥemu[5]) mumewe kwa fâṭiḥa[6]). na kulla mwaka husoma khítima[7]) qaburini[8]) ao nyumbani, na kulla mfunguo tatu hununua manukato — ʿudi, ṭibu, dalia — kupeleka qaburini.

baʿada ya mwaka akitokea mume kumposa, atapeleka shauri kwa ndugu za mumewe: „mimi nimeposwa.“ wakiriḍi — ataolewa. kama hawakuriḍi, atatokea ndugu mume wa yule ndugu aliyekufa amwoe. huyu jina lake mume mwingilizi.

kaẓàlika hʿarusi yao haiwi na furaḥa nyingi, illa mume huoa, marra akaingia ndani, akampa mkewe mkono, hawafanzi magoma na sherehe[9]).

---

1) Gesichtsbemalung. — 2) Seele. — 3) verneinter Infinitiv — 4) herkömmliche Abgabe. — 5) barmherzig sein. — 6) erste Sure. 7) Koranlesung. — 8) am Grabe. — 9) Freudenfest.

khabari ya kubusu[1]).

zamani sana wahenga wetu hawakujua labda khabari ya kujibusu, lakini sasa wameona Waʿarabu kubusu wake wao na watoto — nao wamefuata. Wasuaḥeli wakiwa ndani na wake wao, wanajibusu katika vinywa. na kutakana kwao husema mwanamme ao mwanamke „kitoto nibusu“ ao „ninonce.“ nao hubusu vilevile mtoto wao mdogo, lakini akipata miaka sabaʿ mtoto mwanamume — mama yake ao skangazi[2]) lake ao dada[3]) yake ao mkwewe[3]) — hawambusu, si desturi, lakini babake akitaka kumbusu — haiḍuru[4]). na akiwa mtoto mwanamke haifai kumbusu baba yake wala ndugu yake mwanamume.

kaẓâlika mtoto mdogo wa mwaka mmoja ao miwili, kama amekuja bibi yake ao shangazi ao mwanamke mwingine, huambiwa yule mtoto „mchobee[5]) shangazi lako.“ naye huenda akamchobea. tenna humwambia „mbusu.“ humbusu. tenna huambiwa na mama yake: „mpe tumbaku shangazi lako.“ hunyanyua juu nguo, akamwonyesha mboo[6]) yule shangazi lake, naye huvuta ile mboo, kisha hunusa, kisha huenda chafya[7]), tenna husema: „á, tumbaku kali sana!“ humwambia: „ficha tumbaku yetu.“ na kama wako waanawake wanne ao watano — wote watamnusa, nao hufuraḥi, tenna hucheka sana.

na kubusu namna ya pili — sherifu[8]), ukakutana naye njiani. ao mwʿallimu anaṣalisha katika meskiti, ao anasomesha darasa[9]), ukafika darasani, humbusu. na kubusu kwake — humbusu mkono sherifu na mwʿallim, si katika kinywa.

1) küssen. — 2) Tante. — 3) Schwester. — 4) Schwiegermutter. — 4) schaden. — 5) chobea lieb halten. — 6) penis. — 7) niesen. — 8) Nachkomme Muhammeds. — 9) Schule.

khabari za ngoma za furaḥa[1]).

ngoma za zamani.

desturi ya Wasuaḥeli tangu zamani furaḥa yao kubwa katika hʿarusi, na pasipo hʿarusi, furaḥa kubwa ya ngoma. na wakiwa na mashindano[2]), wakacheza na ngoma. nao wanapenda sana machezo ya ngoma tangu wahenga[3]) wao ḥatta vijana wa sasa. zamani wakicheza ngoma — ḥatta majumbe hucheza ngoma, sababu wanavoipenda wote.

ngoma kuu.

áṣili[4]) yake ndio ngoma ya ujumbe. kupigwa kwake huwekwa ngoma mbili kubwa uwanjani, nazo huwa juu ya vitanda. na kupigwa kwake kwa fito mbili. na anayepiga, iwapo si jumbe, huvua kofia na vyatu. na mpiga zumari[5]), iwapo mtumwa, huvua kofia, na mpiga siwa[6]) vilevile huvua kofia. akiwa mungwana, havui kofia.

na baʿada ya zile ngoma kuu husimamishwa goma kuu la tatu juu ya mti, huitwa goma hilo mkuwiro, ndilo lenyi ʿezi[7]) katika ngoma kuu. bassi zikipigwa zile ngoma, watu hucheza, nao hucheza watu wawili

---

1) Freudentänze. — 2) Wettstreit zwischen den einzelnen Parteien, Cliquen. — 3) Vorfahren. — 4) Ursprung. — 5) Flöte. — 6) Jumben-Horn. — 7) Macht.

tu. na wachezao sherṭi wawe waungwana, watumwa si desturi kucheza ngoma kuu. na hawa waungwana wanapocheza, huvua kofia na vyatu, na majumbe wakicheza, hawavui kofia wala vyatu. lakini shaha[1]) ao waziri, akicheza na jumbe, huvua kilemba, kofia havui. na hao wanaocheza hushika panga mikononi, ndizo wanazochezea, na jumbe akicheza, huwa na wapambe wawili vijakazi wazalia, ndiwo wanaozunguka naye yule jumbe. na machezo hayo hayana nyimbo.

ngoma ya sendemre.

na mno zamani machezo yao, wakiwa na mashindano, huchezwa „sendemre.“ na hilo sendemre huwekwa ngoma uwanjani, iliyo kubwa, na chapuo[2]) mbili na mrungura[3]) na zumari na upatu[4]). na hii ngoma kubwa hutundikwa juu ya panda ya mti, nayo hupigwa kwa vipande viwili vya mti. na mpiga zumari hujengewa dungu juu ya mti. na hilo dungu hufungwa na majamvi — mfano wa nyumba. naye huwekewa kitanda juu, hufanyizwa na mwavuli wa matawi ya tambuu. hupiga zumari na mwimbo katika ile zumari, na watu wako chini wanaitikia kwa maneno, máthali kama:

„tulikuwa sawa, sasa hivi tuwa[1]) mbalimbali,
mwalia[2]) mikungu, majumbani hamna ṣaḥani,
tulishone fumba mtondoo[3]) tulitose pwani.“

1) wir sind. — 2) essen aus. — 3) die mtondoo-Leute. Bei den mashindano stehen sich immer 2 feindlich gesinnte Gruppen gegenüber.

ao huimba:

„sitirihali[1]) watumwa, simameni tuwatume,
mwenyi maraḍi makuu haonani na mtume.“

1) die sitirihali-Leute.

1) shaha und waziri kommen ihrem Range nach gleich nach dem Jumben. — 2) Trommel. — 3) Trommel. — 4) Blechinstrument

ao huimba:

usinichokoze kwimba
Amri [1]), utalia,
nduguyo kajenga nyumba [2])
Unyanyembe ameikimbia.

1) Name. — 2) Haushalt.

na kucheza kwao waanawaume hushika vitara mikononi ao panga ao bakora. na waanawake hucheza vilevile, na mikononi huskika mashadda ya tambuu [1]). na kucheza kwao huzunguka ule uwanja. na marra moja hutoka mwanamume paḥali aliposimama, humqabili [2]) mwanamke uso kwa uso, wakacheza pamoja. na machezo hayo huchezwa siku ya siku kuu, ao siku ya hʿarusi, ao furaḥa tu, ao kwa mashindano, lakini sasa hayako machezo hayo.

khabari ya mashindano.

zamani mrima kulikuwa na mashindano mengi. mashindano yao husema: „tufanye chama [3]) cha umoja beina ya mtaa każa wa każa na mtaa każa wa każa.“ huchagua mkuu wao, na waziri mmoja, na ḥal-mashauri [4]) na kijumbe. huyo mkubwa killa neno juu yake, akifa mtu, ao mtu ataka kuoa, ao mtu amefiwa, mambo yote huyafanya yeye mkuu. na waziri kazi yake. likitokea neno katika mji, hupewa shauri waziri, naye hupeleka khabari kwa mkuu. na ḥal-mashauri kazi yake hushauriwa neno litokeapo. na mjumbe huwalika watu, maʿana huenda kuwambia watu „kesho mkutano kwa mkuu, amekufa mtu,“ ao „tunataka kwenda kuzika,“ ao „twataka kwenda kuhani.“ [5]) hupeleka khabari killa

1) Betelsträußchen. — 2) sich nähern. — 3) Vereinigung. — 4) hali yake kushauriwa. — 5) an der Trauerfeier teilnehmen.

nyumba, „tukutane kesho saʿa ya tatu.“ hushikana chama hicho kwa umoja. na likitokea neno mjini, mkuu wao halikumpendeza, watu wote hufuata maneno yake. ikiwa mtu amemqaṣiri mkuu wao karamuni, karamu itavunjika.

kaẓâlika katika mashindano haẏo hutokea machezo ya ngoma kukesha usiku kucha, siku sitta ao sabaʿ wanacheza ngoma tu. wanatumia feḍḍa nyingi, maʿana watu wa chama moja wakichinsha mbuzi wawili wengine huchinsha mbuzi wanne. siku ya mwisho wa ngoma hufanya karamu, huʿarrifiwa watu wageni na wenyeji. na kufanyiza maandazi killa nyumba. killa nyumba hupelekwa pishi tatu za mchele, na pishi moja unga wa ngano na samli na sukari kuandaa, maʿana isipokuwa hivo — kikao kimoja kimefeḍeḥeka.

na huo ni mwimbo wao wa mashindano:

„mwenyi fulani hojaji[1]) zache,
kesho hʿarusi kesho kutwa fungate,
utafilisika, gongoni[2]) nyache.“ [3])

na chama cha pili huimba:

„sisi twaomba salâma maji yapite,
kolekole[4]) na koana[4]) wajifiche,
panapo ʿadui yako usipite.“

hii ndio khabari ya mashindano yao, lakini sasa hawayafanyi mno kama zamani, maʿana „mikono mitupu hairambwi, ikarambwa — ina punje.“

ngoma ya chando.

huwekwa chapuo (ngoma) moja na vumi moja (ngoma) na mganda (ngoma) na zumari. na kuchezwa

1) Gerede. — 2) Stadtviertel Bagamoyos. — 3) mit den Gongoni-Leuten könnt ihr euch nicht messen. — 4) kleine Fische, gemeint sind die Gegner.

kwake huchezewa uwanjani, waanawaume na waanawake. nao hucheza, tenna hupiga magoti wanapocheza, nao huimba mwimbo:

„chando wê ndio ngoma,
mtoto mdogo wajuaje kwanga?[1])
chando ndio ngoma.“

1) umhertreiben (von Mädchen Nachts)

ao huimba:

tujile[1]) kutia moto na watoto,
tujile kutia moto na watoto,
na wenyewe ni walele[3]), si wa mato[3]),
fungua mlango nipite.“

1) tumekuja. — 2) wamelala. — 3) macho.

na ngoma hii ni ya zamani, lakini sasa hupata siku wakacheza.

ngoma ya kigoma.

áṣili yake kigoma hupigwa panapo h'arusi ao furaha tu. nayo hualikwa waanawake na waanawaume. waanawake wakijua, leo kuna kigoma, hujitengeneza mavazi mazuri na manukato kujitia. na kuchezwa kwake huchezwa nyumba yenyi ukumbi mkubwa. waanawake hukaa juu ya dari, hushika mbiu kupiga, na waanaume hukaa chini. mmoja huimba, naye huitwa sogora[1]), na watu wawili hupiga chapuo, na moja hupiga vumi, na mtu moja upatu, na moja hupiga zumari.

tenna ngoma ikianza, hutoka vijana waanawaume, nao wamevaa mavazi mazuri, na mikononi wameshika vileso. tenna yule sogora huimba mwimbo:

hao hao — hao wê.“

1) Vorsänger.

hucheza tenna wale vijana watu wawili. wakichoka wawili hao, huja wawili huitwa tira yao. na wale waanawake, wakiona waanaume wanacheza, hupiga vigelegele juu ya dari, hufunga na mikufu katika visutu, ao timbi, ao pete, kuwapa waanawaume, wanaocheza, ma'ana ni tunza zao.

naye sogora huimba tenna:

„fulani wa bwana fulani
anacheza na nduguye."

na wale waanawake na waanaume huitikia:

„yôyô bwana, yôyô bwana,
anacheza na nduguye."

ao huimba:

„kalale bwana kalale
uleleko [1]) jana na leo kalale."

---

1) ulipolala.

ao huimba:

„kama wewe kama wewe kama wewe hê
kama wewe kama wewe kama wewe hê
tutampata mwenzio kama wewe."

ao huimba:

„mwendo wa kenge, kenge mwendoe,
killa apitapo, kenge mwendoe,
mwendo wa kenge."

na mwisho wake zile tunza, waanawake walizowapa waanaume, ngoma ikivunjika, hupewa wenyewe waanawake vile vitu. wenyewe wale waanaume huuliza: „mkufu huu wa nani?" ao „pete hii ya nani?" mwenyewe mwanamke hutambua, akaja kuchukua. na yule mwanamume, akimpenda mwanamke yule mwenyi mkufu, hupatana naye, akawa rafiqi yake.

lakini yale maua, yaliyofungwa katika visutu,

huchukua waanawaume, huitwa „vikuba.“ mno hutungwa mkadi [1]) na riḥani [2]), hutia na mafuta ya manukato.

nacho kigoma huchezwa tangu siku tatu ḥatta siku saba‘, hakina karamu. na mchezo wake huanzwa al-‘aṣiri na usiku.

ngoma ya tinge.

áṣili yake imetoka barra. mchezo wake hucheza waanaume watupu. na machezo yake hupigwa makofi, hapana ngoma. nao hujipanga ṣafu [3]), wengine upande huu, na wengine upande huu. na mchezo wao hupiga shindo mguu wa kulia. marra hunyanyua ule mguu wa kulia juu. na mwenyi mguu mwepesi, akinyanyua juu upesi, akishusha upesi, wa pili akikawia kunyanyua katika ule upande wa pili — amefungwa — huja upande huu. na nyimbo zao huimba:

„ajaye hamna [1]) wê
ajaye hamna.“

1) wer kommt, wird geschlagen.

ao huimba:

„pomboo [1]) akiinama akinuka.“

1) Fisch.

ao huimba:

„somo [1]) wê, somo,
lubelege [2]) hê somo.“

1) Freund. — 2) lu auf lugulu (mguu) bezüglich; belega = peleka.

ao huimba:

„mnyanya upandapo huota.“

1) Pandane. — 2) Basiliumkraut. — 3) Reihe.

ao huimba:

„endaye Pemba, endaye Pemba,
salâmu kwa Mbaruku — kisomanga.“

ao huimba:

„hapa pana moja, na moja tenna
mcheza katinge kanyamaa [1]).
hapa pana mbili na mbili tenna
mcheza katinge kanyamaa.
hapa pana tatu na tatu tenna
mcheza katinge kanyamaa.
hapa pana nne na nne tenna
mcheza katinge kanyamaa.“

1) Der tinge-Spieler ist geschlagen.

huimba kama hivi ḥatta kutimia kumi. khalafu huimba:

„hapa patupu, hapa patupu.“

upande utakaoshindwa, huwapiga msokole, husema:

„sókolè [1]) sókolè iyôô.“

1) mmechoka.

huitikia wote pia, khalafu hucheza hivo ḥatta wakichoka.

ngoma ya kiumbizi.

áṣili ya machezo hayo ugomvi. hupigwa ngoma chapuo na vumi na upatu na zumari. na machezo hayo huanzwa al-ʿaṣiri katika saʿa ya kumi ḥatta saʿa kumi na mbili. nao hucheza chini ya mti kama mwembe, uliwo mkubwa, wenyi kivuli chema. huja vijana, wamevaa kanzu nzuri, na mpiga zumari hupiga zumari yake:

„sheṭâni njoo, sheṭâni njoo,
tumpake chokaa.“

vijana hutupiana fimbo, na maʿana ya kumtupia fimbo, anamwita, waje wacheze pamoja. na mchezo wao hucheza kwa fimbo. kwanza hucheza vizuri kwa majivuno, na zile fimbo hugongana, iwapo hawana ugomvi. na iwapo yule anayecheza naye ʿadui yake, amemtwalia mwanamke wake, ao wametukanana tangu zamani, machungu yao hutoleana kiumbizini. na desturi yake hicho kiumbizi waqati wa el-maghribi[1]) kinapotaka kuvunjwa, hupigwa mshindo wa bondogea[2]), huchezwa kwa fimbo nyembamba, hupigana kwa fimbo hizo. ao huwapa watoto wadogo fimbo nyembamba, hujifundisha kucheza kiumbizi, ao nao hupigana wale watoto.

na kiumbizi huchezwa panapo hʿarusi sasa, na zamani wamecheza killa siku.

ngoma ya kidatu ao msoma.

ngoma hii hucheza vijana waanawake vigori na wari na waliwoolewa. nayo huchezwa usiku. na kuchezewa kwake huchezwa uwanjani, hujikusanya waanawake, na waanaume huenda wakatezama. nao waanawake hupiga makofi, wakemba na nyimbo:

„nache[1]) wê nache,
Ramaḍani nache,
usinivumbue mti
kwa kipande cha fenesi.“[2])

1) niache. — 2) Yakfrucht.

ao huimba:

„ʿilimu[1]) mwaisoma ʿilimu,
qorâni na wivu haikusilimu.“

1) Wissenschaft.

1) Sonnenuntergang. — 2) besonderer Trommelschlag.

ao huimba:

„kigori kapewa mimba,
upande mwana mwari — upande.“ [1])

1) zu ergänzen kigori.

ao huimba:

„kalalama [1]) hê leo kalalama,
›ni ngali [2]) mwari‹ — ñgombe kalalama.“

1) schreien. — 2) noch.

ao huimba:

„nache nitwae mimi [1])
nache nitwae mimi
kutwaliwa ku uchungu.“

1) Klage eines Mannes, der Ehebruch begangen und von seiner Frau hört, daß sie dasselbe getan.

ao huimba:

„si kwetu si kwetu, Mkwaja [1]) si kwetu,
kula ngano yako, nile chachu yetu.“ [2])

1) Ort. — 2) ein Mädchen weist ihren Bewerber ab.

ao huimba:

„Bori [1]) kaponzwa [2]) na kalima [3]),
macheche [4]) ya moto — mzinga u nyuma,
Bori kaponzwa ni kalima.“

1) Mann aus Saadani, der in Folge seiner bösen Redereien über andere ermordet wurde. — 2) in Gefahr geraten. — 3) Worte. — 4) Funken.

ao huimba:

„kaudundu [1]) unga kaubwi.“ [2])

1) dunda = twanga. — 2) bwia = ramba.

ao huimba:

„wa [1]) ʿisha wa ʿisha, mshuko wa ʿisha,
radi ya kungwile [2]) yamhangaisha.“ [3])

1) mshuko. — 2) kungwi lake. — 3) in Unruhe versetzen.

ao huimba:

„Mwanakere kukataa, nyonyo [1]) użia wê,
Mparungo kaitia moto mrima wê.“

1) Busen, hier Frau gemeint.

na mchezo wao hucheza waanawake wawili wawili pamoja, wakesha wale, huja wengine wawili. nao huchobeana, maʿana hupeana chambi, huzunguka mduwara.

marra nyingine hualika mpiga zumari, nao humpa mapesa, ao huwapigia burre, lakini ngoma hapana.

ngoma ya mdurenge.

kuchezwa kwake chapuo mbili na yumi moja na upatu na mpiga zumari. nao hucheza watu wawili wawili mwanamke na mwanamume, hushikana mabega, wakazunguka katika uwanja. na mpiga zumari huimba mwimbo:

„mwandani [1]) wa somo [2]) ananipenda,
›pesa moja twaa‹ — ananipenda
›pesa mbili twaa‹ — ananipenda.“

1) Geliebte. — 2) Freundin.

ao huimba:

„ukizinga [1]), ukipata
mwenyi babu [2]) — sina shakka.“

1) zini. — 2) ein Kind.

ao huimba:

„wawili wawili [1]) utawatendani,
moja Mwavi moja Shangani?
tuutie moto upande wa pwani.“

1) waanawake zu ergänzen.

ngoma ya bondogea.

ásili yake ni ngoma ya wazalia. nayo huchezwa ḥatta sasa Unguja na mrima. na mpigo wake chapuo na vumi na upatu na zumari, na waanawake hushika mbiu mikononi. na waanaume hushika panga ao fimbo. na kucheza kwake hucheza duwara, lakini marra moja hutoka mtu moja, akaingia kati ya uwanja kucheza. akiondoka, huja wa pili. waanawake hawachezi. wengine hupiga mbiu, wengine hutazama tu. na mpiga zumari huimba mwimbo:

„Naṣoro naye namtafuta,
kanibie pesa langu la mafuta.“

ao huimba:

„iyô, kachupa kavunja chupa.“

ngoma ya sopai.

ma'ana ya sopai — walipokuja mapolisi[1]) ya kihindi Unguja, wakafanyiza ngoma ya sopai. na mpigo wake sopai chapuo mbili na dogori moja na upatu na mpiga zumari. na kucheza kwake waanawaume hushika fimbo, na waanawake wengine hushika fimbo. na waanaume, wanapocheza, hupania[2]) nguo. na mchezo wao hutazamana usoni mke na mume. nao hucheza kwa shingo, huzunguka duwara. na mwimbo wao:

„sopai amelala nje
sopai amelala nje
kwa kukosa mke.“

ao huimba:.

„kanitwalia shoga langu wê
leo Mazengo.“ [1])

1) Name.

1) vom engl. police. — 2) hochschürzen.

ao huimba:

„nalikwambia usende
kwa Mtambalika [1]),
una nini bata?
una nini bata?“

1) Name eines Mannes.

ao huimba:

„khabari ya Zinjibari kuna mbu na usubi,
masopai wamepigwa na wachezao kinubi.“

ao huimba:

„hapana ugonjwa mbaya, buba na upele,
ajapokuwa mkweo, mkono u mbele.“

ngoma ya msanja.

ngoma yake hupigwa uwanjani ao katika nyumba, haina zumari. huwekwa dogori moja na upatu na chapuo. na waanawake hushika mbiu. huzunguka wote waanaume na waanawake duwara uwanjani. na mghani [1]) husimama kati, huimba nyimbo:

„Salimu wajivuna, kama mtoto wa bwana.“

wale waanawake huitikia:

„hê wallâh“ ao „hê nana.“ [1])

1) des Reimes wegen, ohne Bedeutung.

mghani huimba tenna:

„tashona kanzu yangu ya marefu na mapana,
tezama uwembamba wake, kama mnara wa bwana [1]),
nguo mbili, bwana, sabuni ya kuombea.“

1) Leuchtturm des Sultans.

1) Vorsänger.

ao huimba:
„mwendo wa Mushti[1]) Mâthiyu[2]) watu wanauṭama'ni,
khaṣṣa avae makoti, akimbilie bandani,
khaṣṣa atwae tambuu, aitafune kinywani,
khaṣṣa nguo za ḥarîri, kwake hazina thamani,
kicheko cha mwenye mwanya, mwenye pengo achekani?“[3])

1) vom engl. mister. — 2) Matthews, ein Engländer, der lange Jahre General der Truppen der Sultane von Zanzibar war. — 3) anacheka nini.

ao huimba:
„njia ya ñgambo[1]), njia ya ñgambo, naipitia utumwa,
nikenda chooni, birika mbele na nyuma,
sikutaki wewe, nataka mwenyi watumwa.“[2])

1) Negerviertel Zanzibars. — 2) Klage einer Frau, die einen armen Mann hat, aber gern einen mit vielen Sklaven haben möchte.

ao huimba:
„qiṭimîri[1]) ṭiba[2]) kina mazoea,
fundi wa maḥaba ni yupi? nambia.
fundi wa maḥaba ni moyo kupenda.“

1) ein pepo. — 2) mein Gewährsmann gab mir an, daß qiṭimîri ṭiba bedeute „Liebe, mein Liebling.“

ao huimba:
„nina maṣâibu[1]), nami nayaona,
naona ḥarubu[2]), moyo raḥa[3]) sina,
bana nimetubu[4]), sitatenda tenna.“

1) Schlechtigkeiten. — 2) Krieg, Streit. — 3) Ruhe. — 4) bereuen.

ao huimba:
„bana wanipenda, twende zetu Makka,
twende tukazuru[1]), turudi ḥaraka[2]).
umeniqaṣiri[3]), nimeqaṣirika.“

1) beten. — 2) Eile. — 3) weil du es abgelehnt hast.

ngoma ya dandaro.

huchezwa uwanjani. na ngoma yake dogori moja na upatu na chapuo na mpiga zumari. na machezo yake waanawake na waanaume. waanawake huvaa mbugi miguuni, na waanaume hushika bakora. na kucheza kwao huzunguka na kupiga mguu mmoja mmoja chini. na nyimbo zao hupokeana, sogora wao huimba, na atakayo yoyote huimba.

na nyimbo zao ni hizo:

„kutoka — natoka kwako, kurudi naona shemu[1]),
nitapita njia gani, hatta nitokee kwenu?
sitamwacha ubwa[2]) wangu, mwenyi mali kemkemu.“[3])

1) Scham. — 2) Liebling. — 3) viel.

ao huimba:

„mbaramwezi[1]) rawarawa[2]) tupakie Wabarawa,
teremkia bondeni, maua yamechanua,
usinione mdogo, naweza kukuchukua.“

1) Mondschein, hier menses gemeint. — 2) lawa = toka.

ao huimba:

„nimeʿaṣi kwetu, sababu nakuja kwako,
sikutaki wewe, nataka mwenyi majoḥo.“

ao huimba:

„Somangara[1]), wenzio wanakusema,
Somangara kachukua mabuyu, kwenda kugema,
na uche, dandaro naona shemu.“

1) Name eines Mzegeju.

ao huimba:

„bwana kanunua ndege[1]), mlio wa kakatua[2]),
utumwa wa bwana Sefu mpaka jua kutua.“

1) eine Frau. — 2) ein Vogel.

ngoma ya kasangwa.

machezo yake hupigwa ngoma nne, chapuo mbili na dogori la tatu na mrungura moja, na tenna zumari na upatu. nayo kuchezwa kwake hujipanga watu mduwara, wa amma waanawake upande wao mbali na waanaume upande wao mbali. na mchezo wao ni kuchupachupa. hutoka mmoja, akampa chambi mwenziwe, kisha hurudi, huja wengine kufanya vilevile.

na mwimbo wao:

„kitanda cha msichana[1])
hakina mkeka,
kweli wê sorobea[2]),
kitanda cha msichana
hakina mkeka.“

1) junges Mädchen. — 2) du bist doch so eitel.

ngoma ya mbenda.

mpigo wake dogori tatu, hupigwa na mtu moja, na chapuo ya nne na upatu wa tano na zumari ya sitta. na mchezo wake huchezwa na waanaume tu. nao huvaa mavazi ya kike, vitambi búraa, na kaya za dismali, na vyombo vya feḍḍa mikononi. na mchezo wao hucheza kwa shingo.

nao huimba nyimbo:

„la Mlali[1]) joka kuu la Mlali,
fungeni milango, mzuie wana wari.
kazi imekwisha, gobore[2]) keba mtali.“

1) Ort. — 2) vergl. folgendes Kapitel „ngoma za sasa.“

ngoma ya goma.

mpigo wake chapuo mbili na mpiga zumari. na mchezo wake waanaume pekeyao, waanawake hutezama

tu. nao hucheza kwa bakora. mpiga zumari hutoa mwimbo, nao huitikia pamoja.

huimba:

„kisekeseke [1])
kafungwa na ukole [2])
kisekeseke.“

1) Vogel, gemeint eine Frau die sich gern herumtreibt. — 2) Strick.

ao huimba:

„Mbarangashi [1]) simama dede [2])
âhê sina mwana, tambeba nani?“

1) Name eines Kindes. — 2) aufrecht.

nao huzunguka duwara. na marra nyingi husomea kwa umoja, husema: „sókolê sókolê“ [1]) na wengine huitikia: „iyôô.“

1) wir sind müde.

ngoma ya sasa.

ngoma ya banji.

banji watu hufanyiza chama mashindano vikao viwili. kikao kimoja huitwa „goboreni,“ cha pili huitwa „seneda.“ mchezo wao hujenga banda. na banda lake hununuliwa jora za merikani, likashonwa tanga, kinakwitwa chendarua. husimamisha kwa miti. na kati ya hicho chendarua hutia bendera. wakesha lifunga hilo banda, huweka viti. wakaalikwa waanawake na waanaume. kualikwa kwake hupigwa mrungura killa

nyumba, huambiwa „leo banji.“ nao huwa na mkuu wao na waziri wao mmoja na kijumbe. na waanawake vilevile hutawallishwa[1]) mkuu mwanamke na waziri na kijumbe. na kutawallishwa kwake hao mawaziri na wakuu, hutoa feḍḍa. na inapotoka hiyo feḍḍa, hupigwa banji. wakenda wanaotaka kutawalli[2]) na watu wote wanachama na watu wengine, hutolewa ile feḍḍa. husimama mtu juu ya kiti, na yule anayetaka kutawalli, hukaa juu ya kiti. yule aliyosimama, husema: „muungu amtawalli mkuu.“ na watu wote huitikia: „âye.“ na yule aliyesimama juu ya kiti husema: „amekuja fulani kwetu, anataka machezo, naye ameleta feḍḍa każa wa każa, anatawalli ukuu, mnamtaka?“ na watu wote huitikia: „tunamtaka.“ akesha tawalli, hupewa jina — ya kwamba: „huyu ni mkuu fulani jina lake.“ akisha tawallishwa hutiwa juu ya kiti, watu hushika kile kiti, wakakinyanyua juu na yeye pamoja, humzungusha katika lile banda la banji. waanawake hupiga kigelegele, hupigwa na mrungura nyuma yake. na ile feḍḍa hugawiwa wanachama na wakuu na mawaziri, waliomtangulia yule, aliyotawalli leo. tenna hupigwa banji, ikiwa usiku kucha ao saʿa tatu ao nne.

na machezo hayo hupata siku, wakenda viungani, wakapika karamu, hualika watu wa mji na wenyewe. huenenda hushinda kutwa kiungani, hula vyakula na kucheza, ḥatta jioni hurejeʿa mjini na shangwe.

na mchezo wao waanawake wengine hukaa juu ya viti — wale wakuu na mawaziri na wakuu waanaume, na wanachama hucheza. na kucheza kwao hupangana waanawake na waanaume, huzunguka duwara, huimba na nyimbo:

---

1) in ein Amt einsetzen. — 2) ein Amt antreten.

„msafiri wê, naomba salâma,
mfa maji wê, hachi kulalama.“

ao huimba:

„mwambie mama, nakuta mashakka,
mwambie mama, nakuta mashakka.
tumewadanganya nyabwa [1]),
tumewadanganya nyabwa.“

1) Hund.

ao huimba:

„mchagua jembe, wala si mkulima,
nachezea khiyari, banji si utumwa.“

ao huimba:

tumekula ñgombe saba‘ u thelatha mia [1])
simtaki huyu Matende [2]) kumshuhudia.

1) sagt die eine Partei. — 2) Name.

ao huimba:

„njoo bwana, njoo,
bwana wangu, unipoze moyo.“

ao huimba:

nipe mbili nende, nipe mbili nende,
kama hukunipa, sileti mshindo wa bwende.

ao huimba:

„huyu binti Simba meno kama ngwe [1]),
kazi yake zina [2]) na kulala nje.
Maguru Kutimba inzi kawawinge.“

1) Flußpferd. — 2) Ehebruch.

ao huimba:

„safinati nuhu [1]) tutainunua,

1) Name eines Schiffes.

tutawapakia, maseneda [1]) wawe baḥaria,
wakavute kamba, na kutupikia.“

1) die seneda-Leute.

ao huimba:

„kanitende kanitende,
kanibia kipande changu,
panya kanitende.“

ao huimba:

„njaa mbaya, njaa mbaya,
Manga [1]) kavaa jambia
limempwaya.“ [2])

1) Name. — 2) lockern.

ao huimba:

„msambe [1]) msambe
watoto [2]) nimewadanganya.“

1) glaubt nicht. — 2) die Leute der eigenen Partei.

ao huimba:

„wambiwa wazinga [1]) hukai kitako,
nakwambia kweli, mwenzangu,
tunza moyo wako, ukae kitako,
lataka [2]) kwambiwa
lisilo nathari.“ [3])

1) ehebrechen. — 2) auf shoga Freundin bezüglich. — 3) Verstand.

ao huimba:

„nataka kwimba, kijana, niimbe na nani?“ [1])
„takwimba na wewe kibibi, uliye nyumbani.“ [2])
„kwanza una chongo [3]) na kibiongo [4]),

1) sagt ein junges Mädchen. — 2) sagt ein Mann. — 3) Antwort des Mädchens: du bist einäugig. — 4) Buckel.

pili una tende [1]) na kasende.“ [2])
gobo [3]) lache lende.“ [4]).

1) Elephantiasis. — 2) Syphilis. — 3) goboreni-Mann. — 4) laß sie in Ruh.

ao huimba:

„anguruma kama simba kana mama
âhê ukashindwa bassi.“

ao huimba:

1. „usinitie wasiwasi,
kama hunitaki — bassi,
songa [1]), songa,
songa unipe nafasi [2]).
2. unyumba wa makelele
siutaki, nenda mbele,
songa, songa,
songa unipe nafasi.“

1) gehe. — 2) laß mich allein.

desturi ya wavikao — likaingia neno katika mji, lililo geni, ao mtu amefanya neno la ʿaîbu [1]), naye mkikao, humwimba katika machezo ʿaîbu aliyoifanyiza.

na hii ngoma ya goboreni na seneda ndio inayochezwa sasa killa siku, pakiwa na hʿarusi ao kwa furaḥa tu. na zile ngoma za zamani hazichezwi mno, illa hutokea siku moja, wakitaka ngoma ya chando, ao ngoma ya kiumbizi, ao waanawake wakitaka kidatu, ao wakitaka sopai, ao vijana wana hʿarusi ao furaḥa tu, wakitaka ngoma ya goma — huchezwa namna ya zamani. lakini hizi ngoma nyingine za zamani tulizozitaja — zote hazichezwi sana.

na Wamanyema sasa wanacheza killa siku ngoma

1) Schande.

zao katika mrima, na Wasuaheli huenda kutazama. na mchezo wao huwekwa dogori, likapigwa pasipo upatu wala zumari. na mchezo wao hucheza waanawake na waanaume. nao hutikitiza vyuno, huimba na nyimbo:

„Lubangula[1]) usimwite bwana.“

huitikia:

„kahonga maboga.“ [2])

songora:

„ukamwita bwana,
kichwa kitamvimba.“

huitikia:

„kahonga maboga.“

1) Name einer Frau. — 2) sie hat ihm nur Gemüse gekocht.

khabari ya pepo[1]).

Wasuaḥeli wameshiriki[2]) pepo waanaume na waanawake. mwanamke akiwa na ḥoma siku tatu hujitia pepo kutaka kupungwa, khaṣṣa[3]) akijua mwanamume ana kitu. killa siku ugonjwa unazidi, kitandani haondoki. na wazee wake yule mwanamke, wakimwona mtoto wao mgonjwa, humwambia: „mkeo pepo wa bibi[4]) yake amemrithi[5]), ndiye anayemwuguza. sababu alipokuwa mdogo, tulimpandisha kichwani bibi yake pepo wake, tukasema naye „mlee huyu mtoto ḥatta akikua, akipata mume, tutakupa chano[6]) chako. na sasa bibi yake amekufa, pepo anataka chano chake, amemshika mjukuwe.“[7]) na yule mume kama hakuyashika maneno ya wakwewe, wote watamteta, husema: „mwanamume huyu ana choyo.“[8]) humpa jina la fumbo[9]) „chuma hamegwa.“ na iwapo amequbali[10]) maneno yao, ya kama kweli mke wangu ana pepo, sasa nataka kumpunga, wazee wake watafuraḥi sana, watasema: „mtoto wetu amepata mume ampendaye.“ na mwanamke ataqubali, mume wangu ananipenda. marra atamwita mganga, atazamie ubao[11]) „nini kinamwuguza mke wangu?“ atajibu: „hana kitu illa pepo bassi.“ atajibu mume: „nataka umfanyie dawa.“

1) böse Geister. — 2) Teil haben — 3) besonders. — 4) Großmutter. — 5) erben. — 6) Mulde mit Geschenken für den bösen Geist. — 7) mjukuu wake. — 8) Geiz. — 9) versteckter Name, Spitzname. — 10) einwilligen. — 11) auf dem Zauberbrett nachsehen.

mganga atajibu: „kwanza tumfunulie nyungu [1]), tumtezame ḥali yake.“ na hiyo nyungu namna mbili, kuna nyungu ya mawe na nyungu ya mvuke [2]).

nyungu ya mawe huokotwa vidurazi [3]), ni madongo makubwa makubwa, huchimbwa juu ya hivo vilima vya vidurazi. huleta mawe saba‘, wakafanya moto. na yale mawe huungua. tenna hujenga banda la jamvi. akaja yule mgonjwa, hukaa juu ya kiti, likachimbwa shimo. kisha huja mtungi wa maji, akafunikwa uso, yakazimwa yale mawe na maji ndani ya shimo, moshi wake humpata yule mgonjwa, hutoka na jasho. hii nyungu ya mawe.

na nyungu ya mvuke huchuma majani ya mvuke, yakapikwa katika mtungi ḥatta yakawiva. moshi wake huinamia yule mgonjwa, akatokwa na jasho. na maji mengine ya ule mvuke humpaka maungo mazima. hii ndio nyungu ya mvuke.

mudda wa siku saba‘ killa siku jua linapotua ḥatta jua kutua hufanya nyungu, hukaa sa‘a moja ndani ya ile nyungu. na yule mwanamke hufuraḥi nyungu inapokwisha, sababu qaribu atapungwa [4]). ikesha nyungu, hufanya mashauri ya kumpunga, humwambia yule mganga: „huyu ndiye mteja [5]) wako, wapashe khabari wateja wako, twataka kufanya ngoma.“ mume huenda dukani kununua mavazi ya pepo — bendera [6]), kaniki [7]), bafta [8]). hushonwa na suruali [9]) moja bafta na bendera, marra litajengwa banda, ikiwa shamba ao mjini. jina lake banda hilo kilinge.

jioni mwanamke yule hupelekwa kilingeni, napo kilingeni hupambwa chano. katika chano hutiwa ndizi,

---

1) jd. den Topf aufdecken d. h. jd. mit Dampf behandeln. — 2) Baum. — 3) Termitenhügel. — 4) punga den pepo austreiben. — 5) Klient. — 6) rotes Tuch. — 7) dunkelblauer Baumwollstoff. — 8) weißes Baumwollzeug. — 9) Hose.

sukari, mua, mayayi mabichi, mkate, na kulla kitu cha tamu. mwanzo wa ʿeisha[1]) hurembwa[2]) uso yule mwenyi pepo, humtona madoa madoa meusi na meupe na mekundu. marra huanza mwimbo wa kumchuchia[3]) yule pepo, apande juu ya kichwa. na watu wanapiga ngoma. na mwimbo wao wa kumchuchia:

„naomba yâ rabbi[1])
hê yâ rabbi
nifungua zangu pingu[2])
hê yâ rabbi.“

1) mein Gott. — 2) Fessel.

na watu huitikia, huimba labda mudda wa saʿa nzima. akipanda pepo, hujitingisha[4]) maungo mazima. marra yule mganga hutaranya, maʿana husema na yule pepo. na maneno hayo hajui mtu, illa yule mganga na mwele[5]) wake. fundi[6]) ataamru ngoma kupigwa sana. pepo marra atasimama kucheza. na watu wote waliwo wanachama[7]) wanacheza, na mshindo wa ngoma ukawapata, wengine wanaanguka kilingeni, wakenda majumbani kwao wagonjwa, wanataka kupungwa nao.

na mtu endaye kilingeni, adabu yake panapo kilinge, akiwa mganga ao mtu maʿarufu[8]) katika mji amekwenda kilingeni kutezama ngoma, hupewa mchele kikombeni kumwaga katika kilinge, maʿana ni heshma[9]) ya yule mganga, kama mfano wa kuamkiana. na kofia huvua, tenna hupewa kiti kukaa kitako.

na mudda wake hiyo ngoma siku sabaʿ. usiku na mchana kucheza. na yule pepo anapokuwa hodari[10]) kucheza, hupata tunza[11]) kwa watu, lakini tunza hizo si zake, mwenyewe mganga na wapiga ngoma na zumari.

1) Abendgebet. — 2) bemalen. — 3) locken. — 4) sich schütteln. — 5) Kranke. — 6) d. h. der mganga 7) die früher von dem mganga behandelt wurden. — 8) angesehen. — 9) Höflichkeit, Achtung. — 10) tüchtig. — 11) Geschenke.

sababu killa ajaye kutezama ngoma, huchukua mapesa, si lâzima kuchukua mapesa, illa mtu atakaye. killa ukapigwa mshindo wa ngoma, pepo akacheza, watu humweka mapesa juu ya kichwa.

ḥatta siku ya sitta ndio siku ya kutaja jina lake la yule pepo, ndio siku ya feḍeḥa[1]) kujulikana yeye pepo ao si pepo. maʿana hutaja jina la kijini[2]), hapana mtu alijuaye. akisha taja, watu hufuraḥi sana.

siku ya sabaʿ ndio ya ḳukomoa[3]). huchinshwa mbuzi pwani, hukusanyika na pepo wote kunywa damu ya yule mbuzi. na asiyokunywa damu hiyo — hana pepo. na wasiwo pepo kichwani, wakiona wenzao wanakunywa damu, wote pepo huwapanda kichwani. wakesha kunywa damu, pepo atabebwa, apelekwe nyumbani kwake, amekuwa mzima.

nao waanawake wa kisuaḥeli na wengine wa waanaume wanaṣadiqi[4]), ya kama kweli pepo yuko. mtu akiwa na pepo, lâzima kupungwa. na mwanamke akiwa mgonjwa, humwambia mumewe „nipunge.“ asipompunga — magomvi hayeshi nyumbani, na kulla siku kukonda. na waanaume wanajipunga wenyewe, wanapokuwa na pepo. wengine wanafanya upuuzi.

zamani moja naliugua mbavu na maungo yote. akaalikwa mganga kunifanyia dawa. akaniletea mivuke ya dungumaro siku sabaʿ, kesha akawambia wazee wangu — ya kama: „Mtoro amepatikana na dungumaro. sasa msimpe rukhṣa kula nyama ya kondoo, wala nyama iliyokaangwa na vitunguu.“ wazee wangu wakayaṣadiqi maneno yale. siku moja amesema: „sasa ḥali yake njema, lakini tumpunge, pepo apate kumtuliza.“ maneno yale ya mganga wakayaqirri wazee wangu. mwʿallimu wangu aliposikia maneno yale ya kutaka kupungwa, akanikataza, akanambia: „wewe huna ḥaya?

1) Enthüllung. — 2) Geistername. — 3) befreien. — 4) glauben.

utacheza katika uwanja, watu wote wakuone?“ nikatakhayyari[1]) kwa maneno yake, nikawajibu wazee — ya kama: „mimi sitaki kupungwa.“ mama yangu akafanya khofu ya kukataa kupungwa. na yule mganga aliposikia, akanipigia marufuqu[2]) kondoo nisile, akasema: „iwapo atakula kondoo — Mtoro atakufa.“

siku moja mwʿallimu wangu amealikwa karamu na mimi pamoja. na yule Mwʿarabu alichinsha kondoo. mwʿallimu akanambia: „hii nyama ya kondoo — utakula?“ nikamjibu „sijui.“ akanambia „ṯawákkali[3]) muungu, hakuna pepo, upuuzi.“ nikala nyama ya kondoo. nilipofika nyumbani, nikamwambia mama: „leo nimekula kondoo.“ moyo wake akasituka sana, akanambia: „sababu umekula kondoo, hutaki roḥo yako?“ bassi nikakaa yapata siku tano ao sitta — sikuumwa na kichwa wala mguu, na ḥatta leo nipo hapo Berlin.

1) das Gute wählen. — 2) verbieten. — 3) vertrauen.

ngoma za pepo.

pepo wa kinyamkera.

na katika namna za pepo namna nyingi. pepo wa kwanza kinyamkera, ndiye mkubwa wa pepo wote. na áṣili[1]) yake pepo wa kishenzi. wanaṣadiqi[2]) hukaa juu ya vilima. na anapomjia mtu, kwanza huwa mgonjwa, huwa na kichwa[3]), ao huwa na macho, ao huwa na tumbo. naye hupewa dawa za kichwa ao za macho ao za tumbo. zisipomfa'a dawa hizo, hupewa dawa za kinyamkera, ma'ana mafusho ya kinyamkera. na hayo mafushó ni majani ya mti yaliyokauka makavu. na kulla pepo ana mafusho namna yake, lakini áṣili yake yote ni majani. nayo hutiwa katika kigaye[4]) na moto, hufukizwa yule mgonjwa, moshi wake humwingia katika maungo ya yule mgonjwa. hayo ndiyo mafusho. akipona, ndipo anapojulikana, ya kwamba huyu alipatikana na pepo wa kinyamkera.

akisha pona, yule mume humwambia yule mganga — ya kama: „mshike shikio mwele[5]) wako, tuchume nguvu, mwakani tutampunga.“[6]) na yule mganga husema naye yule pepo, kumpa mudda ḥatta mwakani.

khabari ya kupungwa kwake kinyamkera: mganga anapotaka kupunga, huwalika wateja[7]) wake waanawake,

---

1) Ursprung. — 2) glauben. — 3) d. h. Kopfschmerzen. — 4) Scherben. — 5) Kranke. — 6) pepo austreiben. — 7) die früher wegen pepo in Behandlung waren.

hualika na wapiga ngoma — ya kama: „siku fulani nnapunga paḥali fulani, chukueni ngoma.“

na hao wateja ni waanawake, waliwokuwa na pepo zamani, wamefanyiwa dawa, pepo wametoka juu ya kichwa. lakini wanapokwenda kilingeni, ikapigwa ngoma, pepo huwapanda kichwani. ao akiwa nyumbani mwake, naye amtaka pepo wake aje, hujifukiza mafusho, hupanda juu ya kichwa, akiwa na neno — husema yule pepo, na watu waliopo husikia. anapomtoka yule pepo, watu humwambia „pepo wako amekuja leo, amesema jinsi [1]) każa wa każa“ [2]), sababu mwenyewe hajui.

na huyu mume hununua ʿada [3]) za kinyamkera — ndizi na mua na mayayi. ḥatta usiku hupelekwa yule mwanamke shamba, na wale wapiga ngoma wamekuwa ṭayyari. na ngoma za madogori ya kinyamkera — sabaʿ, maʿana virungura vitatu, huwekwa paḥali pamoja, hupigwa kwa fito nyembamba, na apigaye mtu mmoja. na ngoma ya nne ni dogori kubwa, na ya tano upatu, na ya sitta chapuo na ya sabaʿ chapuo, maʿana chapuo ni ngoma ya kubinda [4]). na wale wapiga wakiwa ṭayyari, na huyu mwenyi pepo kwanza hunyolewa kichwa, tenna hupakwa masizi [5]) kichwani, na uso wake hurembwa [6]) kwa ngeu [7]) na jasi [8]) na masizi, hurembwa matone matone uso wote.

na hapo panapo ngoma hizo, huwekwa gogo la mti, huchomwa moto, likawaka usiku kucha. na ikiwa mchana, gogo hilo huwapo vilevile, maʿana yake ule moto hukaangiwa zile ngoma. maʿana killa saʿa moja hupigwa mshindo [9]) moja, tenna hukaangwa zile ngoma, maʿana zimelegea, na wapiga ngoma wakiziqaribisha zile ngoma

---

1) Art. — 2) soundso. — 3) Geschenk. — 4) mit zwei Trommelfellen. — 5) Asche, Ruß. — 6) bemalen. — 7) rote Farbe. — 8) weiße Farbe. — 9) derselbe Trommelschlag.

panapo moto, huzidi kukazana. na zikapigwa, ṣauti[1]) yake husikiwa mbali.

tenna hucheza yule mgonjwa na watu wengine kwa mudda[2]) waliwopeana, ikiwa siku tatu ao saba'. naye mganga huimba katika nyimbo zake:

„mwari[1]) wê,
tumtwange kitututu.“[2])

1) mwenyi pepo gemeint. — 2) wir wollen dir tututu auf den Trommeln schlagen.

nao watu huitikia vilevile. na kulla saʿa hupigwa mshindo wa namna nyingine, hugeuza na nyimbo nyingine, kama mfano wa mwimbo huu:

„kinyamhunga[1])
baye gwe[2])
kinyamhunga.“

1) kizaramu-Name für kinyamkera; auch die folgenden Worte sind kizaramu. — 2) keiner wie du (d. h. der mich krank gemacht hat).

ḥatta magodori yanapokwisha, wakitaka kukomoa[3]), hufanyiza vikate sabaʿ vya mtama na vikate sitta vya majivu na vipande vya mua na mayayi na kuku mdogo na bisi ya mtama. tenna yule mgonjwa hushika kitunga kichwani kitupu, akenda mbio, ḥatta kunako komoo[4]) yake chini ya mbuyu. na watu humfuata, mganga na watu wengine, na vile vitu huvichukua. akifika — huanguka, hupiga kelele. mganga humshika kifua mwele wake, tenna mganga huimba mwimbo wa komoo:

„sengwa[1]) lawa.“[2])

1) Name für kinyamkera. — 2) toka.

na wale watu huitikia:

„sengwa lawa, ô lawa,
ô na lawe ô.“

1) Klang. — 2) Zeitraum — 3) befreien. — 4) Befreiung.

naye mgonjwa hupiga kelele kwa ṣauti kubwa, anapotaka kutoka yule pepo. akisha komoka yule pepo, yule kuku huchinshwa, na vile vikate vya mtama na vikate vya majivu huwekwa panapo njia panda[1]). na ile bisi humwagwa kidogo panapo njia panda, husema: „hiki ndicho chakula chao vinyamkera.“

khalafu yule mgonjwa humpeleka nyumbani. ḥatta aṣ-ṣubuḥi huoga maungo yake na uso wake, na yule mganga hupewa ujira[2]) wake qádiri[3]) ya riale ao riale u nuṣṣu, na wapiga ngoma hupewa wote pamoja riale.

pepo wa kilima.

na pepo wa pili jina lake kilima, ma'ana ya kwitwa kilima wanasema anatoka Kilimanjaro.

ikionekana mtu, amepatikana na pepo, nao hawajui pepo aliyo naye, hupewa dawa za kulla pepo. ile dawa inayomṭibu[4]), ndiyo wanayoṣadiqi pepo' aliye naye.

na mgonjwa akijulikana, ya kama ana pepo wa kilima, hupatana na mganga kutaka kumpunga. na mganga hualika waganga wenziwe na wapiga ngoma na mpiga zumari. tenna hujengwa banda la kilinge. na hilo banda hutandikwa majamvi chini, tenna huletwa kitanda cha kukalia wapiga ngoma. na ngoma huletwa chapuo mbili, moja ya kudunda[5]) na moja ya kugeukiza[6]), tenna na vumo moja, na upatu moja hutiwa juu ya chano, ma'ana ndipo unapokuwa na ṣauti kubwa. na mpiga zumari husimama juu ya ṣanduqu[7]) ao juu ya kinu.

wakiwa ṭayyari, huletwa mgonjwa. akifika, hufukizwa na mafusho, tenna yule mganga huimba mwimbo kumpandisha pepo kichwani:

---

1) Kreuzweg. — 2) Lohn. — 3) ungefähr. — 4) heilen, wirken. 5) auf einer Seite zu schlagen. — 6) auf zwei Seiten zu schlagen. — 7) Kiste.

„mtitimo mtitimo [1])
mtitimo ôya hê,
kilimanjaro ajapo
aja na mtitimo.“

1) von tetema, weil der pepo Zittern und Schüttelfrost mit sich bringt.

ao huimba:

„kiserere [1]) mguvu akija
mnyonge hondoka
ugeuke rumbi [2]) mwenda polepole,
hamjamba [3]) hê?“

1) Name für pepo. — 2) Schlange. — 3) amba sagen.

ao huimba:

„nimechoka kutwangia ndugu,
nipeni mchele niombe muungu.“

na wateja hushika mbugi [1]) mikononi, huitikia mwimbo, alioimba mganga. na yule mpiga zumari vilevile hufuata mwimbo katika zumari yake.

na mgonjwa anapojiwa na pepo kichwani, hufungwa kileso kifuani, hucheza. na wateja wengine wakijiwa, hufungwa nao vileso. na wanapocheza, mikononi hushika usinga [2]) na rungu [3]) mkononi. na ile rungu imetiwa njumu [4]) juu ya kichwa, ndio uzuri wa wale pepo wanapocheza. tenna hufungwa mbugi miguuni, na wakicheza hulia zile mbugi.

namna hii ndivo wanavocheza wenyi pepo siku tano. siku ya sitta ndio siku ya kutaja jina. nayo mganga humwambia mume — ya kama: „mkeo leo anataja jina pepo wake, tunataka ʻada zetu.“ hutoa riale kumpa mganga. hufanyizwa na mkate wa kumimina [5]), ku-

1) Schelle. — 2) Pferde- oder Ochsenschwanz. — 3) Knüttel. — 4) kleine Messingknöpfe. — 5) aus mchele, sukari, samli, iliki, kungumanga, mdalasini.

pambwa tenna kile chano na ndizi, na vipande vya miwa, na mayayi, na sukari. kikesha pambwa chano, yule pepo hupigwa kilemba cha bafta na bendera. na hicho kilemba huwa na pembe mbili, ni ʿalama[1]) ya kilemba cha shetani[2]). baʿada yake ile riale iliyotoka ya ʿada ya mganga, mganga humwamrisha kijumbe kuwajulisha watu — ya kwamba: „fulani ametoa ʿada riale mkewe kutaja jina leo.“ akisha sema maneno yale kijumbe, watu hupiga kigelegele[3]) cha furaha, tenna hupigwa ngoma wakacheza wote wateja. khalafu hukaa kitako juu ya viti, ndipo anapoulizwa yule pepo jina lake, na anakotoka — ya kama: „mimi fulani bin fulani“ — kwa maneno ya kipepo. na kilima alichotoka hutaja. watu wote hufurahi, anapotaja jina. na asipotaja jina, hulishwa panjo, maʿana huchanshwa ulimi kidogo, akapewa dawa jina lake panjo. tenna hutaja jina lake pepo. na asipotaja sasa pepo, watu husema: „fulani hana pepo, sababu hakutaja jina.“

hupiga tenna ngoma siku ile ya sitta mchana na usiku. hatta siku ya sabaʿ jioni huenda pwani kwenda kunywa mbuzi. wakifika, marra mbuzi huchinshwa, kikaletwa chano kukingwa[4]) damu ya mbuzi. tenna wale pepo hunywa ile damu, lakini kwanza hunywa yule mwenyi ngoma yake. naye yule pepo, akichinshwa yule mbuzi, hawezi kungoja hatta damu kukingwa katika chano, marra huanguka juu ya shingo ya mbuzi kunywa ile damu. na watu wakiona hivo, hufurahi sana, ndipo wanaposadiqi, kwamba ana pepo.

wakesha kunywa damu, mbuzi huchukua mganga, hugawana na wapiga ngoma na wapiga zumari. na mkate na vitu vingine vya chano hugawana mganga na

---

1) Zeichen. — 2) Teufel. — 3) Freudengeschrei. — 4) auffangen.

wapiga ngoma na mpiga zumari na wateja waliwo kilingeni, maʿana ni ʿada.

tenna hukaa pale kilingeni usiku kucha, ḥatta aṣṣubuḥi mgonjwa hupelekwa kwake. tenna mganga hupewa ḥaqqi yake kama walivopatana.

pepo wa dungumaro.

ikionekana mtu ana pepo wa dungumaro hupungwa. na kupungwa kwake hujengwa banda, ikiwa mjini ao shamba, na hilo banda hufungwa majamvi juu na chini, na majamvi mengine hutandikwa chini. huwekwa na viti, tenna huwekwa na vitanda na kinu kimoja. vitanda vya kukalia wapiga ngoma, na kinu husimama mpiga zumari. na banda huzindikwa[1]) kwa dawa, kuchelea waganga wengine wasije kuliroga[2]) lile banda, wakaugua wateja waliomo.

tenna huanzwa kupiga ngoma. na hiyo ngoma chapuo mbili, na dogori moja, na upatu. na zile chapuo mpigo wake hulia „utumbo wa paka[3]).“ na wanapoanza kucheza, mganga humchuchia[4]) pepo, maʿana kumwita aje kichwani, na chuchio zake ni nyimbo:

„hache[1]) lolo[2])
milongo yabinda[3]) — kaye[4]),
hache lolo
milongo yabinda kaye,
kutwaa mwana kumtambalisha[5]),
uchungu wangu hê,
hache lolo
milongo yabinda — kaye.“

1) acha. — 2) Name für pepo. — 3) siku zimekwisha. — 4) Stadt. — 5) krank machen.

1) Zauber legen. — 2) bezaubern. — 3) d. h. Trommelschlag als ob man sagt utúmbo wa páka. — 4) locken.

ao huimba:

„hache lolo, hê lolo,
hache lolo, hê lolo,
tate [1]) dungumalo
keza [2]) mkilalu [3])
ashebukwa [4]) na matindingala.“ [5])

1) Vater. — 2) iza kommen. — 3) kumtezama. — 4) amefuraḥi. — 5) Wasserblumen.

ao huimba:

„taileni [1]) tai [2]) nyiê [3]),
taileni waganga hê,
nipeni kishambo [4]) changu,
nimwelekee [5]) mwanangu.“

1) loben. — 2) Lob. — 3) ninyi. — 4) ubeleko Tuch, in dem kleine Kinder getragen werden. — 5) auf dem Rücken tragen.

ao huimba:

„wanimenya [1]), lelo wanimenya,
simbamwene mazi [2]) wanimenya,
tatu [3]) tumtatule [4]) tatu,
sholozi [5]) wanimenya,
kwetu kuna bene [6]) kulu [7]) lya mgu [8])
simbamwene mazi wanimenya,
tate [9]) — kaya [10]) — lya mgu.“

1) Klagelied des pepo; menya schlagen. — 2) Name, hier Schwur des Kranken. — 3) Name. — 4) wir wollen dem Kranken Beine geben, daß er gesund werde. — 5) Name für pepo-Kranken. — 6) Ziege. — 7) groß. — 8) wunderbar. — 9) Vater. — 10) Stadt.

na pepo akisha chuchiwa kwa nyimbo hizi, hupanda kichwani, tenna hupigwa ngoma na zumari akacheza. na wateja wengine humsa'idia [1]) kucheza naye. nao hufungwa vileso vifuani, na miguuni mbugi, na mkono wa kuume rungu, na mkono wa shoto usinga, na

1) helfen.

usoni mwake amerembwa wanja [1]). hucheza kama siku walizoagana. na kama hawana kitu, hucheza siku moja ao mbili, pasipo kutaja jina na kwenda pwani kunywa mbuzi. lakini hupewa ʿáhadi [2]) yule pepo — ya kwamba: „usimwuguze kiti [3]) chako, mwakani tutakupa ʿada yako mbuzi, na mumewe apate uchumi, maʿana ndiye atakayekupa mbuzi.“ tenna hukomolewa yule pepo, na mganga hupawa ʿada zake.

na iwapo pepo wa kunywa mbuzi, siku ya tano hufungwa bene, maʿana hutwaliwa mkeka mpya, ukatiwa mtama kidogo ndani, kisha hufungwa ule mkeka, huwekwa nyuma ya mgongo wa yule mgonjwa, ndiwo mto [4]) wake wa kuchegamia [5]) ḥatta siku ya kutaja jina.

na siku ya sitta pepo akitaka kutaja jina, hutiwa maji katika chungu na dawa, yanakwitwa maji ya ushombwe, huwekwa mbele ya mganga. tenna huja wale pepo mikono yao nyuma, hupiga magoti panapo lile jungu la ushombwe, tenna kunywa yale maji. tenna hupewa ʿada yake mganga riale, naye hujulisha watu ile riale — ya kwamba: „hii riale ya jina imetoka.“ watu wote hushangilia. tenna hupigwa mshindo wa ngoma kupigwa kilemba. na kilemba chake bafta na bendera na kaniki, nacho huwa na pembe mbili vilevile. ḥatta siku ya sabaʿ huenda pwani kunywa damu ya mbuzi.

pepo wa kigala.

na pepo wa kigala tafauti [6]) yake si kubwa na pepo wa dungumalo, illa kigala hupigwa kwa maṭari [7]), hapana ngoma wala zumari. na kifuani hufungwa vilevile kileso huyu mgonjwa na wateja. na mkononi hu-

1) das ist entweder Lampenruß oder schwarz gebrannter mchele gerieben, mit Sesamöl angefeuchtet und noch einmal auf dem Feuer geröstet. — 2) versprechen. — 3) d. h. der Kranke selbst. — 4) Kissen. — 5) anlehnen. — 6) Unterschied. — 7) kleine Handtrommel, Tamburin.

shika shoka ao mkuki na usinga yule mgonjwa. na ile shoka imetiwa njumu, na mkuki hufungwa udodi. naye pepo huchuchiwa vilevile kwa nyimbo:

„allâhu yâ mûle[1]) wa maûle[1])
akulaye nawe mle wa maûle.“ [2])

1) mola. — 2) wer dir Böses tut, dem tue wieder Böses.

ao huimba:

„yâ maûlâna[1]), shela[2]),
yâ maûlâna!
kama u mganga[3])
inama uokote pembe ya ñgombe.“

1) o unser Herr. — 2) shei 'll 'llâh nichts außer Gott. — 3) zum pepo gesagt.

ao huimba:

„njema njema ya mchana njema,
nipeni kibao nikae kitako,
njema njema ya mchana njema.“

ḥatta siku ya sitta hutaja jina vilevile, na siku ya saba' huenenda pwani kunywa damu ya mbuzi.

pepo wa shamñgombe.

kujulikana kwake mtu ana pepo shamñgombe, — hujulikana ba'ada ya kufanyiziwa dawa ya shamñgombe, akapona, ndipo anapojulikana kwa zile dawa zilizomponya. tenna yule mganga humwambia; „wewe una pepo wa shamñgombe, nyama ya ñgombe usile.“ tenna watu hujua, akenda maḥali, kimefanyizwa chakula kwa nyama ya ñgombe — hali, watu hujua, ya kama huyu ana shamñgombe. pepo wa dungumaro hukatazwa nyama ya kondoo, pepo wa kinyamkera hukatazwa vyakula vipya billa ya mavumba.

na kupungwa kwake pepo wa shamñgombe hupungwa kama pepo tuliwowataja. mwanzo wake hupigwa na

ngoma, chapuo mbili na vumi moja na upatu na zumari, vilevile kama ngoma ya dungumaro. watu husema dungumaro na shamñgombe jama'a moja wanakotoka.

na mgonjwa akichuchiwa, huimba:

„bwana Kisiki [1]) na bwana Manoru [2])
nimechoka kutwangia ndugu [3]),
nipeni mchele, niombe muungu
nimechoka kutwangia ndugu."

1) und 2) der pepo shamñgombe gemeint. — 3) für den Freund zu bitten.

mudda wa siku tano hutaja jina, siku ya saba' hupelekwa pwani kunywa mbuzi.

na mambo wafanyayo kama tuliyotangulia kuyasema mbele.

pepo wa lewa.

pepo wa lewa kupungwa kwake hujengwa banda, hutandikwa majamvi juu na chini. tenna huzindikwa lile banda, na kuzindikwa kwake hufukizwa dawa lile banda kulla pembe hatta pembe nne zishe. na vilevile kama wakicheza katika jumba, namo wamejenga banda, hulizindika. killa ngoma ya pepo banda ao nyumba kwanza huzindikwa kwa dawa ya mafusho, ma'ana majani ya mti. na sababu ya kuzindikwa, wanachelea waganga wengine wasije kuliroga lile banda, wateja wakaugua. ma'ana waganga wengine, wakimwona mwenzao anapunga, wao huwa na kijicho [1]), sababu atapata fedda.

na kuchezwa kwake huletwa ngoma tatu, moja chapuo ya „utúmbo wa páka," na moja ya kugeukiza, na mrungura moja, na mpiga zumari.

na kuchezwa kwake huchezwa kwa fimbo. akijiwa

1) eifersüchtig sein.

mgonjwa, hufungwa nguo kiunoni, kuziwiwa nguo alizovaa zisimvuke. akapewa fimbo yule mgonjwa, na mwanamme moja hushika fimbo, wakazunguka pamoja. khalafu hugongana kwa zile fimbo marra moja, wakazunguka tenna kucheza. killa marra wanafanya kama hivo, ndio machezo yao. na mwanamume moja akichoka kucheza na yule pepo, huja mwanamume mwingine ao mwanamke kucheza naye.

na mwimbo wake mganga huimba:

1. hala hala[1]) mtelehi[2])!
   mbuzi yuno[3]) ni mkulu[4]) mno
   hala hala mtelehi!
   mkeza[5]) kutinda[6]) mwikeni[7]) mwanangu
   hala hala mtelehi!
2. hala hala mtelehi!
   mkate uno[5]) ni mkulu mno
   hala hala mtelehi!
   mkeza kukata mwikeni mwanangu
   hala hala mtelehi!"

1) allah allah, in der pepo-Sprache hala. — 2) Name des Sohnes des pepo-Kranken. — 3) huyu. — 4) mkubwa. — 5) mkija. — 6) kuchinsha. — 7) mpeni. — 8) huu.

ao huimba:

„nna ńdia[1]), sija[2]) kunde
haja[3]) kunde, msusi[4]) navuata[5]),
nna ńdia, sija kunde."

1) nda Bauch. — 2) sili ich esse nicht. — 3) nikila. — 4) mchuzi. — 5) nakunywa.

ásili ya mwimbo huu wa kizigua.

ao huimba:

„Majumaᶜ kaolewa
tutafune mpunga wa lewa."

nao hucheza siku tano ao sabaᶜ. na siku ya komoo

hupelekwa mgonjwa chini ya mti wakamkomoa. na komoo yake hupikwa kande ya muhindi, na nazi huvunja, wakatafuna pamoja na mahindi wote waliopo. tenna mgonjwa hupelekwa nyumbani kwake. katika ngoma hii haina desturi ya kuchinshwa mbuzi.

pepo wa ṭâri.

kupungwa kwake hupungwa kwa maṭâri bassi. na chuchiwa zake huchuchiwa kwa vipokeo vya maulidi, kama mfano wa pepo wa kigala:

„allâhu yâ mûle wa maûle.“ [1])

ao huimha:

„yâ maûlâna shela
yâ maûlâna.“ [1])

na mgonjwa akicheza, mkononi mwake hushika upanga, na mno hutafuna tambuu [2]). na maji yake anayokunywa — huandikiwa kombe kwa ṣaḥani [3]) nyeupe, na hilo kombe huandikwa na zaʿafrani [4]), huoshwa kwa marashi [5]). na anapojiwa, hupiga ukelele, husema kwa ṣauti [6]) kubwa:

„salâmu ʿaleikum.“

na watu huitikia:

„ʿaleikum salâm.“

tenna huwapa mikono watu, husimama akacheza.

naye hupigwa kilemba cheupe, na juu ya kilemba huchomeka [7]) mayungiyungi [8]) na mkadi [9]) kutaka ʿarufu [10]) nzuri.

hucheza kama siku walizoagana. na juu ya chano chake huwekwa vitu vizuri kama mfano wa mkate na mayayi na ḥalwa [11]), sukari ya mawe, ndizi, miwa,

---

1) siehe Uebersetzung. — 2) Betel. — 3) Teller. — 4) Safran. — 5) Rosenwasser. — 6) Stimme. — 7) eingesteckt werden. — 8) Wasserrosen. — 9) Pandane. — 10) Geruch. — 11) süße Speise.

kungumanga[1]), ʿiliki[2]), mdalasini[3]), na tambuu. na yeye mgonjwa hula sana tambuu, na hiyo tambuu hutiwa vyungo kama kungumanga na ʿiliki na mdalasini. na chakula anachokula ni ḥalwa na mayayi, na vitu vingine hula waliopo kilingeni.

ḥatta siku walizoagana zikesha, hutaja jina, kisha akakomolewa. naye huchinshiwa njiwa. na wengine huchinsha mbuzi, lakini karamu yake kubwa — njiwa.

na anapopelekwa pwani kukomolewa, hufanyiziwa dau la mkarara wa mnazi ao la mwale. dau hilo hutiwa tanga na mlingoti, wakatia na vyakula ndizi, mua kidogo, sukari kidogo, na kipande cha mkate. baʿada ya kwisha kumkomoa yule pepo, huliwacha baḥarini lile dau, maʿana wanamsafirisha anakotoka yule pepo baḥarini.

pepo wa qiṭimîri.

pepo wa qiṭimîri na pepo wa ṭâri ni pepo wa kiʿarabu. watu wanaṣadiqi pepo hao wanatoka baḥarini. na pepo hao wa kisuaḥeli watu wanaṣadiqi wanatoka barra juu ya vilima ao juu ya miti, iliyo mikubwa, mfano wa mibuyu.

na pepo wa qiṭimîri anapoanza mganga kutaka kupunga, kwanza huvuta ubao, akatczamia siku njema ya kupunga. na huo ubao hupiga ramli[4]), maʿana huchorachora[5]) mwanzo wa ubao ḥatta kati ya ubao. tenna huandika makoo[6]),· kuzalisha ile ramli, na ndani ya makoo haya manne huandikwa ḥesabu[7]). tenna hujua yule mganga siku njema ya kufanyia ngoma yake na siku mbaya.

na hiyo ngoma huchezwa ndani ya nyumba, nayo

---

1) Muskatnuß. — 2) Kardamom. — 3) Zimt. — 4) Zauber. — 5) kleine Striche (wie Komma) machen. — 6) rundliche Figuren. — 7) Zahl.

nyumba imezindikwa kwa dawa. na ngoma zake ni mbili, moja ngoma ya kugeukiza na vumi moja, na tenna upatu na mpiga zumari. na mchezo wake ni namna nyingine kuliko machezo tuliyoyataja. machezo yake huenda kimbelembele hurudi kinyumenyume, naye mgonjwa akichoka, hukaa juu ya kiti. na desturi ya qiṭimîri kidogo mbali kuliko ngoma nyingine, lakini siku ya saba' hunywa mbuzi vilevile.

pepo wa pungwa.

ngoma hii huchezwa sana Kilwa na Unguja. na mchezo wake huchezewa ugani. nayo haina zumari, illa chapuo mbili na vumi moja na debe. na hapo uwanjani hutandikwa jamvi, waanawake hukaa kitako, mganga huimba nyimbo na waanawake huitikia. na nyimbo zake:

„utikiti wê na utango[1])
na utambaye[2]), mrima una mambo.
kwenda kuni na maji
kero hilo la mume."

1) ufitina na u'adwi. — 2) sich ausbreiten.

ao huimba:

„pita huko wê, nipite huku wê[1]).
tukasimamepi?[2]) ku msagawi[3])
nimwene[4]) ngwese[5]) kajinamia
angojea ninga[6]) za ku dari."[7])

1) Mann und Frau kommen so überein. — 2) tutasimama (kutana) wapi. — 3) Ort. — 4) nimeona. — 5) paka. — 6) Mäuse. — 7) Dach.

ao huimba:

„kuna maganga meupe
mengine matiriyanga[1]).

1) Sinn: Es giebt Männer, die Mitleid mit der Frau haben, andere nicht.

tumbueni [1]) mbolembole [2]),
ndui ngazina uganga
kero hili la mume.“

1) zu ergänzen ndui. — 2) polepole.

ao huimba:
„za lipi [1]) wê
zikalilima za mwamba [2]) hê ?
Billali [3]) wê
utakufa na jambia.“

1) ziko wapi pepo. — 2) zilizovuma katika mwamba. — 3) Name eines Mannes; zu ergänzen hier tulizana.

ao huimba:
„kilingondo [1]) kilingondo kilawa [2]) Malimba [3])
mwana mwari wakukana ? [4])
na kitu ulile [5]) wê Mashamanda ?“ [6])

1) vita d. h. der Mann. — 2) lawa = toka. — 3) Ort. — 4) unakataa. — 5) umekula. — 6) Name der mwari.

ao huimba:
„mwita [1]) kimya usambe [2]) ninyamaa,
wana mama mwasusia [3]) imwe [4]),
uzingwi [5]) umenizingia.“ [6])

1) ita machen. — 2) glaube nicht. — 3) ihr tut mir weh. — 4) ihr (ninyi). — 5) Verdrehung. — 6) zinga drehen.

na mgonjwa anapojiwa, huinuka akacheza. na mchezo wake upande moja waanawaume, upande moja waanawake. na komoo yake siku ya saba' huenenda baḥarini, wakajitosa pamoja na mgonjwa. tenna hurejeshwa mgonjwa nyumbani.

pepo wa mkasia.

na ngoma ya mkasia huchezwa sana Unguja kwa Waḥadimu na Watumbatu. na kuchezwa kwake hu-

chimbwa shimo uwanjani, ukasimamishwa mti, na ule mti huziwiwa na mawe usianguke. nao ule mti hufungwa kamba kumi na mbili. na zile kamba huzishika wale wachezao kuzivuta na kuzunguka duwara, nao wamepiga magoti[1]), na mganga wao huwimbia mwimbo:

„na makasia tieni
na makasia
tanga likiwa mtini[1])
na makasia tieni.“

1) d. h. pepo likiwa kichwani.

ao huimba:

1. muundao vyombo
mtie na pondo,
na makasia wê,
na makasia wê hê.
hamjamba[1]) wê?
2. mwamba wa Kitame[2])
uvundao vyombo
na makasia wê
na makasia wê.
hamjamba wê?
3. tambale[3]) tamba[4])
nifike mwamba wa Kitame
na makasia wê
na makasia wê.
tangu jana wê.“

1) hamjasema d. h. habt ihr euch noch nicht geärgert? (ich nicht). — 2) Ort. — 3) nitambae. — 4) langsam.

ao huimba:

„Mwana Makame ufilepi[1]) mai?“[2])
nifile[3]) Malindi mtoni Singwaya,

1) umefia wapi. — 2) maji. — 3) nimefia.

1) knieen.

mtoni Singwaya, mtoni Singwaya,
nifile Malindi mtoni Singwaya."

ao huimba:

„yanakuelea wê ḥabâbe [1]),
magome yanakuelea
kapewa mti kushika [2])
magome yanakuelea."

1) Geliebter. — 2) nämlich der Hüter.

ao huimba:

„walindao wê ḥabâbe
tuwaole [1]) walindao,
wapewa mti kulinda,
tuwaole walindao."

1) ola = tazama.

ao huimba:

„ondoka ukaṣali,
kuṣali si kuṣali,
ukatia nguo maji [1])
kushongo ukali." [2])
„nilelee mwanangu [3])
mkasia hoya."

1) du hast nur die Kleider ins Wasser gesteckt, anstatt die richtige religiöse Waschung vorzunehmen. — 2) das ist der reine Unsinn. — 3) sagt der Kranke zum pepo, damit das Kind nicht krank werde.

na ngoma ya mkasia haina zumari wala ngoma, illa huimba nyimbo, wakaitikia watu. wala siku ya komoo haina mbuzi. hupika kande za muhindi na nazi kutafuna, ndio chakula chao. na ngoma hii huisha siku moja. saʿa ya nne ya usiku hukomolewa. na kukomolewa kwake hushikwa na mganga kifua chake yule mgonjwa, akamchua [1]) mkono wake wa kuume,

1) pressen, quetschen.

tenna yule pepo humtoka. na namna hiyo hukomolewa hufanyizwa killa pepo tuliwowataja kama hivi, hufanyizwa ba'ada ya kunywa damu ya mbuzi.

pepo wa kizungu.

pepo huyu watu huṣadiqi anatoka baḥarini Ulaya. na ngoma yake hupigwa chapuo moja na vumi na zumari na upatu. na mganga anapomchuchia, huimba mwimbo :

nna mambo meupe [1]) wê,
nna mambo meupe,
mkikaa barazani waanaume,
mwasengenya [2]) waanawake,
mmeziwia vyenu [3]) kina bana,
mwataka vyetu tuwape."

1) hell, hellschend. — 2) verächtlich reden. — 3) vitu vyenu nämlich Geld.

naye mgonjwa na wateja hucheza kama siku walizoagana. na chakula ni mkate wa bisi na biskuti [1]) na yayi na dafu na embe na machungwa na ndizi. akila vyakula hivo, hufuraḥi yule pepo. ḥatta siku ya kutaja jina hukomolewa yule, naye hanywi damu ya mbuzi, illa hushikwa kifua na mkono, akaja mganga kumkomoa, pepo hutoka akenda zake.

1) Biskuit.

kazi za waanawake.

kazi katika nyumba.

waanawake majumbani wanapika, na chakula kikesha humwandikia mumewe. na kuosha vyombo vya nyumba, na nguo zake mwenyewe kufua, na nguo za mumewe huzifua, na nyumba yake kuifyagia, na kisimani kwenda kuteka maji kama hana mtumwa. na usiku kumtandikia mumewe kitanda, na kumsinga na kumpaka mafuta miguuni, na kumpapasa hatta alale. na mchana akisha kula, hutwaa chanzo cha ukili kusuka mkeka.

wengine hufanya vitumbua. ao kufanya ladu [1]), humpa mtoto kwenda kuuza. ao huchansha kuni kuweka mafungu kuza. wengine wanauza unga wa mhogo na wa mtama, na wengine wananunua samaki wabichi, wakawakaanga kwa mafuta ya uto [2]) na pilipili hoho [3]), wanauza moja pesa, wakiwa ghali — moja pesa mbili ao tatu.

na wengine wanapika pombe. pombe wanapotaka kupika, wanatwanga muhogo, kisha huchunga [4]) unga, khalafu huroweka [5]) mtama mudda wa siku saba'. khalafu huutwanga, tenna hupika ule unga wa mhogo siku mbili, khalafu yake hutoa kimea cha mtama, wakachanganya pamoja na ule unga wa mhogo, hu-

---

1) runde Pfefferkuchen. — 2) Sesamöl. — 3) roter Pfeffer. — 4) sieben. — 5) mit Wasser angefeuchtet sein.

pikwa marra ya pili siku moja. khalafu huwacha, ikapoa ile pombe, tenna huichuja [1]) kuitoa makapi.

na togwa kaẓàlika kama inavopikwa pombe, lakini muhogo si mwingi. sana hupikwa kwa mtama tu, ndipo linapokuwa zuri.

Mnyamwezi anaposhuka, anapenda kunywa pombe sana. wanapata matumizi waanawake katika hiyo pombe, sababu wanauzo kibaba pesa. na Wasuaḥeli wengine wanakunywa pombe.

na wengine wanauza tembo kali na tamu, lakini tamu si mno kutoka. waanawake wanapatana na Wasegeju, wanaogema tembo katika minazi. killa siku mwanamke huenda kwa mgema, kutwaa mtungi wa tembo, kuleta mjini kuuza. wengine wanauza mashamba, sababu walewi wengi kuliko mjini, ma'ana mashamba wakilewa, wanafanya kelele nyingi kwimba na kucheza, mjini hawana rukhṣa.

nao hao walewi wana nyimbo zao wanazokwimba wanapiga kinanda, wakaimba mwimbo huu:

„teremkia [1]) njia ya Kizingo [2])
ulikute zoga [3]) lenyi pengo,
ulikate vinyango vinyango,
ulitie jungu lenyi pengo.
mpikaji sharṭi mwenyi chongo
na mlaji mwenyi kibiongo.
haya — mambo [4]) Maua.“ [5])

1) hinuntergehen. — 2) Ort. — 3) Aas. — 4) das sind Sachen d. h. gute Getränke. — 5) Name der pombe-Verkäuferin. Sinn des Ganzen vgl. Uebersetzung.

ao huimba:

„'Abdallah mtoto alia,
mamaye amejizalia,

1) durchseihen.

kiunoni kafungwa jambia
thamanie riale mia,
hakumbuka mzuri [1]) — nalia.“

1) nämlich die Mutter des ʿAbdallah.

ao huimba:

„adunda [1]) adunda, mchawi adunda,
mchawi adunda, mchawi adunda,
kitumbaku dawa.“

1) dunda eigentlich „mit dem Stampfer stoßen,“ hier „zaubern“ gemeint.

turejee kwa wagema wa tembo. na hao Wasegeju wakiamka, hupanda juu ya mnazi, lakini ukope hawezi kufunua, tembo limechelewa kichwani, marra nyingi Wasegeju huanguka juu ya mnazi kwa ulewi, sababu wanalewa kama chozi [1]).

namna ya kusukana nywele.

mwanamke anapokwisha siku zake kutoka katika miezi, ao anataka kusukwa nywele nyingine, hufunua nywele zake, akazitana kwa shanua [2]), tenna huziosha kwa maji ya moto, ḥatta taka zote zitoke. tenna hutia mafuta ya kufukiza ndani ya kikombe, huenda kwa msusi [3]), humwambia: „nimekuja kwako shoga, nataka unisuke nywele zangu.“ msusi humwuliza: „wataka nywele gani? mardufu [4]) ao za kufundika [4]) ao nywele nyembamba?“ [4]) atamjibu namna ya nywele azitakazo. kisha atakaa juu ya kiti msusi, naye anayesukwa chini, anamsuka na kuzungumza. kuzungumza kwao huzungumza khabari zote za katika mji. mazun-

1) Vogel, der gern Palmwein trinkt. — 2) großer hölzerner Kamm. — 3) Haarflechterin. — 4) verschiedene Haartrachten.

gumzo yao hayaeshi ḥatta nywele zishe. ao huimba mwimbo:

„Sitaḥamili wê wiwu wache,
mwanamume ku mgongo kama kenge?“
ao huimba:
„tuli wawili tukipendana,
na moyo kama mtana[1]), utaniua kijana.“[2])

1) mchana. — 2) wenn du eine andere lieben wolltest.

ao huimba:
„ndizi kisukari[1]) zinauzwa ghali,
limenipotea yayi la johali.“[2])

1) d. h. guter hübscher Mann. — 2) johali Edelstein, Juwel; gemeint ist der Mann, den sie verloren hat.

ao huimba:
„kwetu imekuja khaṭṭi
yatoka bendari Nuri
bwana Saleḥe na Ḥamadi
wamezidi kwa uzuri.“

khabari ya kusugua meno.

meno yao wanasugua na mswaki[1]). na miswaki yao ni tawi la mti ao mzizi wa mti, jina lake mswaki. nao hukata kipande kidogo cha mti, wakakitafuna katika ncha, huwa kama mfano wa brashi[2]), nayo huwa na ńchańcha[3]) zinazochomachoma katika meno kuyaṣafisha.

na iwapo mtu meno yake hayatakati, yameḥaribika kwa tambuu, ao ndilo umbo lake, hayana takaso, huchoma maganda ya popoo, kisha huyasaga, makaa yake

1) Hölzchen des mswaki-Baumes, die als Zahnbürste benutzt werden. — 2) engl. brush. — 3) Spitzchen.

ndiyo anayosugulia meno. ao hutwaa makaa ya moto, akayasaga, maivu yake ndiyo anayosugulia meno ḥatta yatakate.

uzuri wa waanawake.

siku anayaqusudia kufanyiza uzuri, humwambia mumewe ao mwanamume wake — ya kama: „nataka mapesa kutumia.“ humpa rupia moja ao rupia u thumni. marra atanunua mafuta ya kufukiza, kisha atakwenda kwa msusi, akamsuke nywele zilizo nzuri, atampa ususi wake pesa ʿasherîni ao nuṣṣ rupia. kisha atanunua ʿûdi[1]) na marashi[2]) na ṭibu[3]) na dalia[4]) na jamieʿi ya manukato, ataingia chumbani, amwite shoga yake, amsinge maungo mazima. kisha atatia moto katika chetezo, atie na ʿûdi katika moto, avae mavazi mengine, tenna atajifukiza. kisha ajimwagie marashi. na kama kuna yasmini nje — atanunua, amwagie juu ya kitanda, nyingine azitunge atie juu ya mkufu. marra atatwaa tunda[5]) zake, atunge nyingine avae kiunoni.

kaẓâlika manukato aliyonunua, usiku wanapotaka kulala, hupika maji ya moto, mumewe akipanda kitandani, sherṭi amshike miguu kwa maji ya moto, maʿana kumwosha miguu, kumpangusa vumbi la mchana. akisha mwosha, humpaka mafuta.

na desturi ya mwanamke anapomshika mume miguu, sherṭi amwamkie, husema „shikamô,“ ndipo amshike. naye mume hutikia „marhaba.“ humwuliza: „wataka nikusinge?“ akiqubali, atatia ṭibu katika kikombe, na maji katika bakuli, marra atamsinga mumewe, ḥatta mwili wote ukesha.

---

1) Aloeholz. — 2) Rosenwasser. — 3) aromatische Salbe. — 4) Pulver, das durch Zerreiben von Stückchen des mdalia-Baumes gewonnen wird. — 5) Hüftenperlschnur.

khabari za manukato.

manukato makubwa ni ʿûdi. na huo ʿûdi kijiti cha mti, chatoka barra ya Maskati, kinapikwa na sukari na mafuta mazuri. hujifukiza watu katika mrima, khaṣṣa waanawake. mwanamke akitaka kutembea, baʿada ya kosha nywele zake, hujifukiza, akesha huvaa nguo nyingine. na akinuka ʿûdi, mwanamume hufuraḥi.

nukato la pili uvumba. nao uvumba mchanga, watoka barra el-Hindi na barra ya ʿArabu. nao hupikwa na manukato mengine. matumizi yake, mtu akiwa na ḥoma, ao amepigwa na mvua, anaona baridi, hujifukiza uvumba, baridi ao ḥoma humtoka.

nukato la tatu ṭibu. na hiyo ṭibu mna manukato mengi. kwanza kipande cha mti, jina lake ṣandali[1]), husagwa juu ya jiwe, linakwitwa jiwe manga. husaga hiyo ṣandali, ḥatta ikawa leini. huchanganya pamoja na maua maulidi[2]) na qarafuu[3]). tenna hutia ndani ya kikombe akaanika. manukato hayo ya kusingana usiku.

kaẓâlika manukato mengine miski[4]) na zaʿafarâni[5]), hutumika maḥali pamoja.

nukato la riḥani[6]) manfaʿa yake kikuba[7]). hutungwa hicho kikuba riḥani na mkadi[8]), hufunga mwanamke juu ya mkufu kunukiza. na wengine huuza vikuba, waanawake hununua.

nukato la yasmini manfaʿa yake hutiwa katika nguo, ao humwagwa katika kitanda, ao hutunga shadda[9]) la yasmini kumnukiza ampendaye.

mafuta ḥalʿûdi — hayo ni bora ya manukato kuliko yote tuliyotaja. mwanamke mrembo[10]) hutumia katika nguo zake. kaẓâlika ḥalwardi[11]) na ḥaliyasmin[12])

1) Sandelholz. — 2) Rosenknospen. — 3) Nelken. — 4) Moschus. — 5) Safran. — 6) Basiliumkraut. — 7) Blumensträußchen. — 8) Pandane. — 9) Strauß. — 10) die sich gern schmückt. — 11) Rosenöl. — 12) Jasminöl.

na ḥalṣṭambûl[1]) na ḥalṣandal[2]) yote hutimiwa katika nguo.

kaẓâlika marashi na ʿûdi hutumika katika ḥalbadri, maʿana mtu akipotelewa na kitu, huenda kwa mwʿallimu kutaka ḥalbadri ya kuonekana kitu chake. ikesha soma ḥalbadri, marashi humwagiwa watu na ʿûdi kufukizwa. ao hutumika yale marashi katika hʿarusi. kaẓâlika katika uzishi hutumika marashi na ʿûdi. baʿada ya kushona sanda, hufukizwa ile sanda, ikamwagiwa marashi. yaliyosalia — humwagiwa watu walio barazani.

kazi ya mkeka.

áṣili ya mkeka watu wanakata ukindu[3]) kokoni[4]), na huo ukindu mti, una majani kama makuti ya mtende. hayo makuti huanikwa, yakikauka, huleta mjini kuuza, kicha[5]) kimoja pesa. na mwingine hupakiwa Unguja ao mrima mwingine. waanawake wakiupata, huuchana chane[6]) nyembamba, kesha husuka ukili[7]) namna mbili — mweusi na mweupe. na huo mkeka namna mbili nao, kuna mkeka mweupe na mkeka wa kazi. mkeka mweupe ndiwo unawoshonewa sanda, mtu akifa, na mkeka wa kazi ndio wa kulalia, ao hutandika vyumbani, ao hupelekwa miskitini.

kaẓâlika huo mkeka wa kazi áṣili yake ukindu, hupika waanawake kwa rangi. na rangi yake mdaa. na mdaa mti wa mwitu, mizizi yake meusi. watu wa mashamba huchimba, wakaleta mjini kuuza. waanawake hununua kicha pesa. wakesha pika ukindu, hugeuka, ukawa mweusi kwa ile rangi ya mdaa.

rangi ya pili ukindu hurowekwa katika maji, ika-

---

1) türkisches Oel. — 2) Sandelöl. — 3) Blätter der Phönixpalme. — 4) im Busch. — 5) Bündel. — 6) Streifen. — 7) Mattenstreifen.

tiwa shabbu[1]) na ukindu pamoja. mudda wa siku nne ukindu hugeuka, nuṣṣu mweupe nuṣṣu manjano.

rangi ya tatu fuwa[2]), wanauza Wahindi, umbo lake mizizi midogo midogo. nao hupikwa upindu na hiyo fuwa pamoja, hugeuka upindu, ukawa rangi ya fuwa.

rangi ya nne mkumbi[3]). na huo mkumbi magome ya mti rangi yake manjano. nao hupikwa na ukingu.

mwanamke akitaka kusuka chanzo[4]), kwanza husuka ukili mweupe pima thalathini, kisha husuka mweusi pima thalathini, tenna husuka ukili wa kazi. na ukili wa kazi chanzo chake hukusanya namna ya ukindu alivopika — mweusi, mwekundu, manjano — hushika mkono moja, akapanga chanzo akitakacho. tenna hufikiri mwenyewe „nitasuka mwezi ao nyota ao kanga.“

kaẓälika na kazi ya kili majina yake mengi sana. iko kazi jina lake qarafuu, sababu rangi yake kama qarafuu. aiḍa iko kazi jina lake gongo, sababu nyekundu imechangamana na kimanjano. yuko ndege jina lake gongo, ndiye mwenyi rangi hii. iko kazi nyingine kito cha pete, maʿana kama kito cha pete. ao ndege, maʿana kama manyoya ya ndege yoyote. ao nzi, mfano wa inzi. ao dema, maʿana ndani ya ukili mna tundutundu kama ndani ya dema ya kuvulia samaki. ao puleki nyekundu, mfano kama uzuri wa zari wa waanawake wa Wahindi, wanowotia katika nguo zao. ao koja la mbe, maʿana hufanyiza vidongevidonge. namna za kili nyingi sana. nyingine huitwa bomba ao upeto, ao maḥaba, ao timbi, ao marjani, ao barrabarra, ao mboni, ao mjusi.

na kulla ukili pimà ʿesherîn. kesha hukusanya

---

1) Alaun. — 2) Färberröte rubia tinctorum. — 3) Kopalbaum. — 4) Anfang der Matte.

mweupe na mweusi — hushona pamoja. kesha hushona mweusi na mwekundu. tenna hutia katika cheo, akashona, ḥatta mkeka ujae. na ukesha, hukata mapande, tenna huupinda, umekwisha mkeka.

na mṣala[1]) namna yake kama hivo, illa unashonwa duwara[2]).

jamvi áṣili yake muyaa[3]). watu hukata muyaa, wakaanika. ukikauka, huchana chane, akasuka bambo[4]), likatimia pima khamsini, huanza jamvi kushona ndani ya cheo, ḥatta likajaa hulipinda. namna yake moja tu.

na matumizi yake pakiwa na h'arusi, ao amekufa mtu, hutandikwa jamvi lililo kubwa, na juu yake huwekwa mikeka, watu wakakaa juu ya mikeka.

---

1) Gebetsmatte. — 2) rund. — 3) Dumpalme. — 4) Streifen.

kazi ya waanaume.

khabari ya uchuuzi[1]) wao Wasuaḥeli.

bi'ashara[2]) zao — kuna watu wengine wazito wa kusafiri barra. ajapotokea tâjiri[3]) kumwambia „nitakupa biḍa'a[4]), uende ukachume“ — hataki. watu hao bi'ashara zao wanachuuza mjini, wanauza vitu vya rejareja[5]). wananunua nazi, na mahindi, na miwa, njugu, vyazi, muhogo mkavu na mbichi, machungwa, ndizi, mafenesi, na vitu vingine, bassi huweka fungufungu, wakauza tangu fungu la pesa moja ḥatta pesa 'esherini. nao hawapati kitu ndani yake, illa matumizi yake na mkewe. apate mapesa ya mafuta na tambuu, yanamtosha matumizi hayo.

sababu mwanamke katika nyumba, ikawa kiza, wala tambuu hana katika jelba yake, huqaṣirika. na kiza husema: „leo tutalala kama madudu?“ sababu Wasuaḥeli hulala usiku kucha na taa, na khofu yao wanaogopa usiku kutokea nyoka, ao kuumwa na tandu[6]), ao nge[7]).

kaẓâlika mtu akimwambia „sababu nini wewe husafiri,“ hujibu: „mimi sitaki kuwa tâjiri, nataka chungu meko, tâjiri atakufa na mkiwa[8]) atakufa, sote[9])

---

1) Kleinhandel. — 2) Handel. — 3) Kaufmann. — 4) Waren. — 5) stückweise. — 6) Hundertfuß. — 7) Skorpion. — 8) Armer. — 9) sisi zu ergänzen.

sawasawa. ya nini kwenda barra kusumbua roho yangu katika nyika? na kulla khatari[1]) juu yangu! mali ya watu yakipotea — nipate ta'abu[2]), ao roho yangu ipotee. nimekhiyari[3]) kula muhogo wa kuchoma na roho yangu imeshuka."

kazâlika wachuuzi wengine hungoja Wanyamwezi, wanaposhuka na ñgombe na mbuzi. hao kazi zao hununua ñgombe kwa Wanyamwezi, nao huuza kwa Wahindi ao Washihiri. na kama hawana themani ñgombe, huwachinsha, wakauza nyama. nyingine huchoma mshkaki[4]), mshkaki moja pesa.

na wasio fedda ya kununua ñgombe kufanyiza bi'ashara, hupatana na Wahindi ao Washihiri. mapatano yao husema: „wewe tafuta ñgombe kambini, ukipata — bida'a kwangu. na kulla ñgombe ukaleta — ijara[5]) yako rupia mbili ao nne." yule mtu huqubali.

khabari ya kuvua samaki.

kazâlika wengine wavuvi wa ngarawa. hulala hatta al-fajiri wanakwenda tanga na tanga na kafi[6]) na upo[7]) na sukani[8]) na mishipi[9]). wakifika pwani, marra hushua ngarawa. hatta ikafika majini, wanafungafunga, marra wanatweka. na uvuvi wao wanavulia mbali, ma'ana wanakwenda kunako madindi[10]) makubwa yenyi papa[11]) na samaki wakubwa. wakifika hutosa nanga, hutia mishipi vyambo, wakatupa baharini kuvua. hatta upepo wa kusi ukavuma, wanatweka ngarawa zao kureje'a. wengine wamepata, wengine wanarudi

---

1) Gefahr. — 2) Mühe, Beschwerde. — 3) wünschen. — 4) am Spieß braten. Der Spieß besteht aus Holz, nämlich aus vijiti vya ukuti. — 5) Lohn, Verdienst. — 6) Schaufelruder. — 7) Eimer zum Wasser ausschöpfen. — 8) Steuer. — 9) Fischangel. — 10) Untiefe. — 11) Haifisch.

na ngarawa tupu. waliwokosa, wakiulizwa „umepata?“ hujibu:

„maji mafu[1])
na mvuvi kafu.“[2])

1) Nippflut. — 2) ist tot.

na inapokuwa shuwali[1]), hapana upepo, hupiga makasia ao kafi, huimba nyimbo:

„na makasia tieni,
na makasia tieni,
tangu likiwa mtini,
na makasia tieni.“

na wengine wavuvi wa madema[2]). watu hao husuka madema ya miti, maji yanapokupwa, hupeleka madema mwambani, wakayatosa, hutia vyambo. vyambo vyao hutia mwani[3]) ao vichwa vya nguu[4]). maʿana ya mwani — majani yatokayo baḥarini. wakesha tega, hulala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, wakenda kutazama madema yao, huyapandisha juu ya mitumbwi, hukamata samaki.

na Waʿarabu na Wadigo wanavua kwa juya[5]). Wadigo wanapokwenda baḥarini, al-ʿaṣiri wanaporudi katika mitumbwi yao, hupiga ngoma, maʿana wanaʿarrifu watu, wajue, kama Wadigo wamerudi. nao Wadigo wavuvi mno, hukaa katika miji yote ya mrima. watu wa mashamba wakisikia, killa mtu anakuja na pesa zake, sababu samaki wanauzwa rakhîṣi. na kulla namna ya samaki huingia katika juya la Wadigo. nao wanauza samaki yao jumla, na wavuvi wa ngarawa na madema wanauza vilevile jumla. wananunua wachuuzi wa samaki. marra huwatia katika mibano[6]) waka-

1) ruhige See, Windstille. — 2) Fischreuse. — 3) Schlingpflanze. — 4) Seebarbe. — 5) Schleppnetz. — 6) Klammer.

wachoma, sababu wasivunde. wasipofanya hivo, samaki huoza upesi. nao huuza samaki moja tangu pesa tatu ḥatta pesa kumi, na wakichelewa, huwapa watoto, kuwatia ndani ya tundu, ao katika mibano, kuwatembeza. samaki waqati wa maji mafu ghali, amma maji makuu rakhîṣi.

każâlika uvuvi wa waanawake. maji yanapokupwa, wanakwenda baḥarini kutanda ushimba[1]) na dagaa[1]). na kutanda kwao hushona nguo kaniki na shuka tatu ao nne pamoja, qiasi ya nguo ndefu, kisha huchukua kapu, wakenda pwani, maji ya kifua ao ya magoti. marra huona madagaa ao ushimba, husema: „namisha upindo.“[2]) watu wawili hushika upindo, na mmoja huchunga dagaa, liingie ndani ya upindo. likaingia, huinua juu upindo, ndani mna dagaa na ushimba, huchota, wakatia ndani ya kapu. nao wanapata jingi, ḥatta samaki wanapata wakubwawakubwa. lakini khaṭari, na khaṭari yake nyenga. nà huyo nyenga mtoto wa taa, hukaa katika pango ya mwamba. akisikia kelele za watu, hutoka ndani ya pango. na khaṭari ya nyenga huchoma mguuni, lakini wenyewe waanawake wanaijua dawa yake. na mwanamke akichomwa na nyenga, huja mwingine, akamtemea mate pale alipochomwa na nyenga. akifika nyumbani, hufanyiziwa dawa ya mizizi. asipopata dawa, donda huendelea, huwa donda ndugu, haliponi.

wakipata dagaa, wanauza fungu pesa na ushimba vilevile. na mwingine wanaanika, hupeleka mashamba kubadili kwa muhogo, sababu watu waliwo mashamba wa katika taʿabu ya vitoweo.

każâlika na usiku, mwezi ukiwa mpevu[3]), vijana

1) kleine Fischsorten. — 2) das Tuch herunter. — 3) Vollmond.

waanawake huenda pwani, kuokota nyambua[1]) na vijino[1]), kupeleka majumbani. wakatia ndani ya majungu, kisha huchemsha. yakiwiva, huchokoa[2]) zile nyama.

na wengine kazi yao hungoja maji kupwa, wakenda pwani kupiga kaa, na kuchokoa pweza[3]) na kombe[4]). nayo ni kazi ya khaṭari kwa mkunga[5]), maji yakipwa mwambani, mikunga inatembea, mfano wa hao mikunga, kama nyoka urefu wake, wengine wanakula, wengine hawali.

nyimbo za mabaḥaria.

na watu wakienda baḥarini na vyombo vyao ao mashua zao, huimba nyimbo hizi:

„kasikazi[1]) vuma,
na umande[2]) vuma,
tukokote dau la bwana,
lisirudi nyuma.“

---

1) Nordwind. — 2) Frühnebel.

ao huimba:

„kiko? kiwa mwambani,
kiko? kiwa mwambani.“

ao huimba:

„chombo chamenyamenya[1]),
chombo chamenyamenya,
nakhoża nenda joshi[2]),
chombo chamenyamenya.“

---

1) hin und herschwanken. — 2) nach rechts halten.

---

1) kleine Fischchen. — 2) herausnehmen, hervorziehen. — 3) Fisch. — 4) Muschel. — 5) Aal.

ao huimba:

„namtaka Zaina, nicheze naye,“
„mwenyi dodo kaja [1]), mkumbatie.“ [2])

1) sagt Zaina. — 2) umarmen.

ao huimba:

„napenda wê, napenda wê
moyoni mwangu kabisa
siku ya kuzaliwa
ya mama na baba
napenda wê, napenda wê
moyoni mwangu kabisa.“

ao huimba:

„nampenda sana, nampenda sana
kibibi mdogo, mzuri kijana.“

ao huimba:

„nipe mbili [1]) — nende
kama hukunipa
sileti mshindo wa bwende.“ [2])

1) zu ergänzen kanga. — 2) ich werde dich nicht durch Beischlaf erfreuen.

ao huimba:

„njoo bwana, njoo, bwana njoo,
bwana wangu unipose moyo.“

ao huimba:

„mṣiba wa nini?
Ḥamadi hakwiba,
kafungiwa nini?“

ao huimba:

„na kidau changu nisafiri Pemba,
meli ya Ḥijjaji imekwisha kwenda,
aḥsante Sefu Sefu uliyonitenda,
aḥsante Sefu Sefu uliyonitenda.“ [1])

1) Klage eines Mädchens, das gern eine Pilgerreise mitgemacht hätte.

ao huimba:

„nna ubwa[1]) wangu, mwembamba mweupe
nampenda macho na nyeusi na kope,
nakupenda wewe, chako usinipe.“

1) Liebling.

khabari ya kuunda jahazi.

kwanza mafundi huenda kokoni[1]) kupasua mbau na kutafuta mkuku[2]) na mihimili[3]) na mataruma[4]) yenyi nguvu. wakiyapata, huleta mjini, wakamwita mtu mzee fundi wao na mwᶜallimu kuwatilia ubani, waanze kazi yao, ipate kuongoka.

na mwanzo wake jahazi kuanza mkuku na mataruma na mbele omo[5]) na nyuma tezi[6]), na ubau wa maliki[7]). na mbau wanagongomea kwa misumari, na katika msumari hutiwa pamba na mafuta ya nazi — msumari ushike sana. jahazi inapokwisha, wanaunda siṭaḥa[8]) ya mbele na ya nyuma. tenna wanakarafati[9]), maᶜana ya kukarafati zinazibwa tundu zilizo wazi kwa pamba na mafuta, wakesha wanadeheni[10]) kwa sifa, na kuijaza maji tele ile jahazi mudda wa siku sabaᶜ ao arbaᶜtᶜashara, kutezama maji yanavuja ao hayavuji. kisha wanaunda sukani[11]). ikesha sukani, wanashona tanga na kutafuta mlingoti na desturi[12]) na foromali[13]) na nanga. tenna husokota kamba za kutwekea na za kutilia nanga, jahazi ikatua.

khabari ya kushua jahazi: inapokwisha, huᶜarrifiwa watu: „kesho jahazi każa wa każa inashuliwa[14]), mkutano pwani aṣ-ṣubuḥi.“ hukutanika Wanyamwezi na

1) Busch. — 2) Kiel. — 3) Binderippen. — 4) Spanten. — 5) Bug. — 6) Heck. — 7) Beplankung. — 8) Deck. — 9) kalfatern. — 10) ölen, firnissen. — 11) Steuer. — 12) Bugspriet. — 13) Segelstange. — 14) vom Stapel gelassen werden.

waungwana. Wanyamwezi wanashua kwa ijara, waungwana burre. nao huimba mwimbo wanaposhua:

„mkono kwa mkono
ṣalla ʿala.“ [1])

1) Friede auf = Friede bei Gott.

huimba ḥatta jahazi ingie majini.

mudda wa siku tatu itasafiri, kujaribiwa tanga na mlingoti. huingia na watu, lakini hawana nauli[1]). huenda mchana kutwa, jioni hurejeʿa.

tenna hutiwa nanga ile jahazi, mafundi wataka bakhashishi[2]) yao kwa yule mwenyi jahazi. huwapa, maʿana ʿada.

na mwimbo wao masermala[3]), wakiunda jahazi, wanakwimba:

„mwambie mama, aombe,
nami niombe,
mwombwa yeye rabbana.“

ao huimba:

„pasua mbau, tuunde,
pasua mbau, tuunde,
masermala, pasua mbau, tuunde.“

na mwimbo wa kutweka jahazi:

„hod yâ 'llâh, hod yâ 'llâh.“ [1])

1) ihn o Gott.

ao husema:

„tumtweke kinyamwezi [1]) ñgombe [2])
tumtweke kinyamwezi ñgombe.“

1) mit der Kraft eines Mnyamwezi. — 2) das Segel gemeint.

1) Fahrgeld. — 2) Belohnung. — 3) Zimmerleute.

nyimbo zinazokwimbwa katika kazi.

wafanya kazi hupenda kwimba, nao huimba:

„kwanza hê leo, kwanza hê,
aṣ-ṣubuḥi na mapema leo,
kwanza tuombe muungu.“

ao huimba:

„kijakazi kina meno, chauma,
sikitaki tenna, kipeleke shamba,
kikalime.“

ao huimba:

„kwa [1]) mama Yaya,
leo kwa mama Yaya,
muhogo [2]) kwa tembo tamu
kwa mama Yaya.“

1) zu ergänzen twende. — 2) zu ergänzen tukale.

ao huimba:

„nipande wangu mkunde
nnataka kuachwa
jina la mume — jambo.“

ao huimba:

„Sitaḥamili [1]) uwiwu wache,
mwanamume ku mgongo kama kenge?“ [2])

1) Name einer Frau. — 2) die gewöhnlich auf einander hocken.

ao huimba:

„suria mtumwa,
leo suria mtumwa,
usione kulalia godoro [1]),
suria mtumwa.“

1) zu ergänzen „daß du eine Freie vor dir habest.“

ao huimba:

„palia, palia,
binti Ḥemedi

kaupiga jembe mqarafuu,
palia, palia.“

ao huimba:

„muhogo mchungu
Magwangwara hiyô!
ukasikia toba
„lâ ilâha illâ 'llâh.“
Feruzi kauawa.

ao huimba:

„shungia mgeni yôyô,
shungia mgeni yôyô,
ndio kwanza kuja,
shungia mgeni yôyô.“

desturi katika kazi ya kulima.

mtu akianza kufiega [1]) mwitu kutaka kulima, huomba muungu: „rabbi [2]), nipe uzima kulala na nguvu kuamka na nguvu ya kufiega shamba yangu, nipande, nije niile, nisipokula mimi, wale wanangu.“

akisha, huchenga [3]) mwitu, akakata magogo, kisha huyapiga moto. ḥatta mvua inapokunya, kwanza hupanda chooko na mbindi na kunde na matango, sababu vyakula hivo vyepesi kuota na kumponya mtu njaa. ḥatta wingu [4]) la pili hupanda mhogo na mbegu nyingine.

na mwanzo wa kupanda mti, matunda yake yanayoliwa kama mdizi ao mnazi, husema: „nnapanda mti huu, muungu anipe uzima, niule, kama sikuja'aliwa [5]) mimi, wale wanangu.“ tenna huipanda ile mbegu. na atakapo kupanda, sherṭi kwa mkumbi. na huo mkumbi Wazaramu ndio waliwo nawo. ikawa qaribu ya mpando, huenda Zaramu kutaka mkumbi, nao huchanganya pamoja na mbegu. wanaṣadiqi, shamba ikapandwa na mkumbi, waqati wa kuvuna huwa na baraka [6]). nao mkumbi magome ya mti, rangi yake kama manjano. na anapovuna, humpa 'ada yake yule mwenyi mkumbi pishi mbili ao tatu.

---

1) urbar machen. — 2) Herr, Gott. — 3) abholzen. — 4) Saat. — 5) bestimmt sein. — 6) Segen.

na vyakula vya shamba vikianza kuwiva, huamia ndege. na kuamia kwao wanajenga dungu. na hilo dungu miti mitatu. na juu huweka miti qádiri ya mtu kuweza kusimama kule juu. na mwamizi huzuka kumbeo[1]) na mawe ya madongo, macho yake kutezama ndege, wasitue juu ya mtama. na wakitua, huamia kwa kumbeo, husema:

„āāah haōōō ndege.“

hupiga dongo la kumbeo.

na wanaoamia huimba mwimbo:

„ndege usile mpungangwa[1])
ntachinshwa.“

1) mpunga wangu.

ao huimba:

„kufa kúikúi[1]),
mwanetu kapewa ndege kuamia.“

1) König der Vögel.

áṣili ya mwimbo huu umetoka katika ḥadithi ya wazee wetu, ndio sababu watu hupenda kwimba katika kuamia.

khabari ya kuvuna.

huenda watu na miundu, waanawaume, kukata chini ya mashina ya mtama shamba yote. hawauchukui marra majumbani, wanauacha mudda wa siku tatu, ndipo wanapoleta makapu kuchukua. tenna huuputa[2]). na kuputa kwake wanatandika jamvi, killa mtu hushika ufito, wakapiga ule mtama, hupukutika punje. wakesha wanapeta[3]), mtama wake hutia katika vikanda.

na iwapo amekuja rafiqi kumtazama, humvunjia

1) Schleuder. — 2) dreschen. — 3) sieben.

shuke[1]) la mtama, ukaputwa, hutiwa katika kiṣaḥani, akapewa kula. na anapoondoka, humvunjia mapute[2]) matatu kumpa zawadi[3]) yake.

kaẓâlika mavuno ya mpunga kama hivo. vilevile akija rafiqi, huvunjwa shuke la mpunga, mwanamke hukaanga, akaletewa rafiqi yake kula. na akiondoka, hupewa mashuke matatu vilevile zawadi.

na mtu akipata mtama ao mpunga mwingi, hutoa ṣádaqa[4]) kuwapa maskini.

nao hawali vyakula vipya illa kwa mavumba[5]). wengi wana pepo ya kinyamkera, dungumaro, shamñgombe, na killa namna ya pepo. Wasuaḥeli haba sana, wasiwo pepo. watu hurithi[6]) mali, wao wanarithi pepo. na mtu mwenyi pepo akila billa ya mavumba, jioni atapata ḥoma ao ugonjwa mwingine.

kaẓâlika mavuno ya muhogo — ukipata miezi sitta, mtu akiwa na njaa, aweza kuñgoa shina la muhogo kupika akala. na anapotaka kuulenga[7]), illa upate ʿomri wa mwaka, ndipo unapoñgolewa. tenna humenywa, ukaanikwa siku tatu ao nne. unapokauka, hutiwa katika magunia ao makanda.

na muhogo namna mbili, kuna muhogo mchungu na muhogo mtamu. mchungu unaitwa nangwa — hautafuniki, ukiwa mbichi, illa ukikauka, hupikwa ugali — hulika.

na muhogo, uliotambaliwa na nyoka, hauliki kwa ugali, unateleza, illa hupikiwa pombe.

shamba ya muhogo Wasuaḥeli wanaipenda, sababu manfaʿa[8]) yake mengi, na chakula chake wanakipenda.

---

1) Aehre. — 2) Aehre. — 3) Geschenk. — 4) Opfer. — 5) bestimmtes Mehl. — 6) erben. — 7) länger im Feld lassen. — 8) Ertrag.

khabari ya mnazi kupandwa kwake na matumizi yake.

auwali ya mnazi mbegu yake nazi yenyi makumbi. huwekwa nyumbani, ḥatta ikawa kavu, hupelekwa shamba kupandwa. nao hupanda kitako mnazi, iwapo wanataka ule mnazi usiwe mrefu sana. na wataka uwe mrefu — huchutama. na mwanzo wa kupanda siku ya kunya mvua, tenna sherṭi chini pawe na mnyevu[1]). na sherṭi yake mwezi arbaʿtʿashara, uwapo kitanga tele. na mudda wake miezi sitta ao mwaka kutoa mcheʿ[2]). baʿada ya miaka mitatu unatoa makuti. miaka mitano unatoa kigogo. mwaka wa sabaʿ unaanza kuzaa.

na kuzaa kwake kwanza huanza karara[3]), ndilo linalochukua vidaka[4]). ndani yake vinapata thalathini karara moja, lakini hupukutika[5]) vyote mwezi mmoja, hutoka vidaka vingine. baʿada ya vidaka huja vitale[6]). vitale mtu akiwa na kiu, aweza kunywa maji, na kifuu[7]) aweza kukila, lakin hamna nyama. baʿada ya kitale huja dafu la ukomba[8]), nalo hamna kitu ndani, kama mchuzi mzito. baʿada yake huja dafu, na kifuu chake kipevu. tenna huja koroma[9]), nuṣṣu dafu, nuṣṣu nazi. lakini mtu hawezi kula jingi. ulapo jingi, kama halikupendi, tumbo hukusokota. baʿada ya koroma huja nazi, ndio mwisho wa uzazi wa nazi.

tunasema matumizi yake nazi: matumizi yake waanawake hupikia vyakula, mchuzi, mboga. killa chakula cha kisuaḥeli sherṭi kiwe na nazi. na kupikia

---

1) nyevu naß, hier mchanga zu ergänzen. — 2) Schößling, Steckling. — 3) holzige Blütenhülle. — 4) kleine saftlose Nuß. — 5) abfallen. — 6) unreife Nuß mit Wasser ohne Kern. — 7) Schale. — 8) auch kukomba, Nuß mit weichem beginnendem Fruchtfleisch. — 9) fast reife Nuß.

kwake nazi inakunwa, tui[1]) lake ndilo wanalopikia. tumio la pili — hupikiwa mafuta. mafuta yake dawa kwa mtu mwenyi upele. huoshwa upele wake, mafuta yakachanganywa na chokaa akapakwa. ao hukaangia vitumbua, na kuwashia taa. manfaʿa ya tatu hufanyiza mbata[2]). na hizo mbata nazi husikuliwa, kutolewa vifuu. kisha huanikwa ḥatta zikawa kavu[3]), hutiwa ndani ya magunia, hupelekwa killa inchi kuuzwa ḥatta barra el-Hindi na Maskati. matumizi ya kifuu cha nazi — mwanamke kana hana pesa ya kuni, hufanya vifuo vya nazi — ndio kuni.

turejee manfaʿa yake ule mnazi. auwali kigogo cha mnazi hufanyizwa vizingiti vya milango, wengine hawawezi kununua vizingiti vya mbao.

kaẓâlika tembo latoka katika mnazi. wagema[4]) huugema mnazi, na kugema kwao hukata kilele[5]) cha mnazi, kisha hufunga vibuyu. machozi yatokayo katika kilele ndilo tembo.

tumizi jengine siki. siki yatoka katika tembo kali. likipata siku tatu, hawezi mtu kulinywa kwa ukali, hulitia katika chupa, wakalifanya siki. na siki yake dawa kwa mgonjwa mwenyi baridi yábisi[6]). maʿana hupikiwa katika kitoweo, ndicho kiungo chake. kama hakupata kitoweo, hutowea ile siki tu. nayo khaṣṣa ikikaa mwaka ni nzuri sana.

matumizi mengine shale[7]). mnazi ukianguka, shale watu wanakula. maʿana wa shale ule moyo wa mnazi, hupatikana katika kilele. na watu hula billa ya kupikwa, hula bichi.

---

1) die aus dem frisch geschabten Kern der Nuß ausgepreßte ölige Milch. — 2) trockene ganz reife Nuß ohne Wasser. — 3) nazi kavu Copra — 4) Zapfer. — 5) Herz der Spitze. — 6) Rheumatismus. — 7) Spitze der Palme.

matumizi mengine makuti. wanaezekea majumba, na kuti zake wanachomea mishikaki ya nyama.

manfaʿa ya makumbi wanatumia waanawake wafinyanzi wa vyungu, na watu wafanyao kamba. maʿana ya kutumia waanawake ndizo kuni za kuokea vile vyungu. na wafanyao kamba, huchuna yale makumbi, kesha wakayagonga, ḥatta yakawa leini, tenna husokota kamba. hii ndio ṣifa inayotoka katika mnazi.

thamani yake mnazi riali, na thamani ya dafu moja pesa, na nazi kaẓâlika moja pesa. illa wachuuzi hukata nazi, wakauza kipande pesa. na zikiwa rakhiṣi mashamba — mbili kwa pesa.

aiḍa mwanguzi wa nazi — ujira wake killa mnazi, atakaopanda — nazi moja. kama walivosema Wasuaḥeli: „mfa juu ya mnazi — kaponzwa na ṭamaʿa zake.“ na waanawake wameimba:

„ya mkwezi moja,
akilewalewa
ya mkwezi moja.“

khabari ya ṭalâqa[1]).

mwanzo wa ṭalâqa.

mwanzo wa ṭalâqa mke na mume huanza magomvi. magomvi yao — mwanamke huwa mtembezi ao mume. mume akimkanya mkewe „tulia nyumbani,“ mwanamke hujibu „wataka univundike kama ndizi? ukinitaka mimi — sherṭi nitembee, na kama hutaki — tafuta mke mtawa.“[2]) mume humwuźi majibu yale. iwapo hataki kugomba naye, atakwenda kwa wazee wa yule mwanamke, atashitaki[3]), kama mambo afanyayo mkewe. nao watamwita, watamgomba sana, watawapatanisha. mudda wa siku chache watareje'a tenna ugomvi. na ma'ana ya kufanya hivo — mwanamume hampendi, amepata mwingine nje.

na mambo hayo mwanamke kijana hayajui, illa hupata shoga, ndiye anayemfunza mambo ya nje. husema „mume moja hajazi kitunga,“[4]) ao humwambia „ukalima shamba, sherṭi uwe na gunda.“[5]) mashikio yake humzibuka yule kijana. kaźâlika akilala, hamsingi[6]), wala hamwoshi miguu. na hiyo feḍeha[7]) kubwa kwa mke na mume. iwapo hawapatani, mume atamwuliza: „wataka, tukae wewe nami, ao hutaki?“ mwanamke atajibu: „nataka unache.“ atamwuliza: „ume-

1) Scheidung. — 2) fromm. — 3) klagen. — 4) Korb. — 5) Pflanzung. — 6) salben. — 7) Schande.

burai[1]) máhari?“[2]) atajibu: „nimeburai.“ ataandika khaṭṭi[3]) — ya kama: „fulani binti fulani iwapo ameburai máhari, yaliyo juu yangu, nami nimemwacha ṭalâqa tatu.“

marra mwanamke atafunga vyungu na mikeka na kulla kilicho chake, atatoka, atakwenda kwao. atawambia wazee wake: „mume wangu amenacha.“ nao watakwenda mwuliza: „ṣaḥiḥi[4]) mke wako umemwacha?“ atajibu: „naʿam[5]), nimemwacha.“ wazee wake watamwita kungwi lake, aje amwoshe. osho[6]) huo ni osho wa kule kuachwa, sababu ataolewa na mume mwingine, na baa[7]) la kule limtoke.

atakaa ʿeda[8]) miezi mitatu na siku kumi, hana rukhṣa ya kuolewa illa ʿeda ishe. tenna ataolewa na mume mwingine. na iwapo beina[9]) yao ilikuwa magomvi na yule mume, hufanyiza shangwe kubwa na nyimbo, maqṣudi[10]) kumkirihisha[11]) yule mume. hiyo ndio khabari ya kuachana kwao.

namna ya kutamka[12]) ṭalâqa.

matamko[13]) ya ṭalâqa namna mbili. kwanza namna ya ṣareḥe[14]). ṣareḥe ni kumwambia mwanamke „fulani nimekuṭalleqi[15]) ṭalâqa tatu ao moja,“ ao kumwambia „fulani nimekuṣareḥe,“ maʿana umekuwa wazi, huna kitu kilichokuzuia. ao kumwambia mwanamke „fâraqtuki,“[16]) maʿana nimekufariqi, wewe si pamoja na mimi. maneno matatu haya matamko yake yanakwitwa ṭalâqa ya ṣareḥe, maʿana mume akasema kumwambia mke, haiḥi-

1) verzichten. — 2) Morgengabe. — 3) Schriftstück. — 4) richtig. — 5) ja. — 6) Waschung. — 7) Schmutz. — 8) Wartezeit. — 9) zwischen. — 10) Absicht. — 11) ärgern. — 12) ankündigen, eigentl. aussprechen. — 13) Ankündigung. — 14) klare Auseinandersetzung. — 15) Scheidung geben. — 16) ich habe mich von dir getrennt.

taji[1]) kuulizwa yule mume ḍamiri[2]) yake, hujulikana, kwamba maneno haya ṭalâqa.

amma hiyo ṭalâqa ya kinâya[3]) ni kumwambia mwanamke „anti khalîyati,“[4]) maʿana unamwambia mwanamke „wewe umekuwa mtupu.“ ao kumwambia mwanamke „istábrai raḥmuki,“ maʿana umekuwa mbali uchi wako na mimi. ao ni kumwambia „alḥiqi bi ahaliki,“[5]) maʿana ni kumwambia „nenda kwenu.“ maneno haya, asemapo mtu, ni matamko ya ṭalâqa, lakini mke hajaachika, illa hurejewa, yule mume kuulizwa, maʿana ya kusema maneno haya ya kumwambia mke „nenda kwenu.“ áṣili[6]) yake maneno ya ṭalâqa, lakini yameingia kifungo[7]). iwapo yule mume amekifungua kifungo — kwamba „nimesema maneno haya — huyu mwanamke nimemwacha“ — bassi ameachika.

barua ya ṭalâqa.

„mimi Ramaḍani wadi[8]) Khamisi nimetundika ṭalâqa kwa Mâsiti binti[9]) Mwenyi Bakari. iwapo amesameḥe máhari[10]), yaliyo katika shingo yangu — nami nimemwacha ṭalâqa mbili, si mtu mke wangu.

shâhidi[11]) Mwenyi Aflaḥa bin Mumbi, wa pili ʿAbdurraḥmani, katábahu[12]) Ramaḍani wadi Khamisi.“

khabari ya ṭalâqa mbili na ṭalâqa tatu.

mwanamke akiachwa ṭalâqa mbili, mume aweza kumrejeʿa. lakini atafute mashâhidi moja ao wawili, atawambia: „twendeni mkashuhudie, nataka kumrejeʿa

---

1) es ist nicht nötig. — 2) Wunsch. — 3) versteckte Hinweisung. — 4) Du bist frei. — 5) arab. ilḥaqî bi-ahliki begib dich zu deiner Familie. — 6) Ursprung. — 7) kifungo = kinaya. — 8) Sohn. — 9) Tochter. — 10) auf die Morgengabe verzichten. — 11) Zeuge. — 12) geschrieben hat er.

mke wangu.“ lakini sheṛi mwanamke awe ʿeda yake haijesha. atamwambia: „fulani binti fulani nimekurejeʿa kuwa mke wangu katika nikaḥa[1]) yangu, na máhari yale ya kwanza.“ mwanamke na wazee wake, kama hawakutaki, mâdâm[2]) mume ametamka maneno hayo, mwanamke wala wazee wake hawana njia ya kukataa. kulla sheriʿa[3]), mume atakayokwenda, atawashinda. illa kama hakujua matamko ya kumrejeʿa, na ʿeda yake imekwisha — hampati kumrejeʿa, illa ampose vengine na máhari mengine, ndipo awe mkewe, na kama hataki — bassi.

na katika ṭalâqa tatu, maʿana mume akimpa mkewe matamko ya ṭalâqa marra tatu kwa maneno tuliyotangulia kuyataja, mume hawezi kumrejeʿa yule mwanamke, ameachika kabisa.

lakini iwapo yule mwanamke anaolewa na mume mwingine, na yule mume amwache, akae ʿeda miezi mitatu na siku kumi — ndio yule mume wa kwanza, akitaka kumrejeʿa, amrejee.

na mtumwa ṭalâqa zake mbili bassi. akimwacha mwanamke ṭalâqa mbili, hana rukhṣa kumrejeʿa, illa ṭalâqa moja akimwacha, anaweza kumrejeʿa.

desturi mwanamume kumwacha mke.

mwanamume humwambia mkewe „ukaingia katika nyumba ya binti Feruzi, mwanamke wewe, nami nimekuwacha, si mtu mke wangu“ — na mwanamke akaingia katika nyumba aliyokatazwa, mwanamke huyu ameachika, si mkewe tenna.

ao mtu kumwambia mkewe máthali[4]) katika mfunguo tatu: „mfunguo sitta ukija — mwanamke wewe umeachika.“ na yule mke ataḥesabu[5]) miezi, ukatimia

---

1) Ehe. — 2) während. — 3) Gesetz. — 4) z. B. — 5) zählen.

mfunguo sitta, lâzima mwanamke atoke. kwa shurṭi hii mwanamume huachika mwanamke pasipo sababu, lakini huweza kumrejeʿa.

ao mtu kusema „nikikuona umesimama na mwanamume fulani, mwanamke wewe umeachika“ — naye mwanamke akasimama na yule mwanamume, mwanamke huyu huachika.

ao mwanamke iwapo nyumbani mvivu, hafanyizi kazi, yule mume anayo njia ya kumwacha mwanamke.

ao kama mwanamke ni mtembezi, ameshiriki[1]) ngoma, mwanamume anayo njia ya kumwacha atakapo.

ḥarâmu[2]) mume kumwambia mkewe: „wewe nakuona kama uti[3]) wa mongo wa mama yangu.“ mume asemapo hivo, mke hakuachika, lakini hana rukhṣa kulala naye mkewe, illa atoe kafâra[4]) kuandikia mtumwa ḥurru.

kaẓâlika ḥarâmu kumwacha mke, naye yu katika miezi[5]), maʿana yu katika damu[6]). maʿana yake ulipomwoa, alikuwa mzima, naye akirejeʿa kwao sasa — vilevile awe mzima.

---

1) teilnehmen. — 2) verboten. — 3) Rückgrat. — 4) Buße, Sühne. — 5) Menstruation. — 6) Blut.

khabari ya maraḍi[1]) na dawa[2]) zao.

maraḍi ya ḥoma[3]).

ḥoma namna mbili. kuna ḥoma ya bardi[4]) na ḥoma ya ḥári[5]). amma ḥoma ya bardi ásili[6]) yake yatoka katika mvua. inyapo mvua, na mtu ametoka nje, na mvua ikampata, akifika nyumbani, maungo yake huwa na bardi na kutetemeka. dawa yake ḥoma ya bardi hupikiwa chayi ya moto, akanywa, na kujifukiza uvumba[7]) mbichi, moshi umwingie maungoni. kisha marra ajifunike nguo. ḥatta jasho limtoke.

amma ḥoma ya ḥari, jua likiwa kali sana, na mtu alikuwa nje, jua limempata, huingiwa na ḥoma. naye huona fukuto[8]) maungo yake, marra huona jasho marra huona bardi, na kichwa kumgonga. dawa yake husuguliwa maungo yake yote kwa dalia[9]) ya maji, na nyingine hupakwa juu ya kipanda uso. ḥatta ikikauka ile dalia maungoni, mwili wake hubaridika, hupata hujambo.

mtoto akiwa na ḥoma, huandikiwa „mafusho“[10]) saba‘ na mw‘allimu katika qarṭâsi[11]). nayo huandikwa

---

1) Krankheit. — 2) Heilmittel. — 3) Fieber. — 4) Fieber in Folge Kälte. — 5) Fieber in Folge Hitze. — 6) Ursprung. — 7) Benzoë. — 8) Schüttelfrost. — 9) ein Pulver, das durch Zerreiben von mdalia-Holz gewonnen wird. mdalia ist ein indischer Baum und dalia wird wie uvumba von indischen Händlern verkauft. — 10) Räucherwerk. — 11) Papier.

majina haya „aḥṭam fashaż,“ [1]) kisha hutiwa katika mafuta ya uto [2]). ukaletwa moto, yakatiwa mafusho ndani ya moto, hufukizwa yule mtoto, ḥatta jasho limtoke.

kaẓâlika mkubwa akiwa na ḥoma, hufanyiziwa mafusho kama hivi.

na iwapo mtu ana ḥoma nyingi, na watu wake huṯhanni [3]) kichwa kimempungua, husema „tumpime kichwa.“ hunyolewa kichwa, kisha hutwaliwa siagi [4]), na tui [5]) la nazi. tui la nazi hubandikwa juu ya pamba, akawekwa juu ya utosi. na ile siagi husuguliwa kile kichwa ḥatta povu humtoka. tenna hufungwa kitambaa cheusi. hufanyiwa hivo mudda wa siku tatu. hujulikana kichwa kimempungua ao hakikumpungua.

ugonjwa wa ndui [6]).

ndui hazina dawa. dawa yake moto. baʿada ya siku sabaʿ, ndui zikawiva, hutumbuliwa [7]). kisha hutwaliwa kitambaa na mchanga uliwo moto, akachomwa yule mwele [8]) wa ndui. na kama hawezi kuvumilia moto, hulemaa [9]) maungo yote. ao zikimpata nyingi usoni, naye moto anaogopa, macho hupofuka [10]). na mudda wake sabaʿ mbili, na killa siku hutiwa moto mvunguni [11]).

kaẓâlika macho yake, kama hawezi kuyafunua, sababu ndui nyingi, hutiwa mkojo [12]) wa mtoto machoni, mtoto wa miaka sitta ao sabaʿ, kuchelea asipofuke.

naye mgonjwa wa ndui haonekani na killa mtu, illa yule amwuguzaye. wala mtu aliyelala na mwa-

---

1) Namen von pepo. — 2) Sesamöl. — 3) glauben. — 4) Butter. — 5) öliger Saft aus dem Kern der Kokosnuß ausgepreßt. — 6) Pocken. — 7) aufstechen. — 8) Kranker. — 9) entstellen. — 10) blind werden. — 11) Raum unter dem Bett. — 12) Urin.

namke, ao mwanamke amelala na mwanamume, akitaka kuonana na mgonjwa wa ndui, hana rukhṣa, sababu kuchelea yule mgonjwa asiḍurike [1]). na mzio [2]) wake samaki, ḥatta apone, mudda wa miezi miwili ao mitatu ana rukhṣa ya kula samaki.

na mwanzo wa ugonjwa wa ndui huanza huumwa na maungo, tenna ḥoma. waanawake wazee wakimwona mtu ana ḥoma na kiuno kumwuma, wanajua atatokewa na ndui. marra hupikiwa muhindi wa kutokosa [3]), akala.

na ndui namna tatu. kuna „ndui za mhindi,“ na „ndui za mtama,“ na „ndui za ufuta.“ za ufuta zikampata mtu — kupona bakhti [4]) yake. zinakuja kwa ubaya sana.

na waanawake hupenda kwimba mwimbo huu:

„kutoka [1]) — natoka kwako,
kurudi naona shemu [2]),
nalitokewa na ndui
za mhindi na mtama,
ulithanni ntakufa
upate kunila nyama,
sasa nimeondokea [3])
kwa nguvu za maulana.“ [4])

1) verlassen. — 2) Scham. — 3) gesund hervorgehen. — 4) unser Gott.

maraḍi ya buba [5]).

buba maraḍi mabaya. mno hukaa puani, ao kwapani, ao mikononi. na umbo lake kama pesa. mtu akitokewa na buba, sherṭi awe na watu wa kumtazama.

1) schädlich sein. — 2) Verbot. — 3) im Wasser kochen, sieden. — 4) Glück. — 5) krebsartige Hautkrankheit.

na kama hana watu, asiwe mchafu. na hao watu humpeleka pwani, kumwosha na kumsugua kwa mabunzi[1]) ya mhindi, ḥatta ivuje[2]) maji. kisha atiwe dawa, jina lake mrututu[3]), unafukuta[4]) sana. akitiwa aṣ-ṣubuḥi, maji kujaa[5]), hainyamazi dawa mpaka jioni maji kujaa. na kama mtu, ametokewa na buba, hana wa kumtunza, itamlemaza[6]) mikono, atavunjika, atakuwa kiwete[7]). nayo inanuka. kaẓàlika inakaa pachipachi ya ukundu[8]). mtu akenda, humwagua, watu humjua, ya kama huyu ana buba.

maraḍi ya ukoma[9]).

haya ndio maraḍi yaliyokataliwa na watu. mtu mwenyi ukoma, wote hawampendi kula naye, wala kukaa naye. tenna hapana dawa katika mrima pwani wala barra ya mwenyi ukoma. na mwanzo wake maungo huwa na mabumbuza[10]) na vyoa[11]). tenna huwiva vile vyoa, hufanya madonda maungo yote. ḥatta yakipevuka, hukatika vyungo, vidole, ao miguu. watu humwita kiratu[12]), ma'ana husema: „wewe si mwenzetu tenna, wewe na nyama sawa, makazi yako mwituni.“ akisikia huqaṣirika sana. majibu yake husema: „kiratu — mamayo na babayo.“

maraḍi ya upele[13]).

upele namna mbili — upele mnene na ukurutu. amma upele mnene dawa yake killa siku kuoshwa kwa maji ya moto ao maji baridi, ḥatta utoke maji. kisha hupakaa mafuta ya nazi, ao mafuta ya nazi na chokaa. lakini haifai koga maji chumvi. na ukurutu dawa yake

1) leere Maiskolben. — 2) i auf buba bezüglich. — 3) Kupfervitriol. — 4) brennen. — 5) Flut. — 6) lähmen. — 7) lahm. — 8) am Afterring. — 9) Krebs. — 10) Bläschen. — 11) Flecken. — 12) Schuh. — 13) Krätze.

ni kama hiyo. lakini maraḍi yake ni mabaya sana. na upele wake mdogomdogo kama punje[1]) za mchanga, hujikuna mtu mchana kutwa.

maraḍi ya mti[2]).

kwanza mtu huumwa maungo mazima, tenna hutembea killa kiungo. na dawa zake huchuliwa[3]) kwa mafuta ya nyonyo[4]), na kukandwa[5]) kwa kaziki[6]) na mafuta. ikiwa mtu bakhti[7]) yake — hupona. kama hana bakhti, hutokwa na kibiongo[8]), ao hulemaa mkono ao mguu ao huwa na kiharusi[9]). na mti ʿila[10]) yake unavunja pua.

maraḍi ya mshipa[11]).

mshipa mtu huzaliwa nao. kama baba yake alikuwa na mshipa, na mtoto hupata. na wengine wanaupata ukubwani kwa kutwaa mno waanawake. na maraḍi hayo feḍeha[12]) sana. huchekana Wasuaḥeli — mtu akiwa na mshipa. humwuliza: „lini mvua itakunya?“ hujibu: „kwani, mimi nna mshipa? nenda kwa fulani mwenyi kitongo[13]), atakupa khabari ya mvua.“ maʿana ya kitonga ni huo mshipa. na feḍeha ya maraḍi haya — mtu akikaa barazani na watu, na nje kuna mawingu, marra pumbu[14]) yake italia kama vyura vimo ndani. watu wakisikia, mtu mwenyi ḥaya[15]), akijua pumbu zangu zinaanza kulia — huondoka. mwenyi mshipa mbaya utamtuna[16]) upande kama chungu, jina

1) Sandkörner. — 2) skrofuläre Geschwüre. — 3) chua in streichender Weise massieren. — 4) Rizinusöl. — 5) in drückender Weise massieren. — 6) rauhe Fläche eines irdenen Topfes. — 7) Glück. — 8) Buckel. — 9) Krampf. — 10) Höhe. — 11) Hodenbruch, eigentlich Ader, Blutgefäß, Nerv, Muskel. — 12) Schande. — 13) Hodenschwellung, Bruch. — 14) Hoden. — 15) Scham. — 16) anschwellen.

lake unakwitwa „mshipa wa ngiri.“ [1]) kuna na „mshipa wa ŋ̃gombe,“ huo si mbaya.

watoto wengine, waliwozaliwa na mshipa, wanapikiwa dawa wakizaliwa. na mshipa hupikwa kwa dawa zake kuku na mzizi wa mwitu.

kaẓ̀alika Wanyamwezi na Wasukuma, wakiwa wazima, huupenda mshipa, wanaita luŋ̃gombe. kwao mtu mwenyi mshipa, hupata héshima [2]), sababu ana pumbu. lakini wao wanajua dawa zake.

maraḍi ya tego [3]) na kisonono [4]).

maraḍi ya tego yakimpata mwanamke ao kisonono, hafai kutwaliwa na mtu. akimwendea mwanamume yatampata magonjwa vilevile. tenna kujulikana kwake mwanamke mwenyi tego ukimtwaa — husituka, kama walivoimba:

„upande wa kusi usende,
upande wa kusi usende,
wanitonesha [5]) kasende [6]),
wanitonesha kasende.“

na dawa zake hilo tego mvuke [7]), huchuma majani, akapikiwa nyungu, hukaa juu ya kiti, na moshi ule humwingia katika uchi [8]). na akafanyiza oga, hawezi kuḥimili [9]) moshi, uchi utamkatika ote; ugonjwa wa tego mbaya. afaḍali kisonono.

dawa ya kisonono mzizi wa papaye dume [10]) na ubani mweupe, hutokoswa na maji, kisha hupewa mgonjwa kunywa mudda wa siku saba‘. kikiwa kisonono cha damu hukatika, akapata nafu‘u [11]). hii ndio khabari ya dawa ya kisonono na tego.

1) Warzenschwein. — 2) Respekt. — 3) Syphilis. — 4) Tripper. — 5) tropfen machen. — 6) kasende oder kaswende Syphilis. — 7) Baum. — 8) Blöße. — 9) aushalten. — 10) Payaye, die keine Früchte trägt. — 11) Gesundheit.

maraḍi ya pumu[1]) na kifua kikuu[2]).

pumu maraḍi yake hushikwa na kifua hukohoa[3]), na pumuzi[4]) zake huwa juu kwa juu, wala hawezi kusema kwa ṣauti[5]) kubwa. wala mgonjwa wa pumu hana nguvu, wala hawezi kwenda mbio, mwili wake mkavu kama samaki wa n̄gonda[6]), hupumuzika kama paka. na maraḍi yake mno humjia waqati[7]) wa mvua. khaṭari[8]), akinywa maji, kumsazia mtu, na kitu alichokitia kinywani mwake. hayana dawa maraḍi hayo.

kaẓälika kifua kikuu. vilevile mwanzo wake hukohoa. na akila kitu hutapika[9]). na kinapoqaribia kuwiva, hukohoa ḥatta akajamba[10]), na kifua humlia kana ngoma. akiwa katika nyumba, mpita njia hujua, mna mtu ana kifua kikuu. na makohóo[11]) yake hutoka damu. khaṭari kuyakanyaga[12]) makohóo hayo, sababu hupata maraḍi yaleyale yule mwenyi kukanyaga. kaẓälika naye kitu, alichokula, haifai kula mtu mwingine.

maraḍi mawili haya yakampata mtu, hapana dawa illa jembe[13]) na kiunza[14]), maʿana qabri[15]). yafaʿa mtu kujilinda na watu wenyi maraḍi haya.

maraḍi ya mdudu[16]).

mwanzo wake kidole huvimba ndani ya ukucha pasipo sababu. mtu akijua kidole kinaniuma, hujua mdudu. dawa yake hutia sifa[17]) ya papa kidole chote, ao hukata tunguja[18]). ukisha kata, huvika kile kidole. mudda wa siku tano ao sitta huwiva kile kidole, nacho huuma mno, hawezi kulala mtu. ḥatta kikesha wiva, usiku hupa-

1) Schwindsucht. — 2) Asthma. — 3) husten. — 4) Atem. — 5) Stimme. — 6) getrockneter Fisch. — 7) Zeit. — 8) Gefahr. — 9) erbrechen. — 10) furzen. — 11) Husten. — 12) auf etwas treten. — 13) Hacke. — 14) Totenbrett. — 15) Grab. — 16) Wurm. — 17) Haifischöl. — 18) nicht eßbare Frucht des Waldes, auch tura genannt, die in der Mitte durchgeschnitten über den Finger gestülpt wird.

suka pekeyake, hutoka usaha[1]) mwingi. kesha hupaka tenna sifa, ma'ana yake usibaqi usaha ndani, tenna huiondoa ile tunguja.

bardi yabis[2]).

mwanzo wake mtu hukonda, na uso wake hauwi na nuru[3]), wala hana nguvu za kwenda mbio, na moyo wake humpiga shindo ao kiñgita[4]). na akenda choo — haipati, na akipata choo — kigumu kama mavi ya mbuzi, naye huona uchungu sana. dawa yake huambiwa: „kula vyakula vya ruṭba[5]) kama nyama ya mafuta, ao kunywa maziwa ya mgandisho.“[6]) hukatazwa kunywa mtindi[7]), na kulla vitu vilivo vikavu, mfano wa nyama isiyonona, ao wali usio samli[8]). ao huambiwa „kula zabibu[9]) ṣafi,“ khaṣṣa[10]) wali wa mtama huambiwa kula sana, na mboga kulla siku. mudda wa mwezi mmoja ḥali yake hureje'a njema.

maraḍi ya bardi ya ruṭba[11]).

mtu huvimba miguu, akavimba na mashavu[12]). iwapo mtu mweusi, uso wake huwa kimanjano[13]) na mikono humvimba, ikawa minene. naye kaẓalika hawezi kwenda mbio. mzio[14]) wake hukatazwa kula nyama za mafuta ao samli. iwapo afanyiwa dawa, hula wali wa mtama — kitoweo papa mchanga[15]), hupikwa na siki ya mnazi — mudda wa siku saba'. na chakula chake hakitiwi chumvi nyingi — huzidi kuvimba. naye hukatazwa kukaa kikao kimoja, huambiwa kutembea. na kulla kitu kilichonona hakili, vitu vinono kama mfano embe mbivu ao ndizi mbivu ao wali wenyi samli nyingi.

1) Eiter. — 2) Rheumatismus. — 3) hat keine Farbe. — 4) beides — Herzklopfen. — 5) saftig, fett. — 6) Milch mit Sahne. — 7) Buttermilch. — 8) Fett. — 9) Rosinen. — 10) besonders. — 11) feuchte Kälte. — 12) Wange. — 13) gelb. — 14) Verbot. — 15) junger Haifisch.

maraḍi ya tambazi.

tambazi maraḍi yake humwingia mtu tumboni, hayatoki nje. watu wajuao, kama ana tambazi, hununua mkaa[1]), wakausaga katika mkungu, humpa akanywa. nao mchungu sana. mudda wa siku tatu hutokea nje yale maraḍi, hujulikana toki[2]) ao uvimbe[3]). huugua yule mtu, ḥatta utumbuke pekeyake. humsagia dawa kumpaka palipotumbuka — mfano wa moshi[4]) wa nyumba, ao husaga dalia akapakwa. hutezama kama dawa inayomfa'a. na mwanzo wa maraḍi yake hayo. kama hawakusaga mkaa kumpa kunywa, maraḍi yakakaa ṭumboni, hufa mtu.

maraḍi ya tende[5]).

tende áṣili yake huvimba miguu, ikawa mfano wa kinu. na maraḍi hayo hayana dawa, hayawivi, wala hayatumbuki. na mwinyi tende hawezi kwenda upesi. wengine huwa na tende mguu mmoja, wengine yote miwili. na Wasuaḥeli wanaṣadiqi tende áṣili yake matenzo[6]), amefanyiziwa kitu, kimewekwa njiani, naye amekikanyaga ndipo miguu ikamvimba. ndio ma'ana kwitwa tende, ma'ana ametendewa kitendo.

maraḍi ya ṣafra[7]).

mwanzo wake mtu huvimba maungo yote ḥatta macho, na rangi yake huwa kimanjano[8]). ma'ana yake maungo yake hana damu[9]) illa usaḥa[10]). ukimgusa hubonyea[11]). dawa yake hutwaliwa makaa ya chuma[12]), hutwangwa, unga wake hupikwa na asali ya miwa[13]), killa aṣ-ṣubuḥi hupewa kidogo kuramba[14]) mudda wa siku

1) Rinde eines Baumes aus Indien. — 2) Ausbruch. — 3) Schwellung. — 4) Ruß. — 5) Elephantiasis. — 6) von tenda handeln, jemand etwas antun, matenzo also böser Zauber. — 7) Gelbsucht. — 8) gelb. — 9) Blut. — 10) Eiter. — 11) einsinken. — 12) Eisenspäne. — 13) Zuckerrohrsyrup. — 14) lecken.

saba‘. na chakula chake wali wa mtama, na kitoweo chake ni mboga ya mchicha [1]) ao papa mchanga [2]) ao siki [3]) mudda wa siku saba‘.

maraḍi ya jongo [4]).

áṣili yake mshipa [5]) hujikunja [6]) maḥali pamoja. iwapo umejikunja juu ya mguu, huchuliwa kwa mafuta ya nyonyo. na hilo jongo hutambaa maungo [7]) yote. na iwapo limefika juu ya mongo [8]), huchuliwa vilevile kwa mafuta ya nyonyo, na kuwekewa kitu kilicho kizito juu ya mongo wake ao kifuani ḥatta apone.

maraḍi ya choa [9]).

choa maraḍi yake hutunga vipele [10]) vidogovidogo maungoni na kufanya mabumbuza [11]). dawa yake husaga pesa, maji ya pesa hupakazwa juu ya vile vipele. na asipopona, maraḍi yakipevuka, hutokewa na ukoma.

maraḍi ya ḥarara [12]).

hupatikana waqti wa kasikazi [13]) kwa sababu jasho jingi ndani ya maungo. maraḍi yake mtu hututusika [14]) maungo yote. dawa yake husagwa dalia ya maji, akapakwa maungo yote. tenna maungo yake huwa baridi, ikikauka dalia, naye amepona.

maraḍi ya kifafa [15]).

áṣili yake mtu hupitiwa na kitu mbele yake usiku, akikiona — husituka [16]). ba‘ada ya kusituka hutokewa na ḥoma, mwisho wa ḥoma — yanapoanza hayo maraḍi ya kifafa huanguka. kulla mwezi huanguka. na

1) Spinat. — 2) junger Haifisch. — 3) Essig. — 4) Gicht. — 5) Ader. — 6) Knoten bilden. — 7) Körper. — 8) Rücken. — 9) Ringwurm. — 10) Pickel. — 11) Bläschen. — 12) roter Hund. — 13) heiße Jahreszeit. — 14) ausbrechen. — 15) Fallsucht. — 16) rschreckt werden.

anapoanguka, hutokwa na povu[1]) kinywani mfano wa frasi. nayo haina dawa maraḍi haya. na akila kitu, ao akinywa maji, haifai mtu mwingine kunywa. anywapo, hupata maraḍi yake.

maraḍi ya chumjua[2]).

áṣili yake huota kipele[3]) maungoni, nacho kina mdomo. na kinapoota hicho kipele, dawa yake hukatwa kwa wembe, tenna hupakwa taka[4]) za mwili palepale palipokatwa, marra hukauka.

áṣili ya vilema[5]).

mtu akiwa na makengeza[6]), mama yake alipokuwa na mimba pevu[7]), akitezama mwezi sana, ao akatezama mtu mwenyi makengeza, akizaa mtoto, naye hupata makengeza. nayo hayana dawa.

amma mtu mwenyi chongo[8]) áṣili yake huugua macho, ao hugomba na mtu, akampiga fimbo ya jicho, likapofuka jicho. na hayo maraḍi ya macho huambiwa mtu kosha macho yake kwa maji ya umande[9]) killa aṣṣubuḥi. ao huchuma majani ya mbazi[10]), yakasagwa[11]), maji yake hukamuliwa[12]) jichoni. ao husagwa njano[13]), maji yake hutiwa pamba iliyo ṣafi, akabandikwa juu ya macho. ao huchumwa majani ya mwingajini[14]), majani yake husagwa vilevile, maji hukamuliwa jichoni. ao majani ya mqablishemsi[15]) yakafanyizwa vilevile. na mwanzo wake hutiwa lile jicho zima kwanza, khalafu likatiwa la pili.

---

1) Schaum. — 2) Warze. — 3) Pickel. — 4) Schmutz des Körpers. — 5) körperliche Gebrechen. — 6) schielen. — 7) reife Schwangerschaft. — 8) einäugig. — 9) Tau. — 10) indischer Bohnenstrauch. — 11) saga mahlen. — 12) kamua pressen. — 13) Gelbwurz. — 14) Baum. — 15) Baum.

áṣili ya kiziwi [1]) — mtu huingiwa na mdudu [2]) shikioni, akafa yule mdudu asitoke. mtu huugua shikio, hufanyiziwa dawa. mwanzo wake hutiwa maji shikioni, kisha huinama, maji yatoke, hutoka na yule mdudu vilevile. na kama mdudu hakutoka, hufanyiza dawa nyingine.

áṣili ya bubu [3]) — mtu huzaliwa nao ububu, na kitembe [4]) na kigugumizi [5]) vilevile. hayana dawa maraḍi hayo.

wa amma maraḍi ya kichaa [6]) áṣili yake mtu amekuwa na mali — yakampotea, ao ni kufiwa na mke, ampendaye. mwanzo wake husema pekeyake, watu wakimsikia humcheka, naye huqaṣirika. tenna hufanyiwa dawa, na dawa yake hutiwa katika chumba chenyi kiza, naye mwenyi hajijui mimi nipo wapi, wala hajui, kwamba watu wananifanyia dawa. hukaa mudda wa mwezi ndani, hutolewa nje kutazamwa ʿaqili [7]) yake. amma dawa ya pili huchinshiwa nyama ya mbwa, naye mgonjwa hajui kama nyama ya mbwa, hupewa pamoja na chakula akala. hupewa marra moja, khalafu hutezamwa — ʿaqili yake imerudi ao haikurudi.

khabari ya nzige [8]).

mwaka, walioshuka nzige katika mrima, yalikuwa taʿabu [9]) kubwa na maraḍi mengi.

kwanza yaliingia maraḍi ya tumbo. mtu akasema „nna tumbo linaniuma“ — akiwa na jamaʿa yake, huenda kwa Mhindi kununua sanda [10]) ṭayyari [11]), ḥatta aṣṣubuḥi amekufa.

---

1) Taubheit. — 2) Wurm, Insekt. — 3) stumm. — 4) anstoßen mit der Zunge. — 5) Stottern. — 6) Verrücktheit. ana kichaa, ana wazimu oder ana mahoka werden gleichbedeutend gebraucht für „er ist verrückt“. — 7) Verstand. — 8) Heuschrecken. — 9) Not. — 10) Leichentuch. — 11) fertig.

tenna akaingia maraḍi ya ndui. mtu akasema „leo siwezi, nna ḥoma,“ atalala — ḥatta aṣ-ṣubuḥi ndui zimemtoka maungo yote. mudda wake siku sitta, ya sabaʿ amekufa. walikuwa wakizikana — ḥatta khalafu waanawake huchukua maiti[1]), wakenda wakazika.

baʿada ya hayo ikaingia njaa[2]) kubwa. mimea killa ikapandwa — haiji juu, sababu ya nzige, walivoshuka wengi. hamkuwa na kitu mashamba — muhogo wala vyazi wala mpunga wala kitu kinacholiwa. kaẓâlika makuti ya minazi — yote yalikwisha, sababu wanaposhuka hao nzige, hushuka juu ya minazi ao ya miembe kula yale makuti. na mtu akataka kutembea njiani, afumbe mdomo, asimeze nzige.

na hao Wanyamwezi na Wasukuma, waliokuwako katika mrima waqati huo, walikuwa wakenda shamba kukamata nzige. huwatia katika magunia, huwaleta katika mji kuuza kwa Mabulushi na Washihiri. nao huwakaanga, wakatia chumvi, kesha huanika, wakawapakia kuwapeleka barra ʿArabu na Makarani zawadi. nao wanawapenda sana kula kama Wanyamwezi. na Wasuaḥeli wengine wanakula nzige, wengine hawataki.

namna ya pili ya hawa nzige wadogowadogo, wanakwitwa vimatu. wakaingia katika shamba la miwa ao la ndizi ao mpunga, wakalala usiku kucha ḥatta aṣ-ṣubuḥi — hapana kitu. na mate yao mabaya. kitu walichokisaza kama mua ao muhogo ao vyazi, mtu akala, huona chungu sana. ukiwa mua — umepooza, ukiwa muhogo — mchungu, ukiwa mpunga — wali wake mbaya.

na kuwafukuza kwao wanaposhuka, hupiga madebe ao hufanya maputo[3]) kuwapiga, lakini hawaondoki.

---

1) Leichnam. — 2) Hungersnot. — 3) von puta schlagen; puto einige Zweige mit Blattwerk daran.

afaḍali mvua inapokunya, wengi wanakufa, ḥatta mayayi yao hayazai watoto.

na mwaka uleule, baʿada ya nzige kuondoka, likaja baa la jua kuwa kali kushinda baa la nzige, vitu vyote vikakauka mashamba. na baa likawashukia jua kuwa kali, ao maraḍi mengi katika mji — husema „muungu ametuqaṣirikia, sababu tuna mambo maovu, tuliyofanyiza,“ husema „wâjibu wetu tulete toba.“ [1]) na toba yao wanapokwenda kuṣali, huomba duʿa [2]) kwa muungu ya kutaka samaḥa [3]), awaondolee baa, lililowashukia, husema: „yâ rabbi, wewe ndiwe unayoona yote, tufanyayo, lakini wewe huonekani, tupokelee duʿa zetu, utuondolee maraḍi na shidda [4]) uliyotuletea kwa fáḍila [5]) zako.“

khabari ya funza [6]).

mrima wameingia wadudu, jina lake funza. wadudu hao wabaya sana. nao wadogo kama punje ya mchanga. na áṣili yake wametoka kèp [7]), wameletwa na wapagazi katika mizigo, wameenea mirima yote. na uḍaʿifu [8]) wao anapoingia katika mguu, mtu hajui, illa huona unyenyefu [9]) mguuni — amekwisha ingia. mudda wa siku tatu amekuwa kama punje ya mtama ao muhindi. naye huingia killa paḥali mkononi ao mguuni ao paḥali pengine.

na kutolewa kwake kwa shindano. na atoaye, sherṭi yataka mtu anayejua, asiyejua kumtoa, akimtumbua yule mdudu, hufanya kidonda, lâzima amtoe mzima. na hao wanaotoa vibaya wadudu, watu wengi wameḥaribika miguu na kukatika vidole, sababu mate yao ni mabaya, hufanya usaḥa. na mtu miguu yake

1) Reue. — 2) Anrufung. — 3) Verzeihung. — 4) Unglück. — 5) Güte. — 6) Sandfloh. — 7) Capland. — 8) Schlechtigkeit. — 9) Kitzel.

iwapo michafu, hufanya ndio nyumba, hawaondoki. yaḥitaji killa aṣ-ṣubuḥi na jioni miguu kuiosha kwa maji ya moto. na anapotolewa yule mdudu, kuoshwa kwa maji ya moto, ijapo wataingia — si wengi. na namna yao wadudu hao kama mfano wa viroboto[1]) vilivo vidogo. na ʿażabu[2]) kubwa wangiapo[3]) katika miguu ya watoto wadogo, wasipotezamwa, huḥaribika miguu yao.

1) Floh. — 2) Strafe. — 3) waingiapo.

khabari ya mtu kuzikwa.

kuzikwa kwake mtu akifa, ukiwa usiku, hutoka mtu kupeleka khabari kwa ndugu za yule aliyekufa. wakifika, wataamru kuchimba ufuo. nao huchimba chini ya kitanda, alipo yule mtu aliyekufa. ma'ana mtu aliyekufa lâzima kutendewa mambo manne. la kwanza akifa huoshwa, la pili hukafiniwa sanda, la tatu huṣaliwa kwa dini yake, la nne huzikwa katika qaburi.

watu wanaomwosha maiti[1]) watu watatu. mmoja „mshika kata“ humtia maji yule maiti, na maji haya huingia katika ule ufuo uliochimbwa chini. na „mkangama“ humfinya mavi, na „mwegamu“ humzuia maiti. na kuosha kwetu huosha kwa maji ya majani ya mkunazi[2]). na mwisho humwaliza kwa garafuu maiti[3]). kisha humfunika mfuniko mpya. hawalali tenna usiku kucha, wake na waume wanalia.

aṣ-ṣubuḥi watapeleka khabari killa paḥali, ambapo yule maiti pamempasha — mashamba ao mjini. watakuja, kulla mtu amechukua sanda[4]) — feḍḍa ao bafta. wale watu waliofika, hupelekwa katika chumba, alichomo yule maiti. killa mtu hummiminia kata tatu za maji kichwani ḥatta miguuni.

---

1) Leiche. — 2) Brustbeerbaum. — 3) Kampfer. — 4) hier Beitrag zum Leichentuch.

marra hutumwa mtu kuitwa mwʿallimu na majumbe. na iwapo aliyekufa kijana wa mji, yule mwenyi maiti yake atawapa shauri majumbe: „tunataka kuzika.“ watajibu: „qaburi imechimbwa?“ kama bado, watauliza wale majumbe: „mtamzika wapi, Kingani ao Nunge ao Pangapanga?“ maʿana katika mrima killa mtu ana paḥali pake pa kuzikwa. Wapangapanga sherṭi wende huko, kama hawakufanyiza hivo — beina yao watagomba, ao nuṣṣu ya watu wataondoka katika maziko. na sababu ya killa mtu ana paḥali pake pa kuzikwa — sababu yake katika uzazi wa mrima, hutezama qabila[1]). qabila ya kina fulani ndio inayofaʿa kuzikwa Pangapanga, na qabila ya kina fulani huzikwa Nunge. lakini wageni, watu wa Unguja, hawazikwi maqaburi hayo, wala watumwa hawendi maqaburi hayo. hio ndio maʿana ya kuzikwa katika paḥali mbalimbali. killa mji wa mrima una maqaburi kama hivo, tulivotaja Bagamoyo, na majina yake ya maqaburi.

watu wakipatana, watakwenda chimba qaburi upande walioelekezana. majumbe watatoa amri kushonwa sanda, watoe na taʿarifu ya mtu aliyekufa. marra atakwitwa kabiri, maʿana mpiga zumari, atasimama mlangoni na shaha mmoja, atasema shaha: „kina mwana, pokeni taʿarifu, fulani bin fulani amefariqi dunya.“[2]) yule mpiga zumari marra atapiga zumari, na uwanjani zipigwe ngoma kuu. waanawake wanalia ndani, na waanaume wanashona sanda.

na sanda ya mwanamume nguo tatu, na kanzu na kilemba, na mwanamke sabaʿ, majamvi matano, na nguo ya kujifunika, na ukaya. na katika sanda kushonwa — watani[3]) wanataka ʿada zao. wakesha shona, watatia ile sanda dalia na marashi, wafukize na ubani.

1) Familienstamm. — 2) sich von der Welt trennen. — 3) Stammesgenossen, Vetternschaft.

wataingia ndani watu watatu, iwapo aliyekufa mwanamume, wamvike ile sanda waifunge maiti katika mkeka. kisha wamtie katika jeneza[1]), waitambushe kizingitini[2]), huganga marra tatu ile jeneza. kesha watashika watu wanne, wawili mbele wawili nyuma, wanyanyue, husema: „lâ ilâha illâ 'llâh, lâ ilâha illâ 'llâh, lâ illâ 'llâh illâ 'llâh, Muḥammed er-rasûlu 'llâhi.“[3]) na wanaofuata jeneza huitikia, ḥatta wafike mskitini. wakifika, wataitia ndani jeneza, waingie na watu wengine, aṣaliwe yule maiti. kesha watakwenda qaburini, azikwe maiti.

na kuzikwa kwao qaburi hufunikwa juu na nguo, hukaa watu watatu katika qaburi kupokea yule maiti. akifika maiti, mtu mmoja huʿaẓẓini[4]). kesha humlaza yule maiti ndani ya mwana wa ndani[5]), wakaweka ubao wa kiunza juu ya yule maiti, kesha hufukia lile qaburi.

na hawa watu watatu, waliochimba qaburi, hawaondoki katika qaburi, hatta lijae, lakini hawafukii pekeyao, wote huwasaʿidia. na wakiwa watani, na utani wao hawakupata, hawampi rukhṣa maiti kuzikwa, ḥatta wapate ʿada yao.

wakesha, huleta mtungi wa maji, akakaa mwʿallimu juu ya kichwa cha qaburi, akafukua tundu, akasoma talaqîni[6]), akatia maji ya shahada, maʿana yake ni kuwa yeye muslim. tenna huzika mibono[7]) pembe zote nne, miti midogo, khalafu yake hukua ile miti, ndio ushâhidi kwa watu kujua, ya kama hii ni qaburi. tenna husoma fâṭiḥa watu, huenda nyumbani. na yule mfiwa lâzima hulia kiwimawima.

---

1) Bahre. — 2) Türschwelle. — 3) muhamedanisches Glaubensbekenntnis, siehe Uebersetzung. — 4) zum Gebet rufen. — 5) Nische unten im Grabe. — 6) Belehrung, Anrede an den Toten. — 7) Rizinussträuche.

khabari ya kuḥani [1]).

watu waliotoka qaburini, wote huenda kule nyumbani kumḥani mfiwa. nao humwambia: „makiwa.“ [2]) naye hujibu: „yangali yakija,“ [3]) ao husema „yamepita.“ ao humwambia: „aḥsana 'llâhu ʿazzaka,“ [4]) hujibu: allâhu al-bâqa,“ [5]) maʿana muungu ndiye atakáyebaqi.

khabari ya matanga [6]).

kesha kuḥani, watu watauliza: „pana tanga ao hapana?“ atajibu: „lipo.“ watamuliza: „lini utaweka tanga?“ atajibu: „saʿa ya tatu ya usiku.“ saʿa ya tatu killa mtu atachukua mkeka wake na mto kwenda lala tangani, na waanawake vilevile. usiku hufanyiza ḥadithi [7]) ndani, na waanaume hufanya ḥadithi vilevile. na wengine wanacheza karata. ḥatta al-fajiri huja mpiga zumari, akapiga mlangoni zumari, waanawake hulia na waanaume wengine hulia. na wengine huenda meskitini.

jua likapata saʿa ya tatu, hukutana tenna waanaume na waanawake kufanyizwa mashauri ya kwenda koshwa mashambizo. wakesha kutana, waanawake hufukia ule ufuo, tenna hutwaa nguo, alizooshewa yule maiti, ndio mashambizo. na mashambizo hutiwa katika chano. wakafanyiza ukingo, maʿana ukingo hufungwa nguo, zikawa ndefu, mfano wa chendarua, na watu huwa ndani, qádiri ya waanawake wanne ao sabaʿ. na waanawake watatu huchukua yale mashambizo juu ya kichwa kwenda pwani kuyaosha. na mpiga zumari nyuma yao huimba mwimbo:

---

1) Beileid bezeugen. — 2) traurige Sache (ist vorbei). — 3) es wird noch mehr Trauer über uns kommen. — 4) möge Gott dein Ansehen schön machen d. h. möge er deine Trauer znm Guten wenden. — 5) Gott ist der Ewige. — 6) Trauerfeier. — 7) Erzählungen.

„mwajeje huo[1]) leô
yô mwajeje yô leô?“

1) mwaonaje huo msiba.

ḥatta wakifika pwani, hujitosa katika maji koga. na wasiwokoga, wenzao huwambia: „kwa nini ninyi hamwogi?“ ʿhufumbiana fumbo, husema: „wengine wana vijani vya mbaazi, hawataki kuonekana.“ wakesha osha mashambizo, hurejeʿa mjini, vilevile kama walivokuja, maʿana huwa ndani ya ukingo. wakifika tangani, yale mashambizo huyagawa, lakini hapati mtu ovyo, illa aliyemkhuṣṣi yule maiti, maʿana ni ʿada kubwa kwao — kunkumbuka yule aliyekufa.

na killa mtu akija kuzikani, huchukua kitu kama alichonacho, máthali kama riale ao rupia ao mapesa ao kitu kinginecho. siku ya kuondoa tanga, baʿada ya siku sabaʿ labda, vitu vile hufanyiziwa ṣádaqa ya yule maiti katika nyumba yake, maʿana husomwa khitima, wakafanya karamu, wakaalikwa watu kuja kula. na huyu mfiwa huwa na masikitiko mengi sana, hulia kwa kurombokeza[1]) — ya kama: „fulani umenitupa, umenacha pekeyangu, watu watanitia vidole vya macho — hapana wa kuniuliza.“ marra huja mtu kumnyamaza, humwambia: „nyamaza, usilie, haya ndio mambo ya dunya, mwanzo kuzaliwa mwisho kufa, si yako wewe pekeyako, killa mtu yatampata.“

na kama mwenyi kufiwa hana kitu, khitima yake husoma mwakani, hungoja ḥatta apate feḍḍa kidogo. na baʿada ya siku arbaʿîni hufanyiza ṣádaqa, jina lake „ʿarbaʿîni ya maiti.“

na kule tangani wazee waanawake hujifunga vitambaa kichwani. zamani tangani wazee waanawake

1) in weinerlich singendem Ton wehklagen.

wengine walikuwa na khaṭari, sababu wanapotanga — huja wanga[1]), hucheza usiku kucha.

zamani moja alikufa mwanamke kule Bagomoyo. alipokufa, watu wamezika, usiku wamelala watu tangani, akaja mwanga, jina lake Mamie Ibrahimu, akaanga tangani. nao wanga áṣili huenda uchi. yule Mamie Ibrahimu alijifunga pweza[2]) kumani, sababu ndio nguo zao wanga.

ḥatta al-fajiri anarudi kwake, akakutana na mtu jina lake Bwana Mzee. akamkamata, akamwambia: „tafáḍḍali nisitiri[3]) ʿaîbu[4]) yangu, nitakupa kitu utakacho.“ Bwana Mzee akasema: „sikuachi, wewe mtu ʿadui sana, umeangamiza roho za watu nyingi.“ akampeleka huyu mwanamke ḥatta tangani, watu wote wakamwona uchi.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi kulivokucha, wakamfunga mapakacha mwili wote pia, wakamtembeza mji mzima. watu wote wakamwona, wakamwuliza: „utarejeʿa kazi yako ya wanga?“ akasema: „sifanyi tenna.“ wakamwambia: „tutakupa yamini, ukafanya marra ya pili — ufe.“ akaqubali, akapewa yamini. baʿada ya miezi michache akarejeʿa kazi yake kwa sirri. muungu akampa maraḍi ya wazimu, hutembea uchi katika njia, na kutukana watu, na mvua ikanya, hujitia tope kichwani. ʿomri wake ukawa mchache — akafa.

na khabari ya kukamata mchawi, yataka mtu awe mpevu. kijana hawezi kumkamata, maʿana ana khofu ataḍurika, ao ataugua. na iwapo umemwona mchawi mbali anakuanga — sumu yake mpige ndimu, akikwambia „piga marra ya pili“ — usimpige, marra nenda ukamkamate. imekwisha khabari ya kuḥani pamoja na wanga.

---

1) zaubern. — 2) Fisch. — 3) bedecken. — 4) Schande.

khabari ya tanzia[1]).

mtu akiwa amefia mbali, huletwa taʿarifu katika mji kwa ndugu zake — ya kama:
„wa baʿadu twawaʿarrifu, ndugu yenu fulani amefariqi dunya. innâ lillâhi wa innâ ileihi râjʿeûna, haża sebîl ed-dunya wa ṭarîq el-âkhera[2]). ao husema: umetupitia mṣiba[3]) wa fulani, amekufa, hii dunya ni njia na njia ya mwisho. maraḍi alikuwa na ndui za mhindi siku tano, ya sitta amekufa.“

wakisikia ndugu zake ile barua — hulia, huamrishwa na ngoma kuwekwa uwanjani, iwapo ni mtu amezaliwa juu ya ngoma, maʿana baba yake na mama yake wana daraja ya ngoma.

khabari ya kufa kwake jumbe.

aliyekufa, iwapo jumbe, aṣ-ṣubuḥi watu wakipata khabari, jumbe fulani amekufa, watu hukusanyika mazikoni. marra hutolewa taʿarrifu ya taʿazia, ya kama: „tunawaʿarrifu, jumbe fulani ametoka juu ya ulimwengu.“ watu wote huvua kofia na kanzu na vyatu, wakabaqi killa mtu nguo moja.

ua iwapo aliyekufa shaha ao waziri, watu wa mji hawavui kanzu, illa vyatu na kofia huvua. na majumbe huvua vilemba.

na mtu wa kimrima akikataa kuvua kwa zamani za kwanza — hupigwa, lakini sasa watu wengine wanamkhaṣimu[4]), sababu daula[5]) imekuwa nyingine.

każa̧lika kuzikwa kwake jumbe: waqati wa koshwa hana rukhṣa mtu mwingine kumwosha illa shaha. na iwapo hapana shaha — mtoto wa shaha. na waqati

---

1) das arab. taʿaziye. — 2) siehe Uebersetzung. — 3) Unglück, Trauer. — 4) feindlich gesinnt sein. — 5) Regierung.

wa kuzika sherṭi majumbe wote wakutanike tangani. na waanawake wengine wanapiga ngoma uani, wengine wanalia. ngoma hiyo jina lake mwanamama. na uwanjani ngoma kuu na siwa na zumari zinalia. na mshindo unaopigwa jina lake kibagaja. huondoka majumbe mawili wakacheza. na killa mtu amechukua sanda yake. na sanda anayozikiwa — iliyotoka katika feḍḍa yake, na zile zilizokuja na watu wengine — hupewa ʿada za watani na wachimba qaburi na wachimba ufuo na waʿallimu, waliopo katika ḥáḍara.

ikesha sanda, ataingia ndani shaha, akamkafini, maʿana kuvikwa sanda. kisha atatiwa katika jeneza, apelekwe qaburini kuzikwa.

na tanga lake siku kumi na nne ao siku sabaʿ, iwapo hana kitu. na kulla al-ʿaṣiri huja watu tangani, hucheza karata na ngoma kuu, na waanawake hucheza mwanamama. ḥatta siku ya kuondoka tanga hununua ñgombe. na huyo ñgombe, anayochinshwa, ana ʿada nyingi sana. majumbe hupewa nundu, na mashaha hupewa mkono pamoja na mawaziri, na kiuno cha ñgombe nyama yake hupelekwa waʿallimu, nyama iliyobaqi hupikiwa karamu.

zamani mtu akafanyiza karamu, amechinsha ñgombe — majumbe kama hawakupewa nundu na mashaha hawakupewa ʿada yao — karamu hiyo hapana mtu atakáyekwenda, sababu husema fulani hana adabu, khasara yake aliyoifanya, maʿana majumbe wameqaṣirika wote. lâzimu awaangukie yule mwenyi karamu yake, atoe feḍḍa.

kaẓálika desturi ya majumbe wanapokula, hawali barazani pamoja na watu, hutandikiwa chumbani, haingii mtu illa mwandazi, wakitaka kitu, humwambia yule mwandazi. wanapokula, hupigwa siwa na zumari.

kaẓâlika iwapo jumbe ni moja, hapana mwingine, lakini katika baraza yupo sherifu, ao mwʿallimu, ataamru kwitwa moja wapo sherifu ao mwʿallimu, lakini mtu mwingine hali naye, illa iwapo nyumbani kwake kama si karamu.

kaẓâlika yule mwʿallimu huvua kofia, illa sherifu havui. ao mwʿallimu hupata rukhṣa kwa jumbe — ya kama: „wewe mwʿallimu haifai kuvua kofia, ukila na mimi.“

khabari ya kuḥallilia[1]) mbwe.

mtu aliyekufa, baʿada ya kuzikwa zikapata siku tatu ao sabaʿ, wenyi maiti wao hutafuta mbwe. na hizo mbwe mawe madogomadogo, ni magumu sana. kisha huyaosha kwa maji, ḥatta yakawa ṭahara. khalafu huenda wakaweta waʿallimu watano ao sabaʿ. watakapokuja, hutandikiwa mikeka, wakakaa kitako. tenna huletwa mbwe mbele zao waʿallimu, wakaziḥallilia. maʿana ya kuḥallilia: hushika killa mwʿallim mbwe moja, husema: „lâ ilâha illâ 'llâhu.“ [2]) na ʿidadi[3]) ya hizo mbwe hupata elfu, nao husema killa mtu: „lâ ilâha illâ 'llâhu“ — marra elf, nao hawasemi na mtu, illa kwisha. na wanapokwisha, hutwaliwa zile mbwe, zikatiwa katika kitambaa, hupelekwa qaburini, zikawekwa juu ya qabri. na wale waʿallim hufanyiwa karamu kula. kisha hupiga fâṭiḥa kumreḥemu maiti aliyekufa. nao hupewa ijara yao ya kuḥallilia mbwe, kama walivopatana toka riale tano ḥatta khamstʿashara.

---

1) ḥallil = taja jina la muungu. — 2) siehe Uebersetzung. — 3) Zahl.

khabari za majumbe.

khabari ya jumbe kutawalli [1]).

mtu mwenyi kuzaliwa katika ujumbe, na baba yake jumbe, naye amekufa, baʿada ya kuchuma akipata, huwapa khabari majumbe waliwomtangulia: „mimi nataka kutawalla.“ nao hujibu: „vema, lakini twataka ʿada [2]) zetu.“ atawapa ʿada zao, maʿana nguo ao mapesa, naye huwapa mashaha [3]), ndiwo wanawopeleka. kisha hutoa ʿada mashaha na mawaziri na vijana wa mji. sababu wasipopata, yule jumbe akitawalli — hawamwamkii, illa ndugu zake na watumwa wake.

na siku zake zikiwa qaribu, bado siku sabaʿ anataka kutawalla, hukutanika majumbe wote, jumbe mmoja husema: „twataka kutoa taʿarifu, siku fulani Mwenyi każa wa każa anatawalli, jina lake jumbe fulani.“ marra huitwa mpiga biu, akazunguka na mbiu mji mzima, naye husema:

„mbiu [4]) ya mgambo [5]) — ikalia haina jambo [6]) — mbiu ya shomvi [7]) na arbaʿini [8]) — mpumbuji [9]) na mjumbe [10]) — mbiu ya pazi [11]) na wana wa pazi — na

1) Amt antreten. — 2) übliche Geschenk. — 3) der zunächst unter dem jumben Stehende. — 4) Büffelhorn. Bei dem Worte mbiu schlägt der Ausrufer jedes Mal mit einem Stock an das Horn. — 5) Bekanntmachung. — 6) es gibt nichts zu verheimlichen. — 7) jumbe. — 8) Leute der Stadt. — 9) Die shaha und waziri. — 10) die wazalia. — 11) Herrscher.

wasengere[1]) na wamganda[2]) — mbiu ya Makame ya Shani[3]) na wangwana wa Winde — Uqasimu[4]) na waungwana wa Shanga — mbiu ya shomvi anawaᶜarrifu — ya kama siku ya jumaᶜ a tatu — kishina[5]) na mwanamama[5]) — siku ya al-khamisi — Mwenyi fulani anatawalla — jina lake sasa jumbe Mkomatembo.“

marra usiku waanawake na waanaume hukutanika ndani ya nyumba, kucheza ngoma usiku kucha ḥatta aṣ-ṣubuḥi. nao huimba:

„yaliyo mumo — ya mumo[1])
wende kutanda ushimba[2])
mtu na mkwewe.“[3])

1) was drinnen ist, laß drinnen bleiben d. h. ein Geheimnis plaudere nicht aus. — 2) Fische fangen mit Tüchern. — 3) Schwiegermutter.

ao huimba:

„utembezi[1]) haulei mwana.“

1) eine Mutter die viel spazieren geht.

ḥatta aṣ-ṣubuḥi hucheza ngoma kuu. na majumbe wanapocheza, killa jumbe ana wapambe[6]) wawili, na kulla mpambe ana upepeo[7]), humpepea yule jumbe. na yule jumbe mpya yumo ndani, anapigwa kilemba ḥatta akisha, hutiwa katika kilili[8]) na mwanamke pamoja juu ya kilili, naye huyu mwanamke huwa mzalia, ameshika mwavuli katika mkono wake. na watu huchukua kilili juu ya mabega kumtembeza mji mzima. ḥatta wakirudi nyumbani, yule jumbe mpya atacheza naye. kesha hukaa barazani na majumbe wenziwe. naye hukalia kikuto[9]) cha mkeka. hucheza killa ngoma za furaḥa siku sitta ao sabaᶜ kama wanavoweza.

1) wazalia. — 2) watumwa. — 3) jumbe von Winde. — 4) jumbe von Shanga. — 5) ngoma. — 6) geschmückte Sklavin. — 7) Fächer. — 8) Bettstelle. — 9) zusammengelegte Matte.

kaẓâlika jumbe si desturi kwenda katika njia kichwa wazi, wala katika nyumba yake hakai kichwa wazi. iwapo hapana mtu atakáyemwona, hukaa kichwa wazi. wala juu ya kilemba, alicho nacho, si desturi kuweka nguo nyingine. afanyapo mambo hayo, wakimwona mashaha, watamtoza ḥokumu[1]), amefanya mambo siyo desturi. naye hafanyi ukaidi[2]), atatoa kama watakacho awape.

qiṣṣa[3]) cha jumbe Simbambili.

ilikuwa qabla ya miaka minne alikufa jumbe Korandi. wakaja watu kutaka kumzika. akatokea jumbe Simbambili, akamwita mnyozi, akamwambia: „ninyoe nywele zangu.“ akamtengeneza nywele. alipokwisha, akenda tangani. majumbe walipomwona, wakamwuliza: „sababu nini umekuja tangani umenyoa?“ akasema: „mtaniḥokumu na kichwa changu?“ wakamjibu: „umefanya mambo si ya desturi ya kimrima.“ akasema: mimi nimenyoa, na kulla mwenyi nywele zake na anyoe.“ wakamkhaṣimu[4]) majumbe wote. wakafanya mkutano majumbe, wakawambia vijana: „msimwamkie Simbambili.“ killa njia apitayo, wanamsema — ya kama: „jumbe huyu ndiye aliyemroga[5]) jumbe Korandi, sababu amekwenda tangani amefanya uzuri.“

siku moja aṣ-ṣubuḥi ametoka nje hana kilemba. watu wakamwuliza: „sababu jumbe huna kilemba?“ akajibu: „mimi si jumbe, siutaki ujumbe, sababu mji wote hawaniamkii.“ ndugu zake wakasema naye: „si vema jumbe, kuji'uzulu[6]) hiyo ni feḍeḥa[7]) kubwa.“ akavaa kofia na kilemba, lakini watu wazima katika mji

---

1) Urteil, Geldstrafe. — 2) Widersetzlichkeit. — 3) Erzählung. — 4) feindlich sein. — 5) bezaubern. — 6) Kopfbedeckung abnehmen. — 7) Schande.

wanasema — ya kama: „jumbe huyu hatakuwa na ma'isha[1]) mengi.“

ba'ada ya miezi mitatu akasafiri kwenda Khutu, ma'ana ndiko kwao. akakaa miezi miwili, akapata ugonjwa wa mshipa. wakamrejesha pwani. akafikia shambani kwake, akakaa siku saba', ya nane aketa[2]) ndugu zake, kuwapa buriani[3]), ḥatta usiku akafa. wakamleta mjini kumzika, majumbe na vijana wakakataa kumzika. akazikwa na jama'a zake, hakupata ḥaththi[4]) ya maziko ya ujumbe.

desturi ya jumbe ya zamani.

zamani jumbe chini yake alikuwa na mashaha na waziri na mwenyi mkuu na amiri. huyu amiri alikuwa ndio mkuu wa vijana. likitokea jawabu katika mji, jumbe humpasha khabari amiri, na amiri huwa'arrifu vijana wote. máthali imekuja barua katika mji, yatoka mji mwingine, amekufa mtu, wanataka kwenda ḥani, amiri huwambia vijana: „nendeni majumbani mkaage, kesho tunakwenda inchi każa wa każa kuḥani.“ na kwenda kwao kuḥani huenda waanawake na waanaume. na jumbe huchukua wapambe wawili ao watatu. na wapambe vijakazi vizalia. ḥatta aṣ-ṣubuḥi huja makabili[5]) wawili, mpiga zumari na siwa. jumbe hutangulia mbele pamoja na shaha na waziri, ndio anawoongea nao. na siwa na zumari inalia, ḥatta wakitoka nje ya mji siwa hunyamazwa. illa wanapofika qaribu ya mji, hupigwa tena siwa. na majumbe wa ule mji huja kuwahongeza njiani. ikiwa kushinda — watashinda, ao watalala. ḥatta aṣ-ṣubuḥi huenda mji mwingine. ḥatta wakiqurubia mji wendao, hutolewa mtu, kupeleka khabari, ya kwamba jumbe fulani anakuja. na ule mji hu-

1) Leben. — 2) akaita. — 3) Abschied nehmen. — 4) Glück. — 5) Musikanten.

tengezwa majumba ya kufikia wageni. watakuja na majumbe, wenyeji wa ule mji, kumhongeza jumbe mwenzao na kuingia naye mjini pamoja. nao huingia kwa siwa na zumari. na wale majumbe huja kwa siwa na zumari. nao iwapo aliyekufa ni jumbe, yule jumbe mgeni huʿuzulu yeye na watu wake. tenna huingia katika mji, huonyeshwa majumba ya kufikia. al-ʿaṣiri huenda tangani, wakifika hupigwa ngoma kuu. majumbe wageni na wenyeji hucheza. nao hukaa ḥatta tanga liondoke.

na iwapo jumbe aliyokufa ni mweza, waliwokuja ḥani, si desturi kununua vyakula na kulipa qoʿdi ya majumba kama siku watakazokaa ḥatta warudi. hio ndio qaʿida ya kuḥani kwa zamani.

amma desturi ya sasa — jumbe hana shauri na vijana wala mashaha. na mawaziri hawana shauri na vijana. shauri yao wameweka vikao[1]). katika hivo vikao mna wakuu waanaume na waanawake. litokeapo neno katika mji, kama tuliyotangulia kusema, jumbe hupelekewa barua yake ya ḥeshma, na vijana huletewa barua yao, lakini huandikwa jina la mkuu wao. naye akisha soma barua, humwita kijumbe kupiga mrungura[2]) killa nyumba. wakisikia mrungura, huuliza: „mrungura wa nini?“ kijumbe huwambia: „mnakwitwa kwa mkuu.“ wakifika, huwapa khabari kama iliyomfikia.

amri za zamani zilizokuwa juu ya jumbe.

zamani amri zao walikuwa na inchi na mashamba. na hayo mashamba mwitu, hamna mwembe wala mnazi. ajapo mgeni, Muhindi ao Mwʿarabu ao Msuaḥeli, anataka shamba kulima, humwambia jumbe, humwuliza: „wataka kununua ao kupanga?“ husema yule mtakaji

1) Partei, Klique. — 2) Trommel.

kama atakavo. iwapo kupanga, humwambia: „nipe ubani wangu rupia tano ao sitta.“ wakesha patana, humwonyesha shamba atakayo. ao hupatana kulinunua. tenna humwandikia khaṭṭi.

na katika mji walikuwa na viwanja. mtu akitaka nyumba kujenga, huenda kwa jumbe kumpa khabari, hupatana naye kwa kupanga ao kununua.

amri ya pili wageni wakiingia mjini, nao wamefikia katika majumba yao majumbe, bi'ashara wanayochukua — hawana rukhṣa kuuza pekeyao illa kwa amri ya majumbe.

kaẓâlika Wanyamwezi safari zao pembe walizochukua — ñgombe, Wahindi, Washihiri, na wachuuzi wengine hawana rukhṣa kununua pekeyao. na kulla anayonunua mbuzi hutoa thumni, na ñgombe hutoa riali. na Mhindi akinunua pembe, bi'ashara ikisha, beina yake mapatano na yule jumbe.

amma amri hizo sasa zimewaondokea, sababu hawana yale mashamba ya kupangisha na viwanja vya kuuza, na katika safari hawapati kitu.

'ada za majumbe.

'ada ya kwanza katika mji, mtu akichinsha ñgombe, akiwa wa kuuza ao karamu, jumbe hupelekewa 'ada yake nundu. na asipopewa, huqaṣirika. na iwapo ameqaṣirika, hupewa takarraḍi [1]) yake kitu kidogo.

'ada ya pili mvuvi akivua papa baḥarini, ao nguva, ao nyama aliye mkubwa, huletewa jumbe kidogo, huitwa hii „mboni.“

na iwapo kimeokotwa kitu baḥarini, ao jahazi imevunda, ndani yake mna biḍa'a, ile biḍa'a itakayopatikana, hupelekwa kwa jumbe. mwenyi jahazi akipata khabari,

1) zufriedenstellen.

huenda kwake jumbe kutaka mali zake. naye hupewa uokozi wake, ni hiyo mboni.

ao mtumwa wa mtu ametoroka, amefika katika mkono wa jumbe, humziwia, ḥatta mwenyeji aje. na kama hana mwenyewe, huwa mtumwa wa mboni, humziwia jumbe.

na atokeapo mwenyewe, huuzwa yule mtumwa. akapewa mboni yake jumbe, na kilichobaqi hutwaa mwenyi mtumwa wake.

ʿada ya tatu: kule Bagamoyo pana paḥali, jina lake Nunge, qaribu ya Kingani. napo ni jangwani [1]) ndani ya koko nyuma ya maqaburi ya wahenga. paḥali hapo killa mwaka huota mlima wa chumvi ya genge [2]). zamani wavuvi waanawake wakiona ule mlima wa chumvi, wakifika mjini, huwambia majumbe na mashaha, ya kwamba Kingani genge limeota. wakipata khabari majumbe, hukutanika kufanya shauri ya kwenda kuvunjwa huo mlima. wakesha shauri lao, hutambika [3]) „tambiko ya ukuu genzi.“ [4]). na wengine hutambika gombo [4]) usiku kucha, sababu si desturi kwenda billa ya tambiko. kwa desturi ya zamani wendapo billa ya tambiko, wakafika qaribu ya hilo genge, hukuta vituko njiani, mfano wa majoka makubwa ao nyuki huwafukuza, warejee mjini, ao mwituni hulia simba ao chui. bassi wakesha tambika, aṣ-ṣubuḥi huenenda maqaburini kufyagilia. wakesha fyagia, siku ya tatu usiku wanakwenda majumbe na watoto wao waanawake na waanaume na wazalia wao kunako chumvi, kwenda kuivunja. na kwenda kwao huenda kwa siwa na zumari. ḥatta wakifika panapo huo mlima, huamrishwa kuvunjwa, kutwaliwa ile chumvi. na ʿada itokayo ka-

1) wüste Niederung. — 2) Korallenfels. — 3) Geister der Verstorbenen anrufen. — 4) Name der Anrufung.

tika hiyo chumvi — nundu vilevile hupewa majumbe, na nuṣṣu ya ule mlima ni sehemu yao na ya mashaha na mawaziri. siku ya sitta ndipo wanapopata rukhṣa watu wa mji kwenda chukua hiyo chumvi. nao hufuatana na wenyeji kwenda kutwaa hiyo chumvi.

amma sasa unapoota huo mlima, wanakwenda kutwaa hiyo chumvi billa ya tambiko, illa humpa khabari serkali tangu mapema, apate jua, ya kwamba watu wanakwenda chukua chumvi Nunge, sababu gházia huwa nyingi.

khabari ya ‘ushuru[1]).

khabari za zamani za ‘ushuru.

zamani hutozwa ‘ushuru katika mrima, na wenyi kutoza ‘ushuru ndio majumbe. máthali wamekuja wageni kama Wanyamwezi na pembe kufanya bi‘ashara katika inchi za mrima, wakafikia kwa jumbe moja, zile pembe hupigwa chapa[2]) kwa amri ya sirkali. zikesha pigwa chapa, kulla frásila[3]) imelâzimu kutoa riale nane kwa seyyid[4]) na riale moja ya „yamvi,“ jumla riale tisa‘, akipawa jumbe mwenyi mgeni wake, hiyo desturi.

aiḍa qabla ya Mnyamwezi hajaingia katika mji, imemlâzimu jumbe kumpelekea mali, akampa, kwa sababu ndio qa‘ida[5]), na jina lake ndio „magubiko.“ mkubwa wa safari na waanawake wake, na walio chini yake, wasagira wake, bassi hao wamelazimiwa na kupawa kisua. aiḍa na wanapotangulia katika safari kaẓâlika nao hupawa kisua.

ba‘ada ya kuingia mjini, mwenyi safari akapanga. akesha panga, naye imemlâzimu kutoa „pembe ya nti“[6]) kumpa mwenyewe inchi, ya‘ani yule jumbe aliyemfikia, ndipo afanye bi‘ashara yake.

na ishapo bi‘ashara zake, imemlâzimu jumbe kutoa kitu „agano,“ akampe yule Mnyamwezi kuagana naye, ndipo asafiri.

---

1) Zoll. — 2) stempeln. — 3) 35 Pfund engl. — 4) Sultan von Zanzibar. — 5) Gewohnheit, Sitte. — 6) inchi.

akesha safiri yule, huenenda jumbe, akatwaa kulla frásila riale tatu, ndio „mrabaha," imelâzimu kupawa kwa amri ya seyyidi. zikiwa frásila mia, jumbe hupewa riale thalatha mia katika pembe zile za mgeni wake.

Banyani na Wahindi kaẓâlika, wanapokuja katika mji na mali zao kufanya biʿashara na kuweka maduka, hufikia kwanza kwa jumbe, sababu ndio mkubwa wa mji. akiwatakia majumba, akiwapangisha, wakesha panga majumba, hupawa khabari ya desturi katika inti yote wakijua. aiḍa baʿada ya hayo kulla nyumba ya tâjiri imelâzimu mwaka riale kumi na mbili, hutoa, akipawa jumbe, mwenyi mji — lâzima, hiyo ndio desturi ya mambo ya áṣili. wa kaẓâlika na kisua na vitu vingine hupawa, qádiri awezavo tâjiri.

na majumbe ʿushuru waliwo wakitoza — safari ikaingia mjini, nao wamechukua nǧombe na mbuzi na kondoo — ndani ya nyama hao ndimo majumbe wakitoza ʿushuru. na kutoza kwao mtu akinunua nǧombe, lâzima apeleke riali moja kwa jumbe, na akinunua mbuzi mmoja, lâzima kupeleka thumni kwa jumbe.

na Muhindi ao Mwʿarabu akitaka wapagazi, mtu atakayempelekea Muhindi ao Mwʿarabu, hupewa rupia kwa kulla mpagazi ʿushuru wake jumbe. na ʿushuru huo haupelekewi jumbe mmoja tu, illa jumbe aliyefikiwa na safari yake.

na majumbe wa barra ʿushuru wao ilikuwa hongo. mtu akifika katika mji, akitoka pwani, lâzima atoe vitambi kama watakavopatana. na akitoka barra, atatoa vitu vya barra.

khabari za ʿushuru wa sasa.

lakin sasa katika sirkali ya kideutschi imeweka desturi ya kutoza ʿushuru katika majumba, na tenna

katika watu wawekao maduka, mfano wa Wahindi na Mabanyani na Waʿarabu na kulla awekaye duka. máthali nyumba za Wasuaḥeli nyumba ya mapaa manne analâzima mwaka kulipa rupia thenʿashara, na nyumba ya mgongo[1]) analâzima mwaka rupia sitta, na nyumba ya mawe ghorfa[2]) moja mwaka rupia sabaʿ u nuṣṣ. na mtu mwinyi duka hutezama thamani ya duka lake, likiwa kubwa — ʿushuru wake mwingi, likiwa dogo — ʿushuru wake haba.

na wengi wa Wasuaḥeli wamethanni, sirkali inataka kula feḍḍa hii, lakini feḍḍa hii sirkali hataki kuitumia, lakini inafanyizwa manfaʿa[3]) ya watu wa mji kama kutengenezwa miji na njia. zamani zalikuwa njia ndogo katika mji na barra, lakin sasa njia pana. na mambo haya yametengenezwa kwa feḍḍa.

manfaʿa ya pili: watu wamelala katika majumba yao, na usiku polisi wanawalinda. na wenyi maduka yao wamelala, polisi wanapita kulla waqti kutazama maduka. na mapolisi wanataka mshahara, na mshahara feḍḍa, sirkali analipa.

manfaʿa ya tatu: mtu amepigwa vita, mali yake amenyanganywa, ao ameuliwa ndugu yake, marra anakwenda kwa sirkali kushitaki, sirkali marra anafanyiza vita kwenda kumtakia ḥaqqi yake.

manfaʿa ya nne: visima vya mrima. zamani vilikuwa vibaya, lakini sasa sirkali amejenga visima vizuri tenna ṣafi. sirkali amelipa feḍḍa katika ʿushuru.

kaẓâlika ametengeneza daraja[4]) popote katika mito midogo, na mto mkubwa ameweka mashua[5]), safari zinavuka — hapana khaṭari[6]). kwanza marra mtumbwi umepinduka, watu wamezama, ao biḍaʿa[7]) zimezama.

---

1) Haus mit zweiseitigem Dach. — 2) Oberstock. — 3) Nutzen. — 4) Brücken. — 5) Boote, Fähre. — 6) Gefahr. — 7) Waren.

kaẓâlika watu wengi zamani walikuwa hawana kazi, sasa sirkali amewapa kazi. na watu hao hawatumiki burre kwa sirkali — wanapata feḍḍa kwa sirkali.

ndio maʿana sirkali anataka ʿushuru. juu ya feḍḍa, inayotoka katika ʿushuru huo, haimtoshi sirkali. sirkali ya Ulaya anapeleka feḍḍa nyingi kulla mwaka katika mrima kujaliza katika feḍḍa ipatikanayo mrima, kutengeneza inchi na kuwasaʿidia [1]) watu.

khabari za mtoza ʿushuru katika mrima.

katika majumba ya Afrika ya mrima nyumba zote zimeandikwa namba [2]) na jina la mwenyi nyumba. lakini desturi za Wasuaḥeli nzito, mambo yao ya mtego. mtu wa sirkali akipita kuuliza nyumba kuziandika, marra nyingi watu hawamwambii maneno ya kweli, sababu wengine wanaogopa majina yao kutiwa ndani ya daftari [3]). na kuuliza killa marra: „ʿishara [4]) yake nini sirkali inaandika majumba yetu na majina yetu?“ sababu watu wengi hawajui maʿana ya ʿushuru, sababu gani sirkali inataka ʿushuru. wengi huthanni sirkali inataka kula mapesa ya watu. na watu wengine husema: „labda mfalme ameleta khabari kutaka kujua majina ya mrima.“ na wengine husema: „wanaandika sababu ya ʿushuru, khalafu labda watataka kuja.“ killa mtu husema neno lake. na waanawake wazee wakimwona mwandishi wa sirkali anakuja kuandika majumba — hukimbia, wakaacha nyumba, husema: „mimi nataka salama ya roḥo yangu, wakitaka nyumba — na wachukue.“

na siku hizi iwapo Mzungu anauliza „nyumba hii ya nani,“ na mwenyewe hayupo, lakini mtu mwingine

1) helfen. — 2) engl. number. — 3) Heft. — 4) Vorzeichen.

akijibu, na mwenyewe akasikia „alikuwapo Mzungu hapa pamoja na fulani, ameuliza nyumba hii ya nani, fulani amemwambia“ — wakionana watagomba, husema „fulani ndio kazi yake fitna.“ [1])

tenna wakikutana na Mzungu, kuwauliza majina yao, ao katika wawili akimwuliza mmoja „jina lako nani,“ mwenziwe akijibu upesi „jina lake fulani“ — watakwenda zao, njiani watagomba.

kaẓâlika khabari ya kutoza qoʿdi [2]) katika mrima ina matata mengi, sababu kuna wengine hulipa na wengine hawalipi. hukusanya qoʿdi ya miezi mitatu ya mwanzo na ya mwisho, huwa juu yake deni nyingi. sirkali akiona katika deftari, watu wengi hawajalipa, huweta wote, wakaja katika nyumba ya shauri, killa mtu humwuliza: „i wapi qoʿdi yako?“ hujibu: „nimempa fulani.“ mawazo yake — ile qoʿdi iliyopita, ya mwisho amesahau. sirkali humwambia: „zimefika, lakini kwako bado rupia tatu.“ naye husema: „nimesikia bwana, nataka nikatafute.“ akaondoka husema: „watoza qoʿdi wanatudanganya.“ sababu tarikhi [3]) ya miezi hawaijui, na desturi ya qoʿdi hawaijui.

nalikuwa nikitumwa na sirkali kwenda katika majumba yote kupokea ʿushuru, hufuatana na ʿaskari wawili, sababu mna watu wengine wagumu kulipa ʿushuru. na katika ḥokumu ya nyumba zilizo mashamba killa miezi minne rupia moja. lakini kazi ya ʿushuru wa mashamba nalikuwa nikipata killa rupia ujira wangu rupia tano, amma kazi ya mjini sikuwa nikipata kitu, illa mshahara wangu. na watu wote wakanichukia.

siku moja nimekwenda shamba kutaka ʿushuru, nikamkuta mtu nyumbani pake, killa siku hunizungusha, halipi ʿushuru. siku hiyo nikamshika kwa

1) Intrige. — 2) Miete, Steuer. — 3) Datum.

nguvu kutaka ʿushuru wa sirkali, akanijibu: „sina, nenda zako.“ nikaqaṣirika, alivonambia maneno yale. naye akaqaṣirika. akashika shoka katika mkono wake, akataka kunipiga. nalifuatana na mtumwa wangu, Serenge jina lake, akamkamata mkono na shoka yake. siku hiyo sikuwa na ʿaskari. nikataka kumpeleka Bagamoyo. wakaja watu wakanibembeleza na kunishika miguu kumwachia. nikamwacha, akaingia ndani, akanipa rupia.

kusafiri kwao Wasuaḥeli.

desturi yao qabla ya kusafiri.

desturi ya Wasuaḥeli — kama anataka kusafiri ao kwenda kukopa, akenda njiani, akakuta mtu mmoja anayekuja, hurudi, husema: „safari yangu mbaya.“ safari hiyo hana furaḥa nayo, kama ataka kwenda. ao atagheiri[1]), arejee nyumbani kwake, ḥatta siku ya pili ndipo asafiri. na akiwa na ḥaraka[2]), atangoja ḥatta nuṣṣu saʿa ipate, ndipo asafiri.

kaẓâlika iwapo atasafiri, akenda katika njia, akakuta watu wawili wanakuja — husema: „hii ndege njema[3]).“ khaṣṣa iwapo ni waanawake, nao wamechukua vitu katika mikono yao — huzidi kufuraḥi, husema: „hii ndege njema kabisa.“

ao akitaka kwenda safari, ao katika shamba, ao kwa Muhindi kukopa, akikutana na mtu mwenyi chongo[4]), maʿana jicho moja, husema: „safari yangu mbaya, nimeona kisilani.“ [5]) vilevile hurejeʿa nyumbani.

ao anakwenda safari ya barra, ao shamba, akikutana nyoka wanapigana, husema: „nendako — nitakuta magomvi, ao tutakutana na vita.“ ikiwa ni safari

---

1) verändern, andern Sinnes werden. — 2) Eile. — 3) Glücksvogel (Glücksstern). — 4) einäugig. — 5) dasselbe wie ndege mbaya (böse Vorbedeutung).

kubwa, wanakwenda kwa nathari[1]) ya kuchelea yatakayowapata njiani.

ao akikuta mwanamke mzee pekeyake, husema: „nimekutana na kisirani, kama namwendea mtu kumtezama, simkuti nyumbani, ao kama nakwenda kopa — sipati.“ vilevile hureje'a.

kaẓâlika na mwinda akitoka nyumbani mwake, akikuta njiani mwanamke mzee, ao mtu mmoja — hendi uwinda wake, moyo wake huwa na oga kukhasiriwa na mnyama, ao kwenda burre kupoteza baruti yake, na kitu asipate.

tenna ukienda njiani, akikuona kima — bassi reje'a, usiende safari hiyo, haifai, utaona vibaya.

aiḍa ukienda njiani, ukamwona nyoka, aliye na vidoa viwili, kwetu huitwa pito jina lake huyu nyoka, naye mbaya, ukimwona joka, utapata khabari mbaya sana.

na iwapo umekwenda safari, ukakutana na chungu njiani, nao wamechukua punje ao vitu vingine — husema: „safari yangu nzuri,“ na iwapo umewakuta hawana kitu, husema: „safari hii mbaya.“

mtu akitoka nyumbani mwake, akitaka kwenda paḥali, akajikwaa na kisiki[2]), mguu wa kuume akajichubua, husema: „nendako kubaya, nitakuta magomvi, ao ntakutana na mtu, mbaya wangu, sababu ndege mbaya nnayokwendea.“ na kule Lindi watu husema, wakijipiga kisiki, wakijiumiza: „mke wangu amezini.“

na mtu akijikwaa mguu wa shoto, pasipo kujichubua — husema: „ndege yangu nzuri.“

ao iwapo ndege amekulilia juu ya mti „kwapé kwapé“ — safari nzuri.

---

1) Blick, Vorsicht. — 2) anstoßen, kujipiga kisiki oder kukwaa na kisiki.

na iwapo mvua nyingi imekunya, akilia ndege huyu, wasafiri husema „mvua imekwisha.“

tuongeze khabari nyingine kama hii, wanazoṣadiqi Wasuaḥeli:

ao iwapo katika mashamba akatua bundi [1]) juu ya mti, akafuuliza [2]) kulia — atakufa mtu katika mji. na kule mgau [3]) kuna ndege, huitwa matonohi, mlio wake ʿajabu, hulia „humhum.“ akilia ndege huyu qaribu ya mji — hufa mtu mkubwa.

na akilia shorwe juu ya mti, uliwo qaribu ya nyumba — atakuja mgeni.

na kule mgau husema, ukimwona mbwa kiuno chake anakokota chini — atakuja mgeni katika mjini.

ao mtoto akifyagia uwanja, husema „atakuja mgeni.“ ao kuku wakinoṉgonezana, husema „atakuja mgeni.“

desturi ya Wanyamwezi: kama anapita katika njia, na mtu akasimama akashika bakora, akafanya mpaka katikati ya njia — Mnyamwezi njia hiyo haipiti, atageuza njia nyingine apite, nawe akutukane. maʿana yake anaṣadiqi, „huyu ameniapiza, nendako nisifike,“ ndio maʿana kukataa kupita.

mapatano ya tâjiri na msafiri.

Msuaḥeli akitaka safari, huenda kusema na Muhindi tâjiri yake, humwambia: „nimekuja kwako Mukki, nataka bidaʿa unikopeshe, sababu nataka kusafiri.“ tâjiri atamjibu: „mimi sikatai, lakini kalete mtu maʿarufu [4]), aje akuḍámini [5]), khalafu ntakupa biḍaʿa.“ yule mtu atajibu: „mimi sina mtu wa kuniḍámini, illa mimi nafsi yangu, wewe tawakkali [6]) utoe mali yako kwa nia ṣafi, wala usiwe na kinyongo [7]), mambo yote mtenzi muungu,

1) Vogel. — 2) fortfahren etwas zu tun. — 3) im Süden (Lindi, Mikindani). — 4) angesehen. — 5) bürgen. — 6) Risiko übernehmen. — 7) überlege es dir nicht so lange, mache nicht so viele Umstände.

inshallâhu taʿâla nikarejeʿa utafuraḥi.“ tâjiri atamjibu: „vema, maneno yako nimeyasikia, lakin nafanyiza shauri na moyo wangu.“ wataagana. atamwambia: „lini nije kusikiliza majibu?“ atamjibu: „mudda wa siku sabaʿ njoo.“ siku sabaʿ zikisha, atakwenda kwa tâjiri atamwambia: „nimekuja kukusikiliza tâjiri.“ atamwuliza: „nini ras il-mali[1]) yako? una shamba ao nyumba?“ atamjibu: „mimi sina ras il-mali, mimi nakwambia mwamini[2]) muungu, ḥaqqi yako, nikiwa ḥai[3]), inshallâh taʿâla, nitakupa.“ tâjiri atajibu: nimesikia, lakin nataka sherṭi uniandikie khaṭṭi ya sirkali.“ atamjibu: „nimequbali kukuandikia khaṭṭi.“ tâjiri atamjibu: „unataka biḍaʿa ya qiasi gani?“ atasema: nataka riale elfu.“ atamwuliza: „mudda miezi mingapi?“ atasema: „miaka miwili.“ atamwambia: „mingi, fanya mwaka mmoja.“ ataqubali mwaka mmoja.

wakesha mapatano yao, watakwenda sirkalini kuandika khaṭṭi ya riale elfu, na sirkali atatia ṣaḥiḥi[4]) yake. watakwenda dukani. atamwuliza: „wataka biḍaʿa gani?“ atamwambia: „nataka jora ʿesherini membei na jora thalathini za sûn, na jora kumi na tano majigam, na jora kumi gamti — hizo ndizo biḍaʿa nyeupe.“ atamwambia: „nataka na visua vitambi.“ atamwuliza: „namna gani?“ akasema: „nataka kitambi kareati, na kitambi buraa na kitambi rehani, na kitambi sturbaḍi na barawaji na kikoi mzinga, na kitambi pasua moyo, na pipa moja la ushanga, na magunia manne viwangwa[5]), na ṣanduqu sabaʿ sukari, na kata[6]) sitta zeñgenge[7]), na khema moja.“

akesha kumḥasibia vitu hivo, atataka na gharama[8]) ya wapagazi, atapatana na wapagazi qádiri ya mizigo

1) Kapitalvermögen. — 2) Vertrauensmann. — 3) lebend. — 4) richtig. — 5) flache Muschel, die als Halsschmuck von den Wanyamwezi getragen werden. — 6) Drahtlast. — 7) Messingdraht. — 8) Kosten.

yake, na kulla mpagazi atampa upagazi wake, killa mtu nuṣṣu ya upagazi. wapagazi wakesha pokea upagazi wao, lâzima kufunga mitumba. wanapokwisha wapagazi kazi ya kufunga mizigo, atakwenda kwa tâjiri yake kumwaga. na tâjiri atamjibu: „kwa ḫeri, salâma.“ yule msafiri atakwenda zake.

khalafu huenda kwa wazee wake kuwaaga na kuwaombea muungu. na kuaga kwake huwapa kitu. na akiwa na mke, humpa maṣurufu [1]), lakini wengine hawafanyi, sababu waume zao wakiondoka, wanajua hufanya uḫaribivu [2]).

na iwapo wazee wake wamekufa, huchukua ubani [3]), akenda qaburini, husema katika qaburi maneno yaleyale kama wazee wake wa ḫai — husema: „wazee wangu, nimekuja kuwaaga. nimekopa mali ya watu, nnataka safari. na ninyi mmekufa, lakini vivuli vizima. muungu anipeleke salama na mali ya watu, nirudi salimini, nilipe mali ya watu. na nikapata, ntakuja kuwakumbuka kwa ṣádaqa [4]) na khítima [5])." tenna hufyagia juu ya qaburi, kana pana majani huñgoa, pakiwa na taka huondoa, kama amechukua ṭibu humwaga. huko ndiko kuaga kwa Wasuaḫeli katika maqaburi wanaposafiri.

na mwanamume akisafari, waanawake huimba mwimbo:

„Mradi [1]) Mradi wangu, ondoka ule,
mume wangu hayuko, ondoka ule,
amekwenenda mashamba, ondoka ule,
kusimamia watumwa, ondoka ule,
na mtumwa ali yeye, ondoka ule."

1) der Liebhaber der Frau.

1) Ausgaben, Kosten (für Lebensunterhalt). — 2) Schlechtigkeiten. — 3) Weihrauch. — 4) Opfer. — 5) Koranlesung.

wakisha agana na wazee wake na mkewe, huwambia buriani [1]) ndugu zake. na mkewe humfanyia mkate, naye hufanya karamu [2]) kuwakirimu watu. wakesha kula, humwamru mtongi wake kupeleka safari shamba. naye atalala mjini, aṣ-ṣubuḥi afuatie safari yake.

desturi ya safari huwa na kirongozi, baʿada ya kirongozi mpiga mganda, baʿada ya mpiga mganda mshika kome.

killa safari lâzima kuwa na mwongozi; maʿana ya kwitwa mwongozi, sababu anajua njia. na iwapo yeye ametangulia, na nyuma kuna watu, ambao wasiwojua njia, killa akafika maḥala panapo njia panda [3]), lâzima aweke ʿalâma [4]), watu waliwo nyuma wapate kujua. na hiyo ʿalâma — njia ikiwa mkono wa shoto, ataweka ʿalâma yake, ataweka majani mabichi ao makavu, ao huchimba chini upande wa mkono. waliwo nyuma, wakaona majani mabichi ao makavu yamewekwa katika njia, hujua, ya kama kunako majani — siyo njia.

kirongozi akifika panapo maji mengi ao panapo kambi ya kuterekeza, lâzima apige mganda. waliwo nyuma wakasikia mganda wa kirongozi — aliyochoka hupata nguvu. ao aliyeshikwa na kiu ya maji, akisikia mganda, roḥo yake hufuraḥi. na aliyetua, marra huchukua mzigo wake, hukimbilia paḥali panapo maji ao hiyo kambi. na hapo katika mapori makubwa waqâti wa jua mna taʿabu ya maji.

safari ikaondoka, lâzima marra ya pili kirongozi kupiga mganda, sababu wengine wamelala, wengine wamekwenda kutembea katika miji ya pili. wakisikia mganda wanarudi mbio. usipolia mganda, watu watawawacha katika mji, na hiyo si desturi ya safari. na mkubwa wa safari, sherṭi atezame sana wapagazi,

---

1) Abschied. — 2) Fest. — 3) Kreuzweg. — 4) Zeichen.

sababu wanakula vitu vya watu billa ya kutaka rukhṣa kwa wenyewe.

aiḍa hiyo kome — fimbo, lakini Wanyamwezi ndiyo yenyi safari yao. mfano wake kama ḥirizi kuwakinga njiani killa mambo ya khaṭari.

na safari ikifika Nyanyembe, kirongozi hupiga bunduqi, huja waanawake na waanaume kufuraḥi ndugu zao na kuwapokea mizigo, huenda panapo kambi wanayotua. hii ndio khabari ya kutoka pwani kwenenda barra.

khabari ya bi'ashara.

ba'ada ya kufika Nyanyembe, wapagazi wakimpa mizigo yake, hubaqi yeye na mizigo yake. hutafuta marafiqi wa kinyamwezi kumsa'idia bi'ashara. nao hupeleka khabari kwa jama'a zao, amekuja mungwana, ana biḍa'a nzuri, huja na pembe na kalasha na ngombe, hufanya nao bi'ashara. na biḍa'a kama haikwisha, atapanda juu ya vilima kutafuta pembe. na mwisho mapatano be'i haishi, illa atoe „kishika mkono.“ pembe ikiwa nzuri, atatoa kitambi, ndio kishika mkono. na ushâhidi wa wanyapara — asipowapa, be'i wataitia fujo — ivunjike.

desturi yao, wakanza ao wakanunua, mwisho sherṭi washikane mkono, nao husema: „uguzi umemala[1]), ndugu yangu.“ ao husema „ufwe[2])“ kwa ḍiḥaka[3]).

naye mwenyi safari akiona bi'ashara nyingi, ataandika barua kumletea tâjiri yake, na kitu alichopata, ikawa pembe ao mpira ao vitu vinginevo, atampa mtu ma'arufu pamoja na barua. na katika barua ataandika: „ila jenab tâjiri wangu salâm sana. ba'ada ya salâm naku'arrifu, anakuwaṣilia fulani na barua yangu, nimempa amana[4]) kukuletea frasilà tatu za pembe. zi-

1) das Geschäft ist abgeschlossen. — 2) es ist gestorben. — 3) Scherz. — 4) Pfand.

taqabbaḍi [1]) mikononi kwake. nami nataka biḍa'a nyingine, kama niliyofunga kwanza. usilete namna nyingine, sababu hiyo inafa'a. uniletee kwa upesi, Wamakua wamekwenda porini kupiga pembe, qaribu watakuja. nami nataka, wakiwaṣili Wamakua, na biḍa'a inifikie, allâh allâh tâjiri wangu! na huyo kijana, aliyoleta barua, mpe kitambi kizuri aḥsante [2]) yake, sababu kijana mwema sana, wa'-salâm."

bi'ashara ya kureje'a pwani.

ba'ada ya kwisha nunua pembe na hivo vitu vingine, hushuka pwani. na kushuka kwake kwanza hutwanga „pamba ya njiani" — unga wa mtama na wa muhindi, huutia katika ngozi ya mbuzi, ndio mifuko yao wasafiri. na katika safari kazi zote juu ya wapagazi, kujenga ḥema ya tâjiri wao, na kutafuta maji kumletea, iwapo hana watu, ḥatta wafike pwani.

wakifika qaribu ya pwani, hutoa tarishi [3]) kupeleka kwa tâjiri yake na nyumbani kwake — ya kama: „Mwinyi fulani amefika Mpapwa, na safari yake njema, amepata khêri, ameagiza kwako, ataka mavazi na vitu każa wa każa." tâjiri akisikia, khaṣṣa akiwa Banyani, winda [4]) humvuka kwa furaḥa. marra atamfungia yule tarishi vitu alivotaka. na nyumbani kwake watafanyiza vitu vya tunu, apelekewe ḥatta akiwaṣili mtoni.

panapo kivuko, atatoa tarishi wa pili, ya kama Mwinyi yuko mtoni, anavuka pamoja na safari. watakwenda marafiqi zake kumngoja mashamba, na kundi la waanawake, ili kumhongeza. nao killa mtu ana mchele katika kikombe. wakimwona, humwagia kichwani ule mchele. wazee wake humwambia „salâma baba! umekwenda salâma, umerudi salâma? ndiwo

1) nimm sie in Empfang. — 2) Dank. — 3) Eilbote. — 4) Lendenschurz.

ukubwa huo, tamba uone, kama hukutamba, huna uonacho.“

kwa zamani watu hupiga bunduqi za shereḥe[1]), ḥatta safari ifike forḍani. mudda wa siku mbili ao tatu, pembe zitapigwa chapa, zitolewe ʿushuru. kisha mwenyi safari hupeleka pembe zote kwa tâjiri wake kufanya ḥesabu naye. hii ndio khabari ya kurejeʿa kwake pwani.

khabari ya biʿashara na tâjiri wake.

baʿada pembe kumqábidi[2]), tâjiri atafanyiza ḥesabu, kitu alichochukua, mwanzo wa biḍaʿa na wapagazi. wakisha fanya ḥesabu, humwambia: „umechukua riale każa wa każa, na ulicholeta każa wa każa, fáyida[3]) yako ao khasara[4]) yako riale każa wa każa. iwapo beina yao mapatano na tâjiri wake — hawagombi. lakini marra nyingi hugombana, sababu tâjiri anataka kuchukua fáyida yote. kwanza huuza biḍaʿa yake ghali, na kama feḍḍa yake imekwisha fika, hutaka tenna fáyida nyingi ya pembe. iwapo anataka safari tenna, ataandika khaṭṭi ampe biḍaʿa, asafiri tenna. labda atapata fáyida záyidi marra hii. hizo ndizo safari za zamani za Wasuaḥeli walivokwenda katika barra kufanya biʿashara.

safari za sasa za Wasuaḥeli.

wale watu wa zamani hawasafiri, wanashika kazi ya jembe. na wasiwo mashamba, wanazunguka njiani kama ngombe, wasiwo wachunga, sababu hawataki safari. illa vijana wanawoondokea sasa, ndiwo wanawosafiri. na safari zao si mno kwenda Unyanyembe na Manyema, sababu wanapata khasara nyingi. Washenzi wa barra wote wameerevuka, thamani ya barra na ya pwani sawasawa. safari walizozishika, huenda Nguu,

1) Freude. — 2) übergeben. — 3) Gewinn. — 4) Verlust.

kununua mpira na tumbaku, ao Uhehe wanapeleka bi-ḍaʿa wakabadili kwa feḍḍa. na Wanguu na Wahehe wameerevuka, lakin wanaona afaḍali kufanya kazi ya burre kama kutembea burre, kama walivosema wazee „mguu uliosafiri, haukosi fungu lake.“

na wengine wanapenda safari, lakin nyoyo zao hazina mwamana, matâjiri hawawapi kitu. na hao wasafiri wa sasa, hawana shangwe wakirudi, sababu „mkono mtupu haurambwi, na ukarambwa una punje,“ maʿana ni maneno ya fumbo. yamekwisha maneno haya.

safari za Wanyamwezi zamani.

Wanyamwezi wakishuka kutoka barra, huchukua ngombe na mbuzi na pembe, meno ya viboko na mbuni. naye hashuki pwani, illa akiwa na rafiqi yake mjini, jumbe ao kijana wa mji, humpelekea khabari: „mimi nimefika Usako, tengeneza nyumba yangu ṭayyari, na pombe uweke nyingi.“ rafiqi yake atapanga nyumba yake na ya wandewa na wanyapara. ḥatta aṣ-ṣubuḥi yule mwenyeji wa mji atawambia waanawake: „kesho takamshangilie rafiqi yetu shamba.“ na kushangilia kwao husema:

„mlô mlô [1]), mgeni wetu apendeza.“

1) chakula.

akifika mjini, ataingia nyumbani mwake, na pembe zipelekwe forḍani. mudda wa siku sitta ao sabaʿ analewa pombe. Wahindi wanakwenda wakirudi kumwuliza mdewa: „lini utafanya biʿashara pembe zako?“ lakini wapagazi wakifika, vitu walivochukua, wamekwisha uza — mbuzi, viboko, vipussa, mikuki. maʿana mdewa wao huwapa rukhṣa kuuza upesi. nao hununua

vitu vya tunu kuvifunga ṭayyari kupelekea ndugu zao barra.

baʿada pembe kupigwa chapa, siku ya kutaka biʿashara huenda yule Mnyamwezi mwenyi pembe zake pamoja na rafiqi yake ḥatta dukani kwa Mhindi, watapangia pembe. biʿashara yao pembe moja anataka vitu vya duka lote, lakini Wahindi maḥodari wa biʿashara hizo. wanaanza mwanzo wa aṣ-ṣubuḥi ḥatta saʿa sitta — pembe moja haijesha. marra anataka rangi hii, marra anataka rangi hii. na katika biʿashara yao sherṭi waletewe tende na nazi, hufuraḥi sana, husema: „Muhindi huyu mzuri sana, anajua kufanya biʿashara.“ Muhindi husema: „nnawapa burre, hapana ḥesabu katika uguzi wetu,“ lakini yeye Muhindi huandika katika daftari yake.

kisha watarejeʿa maneno ya biʿashara, ḥatta wagombane wakasema: „sasa njaa zitauma, leo tuwache uguzi, kesho tukakuja.“ siku ya pili watakwenda, kama hawakupatana — haitakwisha biʿashara, labda siku ya tatu Muhindi atapatana na yule Msuaḥeli: „sema naye rafiqi yako, biʿashara ishe.“ naye atampa maneno mazuri yule Mnyamwezi, atakata biʿashara. na kukata kwake atawatukana wote wawili Mnyamwezi na yule Muhindi, huwambia: „ninyi wajinga, hamjui biʿashara.“ humwuliza Mnyamwezi: „unataka nini mdewa, na Muhindi nini hataki kukupa?“ husema: „nataka rangi każa wa każâ.“ humwuliza yule Muhindi: „huna khasara?“ hujibu: „ninayo khasara.“ husema: „haiḍuru, mpe kitu atakacho, sababu utanunua pembe nyingi kwake.“ atampa. baʿada yake haishi biʿashara, illa wanyapara, waliwo katika biʿashara, wapate ḥéshima yao kitambi ao nguo nyingine. atawashika mkono awapatanishe, biʿashara imekwisha. hii ndio biʿashara yao Wanyamwezi.

kazi ya wapagazi.

baʿada ya kufika katika mji, wanalala ḥatta aṣ-ṣubuḥi, killa mtu hushika shoka, akenda kokoni kukata kuni. na wengine hukata fito, na wengine pau, wengine viguzo, wengine wanachuna kamba. vitu hivo vyote hujengewa nyumba. huleta mjini kuuza, mzigo pesa kumi ao kumi na sitta, ndio matumizi yao. posho wanapata, lakini haliwatoshi kitu.

na wengine wanafanyiza kazi ya mjini, wanazunguka katika mji, husema: „wapi mirimo?“ [1]) watu huwauliza: „mirimo gani?“ wanajibu: „yoyote, kuteka maji ao kukandika nyumba.“ lakin ukamwambia „kazi ya kuchimba choo“ — haqubali, anasema „katika choo mnaingia mambo mengi.“

wengine hufanya kazi ya ukulima, hupatana na waanawake ao waanawaume, huwapeleka mashamba kuwasaʿidia ngwe [2]) zao. ḥatta jioni hurejeʿa mjini, huwapa kama walivopatana. wengine hupatana nao kuwapeleka mtoni kuchukua mizigo ya miwa. nao huwapendeza mno kazi hiyo, maʿana hupata miwa ya burre kutafuna. hizo ndizo kazi za wapagazi wa kinyamwezi wanazofanyiza mjini.

khabari ya safari kurejeʿa barra ya kinyamwezi.

baʿada biʿashara kwisha, Wanyamwezi huenda kokoni kukata mambo. mambo zao fito za kufungia mitumba. kisha hupewa upagazi wao wa kurejeʿa barra. hununua vitu watakavo. tenna hufunga mitumba. mtumba mmoja ndani yake mna jora kumi na vitambi. na uchukuzi wao wanachukulia begani. nao waanawake na waanaume huchukua mizigo. na iwapo ame-

1) Arbeit. — 2) tägliche Feldarbeit.

nunua vitakataka vingi, naye lâzima kuchukua mtumba wa watu, na vitu vyake hufunga kiunoni.

na furaḥa ya wasafiri, inapotoka mjini, wote hupewa mahia mekundu kuvaa, na wengine miguuni wanavaa kengele, wakenda hulia zile kengele. na kirongozi kaẓâlika. lakini yeye huvaa ngara. na hiyo ngara manyoya ya killa ndege, hukusanya pamoja, akayafunga, huvaa kichwani. ḥatta safari ikisha, wakaipeleka shamba, mizigo huipanga ndani ya khema, kisha hurudi mjini. sababu wengine wana vitu wamesahau kununua. huchukua jora kuuza. nao wanauza kwa thamani ndogo, sababu kitu kikatoka dukani kwa Mhindi, ukinunua rupia kumi, Muhindi atakupa tano, sababu ni vinyozi sana, hunyoa watu nywele zisizo maji. wakesha nunua vitu vyao, wanakwenda mashamba, na safari inatoka.

zamani walikuwa Wanyamwezi siku ya kulalia safari hucheza tinge[1]) ao hutambika mapasa[2]). na tambiko yao hupakaa unga usoni na kutukanana waanaume na waanawake, lakini si magomvi, illa ndio desturi yao. tenna huchukua unga na kijungu kipya, hupeleka njia panda, ndio tambiko yao, ḥatta aṣ-ṣubuḥi wanasafiri.

nyimbo za safari.

nao huimba katika safari:

„mtondowo[1]) siwo? mtondowo siwo?
Wambwera washenzi wamekuja
mtondowo siwo?“[2])

---

1) mtondo huo; mtondo Karawane. — 2) diese Lieder sind ein Gemisch von kinyamwezi und kisuaḥeli.

---

1) ngoma. — 2) Anrufung ihrer Vorfahren, mapasa genannt.

ao huimba:

„mayu wane [1]), mayu wane, nahuu! [2])
walungwana kutukongola [3]) wamaweta.“ [4])

1) meine Mutter. — 2) horch auf. — 3) betrügen. — 4) die wohlhabenden.

ao huimba:

„tola [1]) tola, mwana wane
limhu [2]) hami, hâ!
tola mwana wane limhu hami.“

1) nimm. — 2) meinen Speer.

ao huimba:

„hongo na hongo maliro [1]),
hê baba maliro,
ukagwe [2]) niñgwe walungwana, mayu! [3])
twizire [4]) kuwalola [5]), somo [6]) wize [7]),
hê mama wa mashoto [8]), mayu!
twizire kuwalola.“

1) inakwisha mali. — 2) ondokeni. — 3) Schwur „bei meiner Mutter.“ — 4) tumekuja. — 5) lola = tezama. — 6) Freund. — 7) watakuja. — 8) feig.

ao huimba:

„lukucha [1]) lwa ñgʰua [2]),
lukucha lwa ñgʰua
chimo [3]) lya Ugogo, âhe baba!
lukucha lwa ñgʰua.“

1) kucha. — 2) hua. — 3) vita.

baʿada ya kwimba husema:

„mliho mliho?“

huitikia wengine:

„tuliho, tuliho.“

ao huimba:
„walungwana si watu
Katate[1]) wammenya[2]) chuma.“

1) Name. — 2) menya = piga.

marra nyingi ba'ada ya kwisha mwimbo moja husema:
„âho hakutekerwa.“[1])

1) hapo hakupikwa kizuri.

ao huimba:
„tuwaleke[1]) walina[2])
iwuwa[3]) ya wakima.“[4])

1) leka = wacha. — 2) wana. — 3) wana uwivu. — 4) waanawake.

khabari ya usare[1]) kwa Wasuaḥeli.

áṣili[2]) ya usare.

zamani watu wa barra na wa pwani walikuwa wakiogopana kwa kunyanganyana. mtu wa barra akija pwani na bi'ashara — hunyanganywa. na watu wa pwani wakenda barra, hunyanganywa mali zao na kuuawa, ndio ma'ana kutakana udugu wa usare, kutoana khofu[3]) katika nyoyo[4]). wakifanya huo udugu, hawanyanganyani tenna, huwa mtu na nduguye.

khabari ya usare.

ma'ana yake mtu akataka kufanya urafiqi[5]), kwanza huchinshwa kuku ao mbuzi kwa mtu anayejiweza. khalafu hutwaliwa ini la nyama, likachomwa ḥatta likawiva. kisha huja mtu na wembe na kinoo, jina lake mdumilizi, tenna huwadumiliza. katika watu wawili moja wapo kwa jina lake akamwambia: „Mwenyi Kondo, umemtaka Mwenyi Khamisi kufanya naye urafiqi, naye ana ndugu zake, watu hao wataingia katika nyumba yako, wakaona kitu chako — watachukua — usiqaṣirike[6]), ndugu wa Mwenyi Khamisi na wewe ndugu yako, ukiqaṣirika — ufe.“ watu huitikia wale walioshuhudia[7]) „mwiza“ ao „ndio.“

1) Blutsbrüderschaft. — 2) Ursprung. — 3) Angst. — 4) moyo — nyoyo. — 5) Freundschaft. — 6) ärgerlich werden. — 7) bezeugen.

tenna mdumilizi husema marra ya pili: „kama umeona vita, vyataka kumjia Mwenyi Khamisi, nawe wavijua, ukanyamaza, usimwambie ndugu yako — ufe.“ huitikia tenna watu „mwiza.“

„ao unakaa katika mabaraza kumteta ndugu yako Mwenyi Khamisi — mbaya — ufe.“ huitikia watu „mwiza.“

na waqati wa kusema maneno haya, mdumilizi hunoa ule wembe juu ya kichwa katika kinoo, amma kama hana wembe, hunoa upanga, ao sime, ao kisu. na maʿana yake anawatia khofu, wakae vema mtu na rafiqi, usivunjike udugu.

akisha maneno haya, huja mtu mwingine kumdumiliza Mwenyi Khamisi. maneno yake kama tuliyotangulia kuyasema. na watu hao hukaa juu ya mkeka mpya. nao hufunikwa nguo mpya. ḥatta yatakapokwisha maneno hayo, huletwa ini[1]) la nyama, tenna huchanshwa wote wawili. damu[2]) zao hupakwa lile ini, wakala wote wawili. khalafu huondolewa, killa mtu hukaa paḥali pake.

tenna huja watani[3]) kutaka utani[4]) wao. na mashahidi[5]) hutaka utani wao. tenna watu waliopo watataka tandula, maʿana yake kuondolewa mkeka chini na kuvuliwa nguo walizojifunika. na mkeka huchukua mdumilizi moja, na nguo achukue mdumilizi wa pili.

na wengine hawafanyizi usare, wanaṣadiqiana kwa nyoyo tu. hupika chakula, wakaweta watu, wakala chakula, wakawapigia fâṭiḥa[6]) kuwaombea muungu, urafiqi wao kuwa mwema. lakini Washenzi[7]) hawaqubali, illa kwa usare, ndipo anapoqubali huyu ndio ndugu yangu.

1) Leber. — 2) Blut. — 3) Stammesgenossen, Vetternschaft. — 4) übliches Geschenk. — 5) Zeugen. — 6) erste Sure. — 7) Leute aus dem Innern.

khabari za utumwa.

áṣili ya watumwa.

áṣili yake mtu hufikiwa na mawáhibu[1]) kama kupigana vita beina ya inchi hii na nyinginc. katika vita, watu wanaopatikana mateka, hawawaui, hufungwa kamba, wakawachukua mjini huwambia: „ninyi kaeni watumwa wetu.“ nao hukaa, wakajioa wao kwa wao. wakizaa watoto, watoto wao ni watumwa vilevile.

ao utumwa unapatikana katika dia[2]). mtu ameua, na wakwao[3]) wote maskini, naye hana feḍḍa, hulazimishwa kutoa dia, asipoweza, atachukuliwa yeye, atauzwa ao atakwenda kama mtumwa kunako dia. na kama aliyemwua mungwana, dia yake kubwa. akiwa na ndugu ao mjomba, atamfuata katika utumwa.

ao mtu mchawi ameua, naye amejulikana kwambani mchawi — huuawa, ao huenda alikoua — akawa mtumwa.

ao mgoni[4]) amelala na mke wa mtu, hulazimishwa ugoni[5]) kulipa, kama hana — atakuwa mtumwa. na ugoni zamani ulikuwa barra na pwani, ḥatta Wasuaḥeli wakitumia ugoni. ao huingia njaa, wakauzana wenyewe kwa wenyewe.

---

1) mambo. — 2) Blutschuld. — 3) Angehörige. — 4) Ehebrecher. — 5) Ehebruch.

ao huweka rahani[1]) mtoto, ao mpwa wake, na feḍḍa ya kukomboa hana — amekuwa mtumwa. illa mkewe hawezi kuweka rahani, wala kuuza, ijapokuwa njaa kubwa. kama hawezi kumlisha — atamwacha.

turejee maneno ya barra. mateka na rahani na watu waliwotoka katika ugoni, ndugu zao kama hawana feḍḍa ya kuwakomboa — wamekuwa watumwa. wakenda Waʿarabu barra ao wachuuzi wengine wa watumwa, huwanunua kuwaleta pwani. nao huwauza kwa watu wengine. ndio áṣili ya utumwa. nao wanapoletwa pwani, sherṭi aliyewanunua, awatezame sana, maʿana hutoroka. na wengine, wakifika pwani, hujidaʿi[2]) waungwana.

zamani za Seyyid Barghashi ilikuwa njaa mrima, ikawa wanauzana Wazaramu na kuwekana rahani. Waʿarabu wakapata khabari Unguja, ya kwamba mrima watumwa rakhiṣi. wakashuka kununua watumwa wa kizaramu. hulala usiku kucha — Mzaramu ḥatta aṣṣubuḥi ya pili amekimbia, amekwenda kwao. na akifika kwao, shidda kupatikana tenna. na wanaopakiwa Unguja, hukaa mwezi mmoja, mwezi wa pili hujidaʿi: „mimi si mtumwa, mimi mungwana.“ yalikuwa mashitaka[3]) killa siku katika barza. Seyyid Barghash akapata khabari, ya kwamba Waʿarabu huenda mrima wakinunua Wazaramu. Seyyid Barghash akawagombeza Waʿarabu, akasema: „atakayekwenda mrima kununua watoto wa kizaramu — feḍḍa yake ametia baḥarini, naye tamfunga pingu miezi sitta.“ na áṣili yake hawakuwa wakinunuliwa, huenda watokao mjini, huenenda mashamba, wakiona watoto wa kizaramu ao waanawake, huwakamata, wakiwatia vitambaa vya kinywa, wasipate kupiga kelele, tenna huwaleta mjini kuwauza kwa wachuuzi.

1) Pfand. — 2) fordern. — 3) Klagen.

na wengi wa Waʿarabu husafiri barra kuwapiga vita Washenzi, mateka yake huwafanya watumwa. ao Mshenzi huenda kwa Mwʿarabu, akamwambia: „nimekuja kukufuata.“ naye huqubali Mwʿarabu. na akiwa na jamaʿa zake humfuata, mwisho wake huwafanya watumwa. ndio sababu yake watumwa wengine wa barra ao wa Manyema wanaleta matata kulla siku pwani, wanasema: „huyu Mwʿarabu hakuninunua, nimemfuata tu, sasa anataka kunifanya mtumwa.“

namna ya watumwa.

mzalia áṣili yake mama yake ametoka barra. alipofika pwani, akaolewa na mtumwa vilevile, akazaa mtoto. huyu anaitwa mzalia. mzalia namna mbili. kuna mzalia wa marra moja na mzalia wa marra mbili, ḥatta marra sabaʿ. maʿana ya marra sabaʿ: mama yake amezaliwa katika mji, na baba yake kaẓâlika — bassi huyu ḥokûmu yake kama mungwana, huambiwa mtumwa áṣili tu.

kuna na mtumwa mjinga. mjinga — aliyefika pwani, hajui kusema wala hajui desturi za watu, wala nguo hajui kufua, wala kupika chakula — huyo jina lake mtumwa mjinga. akiuzwa, themani yake ndogo kuliko mtumwa mwelewa.

lakini mtumwa mzalia si mno kuuzwa kwa zamani, illa iwapo feḍuli[1]), hutukana waungwana. nao hawa wazalia — waungwana huwaoa. maʿana huwafanya kama ndugu zao. watoto wanaozaa wazalia kwa mume mungwana — si watumwa.

kazi zao watumwa wajinga.

baʿada ya kununuliwa hupewa nguo mpya, marra hununuliwa jembe, hupelekwa shamba. na huko shamba

1) anmaßend.

kuna nokoa[1]) na msimamizi. yule bwana akifika shamba, humwita nokoa na msimamizi, huwambia: „nimewaletea mjoli.“ nao hujibu: „vema tumemwona.“

ḥatta aṣ-ṣubuḥi nokoa na msimamizi humpeleka shamba kumwonyesha paḥali pa kulima, hukatiwa ŋgwe[2]) yake. akapewa na panga yake, maʿana kipande chake cha shamba kulima muhogo wake na kupanda mboga ao kunde. kinachopatikana katika panga hiyo, si lâzima bwana kumpa, illa atakapo mwenyewe. kama amelima mpunga ao mtama, humpa mpunga kidogo, humwambia: „bwana, nnakupa pepeta[3]) zako.“ na ikiwa mtama humwambia: „bwana, nnakupa msima[4]) wako.“ naye humpa kwa wema wake.

na siku zao watumwa wengine wana siku tatu, wengine wana siku mbili zao. nao hulima mwanzo wa aṣ-ṣubuḥi, ḥatta saʿa tano hurejeʿa majumbani. na alʿaṣiri huenda tenna, ḥatta saʿa ḥedaʿashara huondoka.

na mtumwa iwapo mgonjwa, hendi shamba kulima. humwambia bwana wake: „mjoli fulani hawezi.“ na maraḍi, iwapo makubwa, humṭibu bwana wake, ḥatta apone. na akifa, hutoa sanda, huwambia wajoli wake kwenda kumzika.

nyimbo za watumwa kazi inapokwisha.

nao huimba:

„nokoa, kazi yako isha,
tupe kinua mgongo.“ [1])

1) Rückenstrecker.

ao huimba:

„ukenda Malindi, kanzu na fulana,
ukipata pesa, lifutike sana,

1) Oberaufseher. — 2) tägliche Feldarbeit, kleines Stück Land. — 3) mpunga mbichi. — 4) mtama mbichi.

kama Msengesi[1]), atakutawanya.“ [2])

1) Ein in Zanzibar als Päderast bekannter Araber. — 2) sprengen, andere Ausdrücke sind fira und pasua.

ao huimba:

„bwana siwezi, nipeleke shamba,
hachimbe mwafu[1]) na mkoma Manga[2]),
hizi si ndui, ni tete kuwanga.“

1) wilder Jasmin. — 2) Granatbaum; Manga Arabien.

ao huimba:

„riale ya Shami[1]) haisemi uwongo,
ujapoiweka juu ya udongo
moyo hufuraḥi, hauna kinyongo.“ [2])

1) Taler von Syrien; gemeint ist der Maria-Theresien-Taler. — 2) Ärger.

kazi ya wazalia.

kazi za wazalia: hutumika nyumbani kuosha vyungu ao ṣaḥani, ao kufua nguo, ao kufundishwa kupika chakula, na kushona mkeka, na kufyagia nyumba, na kwenda kisimani kuteka maji, na kwenda dukani kununua mchele ao nyama. na chakula kinapokwisha pakuliwa, kumwandikia bwana wake, na kushika birika kumnawya, ao siku nyingine humwosha miguu bwana wake, na kumpaka mafuta, lakin kwa rukhṣa ya bibi yake. ao bibi yake ataka kwenda shamba ao tangani ao katika hʿarusi, hufuatana naye pamoja. bibi yake kama ana mwavuli, humchukulia.

kaẓâlika ikiwa mzalia mwanamume, hufuatana na bwana wake katika safari, kumtezama akiugua. ao nguo zake zina taka — kuzifua, ao anataka kitu dukani — akamnunulie, hutumika katika killa kazi kama atakavyo bwana wake. ao hupelekwa kiwandani kufun-

dishwa kushona kanzu, kutarizi[1]) nguo, vyatu, kushona kofia, hufundishwa usermala, kufanya milango ya nakshi[2]), ao kujenga nyumba ya mawe ao za miti. akijua kazi hizo, pato lake hutumia mwenyewe, na iwapo mzalia mwema, humkumbuka bwana wake kwa kumpa kitu.

adabu ya mtumwa na bwana wake.

mtumwa ni kusikiliza amri ya bwana wake. akiambiwa „tumika“ — marra atumike. aketwa, marra aje upesi, kusikiliza amri. wala asiseme na bana wake maneno ya ujuvi.

adabu ya mtumwa — akiona bwana wake, ameshika kitu, marra ampokee. kaẓâlika akaingia chumbani kwa bwana wake, avue kofia. na wakifuatana pamoja, hatangulii mbele. na wakifika paḥali pana viti, hakai juu ya kiti.

na killa aṣ-ṣubuḥi na jioni kwenda kwa bwana wake kumwamkia na kutumika kazi iliyoko.

mtumwa, akiamkia bwana wake, hampi mkono, ajapotoka katika safari. wala chumbani kwa bana wake haingii billa ya neno.

adabu ya mtumwa: chakula wanachokula maséyyidi zake, naye lâzima kukila, lakini hali pamoja nao, illa mzalia hula pamoja na bana zake.

khabari ya zamani ya watumwa.

watumwa zamani mrima hawakuwa na ḥaththi[3]) mbele za waungwana. kwanza mtumwa akijulikana katika mavazi, maʿana katika mavazi ʿomri wake havai kofia, akifa jumbe ao asife. wala havai vyatu ao kanzu, iliyo ndefu kufunika miguu. wala mungwana hamtaji jina lake, illa humwita „mwinyi,“ maʿana bana. kaẓâ-

1) besetzen. — 2) Schnitzwerk. — 3) Glück.

lika mwavuli njiani, mvua ikinya, hajifuniki. illa zamani walikuwa na miavuli ya miyaa [1]), ikimpata mvua, hujifunika na mwavuli huo. wala katika nyumba yake haweki vyatu vya mtarawanda [2]).

na wakenda katika karamu, hukaa upande wao, si pamoja na waungwana, kama iliyosemwa katika mbiu:

„mbiu [1]) ya mgambo [2])
ikilia haina jambo,
mbiu ya shomvi [3]) na arbaʿîni [4])
mpumbuji [5]) na mjumbe [6])
pazi na wana wa pazi
wazengere [7]) na wamganda.“ [8])

1) Büffelhorn. — 2) Bekanntmachung. — 3) jumben. — 4) junge freie Leute. — 5) die shaha, waziri etc. — 6) die im Lande geborenen Sklaven. — 7) = wazalia. — 8) = watumwa.

baʿada ya maneno haya husema maneno aliyoamrishwa kusema. na watumwa waanawake, wakifuatana na waungwana waanawake, hawajifuniki ushungi, wala hawavai kaya.

kaẓâlika mtumwa hakai juu ya kiti cha kabesera [3]), wala nyumbani mwake hakiweki. na afanyapo, husema „mtumwa fulani ashindana na sisi, aweka viti vya kabesera ndani ya nyumba yake.“

kaẓâlika mwanzo wa watumwa kutakabbari [4]) — qabla ya miaka kumi na mitano. alikuwako jumbe mmoja, alikuwa na watumwa wengi. siku moja akenda dukani, kuwanunulia kanga na kaya vijakazi vyake, akawapa wakavaa. vijakazi vikataʿajjabu [5]) sana. majumbe mjini wakapata khabari, ya kama jumbe Kisoka watumwa wake amewapa kaya. wakajifunga kwenda kwake kumwuliza. akajibu: „mimi nimefanyiza

1) Dumpalme. — 2) Holzsandalen. — 3) Stuhl mit Lehne. — 4) stolz werden. — 5) sich wundern.

kufuraḥisha moyo wangu na watumwa wangu, na atakaye na afanyize.“ wakaqaṣirika majumbe wote. wakafanya shauri ya kutaka kumpiga vita. wengine wakasema: „haifai,“ ana watu wengi, naye amezalika, ana ndugu wengi katika mji.“ wakamkhaṣimu [1]) wale majumbe.

baʿada ya mwaka mmoja mtaa wa Gongoni kulikuwako jumbe Gungurugwa, akasema: „nami watumwa nitawapa kaya na miavuli.“ vijana wa mji wakasema ndivo. akawavika kaya wazalia wake, akawapa na miavuli, wakatembea mjini. majumbe wengine wakaqaṣirika, wakasema: „hawa majumbe wana chura, wanafanya mambo — wahenga wetu hawakufanyiza. mji huu itaingia ʿishara [2]) ya vita. atawalli mfalme mwingine, ikiwa killa mwezi inakuwa namna nyingine kugeuziwa watumwa. marra nyingine jumbe akifa, baʿaḍi [3]) ya mtaa wanavua kofia, wanaʿuzulu [4]), na baʿaḍi ya mtaa hawaʿuzulu.“

killa siku mashindano, ḥatta sasa hawavui kofia. akifa jumbe, haba kabisa wanaovua, sababu huthanni si lâzima. kaẓâlika watumwa kazi walizo wakifanya zamani — sasa hawafanyizi, ni ile kazi atakayo kufanya, na kama hataki — hafanyizi.

na iwapo ni ʿaṣi [5]), bana wake hawezi kumrudi, humpeleka katika nyumba ya sirkali, hunena — ya kama: „huyu mtumwa ʿaṣi, hafanyi kazi nyumbani.“ sirkali humpa adabu. hii khabari ya watumwa ya zamani na ya sasa.

nikaḥa [6]) za watumwa.

zamani mtumwa akitaka mke, humwambia bwana wake — ya kama: „bwana, mimi namtaka mjoli fulani

1) feindlich sein. — 2) Anzeichen. — 3) Teil. — 4) Kopfbedeckung abnehmen. — 5) ungehorsam, widerspenstig. — 6) Ehe.

kumwoa.“ bwana wake huuliza: „umepatana naye?“ hujibu: „tumekwisha patana.“ humwambia mtumwa wake: „nipe kilemba changu riali.“ sababu mtumwa mjinga kilemba chake hutoa riali. moja kumpa bwana wake, na máhari[1]) yake mwanamke riali tano. akisha toa riali ya kilemba kwa desturi ya zamani — nikaḥa yao, hawendi kwa mwʿallim kuwaoza, illa bwana wao husema: „nimekuoza mjoli wako fulani.“ naye huitikia: „ndio.“ marra huenda akaingia nyumbani kwa mkewe.

lakini sasa wanakwenda kwa mwʿallimu kuozwa kama desturi. na hʿarusi yao hawana sherehe[2]) ya kufanyiziwa karamu, na kualikwa watu, na kushonwa magodoro na mito, hawafanyiziwi desturi hii.

kaẓâlika mtumwa, akiwa ameandikiwa uḥurri, kuposa kwake hamwambii bwana wake — ya kama „nataka kuoa mjoli fulani,“ illa hutafuta mwanamke amtakaye, wakipatana, wakisha huenda kwa bwana wake, kumpa khabari — ya kama: „nataka kuoa.“ maʿana yake ḥéshima kumpa shauri. na bwana wake hujibu: „vema, khiyari[3]) yako wewe mwenyewe.“

ḥatta siku ya hʿarusi huja yule bwana wake kusimamia karamu, maʿana ndiye baba yake. na huyo mtumwa khâdimu[4]) akioa, kama ana kitu — hufanyiziwa furaḥa kama mungwana — ngoma na kualikwa watu wengi. na máhari yake mwanamke tangu riali kumi ḥatta ʿesherîni. na kilemba riali tano atapewa baba yake yule mwanamke, ao ndugu yake; kama hana baba wala ndugu, hupewa mwenyewe mwanamke. na khâdim, ao kama Wasuaḥeli husema „fungu la muungu,“ anaoa fungu la muungu mwenziwe. na iwapo khâdimu — mzalia, huoa mungwana, illa mtumwa mjingá haoi mungwana.

---

1) Morgengabe. — 2) Art und Weise. — 3) Wille, Wunsch. — 4) Freigelassener.

kaẑâlika watoto wanaozaliwa mama yake mtumwa na baba yake mtumwa — watoto hufuata utumwa, na kulla kinachozaa — watumwa, na watoto wakizaliwa — watumwa. mungwana akioa mwanamke wa kitumwa, akizaa mtoto — mtumwa. illa mungwana mwanamke, akiolewa na mtumwa, mtoto wake hawi mtumwa, sababu ungwana umepatikana kwa mama.

khabari ya masuria.

suria — mtu hununua kijakazi, akakiweka nyumbani, kikafundishwa kupika, na kulla desturi ya nyumba. ḥatta akiwa mwari, yule bwana humwambia: „wewe suria yangu, huna rukhṣa ya kutembea nje, ukitaka kitu, wambie watu wakakununulie.“ wajoli wake wakimwona — bwana wao amesema maneno yale, humḥeshimu nyumbani. naye hununuliwa kitanda na mkeka na mito, akapewa chumba chake kama mke. yule bwana akiwa na mke — siku tatu hulala kwa mkewe — siku moja kwa suria. na kama hana mke, suria ndiye mkewe. watu wengine hawataki mke, wanapenda suria, sababu wanasema „suria mkoba,“ maʿana ya mkoba — akisafiri huchukua suria yake, lakini mke ukisafiri — kwanza umbembeleze, tenna uwatake shauri wazee wake — ndio usafiri naye. ndio maʿana kupenda suria.

na wengine wanapenda mke, sababu wakipata mtoto, mtoto atasema: „baba yangu fulani, mjukuu wa fulani, mama yangu fulani, mjukuu wa fulani.“ maʿana ana kuke na kuume[1]), ndio maʿana wakapenda wake.

lakini mtoto aliyezaliwa na suria — vilevile mungwana, hana rukhṣa kuuzwa wala kuambiwa mtumwa, illa daraja yake hana kukeni.

1) d. h. man kennt seine Vorfahren von mütterlicher und väterlicher Seite. —

khabari ya mtumwa kutoroka.

mtumwa akitoroka, iwapo umemnunua katika mji, huenda ulikomnunua, ukawambia: „mtumwa wangu ametoroka, tafaḍḍali mkimwona mleteni.“

ao huenda mtoni ao pwani kuwambia watu wana-ovusha — ya kama: „mtumwa wangu ametoroka, ʿalama[1]) yake każa wa każa, amevaa nguo każa wa każa, qabila yake Mganda ao Msukuma, naye mjinga, kimo chake mfupi, naye mweusi, mkamwona anataka kuvuka, msimpe rukhṣa, mkamateni mumlete kwangu, nami nakaa Bagamoyo qaribu ya fulani, na jina langu fulani.“ bassi yule mtu atarudi mjini.

akifika mtoni yule mtumwa, wakimwona wavushaji, watamwuliza: „wataka nini?“ hajui maneno ya kusema. watamkamata, wampeleke mjini hatta nyumba ya yule mtu, naye lâzima atawapa riali moja uokosi[2]) wao.

kwa zamani za kwanza hufungwa yule mtumwa nyumbani — chumba cha pekeyake mudda siku mbili ao tatu, kisha hupewa yamini[3]), huambiwa: „ukatoroka marra ya pili — ufe.“

khabari ya ʿazima[4]) ya mtumwa.

mtu akitoroka, hununuliwa kamba ya mnazi, ikasomewa „yâ sîni“[5]) mafundo sabaʿ na mwʿallim, hupewa yule mwenyi mtumwa aliyetorokewa, huichukua kwake ile kamba, akafika nyumbani, husimama mlangoni, kumwita yule mtumwa kwa jina lake marra sabaʿ. tenna hutundikwa juu ya mlango ile kamba, bakhti[6]) ikiwako — hurejeʿa yule mtumwa, ao hukamatwa na watu wakamleta.

---

1) Merkmal. — 2) Finderlohn. — 3) Schwur. — 4) herbeizaubern. — 5) Sure 36. — 6) Glück.

khabari ya kumweka mtumwa rahani [1]).

killa mwenyi deni aweza kumpeleka mtumwa wake katika rahani, na yule mtumwa akitaka ao asitake, mâdâm [2]) bwana wake amelazimishwa kuweka kitu rahani. na huyu mtumwa ana rukhṣa kwenda siku moja kumtezama bana wake, siku ya pili arudi.

na iwapo huyu mtumwa ana mke, huweza kuwekwa rahani vilevile, ḥatta mkewe anaweza kuwekwa rahani. nao lâzima wafanyize kazi kama walizo wakifanya kwa bana zao. na iwapo wavivu, aweza kuwarudisha kutaka feḍḍa yake.

khabari ya mtumwa kutaka kukopa.

mtumwa hakopeshwi mali pekeyake, illa kwa amri ya bwana wake. iwapo tâjiri amempa feḍḍa mtumwa, naye anajua, kama huyu mtumwa, akachukua feḍḍa, akenda barra, akafa, ao akakimbia, asirudi pwani — feḍḍa yake imeingia baḥarini, hawezi kwenda kwa bwana wake kuda'i.

lakini ikiwa ameandikiwa, naye anataka kukopa, ana rukhṣa kwenda pekeyake kukopa, kama feḍḍa atakayo. sababu akipoteza, itamlâzim pekeyake kulipa pasipo bwana wake.

khabari ya kuandikiwa ḥurru [3]).

mtu iwapo ana watumwa wengi, hutazama mtumwa, aliyekuwa katika amri yake, humwita: „Mabruki ao Majuma' wewe utapata khaṭṭi ya uḥurru, si mtumwa tenna."

ao iwapo ana mtumwa moja tu, amekaa naye miaka mingi kwa vema, humwandikia ḥurru. akiwa na kishamba kidogo — humpa, tenna humfanya ndugu yake ao mwanawe.

1) verpfänden. — 2) während. — 3) freischreiben.

na mno desturi ya kuandikiwa uḥurru, mtu akijiona mzee, naye anataka kufanya neno la thawabu[1]), akiwa na watoto ao hana watoto, huwambia ya kama: „mimi kijakazi fulani nataka kukiandikia fungu la muungu, nikifa awe kama ndugu yenu, msimtupe.“ marra huandikiwa khaṭṭi, akapewa, amekuwa mungwana. na mtu akiandikiwa, hauzwi wala hawekwi rahani.

khaṭṭi ya uḥurru[2]).

mtu akitaka kumwandikia mtumwa wake ḥurru, ataandika katika khaṭṭi yake: „nimeqirri[3]) fulani bin fulani, ya kwamba nimemwandikia fulani ḥurru kwa mweny'ezimgu, mungwana ma'ana. hana mtu wa kumta'arraḍi[4]), ḥai[5]) yangu ḥatta nikifa, hapana njia ya kumta'arraḍi. na mtu mwenyi kupindua haya, niliyoyaandika katika khaṭṭi hii, atapata żambi[6]) kwa muungu kwa kupindua khaṭṭi hii — mimi niliyemfanyiza mungwana. akija mtu, akamfanyiza mtumwa juu ya khaṭṭi yangu — huyu atapata żambi.“

amma hio ndio aqarri kama hayo. lakini sasa wanakwenda katika nyumba ya sirkali, ikaandikwa khaṭṭi yake kule na kutiwa 'alama ya sirkali juu.

---

1) Gott gefälliges Werk. — 2) Freibrief. — 3) anerkennen. — 4) sich entgegenstellen. — 5) Leben. — 6) Sünde, Strafe.

khabari ya ukarimu[1]).

mtu akiwa na kitu, hupenda kufanya karamu[1]), kuwalika watu marafiqi zake, ao wageni wa mji. huenenda kwake, wakala vyakula.

na mtu akipata feḍḍa kidogo ao fáyida[3]) ningineyo, hununua mbuzi, hufanyiza chakula, aketa watu, wakala. ḥatta mpagazi, akipata upagazi wake, hufanyiza karamu ndogo, aketa wenziwe wakala.

ukarimu mwingine — karimu ni kumwona mtu hana nguo, humpa rupia za kumtosha mavazi yake, tenna humwalika kuja kula. lakini yule atoaye karamu, iwapo ya feḍḍa, si adabu kusema „fulani nimempa jinsi[4]) każa wa każa.“[5])

karimu mwingine ni kumwona mtu hana paḥali pa kulala, na nyumba yake nafasi[6]), humwita, akamwonyesha chumba cha kulala, billa ya kumtoza qo'di[7]), tenna humpa chakula.

na mwingine huwaona maskini katika njia watano ao sitta, huwapeleka nyumbani kwake, humpa killa mtu pesa mojamoja ao záyidi, ao huwapa mpunga ao mtama.

na kama mtu ametoka sokoni, amenunua muhindi ao embe, akimkuta mwenziwe, humwambia: „tafáḍḍali[8]) twaa embe moja ao muhindi kidogo.“ na iwapo wa-

1) Freigebigkeit, Gastfreundschaft. — 2) Fest. — 3) Gewinn. — 4) Art. — 5) soundso. — 6) Raum. — 7) Miete. — 8) bitte.

mefuatana pamoja sokoni, naye anataka kununua matunda, hununua mafungu mawili, fungu lake na la pili humpa mwenziwe.

na iwapo moja anavuta sigaretti [1]), akimkuta mwenziwe njiani, humwambia: „vuta unisazie.“ naye huvuta kidogo, kesha humpa, ao humwuliza: „unaitaka tenna, ao nichukue?“

khabari ya mgeni.

kaẓâlika mgeni akifika katika mji, hana nyumba, hufikia mskitini [2]). akimwona mtu, humwuliza: „unatoka wapi?“ hujibu husema: „mimi sina paḥali pa kukaa wala chakula.“ mtu humchukua nyumbani kwake, akamwonyesha chumba, humwambia; „kaa ḥatta siku unazotaka.“ hamlazimishi qoʿdi. na chakula kikesha, hula pamoja. na akiwa na wasaʿa mwenyeji wake — nguo humpa na akiwa si msafiri wa kuondoka, naye mtu mwema, humtafutia mke, wakampa, huwa jamaʿa yao. na iwapo hajui kazi ya kufanyiza, humwonyesha biʿashara ya mji, na akiwa mkulima, humpeleka shamba wakamwonyesha konde ya kulima, ḥatta awe mwenyeji wa mji.

lakini iwapo ni uvivu, hataki kazi, illa kula na kulala, humtolea maneno ya fumbo — kama „ikiwa ńno ni ńno.“ maʿana mtu, akikaa sana, huchukiza, kama iliyosemwa ndani ya „ushaʿiri wa mgeni.“

1.

mgeni siku ya kwanza
mpe mchele na panza [3]),
mtilie kifuuni [4]),
mqaribishe mgeni.

1) Zigarette. — 2) Moschee. — 3) Rest, der in der ausgeschabten Kokosnuß bleibt. Es gilt als besonderes Zeichen der Liebe, wenn die Frau ihrem Manne oder Kinde in die Kokusnuß selbst etwas Reis mit dem Rest des weichen Fleisches (panza) der Kokosnuß mischt und zum essen überreicht. — 4) kifuu Kokosschale.

2.

mgeni siku ya pili
mpe maziwa na sàmli,
maḥaba[1]) yakizidia
mzidishie mgeni.

3.

mgeni siku ya tatu,
nyumbani hamna kitu,
mna vibaba vitatu
pika ule na mgeni.

4.

mgeni siku ya nne,
mpe jembe akalime.
akirudi mwagane,
ende kwao mgeni.

5.

mgeni siku ya tano
mwembamba kama shindano.
nyumbani hauishi mnoñgono[2]),
atetwa yeye mgeni.

6.

mgeni siku ya sitta
mkila mkijificha,
mwingie vipembeni,
afichwa yeye mgeni.

7.

mgeni siku ya saba'
si mgeni, ana baa,
ḥatta moto mapaani
ametia yeye mgeni[3]).

---

1) Liebe. — 2) Geflüster. — 3) d. h. wenn es irgendwo brennt, sagt man „das hat der Gast gethan," um ihn los zu werden.

8.

mgeni siku ya nane
„njoo ndani tuagane.“
akitokea nje,
„kwa ḥeri, nenda mgeni.“

9.

mgeni siku ya kenda
„enenda mwana kwenenda,
usirudi nyuma,
usirudi mgeni.“

10.

mgeni siku ya kumi
kwa mateke[1]) na magumi[2]),
hapana afukuzwaye
afukuzwa yeye mgeni.“

khabari ya kushangilia[3]) mgeni mkubwa.

kama guverneri mgeni amefika mrima, watu wakipata khabari „leo anafika guverneri mgeni,“ wote hukutanika pwani kumtezama na kumwamkia. na wanapokwenda huchukua ngoma na zumari, wakipata rukhṣa kwa sirkali.

ḥatta akishuka — marra hupigwa ngoma na zumari nao hufuraḥi r′no. shangwe[4]) lao wanalochukulia mgeni:

„yôyô[5]) mgeni wetu,
mwana wa s′ûdi[6]) na jâha[7]),
yôyô mgeni wetu,
muungu ametuletea,
yôyô mgeni wetu,

1) Fußtritte. — 2) Faustschläge. — 3) empfangen. — 4) Freude, freudige Begrüßung. — 5) Freudengeschrei. — 6) Glück. — 7) Freude.

ampe chema kikao,
yôyô mgeni wetu,
ḥatta kurejea kwao,
yôyô mgeni wetu!“

watampeleka na shangwe ḥatta wamfikize kwake, nao warejee. na iwapo wakipata rukhṣa, hucheza siku mbili ao tatu.

kaẓâlika desturi ya kushangilia mgeni, alikuwako tangu zamani mtu wa mji, aliye maʿarufu[1]) kama amesafiri miaka mingi, akirudi — hushangiliwa. naye hutoa kitu kuwapa.

ao Mnyamwezi ameshuka, ana mali mengi, akifika, hushangiliwa. naye hutoa tunza kuwapa watu. lakini sasa desturi ya kushangiliwa Wanyamwezi imeondoka. hii ndio khabari ya shangwe la mgeni.

1) angesehen.

khabari ya nážiri [1]).

nážiri — ni kuwa mtu yuko baḥarini, ukatokea upepo, ikawa jahazi [2]) inataka kuzama kwa upepo, wale waliomo katika jahazi hutokea mtu, akanena: „sisi mweny^{e}zimgu [3]) akatunuṣuru [4]) salâma [5]), tunanážiri kwa sherifu [6]) fulani kupeleka feḍḍa każa wa każa.“ [7]) na ule upepo ukiwa umeondoka, lâzima kumpa feḍḍa yake yule sherifu, waliyemtaja, sababu nážiri kama mtu aliyekopa deni [8]), kulipa ni lâzima.

wa amma ni kuwa mtu hawezi, akanena: „mimi nikipoa maraḍi haya, ntasoma »ahli badri.«“ [9]) lâzima asome, iwapo amepona.

każâlika ni kuwa hana mtoto, akanena: „mweny^{e}zimgu akanija^{a}ali [10]), nikapata mtoto, ntapeleka ukaango wa wali katika qabri [11]) ya sherifu fulani.“ akipata — lâzima apeleke.

wa amma ni kuwa mtumwa wake amempotea, akaweka nážiri: „nimwonapo mtumwa wangu, ninanážiri kuteka maji kupeleka miskitini [12]).

wa amma akiwa mtu hawezi, akaweka nážiri, akanena: „niponapo, ntapeleka mafuta miskiti wa el-

---

1) Gelübde. — 2) Fahrzeug. — 3) Gott der allmächtige. — 4) helfen. — 5) heil, unversehrt. — 6) Scherif, Nachkomme Muhameds. — 7) so und soviel. — 8) Schuld. — 9) Buch der Leute von Bedr. — 10) bestimmen. — 11) Grab. — 12) Moschee.

juma'a." [1]) lâzima akipoa kupeleka miskiti wa el-juma'a, lakini sherţi uwe miskiti wa el-juma'a unaoṣaliwa [2]).

wa amma iwapo amenena: „nikipata sijambo — tapeleka mafuta miskitini," naye hakutaja kama miskiti wa el-juma'a ao si wa el-juma'a, yafa'a [3]) kupeleka miskiti uliwo wote.

---

1) Moschee el-juma'a (Freitag). — 2) ṣali beten. — 3) taugen.

khabari ya vyapo[1]).

kiapo cha mundu[2]) ao cha shoka.

mtu iwapo amekwiba, lakini hapana mtu aliyemwona, watu wanamshuku[3]), ao mwanga[4]) amekamatwa, ao wanamshuku, kana „wewe mwanga,“ watu hawo waliwotuhumiwa[5]) — hutaka vyapo. hualikwa mganga, akapewa kiapo cha mundu. na mundu chuma, huandikwa âya ya qorâni[6]): wa qul jaa el-haqqu wa za haqa el-bâṭilu inna el-bâṭilu kana za huqa.“[7]) kesha hupepewa katika moto kwa kuni za mpingo[8]), ḥatta chuma kiwive. ao hutwaa shoka, likatiwa katika moto, ḥatta likawa jekundu. marra hupewa kuramba[9]) yule, anayekula kiapo, kwa waqati wa aṣ-ṣubuḥi qabla hajala kitu. naye husema yule anayeramba: „mimi nimesingiziwa[10]) uchawi, nami siujui kama mweusi ao mweupe. sasa nakula kiapo. iwapo usiku nnatoka nje kwenda kwanga, ao nafanya chakula kumpa mtoto wa jirani, apate kufa — kiapo cha ḥaqqi nigwie[11]). la — mimi wala mama na baba hawaijui kazi hii, illa ninasingiziwa — kiapo nihongeze.“ marra huramba mundu na ulimi. akisha ramba, mganga humwambia „funua ulimi,“ naye

---

1) Gottesurteil. — 2) Sichel. — 3) im Verdacht haben. — 4) Zauberer. — 5) verdächtigt werden. — 6) Koranspruch. — 7) Sure 17, 83. — 8) Ebenholz. — 9) lecken. — 10) beschuldigt werden. — 11) gwa fallen, gwia auf jd. fallen.

humwonyesha. uwapo ulimi haukuchubuka — kiapo kimemhongeza, kama amechubuka — amenasa.

khabari ya kiapo — iwapo kimemnasa yule mtu, humsuta[1]) na wote kumsomea, ya kama fulani ʿadui[2]), ndiye anayekwisha watu mtaani[3]). humwambia: „sasa tutakupa yamîni[4]), usirejee kazi hii. naye huriḍia[5]) kula yamîni.

iwapo kiapo kimemhongeza, yatakuwa matata makubwa, yatamshukia yule mtu, aliyemshika uchawi, sababu yule aliyeshikwa, baʿada ya kuhongea atalia, maʿana ya kulia amesingizwa uchawi. kwa desturi ya zamani utakuwa ugomvi, na watu wapigane, maʿana uchawi neno kubwa kwa Wasuaḥeli. ao atoe hongezi kumpa, na hilo hongezi feḍḍa, ndio ugomvi utakapokwisha. hii khabari ya mwanga na kiapo cha mundu.

kiapo cha mchele.

mtu iwapo amekwiba, naye anakataa — ya kama „sikwiba," akamtuhumu mwingine, humwambia: „kesho twendeni kwa mwʿallimu, tukaṣafi[6]) nyoyo zetu, tumjue mwizi, na asiyekuwa mwizi." wakesha patana, watakwenda mpa khabari mwʿallimu: „kesho tunakuja kwako." atawambia: „leteni mchele." watanunua mchele kidogo, watie katika ṣaḥani, wampelekee mwʿallimu. atawambia: „njooni kesho aṣ-ṣubuḥi, lakini msilale na waanaume, na waanaume msilale na waanawake." kesha mchele atausomea mwʿallimu, maʿana atashika mchele mkononi, asome âya ya qorâni. wengine wa waʿallim hupeleka ule mchele mskitini usiku kucha, aṣ-ṣubuḥi akauleta kwake. na wengine humwacha nyumbani mwao.

---

1) zur Rede stellen. — 2) Feind. — 3) im Stadtviertel. — 4) Eid. — 5) einwilligen. — 6) reinigen.

aṣ-ṣubuḥi watakuja wote. mtu mmoja atasema: „mimi nataka kuanza kuapa.“ mwʿallimu atateka gao la mchele, asomee tenna âya ya qorâni, kisha ampe yule anayeapa. naye yule mwenyi kuapa atasema: „kiapo cha ḥaqqi[1]) — iwapo mimi nimekwiba ḥaqqi ya fulani, ao nimemwona mtu mwingine amekwiba, nasi tumegawana — kiapo cha ḥaqqi nishike. la — sikwiba, watu wananisingizia — kiapo nihongeze.“ marra gao la mchele hulitia kinywani kutafuna. na mchele huu — haukupikwa — mkavu. na mwʿallimu husoma yâ sîni[2]) ḥatta mwisho. kama mwizi — yâ sîni haiishi, marra yule mtu mchele umemjaa kinywani, hawezi kutafuna, umekuwa unga, mwʿallimu husema: „kiapo kimemshika.“ na kama si mwizi — mchele atautafuna, marra kinywani hamna kitu, amehongea.

na iwapo amehongea, watagomba, watatukanana, ḥatta wapigane. „sababu umenambia mwizi, na kiapo kimenihongeza?“ watapatanishwa na watu. ikawa kupewa kitu — atapewa, na kama hataki kitu, atasema: „mimi nimeṣafi moyo wangu, sitaki kitu.“ hii ndio khabari ya kiapo cha mchele.

kiapo cha mwavi[3]).

mwavi — iwapo mtu mchawi ao mwizi, hupikwa uji uliwo moto, ndani yake hutiwa dawa za mwavi. ukiwiva uji, huja watu, wanaotaka kuapa, mbele ya mganga, naye hutia uji katika kijungu, hupewa mtu yule anayeapa. na huo uji u moto. marra hunywa yule mtu, lakini asiogope. iwapo mwizi — ulimi na mdomo utamchubuka, kama si mwizi — haungui, ataona kama anakunywa maji, kiapo hicho — huwapisha mno

1) Recht, Forderung. — 2) Sure 36. — 3) ein Baum, dessen Blätter oder Wurzel zur dawa-Bereitung genommen werden.

watu wa barra. na wengine wa Wasuaḥeli hufanya vilevile. hii ndio khabari ya kiapo cha mwavi.

kiapo cha shindano [1]).

kiapo hicho anaapisha mwʿallimu. kuapisha kwake wanakuja watu, watakao kiapo, huuliza: „nani atatangulia?“ mtu atajibu: „mimi.“ mwʿallimu atashika shindano, aisomee âya ya qorâni. yule mwapaji [2]) atasema: „kiapo hiki cha ḥaqqi, kama mimi nimekwiba — shindano isipenye, kama sikwiba — itoke kama uzi na shindano.“ marra mwʿallimu humshika shikio, akamchoma shindano. iwapo mwizi — shindano haipiti, naye huona uchungu. na kama si mwizi — shindano marra itapita upande wa pili, amehongea.

kiapo cha sanga [3]).

áṣili yake kiapo cha watu wa barra, nayo shindano. alikuwako mzee mmoja Bagamoyo, jina lake Dogori, alikuwa akiapisha sanga. na kuapisha kwake hushika shindano, akamtia mtu katika jicho, humwimbia mwimbo:

„sanga ndekera [4])
mwanangu.“

iwapo amekwiba, sanga haitoki upesi katika jicho, illa watu wembe [5]) mwimbo huu sana, tenna itatoka. na kama hakwiba, shindano haikai ndani ya jicho. na katika kitako [6]) cha ile shindano huwamo uzi, ndio anaoushika, iwapo shindano imekaa ndani ya jicho. na macho ya yule mwizi yote mawili huwa mekundu. na asipokuwa mwizi, hayamgeuki kuwa mekundu. marra atawambia, kiapo kimemhongeza, „nipeni ʿada yangu,“

---

1) Nadel. — 2) der Schwörende. — 3) Nadel. — 4) leka = wacha; lekera relative Form von leka; ndekera = nilekera. — 5) waimbe. — 6) Oese.

ma'ana yalikuwa ndio kazi yake kuapisha, na watu walimqubali [1]) sana kiapo chake. hii ndio khabari ya kiapo cha sanga.

vyapo vya kisuaheli vya zamani.

mtu iwapo hakutenda jambo [2]), na mwingine amshuku ya kwamba „umetenda," naye hukataa, humwambia: „waweza kuapa?" na vyapo vyao, iwapo anayeapa ni mwanamume, husema: „kana mama yangu" [3]) — neno hili sikulitenda.

ao huapa: „kama dumbu [4]) langu Maatumu" — neno hili sikulitenda. ao husema: „kama shangazi [5]) langu Mwana Fatima."

na iwapo anayeapa mwanamke, huapa kama hivi, husema: „baba, Mwenyi Amiri," ao „ndugu yangu Mwenyi Khamisi" — sikulitenda neno hili.

ao huapa waanaume na waanawake, lakini záyidi waanawake: „palipolala [6]) wazee" — sikufanyiza neno hili, ao „vigononi [7]) pa wazee."

ao husema: „mwana Makuka [8]) anikate" [9]) — sikufanyiza neno hili.

ao huapa: „jua likitua, nitue nalo." ao huapa: „dungumaro [10]) linipinde [11]). ao huapa: „pepo punda [12]) linipinde."

waanawake hatta sasa huapa vyapo hivi vya zamani na watu wengine wa mashamba, lakini waanaume hawaapi vyapo hivi, huapa kwa jina la muungu „wallâhi." [13])

---

1) annehmen. — 2) nichts begehen. — 3) d. h. haramu kama uchi wa mama yangu. — 4) Schwester. — 5) Tante. — 6) d. h. Grab. — 7) gona schlafen. — 8) eine Frau aus Ukami, die vor langer Zeit in Bagamoyo gestorben. — 9) nämlich den Hals. — 10) pepo. — 11) spanne mir den Leib. — 12) pepo. — 13) bei Gott.

mifano[1]) ya Wasuaḥeli wanavoth̲anni[2]) mambo aliyoumba muungu.

khabari ya jua.

dunya[3]) hatuijui mwanzo wala mwisho, illa tunaona siku zinaingia zinatoka, na jua tunaliona linatoka likachwa. illa sisi tunaṣadiqi[4]), ya kama jua linapokuchwa qaribu ya katua, kama wahenga[5]) wetu wamesema — lina mshindo mkubwa kana mzinga, likitua majini, lakini watu hawasikii, illa watoto wadogo na nyama.

jua nalo tunaliona killa siku likitoka, lakini maʿarifa[6]) yake hatuyajui. na majira ya saʿa[7]) hatayajui, zamani hatukuwa na saʿa. ukimwuliza mtu „saʿa ngapi?“ atakujibu: „tezama jua.“ ao hutezama kivuli chake, akapima nyayo[8]). jua likawa kichwani, hujua waqati huu saʿa każa wa każa. na kivuli kikawa nyayo tisaʿ, husema: „sasa saʿa tisaʿ.“ na usiku hawajui saʿa tano wala sitta. na siku za mvua wanajua kwa majogoo[9]) kuwika[10]). jogoo likiwika, wanajua saʿa tano ao sitta, majogoo yasipowika, majira yamewapotea. huko ndiko kuṣadiqi kwao Wasuaḥeli katika jua.

---

1) Gleichnisse, Vorstellungen. — 2) glauben. — 3) Welt. — 4) glauben. — 5) Vorfahren. — 6) Wissen, Kenntnis. — 7) Zeitrechnung nach der Uhr. — 8) Fußspuren. — 9) Hahn. — 10) krähen.

khabari ya mwezi.

hatujui kama ni kioo ao kitu gani, tunaona nuru [1]), ameumba muungu. lakini tunasema — mwezi unapopatwa, unakamatwa na joka [2]). sababu umepita njia, iliyowekwa joka, joka likiona mwezi, linauliza: „sababu nini umekuja kwangu?“ mwezi unajibu: „leo nimepotea njia.“ joka huumeza [3]) ule mwezi, ndipo ulimwengu ukawa kiza. tenna desturi yetu hupiga ngoma kwa nyoyo zetu kuwa na khofu. na joka husema: „wewe mwezi watu wanakupenda katika dunya.“ marra joka huutapika [4]) ule mwezi. tenna joka husema na ule mwezi: „jua linaposhikwa, watu hawaliombei, killa mtu anafanya kazi yake.“ hayo ndio mawazo [5]) waliyokuwa wakiwaza [6]) Wasuaheli. wengi sasa wanayashika, wengine hawayashiki.

na mwezi ukipatwa, usiku watu huamka, wakipasha khabari watu waliwolala — ya kama: „mwezi umepatwa, msilale sana.“ marra watashika madebe [7]) kupiga, na wengine waliwolala wakisikia — wote wataamka. killa atokaye ndani ya nyumba, ana debe mkononi ao jembe [8]), huenda wakigonga [9]) mji mzima. na siku hiyo sirkali hawakatazi, ma'ana anajua mwezi umepatwa.

nao wanaimba mwimbo:

„tuombe, tuombe,
watumwa tuombe.“

ao huimba:

„nipande mkunde [1]) wangu
juu ya msikiti,

1) Bohnenstrauch; gemeint ist der Mond.

1) Helligkeit. — 2) große Schlange. — 3) herunterschlucken. — 4) erbrechen. — 5) Gedanken. — 6) nachdenken. — 7) Blechgefäße. — 8) eiserne Hacke. — 9) auf einanderschlagen.

sijaula kunde[1])
muungu kautwaa."

1) ich habe den Mond kaum gesehen, da hat ihn Gott wieder weggenommen.

ao mojà huimba:
„yâ 'llâh[1]) toba[2])!
yâ 'llâh toba!"
na wengine wote huitikia:
„yâ' llâh toba!
yâ' llâh toba!"

1) = ewe muungu o Gott. — 2) Reue.

lakini waʿallimu wakijua mwezi umepatwa, huenda meskitini[1]), na watu wengine huwafuata. wakifika hutawaḍḍa[2]), marra mwʿallimu hutangulia mbele ya qibla[3]), akaṣalisha[4]), na watu kumfuata nyuma. kesha hukhutubu[5]), lakini ṣala[6]) ya mwezi kupatwa ina mudda[7]) mrefu; yule mwʿallim aṣalishaye, sherṭi ajue sura ndefu kwa moyo[8]). baʿada ṣala inapokwisha, husoma fâṭiḥa[9]) kuomba muungu, awaondolee maraḍi[10]) katika mji.

kaẓâlika jua likapatwa, waʿallimu wanaṣalia, watu wa mji hawaombei jua.

khabari ya ulimwengu[11]).

khabari hii hawaijui Wasuaḥeli, hawajui umbo lake dunya[12]), kwamba ni mti ao ni jiwe, illa wanajua jina la ulimwengu. na maʿana ulimwengu ni „ule mawingu." [13])

nao huṣadiqi, ya kwamba ulimwengu umeziwiwa na ngombe katika pembe zake.

1) in die Moschee. — 2) religiöse Waschungen vornehmen. — 3) Seite der Gebetsrichtung, Altar. — 4) beten lassen. — 5) predigen. — 6) Gebet. — 7) Dauer. — 8) auswendig. — 9) Eröffnerin, 1. Sure des Korans. — 10) Krankheit. — 11) Welt. — 12) Welt. — 13) Ich glaube, daß ulimwengu zusammengesetzt ist aus der Vorsilbe u, dann limwi Sonne, Tag und enga = tazama oder anga = nuru.

khabari ya kitingisha[1]).

kaẓâlika ba'ada ya kulla mwaka mrima hushuka kitingisha. mji mzima hutingishika, vikombe na ṣaḥani huvunjika, na watu huwa na kizungu[2]). Wasuaḥeli wanasema: „n̄gombe, aliyeshika dunya, amegeuza pembe.“ hii khabari wanayoṣadiqi juu ya kitingisha.

khabari ja baḥari[3]).

áṣili[4]) yake ya baḥari, inapotoka baḥari, hawaijui; huṣadiqi, ya kwamba baḥari imezunguka inchi yote, na wao wamekaa juu ya kisiwa, na kuna inchi nyingine vilevile visima, navyo vimezungukwa na baḥari ileile. na ndani ya baḥari n̄na majini[5]), nayo majini mfano wake kama n̄gombe, lakini wakubwa kuliko n̄gombe wa dunya. nao huzamisha jahazi zinapopita, hawali watu, illa huwanyonya[6]) damu[7]). na mtu aliyekufa baḥarini, mawimbi yakimleta pwani, husema: „huyu maiti damu yake imenyonywa na majini.“

khabari ya ra'di[8]) na umeme[9]).

tangu zamani Wasuaḥeli wakisikia ra'di, wanasema: „muungu anazungumza na malaika[10]) wake.“ na umeme ukimulika[11]), wanasema: „muungu amefuraḥi, anacheka, mwaka huu utakuwa mvua nyingi na vyakula.“

kama ra'di haikunguruma[12]), wala umeme hawakuuona kumweka[13]), wanasema „mwaka huu muungu ametuqaṣirikia[14]), tutakuwa na ta'abu[15]) ya vyakula.

kaẓâlika ra'di ikanguruma na umeme, wanakataza watoto wao kuvaa nguo nyekundu, wanachelea umeme usiwaue.

---

1) Erdbeben. — 2) Schwindel. — 3) Meer. — 4) Ursprung. — 5) Ungeheuer. — 6) aussaugen. — 7) Blut. — 8) Donner. — 9) Blitz. — 10) Engel. — 11) leuchten. — 12) rollen. — 13) mweka, meta, metameta blitzen. — 14) sich ärgern über. — 15) Sorge.

nao Wasuaḥeli wanauteka umeme, wanaweka sufuria saba‘, safuria ya mwisho wanafunika kitambaa cha bafta [1]) na kitambaa cha bendera [2]), na chini huwa shimo, nako kuna tope. umeme unapopiga, unatoboa sufuria zote, ḥatta sufuria ya mwisho umeme unazama. wanajua sasa umepatikana. lakini haushikiki umoto, lakini hukaa ḥatta siku ya saba‘, huenda ukatwaliwa — hukuta chuma. na chuma hicho kighali [3]) sana, kinakwitwa suwesi. nao hufanyizwa ńno visu ao panga, lakini ghali sana.

khabari za nyota.

nyota huṣadiqi ni kama vijiwe [4]), muungu ameviweka katika mbingu kumeta [5]) ulimwengu.

na iwapo zinapigana, wanasema: „masheṭâni [6]) wanataka kupanda mbinguni kusikiliza khabari kwa muungu.“ malaika wakiona, masheṭâni wanapandana, wanashika vijinga [7]) vya moto, huwapiga, wakarudi. na wengine wanaanguka, na wengine wanapanda. ndio ma‘ana ya nyota kupandana.

na umbo la masheṭâni — mguu moja na jicho moja na mkono moja, lakini marefu kuliko mnazi. ńno kutembea kwao jioni, ndio sababu Wasuaḥeli jioni watoto wao hawawachi kutembea njiani, wala kula chakula njiani wima, huwakataza, sababu masheṭâni yanatembea mchana na jioni.

kaẓâlika nyota zinazoanguka, mtu akiiokota, akipata mtoto, hutunga kaṭika koja [8]) la mtoto, akavaa yule mtoto. nalo ńno ya hilo koja killa namna ya mbegu ya matunda. anapolala yule mtoto, huwekwa

1) weißes Baumwollzeug. — 2) rotes Zeug. — 3) eigentlich ghali. — 4) kleine Steinchen. — 5) erleuchten. — 6) Teufel. — 7) kijinga ist ein im Feuer angebranntes Holzscheit, hier sind „Sterne“ gemeint. — 8) Halskette.

chini ya mchago[1]) wake, na akiamka hutiwa shingoni mchana kutwa, mtoto asipate kuḍurika[2]). ndio kama ḥirizi[3]) yake yule mtoto.

khabari ya mawingu na pinde[4]).

áṣili ya mawingu Wasuaḥeli hawayajui mwanzo wake wala mwisho, husema „mawingu yametanda, itakunya mvua.“ na tukiona pinde husema „pinde limepinda, mwaka huu yatakuwa masika[5]) makubwa.“ lakini áṣili ya pinde linapotoka hatulijui.

kaẓâlika mwezi ukifanya kitanga[6]) tunasema vilevile „mwaka huu masika makubwa.“

khabari ya kuomba mvua.

Wasuaḥeli siku nyingi kama mvua hawakupata, mashamba yamekauka, huomba muungu. na kuomba kwao — kwanza huenda maqaburini kwa wazee wao, kufyagilia. na wakifika maqaburini, huvua vyatu na kofia na kanzu, kesha hufyagilia, husema: „tumekuja kwenu wavele[7]) wetu, mwaka huu jua limetuḍiqi[8]), mashamba hayana kitu. tumekuja ťyagia, muungu atureḥemu[9]) kwa fáḍili[10]) zenu wazee wetu.“

na kama haikunya mvua, huenenda kwa waʿallimu kuwapa khabari: „mwaka huu muungu ametughaḍibikia[11]), hapana mvua, tuna mashauri gani?“ waʿallimu husema: „tufanyize shauri ya kununua n̄gombe, tufanyize ṣádaqa[12]) katika mji, maʿana jua limekuwa jingi, na maraḍi mengi.“ marra watanunua n̄gombe mweusi ao mwekundu, ao n̄gombe wa mawaa[13]) mawili, maʿana ndio n̄gombe wa ṣádaqa. akipatikana, wataalikwa[14])

1) Kissen. — 2) geschädigt werden. — 3) Amulett. — 4) Wolken und Regenbogen. — 5) große Regenzeit. — 6) Hof. — 7) mvele der Alte. — 8) in Not bringen. — 9) barmherzig sein. — 10) Güte. — 11) ärgerlich sein. — 12) Opfer. — 13) zweifarbig. — 14) eingeladen werden.

waʿallimu wa mji mzima na waanafunzi wao. watatia moto katika chetezo[1]) na ubani[2]), wampe mtu yule ñgombe kumshika, atangulie mbele na waʿallimu nyuma. huenda wakisoma „yâ sîni“[3]) qádiri[4]) killa mtu kumi, na wakesha, husoma „burdai“[5]) killa mtu. nà waanafunzi husoma sura ndogondogo wanazozijua. wataanza mwanzo wa mji kuzunguka na ñgombe ḥatta mwisho wa mji, na kupita killa panapo maqaburi, na kusomea fâṭiḥa yale maqaburi. wakesha, yule ñgombe watamchinsha, nyama yake igawiwe maskini. na kulla wanapoṣali katika meskiti huomba duʿa[6]): „yâ rabbi“[7]), tushushie mvua waja[8]) wako, utuondolee balai[9]) la maraḍi katika mji kwa baraka[10]) zako illâhi el-ʿaâlamîna.“[11])

muungu apokeapo duʿa ya waja wake, siku haziwi nyingi — hushuka mvua. wakafuraḥi watu wote mjini na wa mashamba. hii ndio khahari ya kuomba mvua kwa Wasuaḥeli.

---

1) Räucherschale. — 2) Weihrauch. — 3) Sure 36. — 4) ungefähr. — 5) Sure des Korans. — 6) Anrufung Gottes. — 7) o mein Herr. — 8) von kuja; mja der von Gott kommt = kiumbe Geschöpf. — 9) Uebel. — 10) Segen. — 11) Gott der Welten.

khabari ya siku kuu.

khabari ya „koga mwaka.“ [1])

mwaka kwa Wasuaḥeli siku zake zinapokwisha, zikibaqi [2]) siku mbili kuingia mwaka mpya, siku hizo — ya kwanza inakwitwa „kibunzi,“ na siku ya pili inakwitwa „chenda utupu.“ siku ya kibunzi hukaanga bisi [3]) na maivu, wakamwaga ile bisi pamoja na maivu pembe [4]) za nyumba. tangu zamani ni desturi yao. na maʿana yake wanaṣadiqi [5]), siku ya kibunzi na chenda utupu masheṭâni [6]) hutembea killa paḥali, huwawekea bisi ndio kiziwio [7]) chao.

na siku ya chenda utupu killa nyumba, mtu anayejiweza, hupika jungu la kande ya mhindi [8]) na kunde pamoja, zikawiva hupakua, wakatoa barazani, killa mtu apitaye hula kande hiyo. si desturi kulia ndani, imekuwa kama fuṭari [9]) ya ramaḍani. hakatazwi mtu kula, ni yule atakaye.

kaẓâlika watoto wa chuoni siku tatu wana rukhṣa siku ya kibunzi na chenda utupu na siku ya mwaka. lakini siku ya mwaka mbao zao huzipamba kwa rangi killa namna ya rangi. nao hutoka na mbao zao, nao huimba, mwimbo wao:

---

1) Baden bei der Jahreswende. — 2) übrig bleiben. — 3) ya mtama. — 4) Ecke. — 5) glauben. — 6) Teufel. — 7) von zuia oder ziwia; kiziwio Abwehr. — 8) Topf voll in Wasser gekochter Kasawa. — 9) Fastenessen am Ramasan.

„si chetu si chetu, cha mwʿallimu wetu,
upanga [1]) na mbao na kalamu — zetu,
tupeni kidogo tujendee zetu.
kama ni waume tujieni kwetu,
tuwapondeponde [2]) tuwasagesage.
ʿaqida ʿAbdallah kibebeza.“ [3])

1) Stock hier. — 2) schlagen. — 3) läuft den Frauen nach.

tenna huimba:

„Magubeda, ya Magubeda,
utumbo wa chafi [1]) kwa kunona.“

1) Fisch.

mwimbo huo huenda wakemba killa nyumba, husimama killa nyumba hupewa pesa. zamani walikuwa wakipigana siku ya mwaka beina ya chuo hiki na kingine wakikutana.

kaẓâlika watu wa mji killa inchi siku ya mwaka huamka aṣ-ṣubuḥi sana, waanawake na waanuume, watoto na wakubwa, kwenda pwani kujitosa, maʿana ndio koga mwaka. huchukua mikeka na vitanda kwenda kuviosha, maʿana yake wanaondoa baa [1]) lililopita katika nafsi zao na katika vitu vyao, kutezama mwaka mpya uliwoingia.

na mtu akijitosa — husema: „muungu anondolee maraḍi [2]), anipe uzima, noge mwaka huu na mwakani.“ tenna hujitosa.

khabari ya ramaḍani [3]).

desturi ya Wasuaḥeli katika mwezi wa ramaḍani: Wasuaḥeli wote hufunga mwezi wa ramaḍani siku thelathini, maʿana mchana hawali, wala hawanywi

1) Schmutz. — 2) Krankheit. — 3) Fastenmonat Ramasan.

maji, wala hawavuti tumbaku, mwanzo wa saʿa nne ya al-fajiri[1]) ḥatta saʿa sitta ya jioni, ndipo wanapokula vyakula, jina lake fuṭari. vyakula vyao uji na maandazi na tambi, ao hupika muhogo na ndizi na nyama, ao samaki wa kupaka. na usiku katika saʿa ya tatu wanakula daku — wali na nyama mpaka saʿa nne. na desturi hiyo mpaka mwezi wa ramaḍani ishe.

na unapokwisha mwezi, hufanya karamu[2]) jina lake „siku kuu ndogo.“ watu, walio matâjiri[3]), huweta[4]) watu wengi, wakenda wakala vyakula. na wengine hupika kombe la wali, akenda jirani[5]) zake wakala. na mtu mwenyi mke humnunulia mavazi mapya, na mtoto kaẓâlika. na watu wakubwa huenda wakapewa mikono, wanaambiwa „mkono wa ʿeîdi.“[6]) nao hutoa vitu kuwapa, tenna hupika na karamu kubwa kualika watu kula, na marashi kuwamwagia, na ʿûdi[7]) huwafukiza.

kaẓâlika khabari ya waanawake katika mwezi sabaʿ u ʿesherini ramaḍani: hupika vyakula, wakapeleka kwa wapenzi wao. chakula hicho huitwa „bembe,“ lakini huwa gharimu[8]) sana, maʿana hufanya maandazi na nyama za kukaanga, na killa tunu[9]) iliyo nzuri. wengine hupelekea wazee wao na wachumba wao. na wale waliwopelekewa bembe, wakesha kula, hununua vitu, mavazi yaliyo mema, kurejesha lilikotoka bembe.

na katika mwezi wa ramaḍani aliyolazimishwa kufunga — mtu mkazi wa mji ao mzima, mgonjwa hana lâzima kufunga, wala msafiri hana lâzima, lakini watu hao wana lâzima kuzilipa ṣaumu[10]) zao, mgonjwa anapopona, na msafiri anaporudi katika mji.

---

1) Tagesanbruch. — 2) Fest. — 3) reich. — 4) huwaita. — 5) Nachbar. — 6) Fest. — 7) Aloe. — 8) kostspielig. — 9) Seltenheit. — 10) Enthaltung, Fasten.

na ḥokumu ya waanawake: mwanamke akizaa, ananyonyesha, ana rukhṣa kula mchana. na mwanamke, akiwa na mimba[1]), kama hawezi kufunga, ana rukhṣa kula mchana. nao wana lâzima kuzilipa kwa siku nyingine, baʿada ya mtoto kuwa anakwenda.

na watu wazee, iwapo hawawezi kufunga, wana rukhṣa kula mchana, lakini ṣaumu zao hufungiwa na watu wengine, nao hulipa feḍḍa.

na watoto huamrishwa kufunga mwanzo wa miaka sabaʿ, lakini hawafungi wote — si lâzima kabisa. lakini akipata miaka kumi na mitano, ni lâzima juu yake.

na mtu anayefunga, akilala na mkewe mchana, ṣaumu yake imebaṭilika[2]), ana lâzima juu yake siku moja kuilipa kwa siku settini, ao kutoa kafara[3]). kafara yake mtumwa huacha ḥurru[4]), ao kutoa vibaba settini vya mtama kuwapa maskini.

khabari ya ʿeîdi[5]) kubwa.

na ʿeîdi katika mrima marra mbili — marra ya kwanza mfunguo mosi, marra ya pili mfunguo tatu mwezi kumi, jina lake „ʿeîdi kubwa.“ na siku ya ʿeîdi vijakazi hununua mua[6]) mrefu ao mwanzi[7]), wakaupamba. vikombe na mabaquli madogomadogo na viṣaḥani na bendera hutundika juu ya ule mua, wakatembeza mji mzima mudda wa siku tatu, huimba na mwimbo:

„tuyatungeja maua?
hayana shindano maua,
hayana shindano maua,
tuyatungeja maua?“

na watoto waanaume huimba mwimbo wao:

---

1) Schwangerschaft. — 2) ungültig sein. — 3) Sühne. — 4) frei. — 5) Beiramsfest. — 6) Zuckerrohr. — 7) Bambus.

„Kîndu Kîndu hana meno,
pwani — forḍani.“

maʿana ya Kindu jina la mtu alikuwa kibogoyo [1]).

killa watoto kwa kikao [2]) chao, sababu miwa huwa miwili ao mitatu, na killa mtaa hutoka mua mmoja na watu wake.

na usiku waanawake hucheza msoma [3]). kaẓâlika waqti wa al-ʿaṣiri [4]) vijana waanaume huvaa kanzu zao, wakenda chini ya mwembe, pana kivuli, hupiga kiumbizi [5]) ḥatta wakichoka.

1) ein Zahnloser. — 2) Partei, Klique. — 3) ngoma. — 4) Nachmittag. — 5) ngoma.

maneno ya fumbo [1]).

maʿana ya maneno ya fumbo wanayasema Wasuaḥeli — mtu afanyapo neno lisilo njia, watu husema maneno ya fumbo, asipate kujua. akijua fumbo, hutambua mwenyewe, na kama hajui hatambui. kulla wakitaka maneno yao, mtu asiyajue, husema kwa maneno ya fumbo, máthali [2]) kama kusema:

„ukega [3]) *tembo, kunya, utapasuka mkunda.“* maʿana yake — kama kumwona mtu amejenga nyumba nzuri, nawe waitaka kama ile, lakini huna feḍḍa ya kujengea, ukitaka kujenga — utakwiba, upate ʿizara [4]); hii ndio maʿana yake.

ao *„wa mbili* [5]) *havai moja.“* maʿana yake — aliyojaʿaliwa na stara [6]), atakufa na stara.

„wa mbele hakai nyuma.“ maʿana yake — mtu aliye mbele za watu, harejei nyuma.

1) versteckte Redensarten, fumba zumachen, fumbo zugemachte versteckte Rede. — 2) z. B. — 3) iga nachahmen. — 4) Tadel, Zurechtweisung. — 5) mtu wa nguo mbili. — 6) Ruhe.

„mti hauendi, ʻilla kwa nyenzo.“ [1]) maʿana yake — neno halipatikani, illa kwa kutoa kitu.

„mpanda ngazi hushuka, usingie ujingani.“ maʿana yake — mtu alikuwa mfalme katika inchi, akawa na kibri [2]) na watu, kisha akaondolewa katika ufalme.

„paka akiondoka, panya hutawalla.“ [3]) maʿana yake — mwʿallimu ameondoka, ao mfalme ameondoka katika mji, watu hufanyiza watakavo.

mwezeka [4]) *viwi* [5]), *mtupie nyasi.“* [6]) maʿana yake — ʿadui yako — mzidishie wema.

„mwenda pole haumii migau.“ maʿana yake — mtu mwenyi ṣubira [7]), hapati ḥasâra [8]).

ahenga [9]) *haambiwi mwana.“* maʿana yake — maneno ya ásili haifai kuambiwa mtoto yote.

majuto huja kinyume.“ maʿana yake — mtu amefanya neno la kuua, mwisho wake ataleta majuto.

„mwana umleavyo, ndivyo akuavyo.“ maʿana — mke ao mtu mwingine ulivomzoeza, ndivo atakavofuata.

„mgema akisifiwa, tembo hulitia maji.“ maʿana yake — mwimbaji akemba sana, na watu wakimtunza, hubadili nyimbo zisizofaʿa.

„mkono huo haukati huu.“ maʿana — mtu na nduguye, ao mtu na mtoto wake hampendelei maovu kumfikia.

„mtoto akililia wembe — mpe.“ maʿana yake — mtu asiyesikia neno akakatazika — mwache ende.

„kidole kisicho pete — huvikwa.“ [10]) maʿana yake — mtumwa amefanya kazi nzuri kwa bwana wake, hupewa ijara [11]).

„tanga Pembamnazi [12]) *ḥatta gogo la Mwenyi Shebani.“* [13])

---

1) Beihülfe. — 2) Stolz. — 3) herrschen. — 4) Dachdecker. — 5) -wi schlecht. — 6) Gras. — 7) Geduld. — 8) Schaden. — 9) Vorzeit. — 10) nämlich pete. — 11) Lohn. — 12) Ort. — 13) Name.

maʿana — mwanzo wa mṛima ḥatta mwisho wa mrima, ao mwanzo wa mji ḥatta mwisho wa mji.

„mtaka cha mvunguni, sherṭi uiname.“ maʿana yake — mwenyi kutaka ḥaja[1]), sherṭi awe chini ya watu.

„ashibaye, hamjui mwenyi njaa.“ maʿana — tâjiri[2]) hamjui maskini.

„mrima nyarima[3]*), usipoliwa na nyani, utaliwa na kima.“* maʿana yake — mrima ni barra, usipoliwa na watu wa mji, utanyanganywa na watumwa shambani.

„kendwa[4]*) hayendwa, mkenda kumi, hurudi kenda.“* maʿana — kendwa ni mrima, ukichukua mia, utarudi na tisaʿini, feḍḍa ningine imechukuliwa; ao wakienda watu mia, kumi hufa njaa.

„pendo la mwana liwa[5]*) magoni*[6]*) kwa nina.“*[7]) maʿana yake — mtoto hapendezi, illa mama yake kupendwa na mume.

„uchungu wa mwana wajua mzazi.“ maʿana yake — aonaye uchungu — yule — neno lililompata, mtu mwingine hana uchungu.

„ʿaẓabu[8]*) ya qaburi*[9]*) yajua maiti.“*[10]) maʿana — aonaye uchungu ni yule mgonjwa kitandani.

„kheri[11]*) kuwa mbichi kuliko kuungua.“* maʿana yake — afaḍali[12]) kupata nuṣṣu kuliko kukosa kabisa.

„akuwingaye[13]*) kwake, hakwambii ndokea*[14]*), hukutendea vitendo, ambavyo vya kukuchukia.“* maʿana — anayekufukuza nyumbani kwake, hakwambii „nenda zako,“ hukufanyia mambo yasiyokupendeza.

„ukichungua[15]*) alacho kuka — hatamla.“* maʿana — ukimpeleza sana mke — hamkai sana.

1) Wunsch. — 2) Reiche. — 3) räuberisches Land; enya rima besitzend Fallgrube. — 4) Bezeichnung für die Küste (mrima). — 5) praes. von kuwa. — 6) im Schooß. — 7) seine Mutter. — 8) Strafe. — 9) Grab. — 10) Leiche. — 11) gut, es ist besser. — 12) es ist besser. — 13) winga fortjagen. — 14) niondokee. — 15) hinsehen.

„ulacho ndicho chako, kilichobaqi cha mchimba lindi.“ [1]) maʿana yake — ḥaqqi [2]) yake mtu atumiayo katika uzima, akifa — watachukua mawarithi [3]).

„maskini akipata, matako humlia mbwata.“ [4]) maʿana — maskini akipata, hufurahi [5]) sana.

„njia ya mwongo fupi.“ maʿana — mudda [6]) mdogo hujulikana kama ni mwongo.

„ukungiao [7]) *jichoni — huujui.“* maʿana yake — wakikaa watu thalathini, hujui yupi mwema wangu — yupi ʿadui [8]) wangu.

„maji — kumbe [9]) *na kinywea* [10]), *matupu — yasonga* [11]) *moyo.“* maʿana yake — maji mtu hawezi kuyanywa, illa kupata kifungua kinywa [12]), ukinywa matupu, yatakuumiza tumbo.

„mancno fedda [13]), *majibu ẓahabu.“* [14]) maʿana yake kunena si kazi, kujibu ndio jambo kubwa.

„moyo ni nyongo [15]), *ukigeuka udongo.“* maʿana yake — moyo wa bin Adam [16]) marra hugeuka hivi, marra ukageuka hivi.

„mangwana asiyoʿari [17]) *— kama ñgombe asiye pembe.“* maʿana yake — mtu asiyekhofu watu — kama nyama.

„ukiona wako waungua — wa mwenzio wateketea.“ maʿana yake — ukisema mimi sina rupia tatu — mwenzio hana ḥatta pesa tatu.

„wewe jiwe — mimi nazi.“ maʿana yake — wewe mfalme, mimi raʿia [18]), ao wewe kisu mimi kipini.

„makaa hayakeka nyama.“ maʿana — khasâra [19]) mimi sikuwako kule.

---

1) Grab; mchimba lindi Totengräber. — 2) Recht. — 3) Erben. — 4) macht mbwambwa. — 5) sich freuen. — 6) Zeitraum. 7) ukuingiao. — 8) Feind. — 9) Grund. — 10) Trinken. — 11) drücken. — 12) erste Morgenbissen. — 13) Silber. — 14) Gold. — 15) Galle. — 16) Menschenkind. — 17) fürchten, Achtung haben vor jd. — 18) Untertan. — 19) Verlust.

„kulimbika[1]) *kucha — ugonjwa wa kujitakia.“* maʿana yake — kuvumilia — neno la kutaka, asipotaka — aweza kwenda zake.

„joka[2]) *la mdimu halitundi*[3]) *wala halili, huwasa*[4]) *watundao na walao.“* maʿana yake — ni mtu ʿadui[5]) ao fitna[6]), akatazaye watu kupewa vitu.

„mshare usiwe ngoya[7]) *— hawendi mbali.“* maʿana yake — mfalme asiyo ʿaskari hana nguvu.

„dau la mnyonge[8]) *halendi joshi*[9]), *na likenda joshi, litazama.“* maʿana yake — neno la mtu maskini halisikilizwi, na likisikilizwa, ikatokea jawabu — yatampata matata[10]).

„ya[11]) *mkiwa*[12]) *haiti*[13]), *na ikata*[14]) *hupapata.“*[15]) maʿana yake — biʿashara[16]) ya mkiwa haitii fáyida[17]) upesi, na ikipata fáyida — imekuwa ni bakhti[18]).

„jongo mavunda.“ maʿana yake — ni mtu ʿadui ao fitina anayegombanisha na watu.

„mbuya[19]) *kafiwa, nikamḥani*[20]) *mbuyangu*[21]), *leo mbuya kafa, nikamḥani nani?“* maʿana yake — rafiqi yangu amefiwa, nikamḥani, leo rafiqi yangu amekufa, nikamḥani nani? hapana atakayenijua.

„gomba kwa nguruwe, kwa walimwengu[22]) *li*[23]) *uchungu.“* maʿana yake — qaṣirani[24]) ikufikie wewe, utaona uchungu, lakini ikinifikia mimi, huoni uchungu kama ilivokufikia wewe.

---

1) lang werden lassen. — 2) kleine Schlange, die sich gern auf Zitronenbäumen aufhält. — 3) tunda = chuma; li hier auf dimu bezüglich. — 4) wasa = kataza. — 5) Feind. — 6) Intrige. 7) Gefieder. — 8) Armer. — 9) nach links. — 10) Unannehmlichkeiten. — 11) zu ergänzen kazi oder biʿashara. — 12) Armer. — 13) ita tun. — 14) ikaita. — 15) hin und hertasten. — 16) Handel. — 17) Gewinn. — 18) Glück. — 19) Freund. — 20) Beileid bezeugen. — 21) mein Freund. — 22) Menschen. — 23) ist. — 24) Aerger.

„meno pembe[1]) *hayanyimwa*[2]) *mchesi.“*[3]) maʿana yake — mimi ninacheka tu, lakini nimeqaṣirika[4]).

„umeingiwa ndi.“ maʿana — mtu mkubwa mgonjwa, ameingiwa na maraḍi[5]).

„tembo ameanguka.“ maʿana — mfalme amekufa.

„mjengo begani.“ maʿana yake — mwanamke agombaye na mumewe killa siku, nao hawatulii paḥali pamoja, hupenda kukaa marra nyumba hii marra nyumba hii.

„kenda qaribu ya kumi.“ maʿana yake — vumilia.

„akimpa paka utumbo, mwenyewe utakula nini?“ maʿana yake — afumbiwa mtu bakhili[6]), asiyetoa kitu.

„mwiza[7]) *mbili — moja humwacha.“* maʿana yake — ni mtu mwenyi ṭamaʿa[8]) nyingi.

„ḥámadi[9]) *kilicho bindoni.“*[10]) maʿana yake — kitu kimfaʿacho mtu kilichomo katika mfuko.

„duʿa ya kuku haimpati mwewe.“ maʿana yake — mtu anayemwapiza mwenziwe pasipo sababu, hakufanyiza neno, duʿa yake haimpati.

aiḍa[11]) desturi ya Wasuaḥeli — iwapo amekaa na jirani zake ao watu wengine hawakukaa kwa vema, akinunua mtumwa, humpa jina la fumbo[12]) kuwafumbia majirani zake na watu wengine, kama kumwita: „mwatakani,“ maʿana yake mnanitaka nini ninyi walimwengu? ao humwita „mambo kwa muungu,“ maʿana yake killa jambo latoka kwa muungu, halitoki kwa waana Adamu, machukivu[13]) yenu hayafai.

---

1) meno kama pembe. — 2) nyima verbieten. — 3) Lacher. — 4) ärgerlich sein. — 5) Krankheit. — 6) geizig. — 7) von ku-iza kommen, mwiza ṭamaʿa mbili wer zwei Wünsche hat. — 8) Verlangen. — 9) Lob, Dank. — 10) oberer Saum des Lendentuchs, in dem der Suaheli gewöhnlich sein Geld aufbewahrt. — 11) ferner. — 12) Spitznamen. — 14) Haß.

Khabari za desturi za sheri'a

za Wasuaḥeli.

vifungo[1]) vyetu vya zamani.

khabari ya kongwa.

zamani hatuna gereza[2]) wala minyororo[3]). watu hufungwa gogo[4]) la mti, jina lake kongwa. hutiwa katika mguu moja, nayo hufungwa killa mtu na gogo lake. na akitaka kwenda, anaweza kwenda kidogo, lakini lâzima ashike kamba mkononi kuinua lile gogo, apate nafasi[5]) ya kwenda.

na iwapo watu wamelala, anaweza kufungua kwenda zake, lakini si desturi yao kufanyiza hivo. huchelea kuwaletea matata[6]) ndugu zao. sababu desturi ya watu — mtu aliyefungwa akakimbia, watu watakwenda katika mji wao, aliwotoka, kukamata kole, maʿana ya kole ni watu waliomkhuṣṣi[7]). wakipatikana — watafungwa, ḥatta arudi yule mkimbizi. hii sababu hawawezi kukimbia, illa watu wasiwo mji, wakifungwa, hutezamwa sâna. hao huvunja kongwa, wakenda zao. na kuvunja kwao — hutia mti katikati, akilivunja komeo[8]), marra hutoa mguu wake, akenda mbio. hii khabari ya vifungo vya zamani katika mrima na kwa watu wa barra.

---

1) Haft. — 2) Gefängnis. — 3) Kettenstrafe. — 4) Klotz. — 5) Raum. — 6) Unannehmlichkeiten. — 7) nahe stehen. — 8) Riegel.

khabari ya mbano[1]).

mtu iwapo mchawi, wamemwuliza „umeroga“[2]) — naye anakataa, hufungwa mbano. na huo mbano ni mti, hufanya pembe mbili, humfunga juu ya kichwa, wakafunga kamba. iwapo ameona uchungu, naye kweli ameroga, husema: „mimi nimemroga fulani.“ humfungua mbano, humwuliza: „na nani tenna?“ hutaja kama aliwowaroga. tenna humfanyizia ḥokumu[3]) ya uchawi. ikiwa kuchoma moto ao kutoswa[4]), ao kumpa yamini[5]), asiroge tenna. hii ndio khabari ya mbano.

ao mtu amekwiba mtoto, amempeleka mbali kumwuza, na watu wamemwona, wamemwuliza — amekataa, humfanzia ḥokumu kama hiyo ya kumfunga mbano juu ya kichwa, apate taja.

khabari ya magandalo[6]).

walipokuja maluwali[7]) katika mirima, wakaleta miqaṭale. gandalo ndiwo mqaṭale. na hilo gandalo gogo la mti, urefu wake pima[8]) nne ao tano, lililoziuliwa[9]) tundu katikati. na ʿidadi[10]) ya tundu zinazoziuliwa tangu kumi ḥatta ʿesherini. mtu akiwa amefanyiza neno la ukhalifu[11]), hutiwa katika gandalo. na kufungwa kwake mtu hukaa kitako, likanyanyuliwa gandalo la juu, marra mtu hutia mguu wake, kesha hufungwa. na watu, walio katika kifungo hicho, hawakai upande mmoja, wawili upande huu na wawili upande huu, ḥatta ḥesabu[12]) ya tundu zilizo katika gandalo zijae.

1) Kopfklammer. — 2) jd. durch Zauber umbringen. — 3) Urteil. — 4) ins Wasser werfen. — 5) Eid. — 6) große Fußfessel, Beschreibung folgt. gandalo ist die Suaheli-Bezeichnung, mqaṭale die arabische von mqanṭar (auf Bogen ruhendes Holz). — 7) die arabischen Statthalter der Sultane von Zanzibar. — 8) etwa. 2 Meter. — 9) ziua durchbohren. — 10) Zahl. — 11) Widersetzlichkeit. — 12) Zahl.

nao huwa na mabawabu [1]), wakitaka kwenda chooni, humwambia bawabu, illa choo kidogo huwa na chupa ao kibuyu. ḥatta aṣ-ṣubuḥi huenda wote pwani kumwaga mkojo [2]) wao.

kaẓâlika kufungwa kwake hilo gandalo — mwisho wa lile gandalo kuna kipande cha mti, jina lake kikwamizo. watu wakitia miguu yao yote, marra bawabu huleta gandalo la juu na hicho kipande, akagongomea.

kaẓâlika zamani hawakuwa na magereza, illa hutiwa katika chumba chenyi kiza majumbani mwao wanamolala, ndio gereza lao.

zamani moja qabla ya miaka thalathini kulikuwa na jamadari [3]) mrima, jina lake jamadari Ṣaburi, alimleta Seyyidi Majid [4]) mrima, kuwa ndiye luwali wa Wasuaḥeli. amekaa mrima, hana gereza. watu wakhalifu huwatia katika gandalo, kisha huwawacha nje, amejenga banda. siku moja watu wote wamelala, wakaja chui wawili, wakafika pale panapo watu waliofungwa, wakataka kuchukua wale watu, lakini hawachukuliki, sababu wamefungwa. ikawa wale chui wanaruka huko na huko, wakatia madonda watu wengi. mtu mmoja alikufa, sababu alimparura sana. wale waliwofungwa, walipoona chui, wakalalama. wakaamka Mabulushi [5]), ndio ʿaskari wa yule jamadari. wakatoka nje, wakaona chui. palikuwa Bulushi moja ana mraho [6]), ametaka kumpiga chui, isimpate, ikampata Bulushi mwingine. palikuwa na Bulushi mwingine, naye ana mraho, huyu ndio aliyempiga chui akafa, lakini riṣaṣi [7]) imepisha khasâra [8]), imeua mtu mwingine.

---

1) Türhüter, Wächter. — 2) Urin. — 3) Befehlshaber. — 4) Sultan von Zanzibar. — 5) Beludschen. — 6) lange Flinte der Araber. — 7) Blei. — 8) Schaden.

turejee kwa Seyyid Majid. alipopata khabari, iliyopita mrima, akamwita jamadari, akamwuliza: „sababu watu unawafunga unawawacha nje?“ akajibu: „mimi sina gereza.“ Séyyidi marra akapeleka watu kujenga gereza mrima. ndio mwanzo wa gereza katika mrima, na paḥali palipokuwa gereza, ndio qaribu ya nyumba ya shauri sasa kule Bagamoyo.

khabari ya gereza na minyororo.

na baʿada ya kujengwa gereza katika mirima, hao Waʿarabu, maluwali wa sulṭâni wa Unguja, ndiwo waliwoleta vifungo vya minyororo na pingu, wakafanya na chumba cha ukhalifu[1]) na cha wadeni[2]).

mtu mwenyi kushitakiwa[3]) kwa ájili[4]) ya deni, ao amempiga mwenzi wake fimbo, ao amefanya neno la makosa, neno lile si neno kubwa sana — amma ʿażabu[5]) yake kufungwa katika chumba cha wadeni. walakin si lâzima kumfunga katika minyororo kabisa, ájili tukinena hayo: hiki kifungo cha minyororo ni kifungo kikubwa sana, nacho ḥakimu hiki kifungo cha minyororo katika desturi yote Waʿarabu na Wasuaḥeli yaḥitaji[6]) mtu, aliyokhálifu amri kubwa sana.

na akiwa mdeni, aliyofungwa katika chumba hiki, ikiwa yuko mtoto wake ao ndugu yake ao rafiqi[7]) yake, qádiri[8]) ya mtu anayomjua, akitaka rukhṣa[9]) kwenda onana naye — hupawa rukhṣa, ájili labuda hutokea katika watu wale yumo mtu atamletea shauri ya kumletea mali, alipe deni yake.

walakin[10]) hicho chumba cha ukhalifu hatiwi mtu, illa aliyokhálifu amri ya ḥakim, máthali kama kuua

1) Gefängnis für schwere Verbrecher. — 2) Schuldgefängnis. — 3) angeklagt werden. — 4) Grund. — 5) Strafe. — 6) erfordern. — 7) Freund. — 8) das Maß des = ungefähr. — 9) Erlaubnis. — 10) aber.

mtu, ao amefanya vita kupigana na ḥakim, ao amefanya shauri kupoteza milki[1]) ya ḥakim — huyo ndio atiwaye katika chumba hicho, naye hufungwa pingu. naye hana rukhṣa ya kufunguliwa mlango, illa kwa kupelekewa chakula, wala hana rukhṣa ya watu kwenda mtazama illa siku ya el-jumaʿa[2]), ndipo apatapo rukhṣa ya watu kwenda mtazama. na mlango wake hufunguliwa, ukiwa wazi siku hiyo el-jumaʿa, naye siku ile hatiwi minyororo, illa pingu bassi.

desturi ya zamani: hivi vifungo si namna moja, sababu makosa nayo kaẓâlika si namna moja. yule mtu aliyokosa neno dogo — bassi na kifungo chake kaẓâlika, na ḥokumu yake huwa kidogo, yaḥitaji atiwe chumbani, ndio ʿaẓabu yake.

na iwapo yule aliyofanya amri ile — mtu yule mtumwa — yafaʿa kutiwa katika minyororo, sababu yule mtumwa áṣili yake ni mtu wa kutumika, na iwapo atatiwa minyororo, atapata kutumika vilevile. na mungwana hafanyiwi hayo, illa afanyize makosa makubwa, walakin haiyumkini[3]) mtu aliyoua atiwe katika minyororo, na mtu mwizi atiwe katika minyororo, na mdeni atiwe katika minyororo, na mtu máthali anayemtukana mwenzi wake atiwe katika minyororo, na mtu aliyokhálifu amri ya ḥakimu atiwe katika minyororo. na makosa hayo kulla neno lina daraja[4]) yake, liko neno kubwa na neno dogo — si sawasawa. kaẓâlika na ḥokumu yake vilevile haiwi sawasawa. haiyumkini mtu aliyoua adabu[5]) yake ikiwa pamoja na mtu anayewiwa mali, wa amma mtu mwizi adabu yake ikiwa pamoja na mtu anayowiwa mali, nayo haiyumkini.

---

1) Herrschaft. — 2) Freitag. — 3) es ist nicht möglich. — 4) Stufe. — 5) adabu Anstand und ʿaẓabu Strafe werden beide für Strafe gebraucht.

I.

desturi ya sheri'a[1]) ya uwizi.

maneno hayo yaliyomo humu yameandikwa katika vitabu vya sheri'a, lakini hao wazee wahenga wa zamani hawakuyaona, labuda yametendekana katika inchi yetu qabla ya miaka mitên ao záyidi.

iwapo mtu amekwiba, naye mwenyi kuibiwa ameona kweli, ya kama kile kitu kilichoibiwa ni chake, amma hapo ndipo alipokuwa mwizi, ḥokumu yake yule mwizi kwa desturi ya zamani — hukatwa mkono, na mkono wenyewe unaokatwa — wa kuume. lakini yaḥitaji[2]) yule mwizi ni kuwa bâleghi[3]), asiwe kijana. shuruṭi[4]) ya pili ni kuwa yule mwizi ana ʿaqili[5]) kichwani mwake, asiwe ana wazimu. hapo hakatwi mkono, kwa sababu majununi[6]) hana ʿaqili. shuruṭi ya tatu ni kwiba kitu cha thamani[7]) — hapo hukatwa mkono, isiwe emekwiba pesa mbili ao nane ao kumi ao kitu kilicho ndani ya ḥirizi[8]) — hapo hakatwi mkono. amekwiba, lakini ḥokumu[9]) yake huḥokumiwa ya tartibu[10]).

inapokuwa amekwiba marra ya pili, naye amekwisha katwa mkono, ḥokumu yake hukatwa mguu wa kushoto chini.

---

1) Gesetz. — 2) es ist erforderlich. — 3) mannbar. — 4) Bedingung. — 5) Verstand. — 6) verrückt. — 7) Wert. — 8) Amulett. — 9) Urteil. — 10) Ordnung d. i. bedächtig.

inapokuwa amekwiba marra ya tatu, hukatwa mkono wa kushoto.

inapokuwa amekwiba marra ya nne, hukatwa mguu wa kuume.

amekwiba tenna — huʿaziriwa[1]), na qaûli[2]) nyingine — huuawa. walakini kuṣaburi[3]) záyidi[4]), ájili[5]) roḥo[6]) ya mtu nzito kumwua mtu — żambi[7]) kubwa ŕ no za ʿajabu[8]).

wa amma kwa mila yetu ya kisuaḥeli mwivi akipatikana, na kitu alichokwiba anacho, hunyañganywa kile kitu, naye hupigwa bakora[9]), kisha akaaswa[10]) asitende marra ya pili.

wa amma ḥokumu walizokuja nazo Waʿarabu katika mrima, baʿada ya kule kupigwa, hupelekwa gerezani akafungwa. na akifunguliwa, huambiwa asitende marra ya pili.

aiḍa[11]) na desturi ya zamani: mwivi akija usiku, akichimba nyumba, akiingia ndani qáṣidi[12]) yake kwiba mali, akiondoka mwenyewe nyumba katika usingizi, akamwua mwizi — bassi hana lâzima[13]), kwa sababu mwizi hapo zamani akiingia nyumbani, akimwona mwenyewe nyumba, desturi yao walikuwa wakaḍuru[14]), humwua mwenyi nyumba yake, ndipo nayo anapotanabbahi[15]) mwenyi nyumba, akamtangulia kumpiga mwizi akamwua. bassi fahamu[16]) hiyo ndiyo desturi ya zamani.

na ḥokumu ya mwizi katika hii barra ya Suaḥeli máthali mwizi amekwiba shamba, ndani ya shamba matakataka mangi, naye mwizi asiende mchana, aenende usiku, endapo usiku akauawa — bassi hapana lâzima

---

1) gezüchtigt werden. — 2) Wort. — 3) Geduld haben. — 4) mehr. — 5) Grund. — 6) Seele, Leben. — 7) Sünde. — 8) Wunder. 9) Stockschläge. — 10) verboten werden. — 11) ferner. — 12) Absicht. — 13) es trifft ihn keine Schuld. — 14) verletzen. — 15) aus dem Schlaf erwachen. — 16) verstehen.

kwa desturi ya zamani. anapokuja, ukimwona mchana, haifai kumwaḍiri [1]), si lâzima kumwua, lâzima kumkamata na kumpeleka mbele ya ḥakîm.

aiḍa na khabari za wanyañganya njiani: iwapo mtu akaa njiani kuwavizia watu, wanaopita njiani, akawaua, lakini mali yao, akesha waua, asichukue — bassi mtu huyu ḥokûmu yake huuawa naye, kama alivomwua mwenziwe. ikiwa mwenziwe amempiga riṣaṣi [2]) — naye atapigwa riṣaṣi, ikiwa mwenziwe kamwua kwa upanga — naye atapigwa kwa upanga, ikiwa amemwua kwa kisu — naye atauawa na kisu, na ikiwa mkuki ao mshare — vilevile alivomfanza mwenziwe.

na anapokuwa akikaa njiani, akiona watu akiwaua, akatwaa na mali, huuawa naye bassi, akesha akaṣulubiwa [3]), maʿana watu wote wamwone.

aiḍa na ikiwa yeye hukaa njiani, akiwanyañganya mali ya watu, walakin hawaui wale watu, ḥokumu yake huyo hukatwa mikono yake na miguu yake.

na akiwa yeye huwatisha watu njiani, na wale watu wakimkhofu [4]), walakin hatwai mali zao, wala hawaui wale watu, lakini wao hukimbia tu, na vitu vyao walivyochukua huvitupa, walakin hatwai yeye vile vitu — bassi ḥokumu yake mtu huyo hufungwa, wala hauawi wala hapigwi, lakini huʿaziriwa [5]). na anapotubu [6]) yale aliyoyafanyiza, maʿana akileta majuto [7]) roḥoni [8]) mwake — huondoka kile kifungo, akiwa ḥakîm yafaʿa [9]) kumsameḥe [10]).

wa kaẓâlika mtu mwenyi kuquṣudia [11]) kutwaa mali yako, ukamjua, ya kama huyu anakuja nyañganya mali yangu, ao atakuja twaa roḥo yangu, ao ikiwa una mtoto

---

1) Leid antun. — 2) Blei. — 3) ans Kreuz gehängt werden. — 4) Angst haben. — 5) getadelt werden. — 6) bereuen. — 7) Reue. — 8) in seiner Seele. — 9) es taugt. — 10) verzeihen. — 11) beabsichtigen.

wako njiani, anataka kuja kunyaŋ̃ganya — bassi mwue, umjuapo, ya kama huyu atakuja nyaŋ̃ganya ao atakuja niua, tangulia kumwua weye. na umwuapo — huna qiṣâṣi [1]) kuuawa weye kwa ḥakim, kwa sababu alitaka kukunyaŋ̃ganya ao kukuua, nawe ukanena „afaḍali [2]) ntamwua yeye,“ ndipo ilipokuwa huna qiṣâṣi. lakini yaḥitaji wawepo mashâhidi [3]) watakáyokushuhudia, ya kama alitaka kukuua weye.

wa kaẓâlika na mtu mwenyi kupanda nyama farasi ao punda mle njiani, akaḥaribu [4]) kitu cha watu, hulipa yule mwenyi kupanda nyama, kwa sababu ameḥaribu kitu cha watu, ni vilevile kama kunyaŋ̃ganya mali yao.

khabari ya mwenyi kumpiga ao kumwua mwenziwe.

ḥatta wahenga [5]) wetu wamesema zamani: „maneno ya mrima hayaeshi illa katika mwitu.“ iwapo pana maneno zamani, ameuawa mtu, bassi hukutana watu jeshi [6]) mbili za wale watu wanao maneno, wakija kwa jumbe, mkubwa wa mji. na yule jumbe hupeleka zamani maneno yake kwa pazi, akamwambia — ya kama: „kwangu yako maneno ya khitilafu [7]), walakini maneno hayo takupa wewe, ndio ḥakîm, utazame maneno yao mwenyi ḥaqqi [8]) na bâṭili [9]), uwapatanishe watu wangu.“ na pazi humjibu jumbe, akimwambia: „nimequbali [10]), kwa siku fulani, na tukutane katika uwara [11]) fulani.“

1) Strafe, Vergeltung. — 2) es ist besser. — 3) Zeugen. — 4) zerstören. — 5) Vorfahren. — 6) Heer d. i. Partei. — 7) Unterschied. — 8) Recht. — 9) ungültig d. i. Unrecht. — 10) einwilligen. — 11) freier Platz außerhalb des Ortes, wo die Gerichtssitzungen abgehalten wurden. —

bassi siku, walizopana áhadi[1]) kukutana, kulla mtu hutafuta jeshi yake katika wale watu wawili wenyewe maneno yao, kulla mtu na jeshi yake na silaḥa[2]) zao, na yule pazi kaẓâlika naye huja na jeshi yake na silaḥa zao.

wakesha fika mawarani, hukaa baʿaḍi[3]) tatu. baʿaḍi mbili za ḥaṣima[4]) wawili, wanaosemezana, na baʿaḍi moja hukaa yule pazi, ndio ḥakîm, na jeshi yake. wakesha kutana, áuwali ḥakîm hutaka maṣaḥafu[5]), akaapa yamîni[6]): „billâhi, ya kwama katika maneno yenu tapendelea baʿaḍi, illa tasema maneno ya ḥaqqi. nnenapo maneno ya bâṭili — yamîni ineue, nnenapo maneno ya ḥaqqi, ntaqabali yamîni hii, nilayo, iwe ndio ḥirizi[7]) yangu.“

akesha apa yamîni, ndipo anapowasaili[8]) ya kwama: „nenani maneno yenu.“ ndipo anapotagusa kitara[9]) pazi, akasikiliza. watasema mwanzo wa saʿa ya tatu illa saʿa ya kumi, kulla mtu humpindua mwenzi wake kwa maneno, ili[10]) qáṣidi[11]) yamshinde maneno yake. zama inapotimia saʿa ya kumi, ḥakîm wao pazi maneno yao waliyoyasema yamekwisha mwelea, huwakataza, ndipo anapowaḥokumu, akawambia: „kulla mtu na ashike silaḥa yake ṭayyari[12]), niwaḥokumu kama sheriʿa.“[13]) bassi kulla mwenyewe silaḥa yake hukamata, wakiwa ṭayyari akiwaḥokumu, nao hufuata.

illa inapokuwa ḥokûmu ya damu[14]), kama hawakuona vyema wenyewe damu yao[15]) — marra hupigana papo hapo, ikiwa vita vyao na ḥaṣimu zao. ndio desturi ya zamani sana.

1) Versprechen. — 2) Waffen. — 3) Teil, Gruppe. — 4) feindliche Partei. — 5) Koran. — 6) Eid. — 7) Amulett. — 8) fragen. — 9) Gerichtsverhandlung leiten. — 10) um. — 11) Absicht. — 12) bereit. — 13) Gesetz. — 14) Blut d. h. daß jemand ermordet worden war. — 15) d. h. wenn sie mit dem Urteil nicht einverstanden waren.

ba'ada ya haya: ikiwa mtu amemwua mwenziwe, lâzima mtu yule ḥakîm amkamate amfunge. naye hauawi wala haḥokumiwi, illa kwa shauri[1]) ya wale wenyi kuuliwa mtu wao. kwanza ashauriwa baba ya maiti[2]). hana baba — atashauriwa nduguye baba moja mama moja ao mama moja. na kama hawapo hao — atafutwa aliye afaḍali[3]) ya yule maiti. na yule ḥakîm atawasaili: „ndugu yenu ameuawa, na fulani ndiye aliyemwua, na sasa nimemfunga, shauri yenu mwanenaje? mwataka auawe, kama alivouawa ndugu yenu, amma mwataka, tumtoze dia[4]), awape feḍḍa?“ bassi zama hiyo khiyari[5]) iko kwa wale wenyi ndugu zao, wanenapo „twataka auawe kama alivouawa ndugu yetu,“ ḥakîm huzidi[6]) kuwanaṣiḥi[7]) watu wale, walakin si kwa nguvu, ḥatta wariḍi[8]) dia kwa naṣaḥa[9]), wenyewe wawe raḍi[10]).

na wasiporiḍi naṣaḥa ile ya ḥakîm, wanenapo „sisi twataka qiṣâṣi“ — lâzima ḥakîm atawatolea qiṣâṣi chao wale wenyi ndugu yao, aliyouawa, naye atamwua.

na iwapo watariḍi dia watu wale, lâzima atapatana nao tangu riale 'esherini ḥatta thalathini awape, na yule atafunguliwa.

wa kaẓâlika na rupia hizo za dia mafungu manne, moja la ḥakîm na matatu watwae wenyewe. na katika matatu — mawili ya baba na moja ya mama, kama hana baba wala hana mama — wale nduguze baba na nduguze mama hugawana mafungu matatu, ndio desturi yetu ya zamani.

na iwapo mtu amemwua mtumwa wa mwenzi wake, lâzima ḥakîm atamtaka amfunge, apate 'aẓabu[11]) kwa ḥakîm. kisha yule ḥakîm atamtaka yule bana wake, anene dia ya mtumwa wake. iwapo yule, aliyouawa,

1) Rat, Anhörung. — 2) Leiche. — 3) näher stehend. — 4) Sühne. — 5) Wunsch. — 6) vermehren. — 7) ermahnen. — 8) einwilligen. — 9) Ermahnung, Rat. — 10) zufrieden. — 11) Strafe.

ameuawa maqṣûdi[1]) — bassi ile dia huwa ya gharaḍi[2]), na iwapo si maqṣûdi — bassi ile dia itakuwa mkhafafu[3]). amma hiyo ni desturi ya zamani.

wa kaẓâlika na watu wenyi kugombana, wambao wamepigana, wala wasitoane damu — amri mwenyewe ḥakîm qádiri atakavofanza, kufunga siku mbili tatu — pia amri kwake. na iwapo amemḍuru[4]) kwa ḍarba[5]), humfunga mwenyi kupiga mwenziwe, jumbe akaweta nduguze na babaze, akawauliza shauri: „amemkata, naye tumkate, ao tumtoze mali?“ watakapo mali, atawambia haḍerina[6]): „watu mliopo hapa, uthaminini[7]) mkata huu, wapataje?“ bassi wakasema watu watatu ao wanne, watu wa ʿaqili: „imekuwa ndio themani qadri każa wa każa.“

na iwapo amemkata, pua yote imeondoka, ao shikio lote ao jicho limeondoka, halioni kabisa, ao mkono ameukata, kipande kinakunga, ao umo, lakini haushiki, ao mguu ameukata kipande, enda kwa mguu mmoja, ao amemwĩgoa jino, ao akimḥaṣi[8]), maʿana kumkata mboo — vitu sabaʿ hivi themani kulla kimoja tangu rupia khamso u ʿesherîn ḥatta thalathîn, lakini mungwana si mtumwa.

na kwa mila yetu watu husema „mwenyi kumtoa mwenziwe jicho — naye hutolewa lake, na mwenyi kumkata shikio mwenziwe — naye hukatwa lake, na mwenyi kumwĩgoa jino — naye huwĩgolewa lake, kulla kiungo kwa ḥokûmu yake sawasawa. lakini mtu atendapo kama hivyo, wendapo kwa ḥakîm wao, naye husema: „fulani naye làzima atendwe, kama alivotenda; kama amemtoa mtu jicho, naye lake lâzima litolewe, maʿana hii ni ḥaqqi ya muungu.“ lakini hawa wasemi waliopo humnàṣiḥi ḥakîmu na mwenyi kutolewa jicho

---

1) mit Absicht. — 2) Ziel, Absicht, Wunsch. — 3) gering. — 4) verletzen. — 5) Schlag. — 6) Versammlung. — 7) abschätzen. — 8) kastrieren.

na ndugu zake, ḥatta wapatane, wakiwa mashauri mamoja kutoza dia.

na iwapo mwenyi kutolewa jicho mtumwa, kimba[1]) chake ni ile themani yake, na nuṣṣu[2]) ya themani ndio apewayo bana wake, akagawa mafungu matatu, mawili bana wake moja la mtumwa. ndio desturi ya zamani.

na iwapo mtu amempiga mwenziwe kisu ao mkuki, bassi ḥakîm humfunga kutazama donda la yule aliyopigwa. akipona, hulazimishwa themani ya donda, na akifa hulazimishwa dia.

aiḍa[3]) ikiwa amempiga fimbo, na aliyopigwa amekufa, hulazimishwa dia, tenna ile dia itakuwa ḥafifu[4]), kwa sababu fimbo si qáṣidi ya kuua, kilichokhuṣṣika[5]) na kuua — chuma, ndicho kinachoqáṣidi ya kuua.

---

1) Sühnegeld. — 2) Hälfte. — 3) ferner. — 4) gering. — 5) eigentümlich sein.

II.

desturi ya sheri'a ya deni[1]).

zamani sana iwapo mtu anawia[2]), na yule mdeni[3]) hataki kulipa, yule muda'i[4]) huenenda kwa watu, akawambia — ya kama: „fulani hataki kunipa ḥaqqi[5]) yangu, nataka tafaḍḍalini[6]) twendeni mkanisa'idie.“[7]) naye hutoa kitu kuwapa tangu rupia mbili ḥatta kumi. nao hujifunga, wakenda kwa yule mdeni, humwambia: „mpe fulani ḥaqqi yake.“ na kama hakutoa, akiwa na mtumwa ao kitu kingine — hukikamata. na yule mdeni akiwa na jama'a[8]) na marafiqi, wakiona anaonewa — humsa'idia kwa maneno ao kwa mapigano, ḥatta watokee watu kuwapatanisha.

desturi nyingine ya zamani: mtu anayowiwa deni na Mhindi ao Banyani, na deni ile ikiwa imempata kwa ájili[9]) ya ḥasâra[10]) ya bi'ushara[11]), máthali[12]) ni kuwa kampa biḍa'a[13]) kwenda barra kufanyiza bi'ushara, na kule barra ikijiri[14]) khitilafu ya vita[15]), ikipotea mali ile. ao ni kujiri khitilafu ya wezi, ile mali ikiibiwa na wezi, ao ni kujiri khitilafu ya moto, yale mali ikiwa yalikuwa katika nyumba, na ile nyumba imewaka moto — kama khitilafu tatu hizi zote zikimpata mtu,

1) Schuld. — 2) fordern. — 3) Schuldner. — 4) Forderer, Gläubiger. — 5) Recht. — 6) bitte. — 7) helfen. — 8) Familie. — 9) Grund. — 10) Verlust. — 11) Handel. — 12) z. B. — 13) Waren. — 14) sich ereignen. — 15) Kriegszustände.

aliyokopa mali hiyo — lâzima atalipa mali ya watu. walakini kulipa — kwake. iwapo anayo mali ya kulipa — ndivo, na iwapo hana mali — hupawa mali mengine, akenda akifanyiza bi'ushara tenna. kile atakachopata katika fáyida[1]) yake, akalipa deni ile, wala hafungwi wala hafilisiwi[2]) kwa ájili ya mambo matatu haya.

kaẓâlika neno la nne ni kuwa — mtu amekopa mali, anakwenda fanyiza bi'ushara ya pembe ao mpira[3]) ao sandarusi[4]), na pale mjini vitu vile thamani[5]), akaondoka kwenda barra, ili ḥali[6]) ya kujua vitu hivi kimoja vipo ndicho kinacho thamani, akanunua barra vitu vile, ḥatta khalafu anarudi, ao kulekule barra akapata khabari, ya kama kitu fulani kimeshuka thamani, naye kesha nunua, akanena „sina hila[7]), ájili nimekwisha nunua", akija nacho kitu kile kwa tâjiri[8]) yake, akamwuzia kwa thamani ya ḥafifu[9]), ikimpata ḥasâra katika mali ile — lâzima atampa mali nyingine, akafanyiza bi'ashara, ḥatta amlipe mali yake. wa amma atampa mudda[10]), kilichombaqi[11]) amtafutie, walakini haiyumkini[12]) kumshitaki[13]).

na ikimkinika[14]) kumshitaki kwa ḥakîm[15]), na ḥakîm akamsaili[16]), akamjibu khabari kama hiyo ya khabari yake ya ile ḥasâra — lâzima ḥakîm atamwambia: „patana naye mtu wako, mpe mudda kutafutia mali yako, wa amma mpe mali, akafanyize bi'ashara, na atakachopata katika fáyida yake ujilipe." wala haiyumkini ḥakîm kumfunga yule kwa ájili ya deni kama hiyo, amma kumfilisi yule kwa palepale kwa ájili

---

1) Gewinn. — 2) bankrott erklärt werden. — 3) Kautschuk. — 4) Kopal. — 5) Wert. — 6) im Bewußtsein. — 7) List. — 8) Kaufmann. — 9) gering. — 10) Frist. — 11) übrig bleiben. — 12) es ist nicht möglich. — 13) verklagen. — 14) nötig sein. — 15) Herrscher, Richter. — 16) fragen.

ya deni kama hiyo, qabla hajapawa mudda kutafuta mali ile.

iwapo watu wawili wanawiana, moja akakana, anena „haniwii," na yule anena „namwia" — lâzima yule ḥakîm amsaili yule anayowia, amwulize: „weye unayo baina[1]) ya kumdaʿi[2]) huyu fulani?" na yule anayodaʿi atamjibu ḥakîm — ya kama „nnayo baina," atamwambia „lete baina." atatoa baina yake, ikiwa anayo khaṭṭi[3]), wa amma anayo mashâhidi[4]), wakiomshuhudia[5]) yule, ya kama ḥaqîqa[6]) anamwia — watanena. na khalafu ḥakîm atamsaili yule, anayowiwa, atamwambia: „baina yako ni hii."

na yule anayodaʿiwa, iwapo atakana, na yule anayodaʿi mashâhidi hana, lâzima kwake mwenyi kudaʿiwa aape yamîni[7]), ndipo awe hana daʿawa[8]). ao ḥaqîqa yule anayodaʿiwa atanena „mimi sitaki kuapa, walakin na aape yeye, khalafu mimi tatoa mali ntampa" — lâzima yule anayodaʿi aape yamîni ya náqala[9]), achukue mali yake. wala hawezi kumrejesha ile yamîni yule mtu aliyomdaʿi.

wa aiḍa[10]) mdeni hafungwi kwa ájili ya deni, illa iwapo mali anayo, hataki kulipa, naye ni kuwa ameshitakiwa marra ya kwanza, akataka mudda, marra ya pili akitaka mudda, marra ya tatu ḥakîm humfunga. na iwapo anayo mali — atalazimishwa[11]) kulipa. na iwapo aliyo nayo machache[12]) — hufilisiwa, wakilipwa wadeni wake.

na áṣili[13]) ya kule kumfunga ni sababu ya kuwa anayo mali, naye kulla siku hunena urongo[14]) kwa ḥakîm,

---

1) Beweis. — 2) fordern. — 3) Schuldschein. — 4) Zeugen. — 5) bezeugen. — 6) Wahrheit. — 7) Eid. — 8) Klage, Prozeß. — 9) Uebertragung. — 10) ferner. — 11) gezwungen werden. — 12) wenig. — 13) Ursprung. — 14) Lüge.

bassi imekuwa yeye áuwali [1]) hana adabu [2]) kwa kule kunena urongo kwa ḥakîm, pili thâlim [3]), kuwa na mali anayo, naye asilipe, hapo ndipo anapofungwa.

na iwapo hana mali, hufungwa, ili kutiwa adabu na kutezama, kama kweli ana mali ao hana. akijulikana hana mali, hufunguliwa.

---

desturi ya sheri'a [4]) ya kuḍámini [5]).

shurṭi [6]) za ḍamâna [7]) ni hizi: ḍámini [8]), na mwenyi kuḍaminiwa, na yule mwenyi mali yake, na mali yanayoḍaminiwa yajuikane.

haifai kuḍámini kitu, kisichojuikana qádiri [9]) yake kile kitu chenyewe. máthali [10]) ni kuwa mtu anawiwa feḍḍa [11]), ukanena „nimemḍámini fulani,“ na zile feḍḍa zenyewe huzijui qiâsi [12]) chake, kama kumi ao 'asherini huzijui, ikiwa utaḍámini tu, kwa sababu umesikia jina la feḍḍa anawiwa fulani — amma hapo haifai kuḍámini kwako. illa ukijua kile kitu chenyewe qiâsi chake, kama yule anawiwa feḍḍa każa wa każa, uḍámini kwa neno lijualo. amma ni kuwa anawiwa watumwa każa wa każa, ao anawiwa frásila każa wa każa za pembe, ao frásila za mpira, ao frásila za sandarusi [13]), — hapo umejua qiâsi chake, ukaweza kuḍámini. na ikiwa sandarusi — sharṭi ujue, ya kama unamḍámini sandarusi ya chini ao ya juu. na usipojua qiâsi cha kitu chenyewe — bâṭili [14]) kuḍámini kwako.

wa każâlika hiyo ḍamâna yaḥitajia huyo mwenyi kuḍámini ewe mungwana, na akiwa mtumwa haifai

1) zunächst. — 2) Anstand. — 3) Betrüger. — 4) Gesetz. — 5) bürgen. — 6) Bedingung. — 7) Bürgschaft. — 8) Bürge. — 9) Maß. — 10) z. B. — 11) Silber, Geld. — 12) Betrag. — 13) Kopal, das Suaheli-Wort dafür ist mnangu (II). — 14) ungültig.

ḍamâna yake. tenna awe na ʿaqili, na akiwa ana wazimu, haifai naye ḍamâna yake. tenna awe mwanamume, asiwe mwanamke. wala akiwa mtoto, haifai ḍamâna yake, lâzima awe bâleghi [1]), ndipo itakápofaʿa ḍamâna yake.

tenna imelâzima huyu mwenyi deni akaqubali, ya kama fulani amḍámini fulani.

wa każâlika imeshuruṭiwa, ile deni iwe deni, iliyolâzima kwa kuwa ṣaḥihi [2]) anawiwa. utakapojua kweli anawiwa qadri każa wa każa — umḍámini.

bassi zama ufikapo mudda [3]), yule mdaʿi [4]) ana khiyari [5]) kudaʿi [6]) kwa watu wawili, kwanza kwa mwenyi kuḍaminiwa, pili kwa mwenyi kuḍámini, ijapokuwa amepata nuṣṣu [7]) upande moja, na kilichobaqi atakwenda taka kwa mtu mwingine. pindi inapokuwa yule mwenyi kuḍámini hana kitu, atarejeʿa kwa mwenyi kuḍaminiwa, atake ḥaqqi [8]) yake apawe. wala haifai kunena yule mwenyi kuḍaminiwa — ya kama „mimi sitoi kitu, nenda kamdaʿi fulani aliyoḍámini“ — hayo haifai. ikhiyari hiyo ina yule mwenyi kutaka ḥaqqi yake, popote atakápotaka atataka.

na khaṭṭi [9]) za kuḍámini ni namna mbili. namna ya kwanza kumḍámini mtu na feḍḍa, namna ya pili kumḍámini mtu apoteapo ao akifa.

khaṭṭi ya kuḍámini mtu na feḍḍa huandika:

„mimi fulani bin fulani nimemḍámini fulani katika feḍḍa, anayomwia fulani, riale każa wa każa. pindi asipomlipa feḍḍa yake, lâzima juu yangu mimi kulipa. nimeqirri [10]) kwa haya. sháhidi fulani bin fulani.“

khaṭṭi ya kuḍámini mtu:

„mimi fulani bin fulani nimemḍámini fulani katika feḍḍa, anayowiwa na fulani, riale każa wa każa. pindi

1) mannbar. — 2) richtig. — 3) Termin, Frist. — 4) Gläubiger. — 5) Wahl. — 6) fordern. — 7) Hälfte. — 8) Forderung. — 9) Schriftstück. — 10) anerkennen.

apoteapo ao akifa — mimi lâzima kulipa ḥaqqi hii. nimeqirri kwa haya. sháhidi fulani bin fulani.“

---

khabari ya desturi ya be‘i [1]).

be‘i ina shuruṭi [2]) hizi:

shurṭi ya kwanza — kile kinachouzwa kiwe mali yake, kisiwe cha mtu mwingine. máthalan [3]) amepanga nyumba, amekuja mtu mgeni, amemwambia — ya kwamba: „nyumba hii nitakuuzia wewe kwa be‘i rakhiṣi [4]), sababu mimi msafiri.“ na yule mgeni atamṣadiqi [5]), akainunua — be‘i yake bâṭili [6]).

shurṭi ya pili — yule mwuzaji [7]) asiuze kitu kilicho kibovu, watu wasichoweza kukitumia, sababu kile kitu, utakáchonunua, lâzima kiwe na manfa‘a [8]).

na shurṭi ya tatu — ni kununua kitu, kilichoṣifiwa [9]) na yule mwenyi kitu chake. ikiwa mtumwa ni kukwambia „mtumwa wangu mweusi, naye mrefu sana, na miguu yake minene.“ akakutajia ṣifa [10]) qádiri aliyo nayo yule mtumwa wake. bassi kama inapokuwa ile ṣifa aliyokuṣifia — thâbiti [11]) — imejûzu [12]) be‘i yake, na kama ṣifa alizokwambia zimepungua — be‘i bâṭili.

shurṭi ya nne inaḥitajia [13]) yule mwenyi kuza awe bâleghi [14]), asiwe kijana, tenna awe na ‘aqili [15]), asiwe ana wazimu, tenna awe mwanamume, tenna awe mungwana, asiwe mtumwa.

akiwa mtumwa, sherṭi apewe ízini [16]) ya bana wake, haijûzu kuuza wala kununua kitu, illa kwa ízini ya bwana wake. na iwapo ameuza kitu, amma amenunua

1) Kauf und Verkauf. — 2) Bedingungen. — 3) z. B. — 4) billig. — 5) glauben. — 6) ungültig. — 7) Verkäufer. — 8) Nutzen. — 9) beschreiben, loben. — 10) Lob, Beschreibung. — 11) wahr, richtig. — 12) erlaubt, zulässig sein. — 13) erforderlich sein. — 14) mannbar. — 15) Verstand. — 16) Erlaubnis.

kitu, ijapokuwa mali yake yule mtumwa, ajapo bwana wake, akakataa kule kununua kwake ao kuuza kwake — yajûzu beʿi yake kwa sheriʿa kubaṭilika, kwa sababu yule mtumwa mamelûki [1]), na kile alicho nacho kimemmilikiwa [2]).

wala haijûzu kumkopesha feḍḍa [3]) mtumwa wa mtu, illa kwa ízini ya bwana wake. umwite bwana wake, umwambie: „mtumwa wako anataka feḍḍa kwangu nimkopeshe, nimpe ao nisimpe?“ akupe ízini bwana wake — bassi, akwambiapo „mpe“ — mpe, na akwambiapo „usimpe“ — usimpe. na anenapo „mpe,“ ijapokuwa amekufa yule mtumwa. naye anayo râs il-mali [4]) — lâzima atatoa bwana wake. na iwapo hakukhálifu [5]) mali yule mtumwa, lâzima bwana wake kulipa ile deni [6]) sababu yeye kama ḍámini [7]) kwa mtumwa wake.

tenna haijûzu beʿi ya kughuriana [8]). na huko kughuriana ni kuondoka mtu mjini, akenda mashamba kungoja wasafiri, wanaoshuka na biʿashara [9]), akawambia: „biʿashara hizi, mlizochukua, sasa mjini hazifai, sababu frásila ya mpira sasa mjini rupia tano, lakini mimi nitanunua kwenu kwa rupia sitta.“ na wale wageni wakayaṣadiqi maneno yake, wakamwuzia, na wakija mjini, hupata khabari, ya kama mpira frásila rupia kumi. wakimjua yule mtu, wanaweza kumshitaki [10]), na beʿi inabaṭilika [11]).

wala haijûzu beʿi ya feḍḍa kwa feḍḍa, illa kwa shurṭi tatu. shurṭi ya kwanza ni kama rupia kuvunja kwa riale, shurṭi ya pili ni kuwa imevunjwa ile feḍḍa yenyewe mtali amma mkufu, pale inafaʿa kununua kwa feḍḍa, kwa sababu ni chombo za manufaʿa. shuruṭi ya tatu ni kuwa kumkopesha mtu, akakurejesha vilevile — inafaʿa.

---

1) Sklave. — 2) beherrscht, verwaltet werden. — 3) Silber, Geld. — 4) Vermögen, Kapital. — 5) hinterlassen. — 6) Schuld. — 7) Bürge. — 8) einander betrügen. — 9) Handel. — 10) verklagen. — 11) ungültig sein.

imejûzu kuza žahabu[1]) kwa feḍḍa, kwa sababu imezidi ile žahabu, themani yake kubwa, wala haijûzu kuza mtama kwa mtama, illa mtama kwa mpunga, amma mtama kwa mhindi, kwa maʿana namna yake ni mbalimbali, si moja, kulla kitu kwa themani yake.

wala haijûzu kuuza nyama iliyokwisha chinshwa kwa nyama mzima.

wala haijûzu kuuza matunda yaliyo mtini kukata beʿi máthali kama embe. kutokea mtu, naye ataka embe zilizo juu ya mwembe, yafaʿa kupatana, walakin hamkati themani kabisa — haifai.

wala haijûzu mhogo kukata themani kumwuliza mtu, qabla haujaṉgolewa katika shamba — haifai.

wala haijûzu kuuza kitu, ulichokinunua, illa uwe nacho mkononi mwako, ndio uze.

wa kažâlika wale watu wawili wenyi kufanza beʿi, yule mwenyi kuza na yule mwenyi kununua, wana khiyari[2]) shurṭi yao mudda[3]) wa siku tatu kama amenunua kitu. máthali kama mtumwa akamnunua mtu, mudda wa siku moja amma mbili akamwona hawezi, humrejesha kwa mwenyewe mwenyi mtumwa wake, huenda akimwambia: „huyu mtumwa wako ana ʿaîbu[4]) ya ugonjwa fulani.“ lâzima kutwaa mtumwa wake.

ndio sababu tunazo beʿi namna mbili, beʿi maqṭʿaâ[5]) na beʿi khiyari[6]).

beʿi maqṭʿaâ ni kuuza kitu, mtu akanunua, marra akatoa feḍḍa, akachukua kitu chake, akenda zake.

na beʿi khiyari — mtu ni kuuza kitu, na mwenyi kununua akapatana naye mudda siku tatu, kitokeapo ʿaîbu — kitu alichokinunua kukirejesha kwa khiyari ya wote wawili, na feḍḍa kurejeʿa.

1) Gold. — 2) Wunsch. — 3) Frist. — 4) Schande, Fehler. — 5) endgültiger Kauf. — 6) Kauf unter Vorbehalt.

khabari ya kuweka rahani.

hii khabari ya rahani — kulla kilichojûzu[2]) kuuzwa na kununuliwa, imejûzu kuwekwa rahani, kama shamba, ao nyumba, ao nguo, amma chombo, ao kitu cha feḍḍa cha kuvaa, ao mtumwa — kilicho chote qádiri kifaʿacho kuuzwa na kununuliwa yafaʿa kuwekwa rahani. kumweka mtumwa rahani sheriʿa imeziwia, lakini kwa desturi ya mila watu wanafanya. bassi na hiyo rahani huweka mtu kwa ndia[3]) mbili. ndia ya kwanza anawiwa, naye hana cha kulipa, yafaʿa kuweka rahani mali yake, alipe ile deni anayowiwa. hiyo lâzima, iwapo ile deni yenyewe anayowiwa ya thâbiti[4]) — huweka rahani kitu chake.

ndia ya pili huweka rahani ḥaqqi[5]) yake kwa ḍîqi[6]). iwapo emeḍikika, hana chakula cha nafsi[7]) yake ao kuwalisha alio nao watoto wake ao watumwa wake ao mkewe, na hao lâzima kuwapa ċhakula, naye anaye ṭamaʿa[8]) kama siku moja mbili ao mwezi ntapata feḍḍa, máthali yake kama mtu anakaa mshahara maḥala, na mwezi haujafika kupata mshahara wake, na yule anayokaa kwake kwa mshahara hataki kumpa feḍḍa, illa utimu[9]) mwezi wake, na kungojea hawezi kwa siku hizo, kwa sababu hana kitu nyumbani — lâzima aweke rahani, apate feḍḍa ao chakula, ale na watu wake. ikipata mudda wa mshahara wake, arejeshe feḍḍa ya watu.

na ikiwa hana taratibu[10]) ya kupata feḍḍa, hakai mshahara, wala hana mtu, anayomwia, kama atamlipa feḍḍa, wala hakusafirisha, kama itakuja safari yake — hapo yafaʿa alicho nacho kuuza.

---

1) Pfand geben. — 2) erlaubt sein. — 3) njia. — 4) wirklich. — 5) Recht. — 6) Not, Hunger. — 7) Seele. — 8) Sehnsucht, Aussicht. — 9) zu Ende sein. — 10) Ordnung, Gelegenheit.

wa kažâlika na yule mwenyi kuweka rahani yaḥitajia [1]) awe mtu mzima, asiwe kijana. amma huyu kijana, ijapokuwa mali yake, mâdâm [2]) kijana, hajabâleghi [3]) — haijûzu rahani yake.

tenna asiwe mwanamke yule mwenyi kuweka rahani. na akiwa mwanamke, yaḥitaji kushuhudia mawaliyi [4]) zake wawili vile anavoweka rahani.

na yule mwenyi kuwekewa rahani yaḥitajia awe mwanamume, asiwe mwanamke. na akiwa mwanamke, yaḥitajia washuhudie mawalii zake, anavotwaa rahani. tenna na yule mwenyi kuwekewa rahani yaḥitajia awe mtu mzima, asiwe kijana.

tenna imemlâzimu mwenyi kuweka rahani awe na ʿaqili, asiwe mwenda wazimu, ote watu wawili — mwenyi kuweka na mwenyi kuwekewa.

wa kažâlika ajapokuwa ana ʿaqili, asiwe mbáźiri [5]), shughuli [6]) yake hutwaa mali zake akiweka rahani kwa ájili ya ulevi — haifai rahani yake.

tenna mgonjwa hawezi kitandani hana ʿaqili — haifai rahani yake.

na mtumwa, asiyopewa íźini ya bwana wake — haifai rahani yake.

wa kažâlika na kile kinachowekwa rahani yaḥitajia iwe mali yake yule mwenyi kuweka rahani, isiwe mali ya watu, hapo haifai kuweka rahani.

wala isiwe mtoto kaweka mali ya babaye rahani, si thâbiti rahani yake, maʿana mtoto hana rukhṣa ya kuza ao kuweka rahani ḥaqqi ya babaye, mâdâm hajafa, yu ḥai [7]) dunyani [8]). na ikiwa ameweka rahani ḥaqqi ya babaye iliyo yote, akija mwenyewe babaye, ikiwa hakuriḍi [9]) — lâzima atatwaa ḥaqqi yake.

---

1) erforderlich sein. — 2) während. — 3) erwachsen sein. — 4) männliche Anverwandte. — 5) Verschwender. — 6) Arbeit. — 7) lebend. — 8) in der Welt. — 9) einwilligen.

amma babaye mtu, aonapo mtumwa wa mwanawe, akimweka rahani — yafaʿa rahani yake, haibaṭiliki, kwa sababu yule mtoto na baba yake — mameluki mtoto, na mâdâm amemilikiwa mtoto, na alicho nacho kimemmilikiwa.

amma mtoto haifai kuwekwa rahani, illa ameriḍi mwenyewe kuwekwa rahani. hapo mbali, babaye ana rukhṣa ya kumweka, sababu ametoa rukhṣa mwenyewe.

rahani hukaa ḥatta deni imelipa kwa mwenyi feḍḍa, ḥokûmu yake kama mtumwa wa bana wake. ajapokuwa mungwana — hutumika killa kazi kama mtumwa. kutumika kwake ndio fáyida[1]) ya yule mwenyi feḍḍa. naye ana rukhṣa kutazama bana wake ao kama ni mungwana kutazama wazee wake ao ndugu zake siku moja, kisha hurejeʿa. mudda wao akikombolewa — hurejeʿa kwao, huwa mungwana kama zamani.

na yule, aliyepewa mtu rahani, hana rukhṣa ya kuuza rahani ile, ijapokuwa feḍḍa imekawia kuja.

kaẓâlika rahani ya nyumba hupatana: „mimi nitashika nyumba yako rahani, lakini ukae kwa qoʿdi[2]), killa mwezi unipe riale tatu ao nne, ndio fáyida yangu.“ na rahani ya shamba kaẓâlika hupatana: „kaa katika shamba yako, lakini i katika mikono yangu, huna rukhṣa kuuza illa kwa amri yangu.“

ikawa yule mtu hawezi kukomboa, na mudda umekwisha, hutaka feḍḍa yake, shamba hutiwa mnadani[3]). ikawa deni nyingi, kilichobaqi[4]) atalazimishwa kulipa. iwapo deni haba, kilichobaqi mwenyi shamba lake.

aiḍa kama mtu amepewa rahani mtumwa, ametoroka yule mtumwa, ao amekufa yule mtumwa, ao amepewa farasi ao punda, ikiwa wamekufa ao wamekimbia — halipi mwenyi kuwekewa. haifai kusema „mtumwa

1) Gewinn. — 2) Miete. — 3) zur Versteigerung. — 4) übrigbleiben.

wangu amekufa — „mlipe,“ ao „amekimbia — mlipe.“ walakin hulipa, iwapo amempiga yule mtumwa, akatoroka yule mtumwa kwa uchungu ya fimbo zilizompata — hapo lâzima atalipa, maʿana amemtorosha. lakini kule kumpiga kwake yaḥitajia wawepo na mashâhidi, wamwone anavompiga — ndipo itakápokuwa lâzima kulipa.

na pili ni kumkamia [1]) yule mtumwa — akimwambia „weye ikifika usiku, ntakupiga, amma ntakuua“ — akatoroka yule mtumwa kwa khofu [2]) ya maneno aliyomwambia, na pale aliponena ikiwa mashâhidi wapo wanamshuhudia kule kunena kwake — lâzima atalipa.

na watu wakiweka rahani, wanaandikiana khaṭṭi [3]) kwa mudda. na hiyo khaṭṭi:

„mimi fulani nimetwaa feḍḍa kwa fulani riale każa wa każa. nimempa shamba yangu rahani katika mikono yake kwa mudda wa miezi każa wa każa. jirani ya hilo shamba kusi fulani, na kaskazi fulani. shâhidi fulani.“

---

khabari ya kuokota kitu njiani.

desturi ya zamani: mtu aliyookota kitu njiani, wâjibu [4]) kitu kile, kikiwa cha mali, apeleke kwa ḥakîm [5]). na hakîm atampa amri ya kukitembeza [6]) kile kitu killa panapo njia panda na panapo soko, ḥatta apatikane mwenyewe, akampe mbele ya ḥakîm. ao ḥakîm ataweka kitu kile, zama atokeapo mwenyewe, akitafuta kitu chake, lâzim yule ḥakîm atamsaili [7]): „kitu chako namna gani? kimekupotea siku gani? maḥala gani?“ ni iwapo ni feḍḍa, atamsaili: „riale ngapi?“ iwapo yule mtu ḥaqîqa [8]) amepotelewa, atamjibu ḥakîm: „riale każa wa każa, nazo zilikuwa katika kitambaa, na kita-

1) drohen. — 2) Furcht. — 3) Schriftstück. — 4) Pflicht. — 5) Herrscher. — 6) öffentlich bekanntgeben. — 7) fragen. — 8) Wahrheit.

mbaa hicho namna yake cheupe ao cheusi ao chekundu. na iwapo yale maneno anenayo ni kweli, lâzima apawe ḥaqqi[1]) yake.

na isipokuwa maneno anenayo si kweli, máthali kama kunena „mali yangu riale settîn,“ na ile feḍḍa iliyookotwa ni riale arbaʿîn ao nakhiṣ[2]), hutazamwa bassi katika maʿarifa[3]) kwanza, li ájili[4]) labuda yumkini[5]) yule aliyookota ameficha kitu, khitilafu[6]) ile imekuja kwa ájili yule aliyookota, huangaliwa, naye iwapo anayo dalili[7]) na baina[8]), bassi maneno ya yule aliyopotelewa ṣaḥiḥi[9]) — lâzima apewe ḥaqqi yake.

na iwapo yule aliyookota ni mtu ṣâliḥi[10]), naye akitazamwa hana dalili ile, imekuwa maneno ya yule khitilafu, huzuiwa ḥaqqi hii kwanza.

na kama hakuonekana mwenyewe, nacho ni kitu cha mali, ḥakîm atakizuia. na kama hakina thamani[11]) kubwa, ḥakîm atampa mwenyi kukiokota.

ao iwapo mtu ameokota kitu kidogo — hukinadi[12]), na kukinadi kwake huenenda katika mskiti[13]), mno katika mskiti wa el-jumaʿ[14]), sababu huja watu wengi kule, tenna huuliza: „hapana mtu aliyopotelewa?“ na iwapo yupo mtu, aliyopotelewa, akanena: „ni mimi, kimenipotea kitu każa wa każa.“ iwapo ṣaḥiḥi, atampa mwenyewe. na iwapo sicho — hampi, atazidi kutafuta mtu mwingine.

wa aiḍa máthali imeokotwa kitu katika baḥari[15]) ao katika barra, kikawáṣili[16]) kwa mkubwa wa inti[17]), kama máthali ya jumbe, bassi fahamu[18]) yule mkubwa wa nti[17]) huamru[19]) kugawiwa mafungu mawili, fungu

1) Recht. — 2) weniger. — 3) Kenntnis. — 4) Grund. — 5) vielleicht ist es möglich. — 6) Unterschied. — 7) Anzeichen. — 8) Beweis. — 9) richtig. — 10) rechtschaffen. — 11) Wert. — 12) öffentlich ausbieten. — 13) Moschee. — 14) Hauptmoschee (Freitagsmoschee). — 15) Meer. — 16) ankommen. — 17) inchi. — 18) verstehe. — 19) befehlen.

moja lake mkubwa wa nti, na fungu la pili hupawa mawaziri wa mji pamoja na watu walio katika nti, wakagawana. desturi anayookota kitu cha mali, hana rukhṣa kukitwaa yeye, illa kupeleka kwa jumbe.

na iwapo mtu ameokota kitu, amekula — ataḥokumiwa, atozwe mali, awapo ana mali, kama hana mali — bassi hana ḥáḍara[1]). ikitokea karamu[2]) ao neno jingine kama máthali hʿarusi[3]), qadri ya jawâbu[4]) linaloḥuḍuria[5]) mkubwa wa inti, henendi yule aliyokula mali ya inti, labuda atoe mali kwanza, kama alivoḥokumiwa kwa mila ya Wasuaḥeli, ndipo enende katika karamu ya watu.

na mtu anayokaidi[6]), hutolewa katika mashauri — asiwemo, wa każâlika huandikwa barua, zikipelekwa katika miji, wakaʿarrifiwa[7]) — ya kwamba: „fulani hayumo katika mashauri ao karamu. bassi fahamu kulla endapo, ikiwapo karamu ao hʿarusi ao amekufa mtu, mkimwona katika baraza, hufukuzwa asikae.“

aiḍa iwapo huyu mwenyi kukhálifu[8]) akenda kwa mkubwa wa nti akaangukia, humpokea yule mkubwa wa inchi, naye humpeleka kwa jumbe — ya kama: „fulani amekuja kwako kuangukia kwa makosa aliyoyatenda.“ naye humpokea, wakiwa naye kama zamani.

desturi ya kuokota mtumwa:

mtu humpeleka kwa jumbe, naye jumbe humziwia yule mtumwa. mwenyewe anapokuja, akisema, ya kwamba amepotelewa na mtumwa, humwuliza: „qabîla[9]) gani?“ hujibu. tenna humtoa nje yule mtumwa kumwuliza: „huyu ndiye bwana wako?“ hujibu: „ndiye bwana

1) Gegenwart, Anwesenheit d. h. hier „er hat kein Recht anwesend zu sein.“ — 2) Fest. — 3) Hochzeit. — 4) was immer für eine Gelegenheit. — 5) anwesend sein. — 6) widerspenstig sein. — 7) mitgeteilt werden. — 8) zuwiderhandeln. — 9) Stamm.

wangu.“ bassi humpa, naye hutoa uokosi[1]) rupia mbili. na zile rupia mbili hupewa yule aliyookota.

na kama mtumwa akikataa, akasema: „huyu si bwana wangu — humziwia jumbe, kamwambia bwana wake, alete mashâhidi, washuhudie, kama kweli huyu mtumwa wake.

na kama hana mwenyewe yule mtumwa, huwa mtumwa wa jumbe, huambiwa mtumwa wa mboni[2]).

na iwapo mtumwa amegomba na bwana wake, wala hamtaki bwana wake, hutoroka, akenda akashika ngoma kuu za jumbe, ma'ana ameangukia miguu, naye anataka ḥemâya[3]) ya jumbe. naye humwuliza jambo alilo nalo, tenna huitwa bwana wake. huulizwa mtumwa: „wataka kwenda kwa bwana wako?“ akikataa, humziwia yule jumbe, akafanya kazi kwake.

---

desturi ya sheri'a ya amâna[4]).

desturi ya Wasuaḥeli amâna zao shidda[5]) kuweka majumbani mwao, wanapatana na matâjiri[6]) zao kuwawekea, sababu majumba yao mabovu. marra huingia mwivi, marra huingia moto, na paḥali pema pa kuweka hana. na iwapo anapatana na Msuaḥeli mwenziwe, humtezama sana mwenyi moyo wa imani[7]), na nyumba yake iliyo njema — humpa kumshikia.

mtu aliyompa amâna mwenzi wake, kumwekea nyumbani mwake, na mle nyumbani wakija wevi, wakeba amâna ile, ao ikija vita, vikachukuliwa vitu vyake katika nyumba pamoja na amâna ile, ao ukingia moto, ikiungua nyumba na amâna ile, katika desturi ya sheri'a haimlâzima kulipa yule, aliyopawa ile amâna kuweka.

1) Finderlohn. — 2) Sklave des Augapfels, weil er mit dem Auge gefunden wurde. — 3) Schutz. — 4) Sicherheitsdokument, Depositum. — 5) selten. — 6) Kaufleute. — 7) Vertrauen.

na iwapo yule mwenyi amâna hakuṣadiqi [1]), ya kama amâna yake imeibiwa, ao imekhitalifu [2]) kama hivo nilivonena kwa vita ao kwa moto — bassi lâzima atamṣadiqia kwa yamîni [3]).

iwapo mtu ametoa amâna kumpa mtu „niwekee,“ na yule, aliyopawa, akimpa mtu mwingine kumwekea, na kule alikoweka ikapotea ile amâna — lâzima yule aliyopawa amâna ile kwanza atalipa, kwa sababu ameta'adi [4]) kuaminiwa [5]) yeye, na yeye akatafuta amîni [6]) wake, amtakayo, kwa juu ya amâna ya mtu mwingine — hapo ndipo atakápolipa.

lakini amwambiapo yule mwenyi amâna yake — ya kama „umenipa amâna yako kuweka, lakini mimi katika nyumba yangu si amîni kuweka kitu, vitu vyangu mimi huweka kwa fulani, na amâna yako kaẓâlika ntakwenda weka kwa fulani, iwapo umeridi [7]) haweke [8]) huko, takwenda weka, na iwapo hukuridi, nijibu“ — akamjibu yule mwenyi amâna yake „nimeridi kaweke,“ akenda akiweka kwa íẓini [9]) yake yule mwenyi amâna yake, amma ikija khitilafu [10]) — haimlâzimu kabisa. illa akanapo yule mwenyi amâna yake, ya kama hakumpa rukhṣa — hapo da'awa [11]) yao hukatika katika yamîni.

na iwapo mtu amempa amâna mwenzi wake kwenda mnunulia kitu ao mtumwa barra, kitu kile kikaibiwa, ao yule mtumwa akikimbia — haimlâzima, illa iwapo amâna ile naye alimpa mtu mwingine kwenda nunua ile bia'shara, ḥokûmu yake kama tuliyoinena áuwali. amma hio ndio desturi ya sheri'a ya Wasuaḥeli.

---

1) glauben. — 2) zu Grunde gehen, verderben. — 3) Eid. — 4) sündigen. — 5) vertraut zu werden. — 6) Vertrauensmann. — 7) einwilligen. — 8) nikaweke. — 9) Erlaubnis. — 10) Verderb. — 11) Klage.

khabari ya shirka[1]).

shirka — mwanzo wake ni kuondoka watu wawili wakataka kufanyiza kazi pamoja, wakesha patana, killa mtu hutoa mwanzo wa mali yake kumwonyesha mwenziwe. tenna hupatana katika biʿashara[2]) ambazo[3]) watanunua. wakisha, hupatana fáyida[4]) na khasâra[5]), tenna huingia katika biʿashara.

na hiyo biʿashara iwapo mjini, killa mtu huenda upande wake kufanya biʿashara atakayo kuuza na kununua. ḥatta jioni hukutana paḥali pamoja, kuoneshana walichokipata. na wengine kwanza hupatana kupeana yamîni[6]) kuchelea kufichana na kudanganyana katika kupata na kukosa.

kaẓâlika na iwapo wanafanya biʿashara ya barra ni kama hivyo, killa mtu huenda barra, ao huagana mmoja kwenda barra, na mmoja kukaa katika mji. yule anayekaa mjini, kazi yake huuza biḍaʿ[7]), itokayo barra, na kununua biḍaʿ ya mjini, kumpelekea mwenziwe barra. na wakipata fáyida, hugawa sawasawa, na khasâra vilevile.

kaẓâlika na shirka yao hukaa, mâdâmu wanataka, wala hawathulumiani[8]), amma huisha shirka yao kwa sherṭi mbili — kufa moja wapo, ao mmoja mlevi, na kutumia mali billa ya náthari[9]), hapo shirka hubaṭilika[10]).

na sharṭi ya hao washirka — sharṭi wote wawili wawe mabâleghi[11]), tenna wawe na ʿaqili, haifai shirka kwa mtu asiye bâleghi, wala asiye ʿaqili.

wa kaẓâlika hawana rukhṣa wote wawili katika feḍḍa ya shirka kukopesha wala kukopa feḍḍa, illa kwa kushauriana.

1) Gesellschaftsunternehmen. — 2) Handel. — 3) veraltetes Relativ. — 4) Gewinn. — 5) Verlust. — 6) Eid. — 7) Waren. — 8) betrügen. — 9) Ueberlegung. — 10) ungültig sein. — 11) erwachsen.

na wao hawalazimishani feḍḍa ao mali, iliyopotea, sababu nyumba alimokaa imeingia moto, ao mwizi amekwiba, na watu wote wanajua.

na iwapo wamesafiri, sherṭi wendako — wote waweane raḍi[1]). lakini moja akimkataza mwenziwe — ya kama „maḥali każa wa każa usende,“ naye akenda kwa khiyari[2]) yake, akapata khasâra — yake pekeyake.

na iwapo wamepata khasâra, na mwenziwe anakataa khasâra, billa hakufanya neno lisilo njia, naye hataki kulipa ile khasâra — sheri'a haimsikizi, ma'ana alivokula tamu — na uchungu lâzima aule.

---

desturi ya sheri'a[3]) ya shâhidi[4]) na ya yamîni[5]).

áuwali[6]) yule shâhidi yaḥitaji[7]) awe islâmu[8]), naye ewe[9]) anaṣali[10]), kulla siku anaṣali, na kufunga hufunga, ikifika mwezi wa ramaḍani[11]) — mtu huyu ushâhidi[12]) wake huqubaliwa[13]) kwa ḥakîm[14]). khaṣṣa[15]) iwapo yule mwenyi kushuhudiwa anaṣali, lâzima na yule shâhidi awe anaṣali, ndipo ukamilike ushâhidi wake. na iwapo yule shâhidi haṣali, na yule anayoshuhudiwa akanena „huyu si shâhidi, kwa sababu haṣali“ — hubaṭilika[16]) ushâhidi wake kwa ḥakîm.

na pili yule shâhadi yaḥitaji awe mungwana, wala haufai ushâhidi wa mtumwa, ijapokuwa mwanamume.

wa każâlika ushâhidi wa mwanamke bâṭili[17]), hana ushâhidi kabisa.

---

1) zufrieden. — 2) Wille. — 3) Gesetz. — 4) Zeuge. — 5) Eid. — 6) zunächst. — 7) es ist erforderlich. — 8) dem Islam angehörend. — 9) awe. — 10) beten. — 11) Fastenmonat Ramasan. — 12) Zeugnis. — 13) angenommen werden. — 14) Richter. — 15) besonders. — 16) ungültig erklärt werden. — 17) ungültig.

haqubaliwi mtu kwa shâhidi mbele ya ḥakîm, illa ajuilikane, ya kama huyu ʿádili [1]), na maʿana ya ʿádili ni mtu, anayokucha muungu, hataki ḥaqqi ya mtu kuthulumu [2]), tenna asiwe fasiqi [3]), shughli [4]) yake kuzini [5]) amma kulewa — haufai ushâhidi wake, ajapokuwa mungwana.

wa kaẓâlika yule shâhidi yaḥitaji awe bâleghi [6]), asiwe mtoto mdogo, na tenna awe na ʿaqili [7]), asiwe mwenda wazimu, haufai ushâhidi wake.

wa kaẓâlika haufai ushâhidi wa mtoto kumshuhudia babaye. míthili [8]) kama mtu anamwia mtu, na huyu mwenyi kuwiwa akikana, ya kama hawiwi kitu, na yule ḥakîm akimwuliza yule mwenyi kuwia: „unayo shâhidi?“ na yule akanena „nnayo shâhidi mtoto wangu, ya kama namwia huyu“ — bassi hauqubaliwi ushâhidi ule kwa ḥakîm, kwa sababu yule mtoto na yule babaye hana buddi [9]) kumpendelea babaye, ndipo ulipokuwa haufai ushâhidi ule na mtoto kumshuhudia baba yake. wa kaẓâlika hauqubaliwi ushâhidi wa mtoto kumshuhudia mama yake.

wa kaẓâlika haifai mtu kumshuhudia ʿádui [10]) yake. míthili kama watu wawili wanagombana, hawasemi beina [11]) yao, bassi watu wawili hao haifai kushuhudiana, maʿana beina yao uʿádui, kulla mtu hampendi mwenziwe, bassi haifai kushuhudiana.

wa kaẓâlika yule asiwe nduguye anayodaʿi, wala asiwe mshirika wake yule anayodaʿi, wala asiwe anamwia yule anayodaʿi, anashuhudia qáṣidi [12]) apate yule, naye apate mlipa. ushâhidi wa watu hao haufai.

wala haiqubaliwi barua ya qâḍi [13]) kwenda kwa qâḍi katika ḥokûmu [14]) — illa washuhudie masháhidi watu wawili maneno, anayosema qaḍi, na maneno wa-

1) gerecht. — 2) jd. an seinem Rechte schädigen. — 3) liederlich. — 4) Geschäft, Arbeit. — 5) Ehebruch treiben. — 6) mannbar. — 7) Verstand. — 8) z. B. — 9) Ausweg. — 10) Feind. — 11) zwischen. — 12) Absicht. — 13) Richter. — 14) gerichtliche Angelegenheit.

nayosema wale wagomvi wawili. inaḥitajia wawe watu wawili.

wa każàlika masháhidi, wanaoshuhudia watu wawili, wanaowiana, sherṭi waqubali kushuhudia, wawambiwe — ya kama: „sisi watu wawili — moja anamkopesha mwenziwe, na moja anakopa, bassi tunataka mtushuhudie tunavowiana.“ na wale masháhidi watauliza: „qadri gani[1]) mnachowiana?“ watanena: „qadri każa wa każa.“[2]) wale masháhidi watanena: „mmeriḍi[3]) tushuhudie?“ na wale wanenapo „tumeriḍi, tushuhudieni“ — hushuhudia wale masháhidi, na usháhidi wao tamma[4]).

wala hana yamîni sháhidi kuambiwa marra: „utaweza kuapa. ya kama umeshuhudia weye fulani kuwiwa qadri każa wa każa?“ amma hii si lâzima kumwapisha sháhidi, na aape mwenyi kuwia ao mwenyi kuwiwa kwanza.

na iwapo ḥakîm anataka kumwapisha mtu yamîni, atamwambia: „wewe unakana? hukutwaa kitu cha fulani, wala hakuwii fulani?“ na yule atasema: „nakana, sikutwaa, wala haniwii.“ atamwambia: „utaweza kuapa yamîni?“ na yule atasema „naweza.“ asemapo „naweza,“ lâzima ḥakîm kumshauri yule mwenyi mali yake kumwambia: „huyu anakana, naye ameriḍi kuapa yamîni, tumwapishe ao tusimwapishe?“ anenapo mwenyi ḥaqqi[5]) yake „mwapishe“ — lâzima kumwapisha. na anenapo „usimwapishe, na mimi nimesameḥe[6]) daʿawa[7]) hii“ — hana ḥaja[8]) ḥakîm kumwapisha, iwapo mwenyi kudaʿi[9]) hataki.

na sherṭi[10]) ya hiyo yamîni kula — yule mlaji[11])

---

1) welche Summe. — 2) soundsoviel. — 3) einverstanden sein. — 4) vollkommen. — 5) Recht, Forderung. — 6) verzichten. — 7) Klage. — 8) Verlangen. — 9) fordern. — 10) Bedingung. — 11) der Schwörende.

yamîni kwanza hutawaḍḍa[1]), ma'ana hunawa viganja vya mikono, kisha akaosha uso, tenna huosha mikono miwili, tenna hupaka maji juu ya kipanda uso, tenna hutia maji mashikioni, tenna huosha miguu. na shurṭi hizo killa paḥali huosha marra tatu, ma'ana yake awe na ûḍû[2]), ma'ana awe ṭaḥara[3]), ndipo ashike ule mṣaḥafu[4]), tenna ndipo anapokula yamîni.

na maneno yake ni haya tunayoyasema:

„wallâhi wa billâhi wa tallâhi el-'aṯhimu — kama amri hii nimetenda — yamîni inangamize[5]), na kama sikutenda — yamîni inilee."

ao husema:

„a'ûżu bi'llâhi mina 'n-nâri wa-min sherri 'l-kuffâri wa-min ghaḍabi 'l-jabbâri; el-'izzatu li'llâhi, wa-li rasûlihi wa li'l-mu'minîna barâ'atun mina 'llâhi." [6])

na wengine huapa sûra mia wa arba'ta'shara.

---

1) religiöse Waschungen vornehmen. — 2) religiöse Waschung. — 3) rein. — 4) Koran. — 5) töten. — 6) Ich flüchte mich zu Gott vor dem Höllen-Feuer und vor der Bosheit der Ungläubigen und vor dem Zorn des Tyrannen; die Macht gehört Gott und seinem Sendboten (Propheten) und die Gläubigen haben einen Freibrief vor Gott.

III.

desturi ya sheri'a ya kuoa.

akiwa mwanamke, akija mwanamme kuja kutaka kumwoa, huenenda kwanza kwa baba yake, si lâzima kumshauri mtoto wake. iwapo yule mtoto kijana, hajaolewa na mume mwingine, illa huyu anáyomtaka sasa — bassi huoza baba yake aliyomzaa. na yule mtoto akimtaka yule mume, amma akimkataa — babake humwoza kwa nguvu. wala si lâzima yule mtoto yule mume iwe sherṭi[1]) anampenda, ḥatta asipompenda — humwoza baba yake kwa nguvu. nayo inajûzu[2]) katika sheri'a yote Wa'arabu na Wasuaḥeli.

na yule babaye mno huenda, awatake mamaze[3]) yule mtoto, awape mashauri yale. iwapo wameriḍi[4]) kwa ote, humwoza mume yule mtoto wao. na iwapo wale mamaze hawataki, lakini yule babaye anataka, atamwoza mume mtoto wake. na iwapo mamaze wanamtaka mume yule, illa babaye hamtaki — hapana rukhṣa kuolewa kijana huyu, ndio kabisa kwa sheri'a na desturi.

na kama huyu mwanamke amekwisha olewa na mume mwingine, akiwa emeachwa na yule mume, ao mume amekufa — haifai baba yake kumwoza kwa

1) Bedingung. — 2) erlaubt sein. — 3) mama zake d. h. Mutter, Tanten etc. — 4) einwilligen.

nguvu, illa amshauri mwenyewe kwanza — ya kama: „amekuja fulani, anakutaka akuoe.“ akiriḍi mwenyewe mtoto, hapo ndipo anapomwoza.

na mtoto yatîma[1]) si lâzima kumwoza mume kwa nguvu, illa ariḍi mwenyewe, ijapokuwa kijana, kwa sababu yatîma, na yatîma lâzima kumtaka shauri mwenyewe, ḥatta yariḍi, ndio aolewe.

na mtoto áuwali humwoza mume babaye. ikiwa babaye amekufa — husimama babuye. na ikiwa hana babuye — husimama nduguye wa baba moja mama moja. kama hana nduguye wa baba moja mama moja — husimama nduguye wa baba moja mama mbalimbali. kama hawapo hao — huozwa na mtoto wa nduguye baba moja mama moja, lakini yule mtoto sherṭi ewe mwanamume. kama hayupo mtoto wa nduguye — husimama mtoto wa nduguye wa baba moja mama mbalimbali. kama hawapo watu hao — huoza nduguye babaye, babaye mdogo, baba moja mama moja na babaye. kama hayupo huyo — huozwa na nduguye babaye, baba moja mama mbalimbali. kama hawapo hao — huozwa na mtoto wa nduguye babaye, baba moja mama moja. kama hayupo huyu — huozwa na mtoto wa nduguye babaye, baba moja mama mbalimbali. kama hawapo hao, tuliowataja — huozwa na nduguye wa mama moja baba zao mbalimbali. kama hayupo huyu — huoza ḥakîm[2]), kwa sababu hana áṣili[3]).

na mwanamke aliyoandikwa ḥurru[4]) — humwoza bana wake, aliyemwandikia ḥurru.

mwanamume mungwana ana rukhṣa kuoa wake wanne kwa sheri'a. akizidisha wa tano ao wa sitta, si wakewe wale, huḥesabiwa[5]) katika masuria[6]) yake.

---

1) Waise. — 2) Oberhaupt des Ortes. — 3) Ursprung. — 4) frei. — 5) gezählt werden. — 6) Kebsweiber.

na masuria yafaʿa kuweka qádiri atakavyo na awezavyo kwa mali yake.

aiḍa mtumwa ana rukhṣa kuoa wake wawili, na akitaka kuweka masuria — ḥatta kumi na aweke.

wa kaẓâlika haijûzu mwanamume mungwana kumwoa kijakazi cha mtu — illa kwa shurṭi tatu. áuwali awe hana chakula cha kumlisha mwanamke wa kiungwana, ya pili awe hapati máhari[1]) ya kumwolea mwanamke wa kiungwana, na tatu ewe ana khofu[2]) nafsi[3]) yake kuchelea kuzini[4]), ao labuda hatafaʿa, atakuwa khánithi[5]), hataweza kulala na mwanamke mungwana — hapo mungwana humwoa mtumwa wa mtu mwingine.

na shuruṭi ya kuoa haijûzu kumwoa mwanamke, illa kwa waliyi[6]) wake mwanamke, wapatikane na mashâhidi wawili, washuhudie ile nikaḥi[7]).

na hawa mawaliyi na hawa mashâhidi hutazamwa kwa shuruṭi sitta: kwanza wawe islâmu, pili wawe bâleghi, tatu wawe wenyi ʿaqili, nne wawe waungwana, tano wawe waanaume, sitta wawe ʿadili[8]).

na ikiwa mwanamme amemwoa mwanamke, na hapo alipomwoa anazo nguvu za kulala naye, lakini khâtima[9]) akiwa hana nguvu — aonapo namna hiyo mwanamke mudda wa mwaka — hufâsikhi[10]) nikaḥi, mwanamke akenda zake, akaolewa na mwanamme mgine.

wala haijûzu kumwoa mwanamke, aliyefiwa na mumewe, illa ishe ʿeda[11]) yake, maʿana miezi minne na siku kumi.

na ikiwa ameachwa na mumewe, haijûzu naye kuolewa kwa siku zile anazoachwa — illa kupata miezi mitatu baʿada ya kuachwa, ndipo aolewe na mtu mwingine.

---

1) Heiratsgut. — 2) Furcht. — 3) Seele. — 4) außerehelich verkehren. — 5) impotent. — 6) männliche Anverwandte. — 7) Ehe. — 8) gerecht. — 9) schließlich. — 10) trennen. — 11) Wartezeit.

ikiwa mwanamke aliyoachwa ana mimba[1]), naye siku mbili tatu baʿada ya kuachwa akazaa mtoto, na ʿeda yake imekwisha — hana njia kukaa miezi mitatu ʿeda. akitokea mume, anayo rukhṣa kumwoa.

aiḍa hurejeshwa mwanamke kwao kwa ʿaîbu[2]) tano:

kwanza: mwanamke akiolewa, akionekana ana wazimu[3]) — yule mwanamke hurejeshwa kwao.

pili: akiwa yule mwanamke ana maraḍi[4]) ya ukoma[5]).

tatu: yule mwanamke akiwa anachunika mkono[6]).

nne: akiwa mwanamke akikojoa kitandani.

tano: ikiwa mwanamke ana kipembe[7]) katika ule uchi[8]) wake, hawezi kumchukua mume.

wa każâlika na mwanamke humkataa mumewe, inapokuwa ana ʿaîbu tano:

áuwali: akawa na wazimu mwanamme.

pili: akiwa na ukoma.

tatu: akawa na mabalanga.

nne: ikiwa mboo yake itakuwa ndefu sana ya kumwuma mwanamke.

tano: anapokuwa mwanamme hafai, hawezi kulala na mwanamke.

na watu, wasiofaʿa kuolewa, ni watu uliozaliwa nao — kama: mamayo, ao bibiyo, ao mtoto wako, ao mjukuo, ao nduguyo, ao mtoto wa nduguyo, ao nduguye babayo, ao mtu uliyonyonya[9]) naye ziwa[10]) moja, ao emenyonya na mamayo ziwa moja. tenna imekatazwa kulala na mamaye mkeo, inapokuwa yule mkeo umelala naye. iwapo yule mke hukulala naye, ulipomwona alikuchukia, ukamkataa, qabla hujalala naye — ukamwona mamaye, ukampenda — hapo yajûzu kulala na kumwoa mamaye. tenna haifai kulala na moja wa wakewe ba-

1) Schwangerschaft. — 2) Fehler. — 3) Verrücktheit. — 4) Krankheit. — 5) Krebs. — 6) Hautkrankheit mabalanga. — 7) auch kishipa genannt. — 8) Blöße. — 9) saugen. — 10) Brust.

bayo, ao na mkewe wa mtoto wako, ao na nduguye mkeo, wala baifai mwanamke na shangazi lake kuwaoa pamoja. watu hawa ḥarâmu[1]) kuwaoa.

---

desturi ya sheri'a ya ṭalâqa[2]).

aiḍa mwanamume akitaka kuacha mkewe, naye hana sababu, anataka kumwacha tu — lâzima mwanamume ampe máhari[3]) yake riale arba'în. na tenna imemlâzima kumpa jumla[4]) ya vitu katika nyumba nuṣṣ bi nuṣṣu[5]). ba'ada ya hayo mwanamke anakwenda kwao.

na iwapo mwanamke anataka kuachwa na mumewe, naye hana sababu, anapata kula, anapata na nguo, na mwanamme anafa'a kulala naye, halali nje kwa waanawake wengine mahawara[6]) zake yule mwanamme, anataka kuachwa yule mwanamke kwa upuzi[7]) wake tu, hana sababu wala hana sheri'a — lâzima mwanamke huyo kununua ṭalâqa kwa mwanamume, vile atakavotaka mwanamme. akimwambia „nipe rupia arba'în," ao akimwambia „nipe rupia settîn," ao „nirudishe máhari" — lâzima kutoa mwanamke kumpa mumewe, ndipo apate ṭalâqa, amwache.

na mwanamume akisema „nipe rupia khamsîn, nimekuacha," naye mwanamke akitoa palepale, usipite mudda[8]) — hapo mwanamke ameachika, naye ana rukhṣa kwenda kwao.

na iwapo yule mwanamke hakuweza kutoa palepale zile feḍḍa, ikipita mudda — hakuachika, kwa sababu mwanamume kamwambia „nipe papahapa."

---

1) verboten. — 2) Scheidung. — 3) Morgengabe, Heiratsgut. — 4) Summe. — 5) zur Hälfte. — 6) Geliebte. — 7) Unsinn. — 8) Frist.

illa anenapo mwanamume, akimwambia mwanamke: „zama utakáponipa rupia khamsîn — nimekuacha," ijapokuwa amekaa mwanamke miezi miwili, akapata zile feḍḍa kumpa mwanamme — hapo ameachika, kwa sababu amemwambia: „popote utakáponipa rupia khamsîn nimekuacha." hana hila [1]) mwanamume kunena „mimi siqubali," lâzima akitoa — ameachika, atakwenda kwao.

na akiwa mwanamke anataka kuachwa, na mwanamme hataki kuacha — hapo si lâzima mwanamke kuondoka nyumbani, qabla hajaachwa.

na iwapo mwanamke ana mwanamume, anayomkhada'a [2]), qáṣidi [3]) mumewe amwache, bassi huleta shuruṭi [4]) yule mumewe, akimwambia: „mimi nimeriḍi [5]) kukuacha, walakin fulani asikuoe, sababu namtuhumu [6]), yeye ndio aliyokufitini [7]) wewe, ḥatta ukanikataa, na sasa fulani asikuoe." hapo lâzima, akiwa amemwacha kwa shuruṭi hizo, yule mwanamme haifai kumwoa mwanamke yule.

na iwapo atamwoa, beina [8]) yao hudakhiliana [9]) kwa ḥakîm [10]), na ḥakîm atamsaili [11]) yule mwanamme: „ṣaḥiḥi [12]), weye umezini [13]) nayo huyu zamani, alipokuwa mkewe?" akinena „sikuzini naye, wala sikumfundisha, mumewe amwache, nipate mwoa mimi" — ḥakîm atamsaili: „utaweza kuapa yamîni [14]), ya kama hukuzini naye, amma hukumfundisha mumewe amwache, qáṣidi umwoe weye? sababu huyu mwanamume, aliyokuwa mumewe, ametuhumu weye ndio fitina, uliyomfitini na mkewe." na yule mwanamme iwapo ataweza kuapa yamîni, ya kama hakuzini naye mwanamke yule, wala hakumfundisha, amwambie mumewe amwache, hana lâzima mbele ya sheri'a, na nikaḥa [15]) yake bâṭili [16]).

1) List, Ausweg. — 2) betrügen. — 3) Absicht. — 4) Bedingungen. — 5) einwilligen. — 6) im Verdacht haben. — 7) aufstacheln. — 8) zwischen. — 9) Vermittlung suchen. — 10) Herrscher, Richter. — 11) fragen. — 12) richtig. — 13) Ehebruch treiben. — 14) Eid. — 15) Ehe. — 16) ungültig.

mtu iwapo amelewa, kileo [1]) kimempoteza fahamu [2]), akasema „mke wangu binti fulani nimemwacha — si mke wangu," khalafu kileo kimemtoka, na ʿaqili [3]) imemrudi, akadaʿi [4]) mkewe — sheriʿa haimsikizi, iwapo aliposema neno hilo pana masháhidi.

ikiwa mwanamke anataka kuachwa na mwanamume kwa viṣṣa [5]) alivofanyiza mwanamume, vikamwuźi [6]) mwanamke, na yule mwanamke na mwanamume wana kitu cha shirka [7]), ikiwa nyumba ao shamba ao mtumwa, qadri kitu walicho nacho cha shirka kile kitu chenyewe, na yule mwanamme akamwacha mwanamke — lâzima mwanamume kumpa máhari yake, na kile kitu cha shirka wagawane, mwanamume atoe ḥaqqi [8]) yake na mwanamke atoe ḥaqqi yake.

na iwapo yule mwanamume akikana, akimwambia mwanamke „katika kitu hiki humo weye" — lâzima yule mwanamke alete sháhidi, atakayojua, kile kitu kama shirka yeye na mumewe. atokeapo sháhidi, akashuhudia, kama kile kitu shirka mwanamke yule na mwanamume yule — lâzima ḥakîm amtoze mwanamme, agawane sawasawa na yule mwanamke, iwapo kile kitu wamegharimu [9]) sawasawa. na ikiwa moja wapo amezidi, atachukua ḥaqqi yake iliyozidi. na iwapo hakutokea sháhidi, lâzima yule mwanamke, anayodaʿi, amwambie mwanamume ampe ḥaqqi yake.

na ikiwa yule mwanamke anakana, lâzima ḥakîm kumwambia yule mwanamme: „utaweza kuapa yamîni, ḥaqqi hii shirika weye na huyu mwanamke?" awezapo mwanamume ile yamîni — bassi lâzima kugawana. na asipoweza kuapa yule mwanamme, akanena: „na aape

---

1) Rausch. — 2) Verständnis. — 3) Verstand. — 4) beanspruchen. — 5) Sachen. — 6) kränken. — 7) Gesellschaft. — 8) Recht. — 9) verpflichtet sein.

yeye huyu mwanamke," akaapa yamîni mwanamke — bassi imekuwa hana da'awa[1]), amma hio ndio desturi.

na ikiwa yule mwanamke na yule mwanamume shirka yao waliyofanyiza máthalan kama wameandikia na khaṭṭi[2]) za usháhidi ya shirka yao, akatoa khaṭṭi yule mwanamke, ukaonekana na usháhidi wa yule mwanamme, akaqirri[3]) katika khaṭṭi, ya kama kitu kile shirka yeye na mkewe, iendapo ikionekana kama hayo — lâzima kugawa na mkewe.

wa amma ikiwa yule mwanamke na yule mwanamume wana kitu cha shirka, khalafu wakaachana, na aliyotaka ṭalâqa yule mwanamke, mwanamume akajibu: „sikuachi, na ukitaka kuachwa, sameḥe[4]) máhari yako, na hiyo nyumba yetu, tuliyojenga shirika, unachie mimi katika khiṣṣa[5]) yako, na tenna huyu mtumwa wetu niachie mimi katika khiṣṣa yako." na yule mwanamke akinena „nimeriḍi, nimekusameḥe mtumwa wetu wa shirka katika khiṣṣa yangu na nyumba yetu ya shirka, — lâzima ameachika mwanamke, na kile chake hapati, sababu amesameḥe mwenyewe kwa khiyari[6]) yake.

ikiwa mwanamke na mwanamume wamegombana, khalafu wakaachana, nao wamezaa watoto wao, iwapo wale watoto vijana, hawajapata miaka saba' — lâzima atawalea yule mwanamke, walakin kula na nguo itatoka kwa baba yao. na yule mwanamke anenapo „mimi siwalei watoto hawa, illa unipe ḥaqqi yangu ya újira[7]) kulea watoto wako — lâzima yule mwanamume kumpa mwanamke ujira wake, amlelee watoto wake. ikipata miaka saba' yule mtoto, husailiwa: „wataka kwenda kaa kwa babayo amma utakaa na mamayo?" na mtoto akipata miaka saba', 'aqili huanza kuingia, anajua neno jema na baya analijua. bassi lâzima kusailiwa. anenapo

1) Klage. — 2) Schriftstück. — 3) anerkennen. — 4) verzichten. — 5) Anteil. — 6) Wunsch. — 7) Lohn.

„ntakaa kwa baba“ — atakwenda kwa babaye, anenapo „ntakaa kwa mama“ — atakaa na mamaye. wala si lâzima yule babaye mtu kumchukua kwa nguvu yule kijana, mâdâm amenena „ntakaa na mama,“ wala si lâzima mamaye mtu kumtaka mtoto kwa nguvu anenapo yule mtoto „ntakaa na baba yangu,“ kwa sababu si mtumwa — mtoto mungwana, na mungwana popote atakapo kukaa hukaa. hio ndio desturi ya sheri'a.

desturi ya sheri'a ya kuzini[1]).

mtu mwenyi kuzini emeta'adi[2]), ájili[3]) kuzini ḥarâm[4]), mweny'ezimgu[5]) amekataza kwa waanawake na waanaume.

na hii zinâ[6]) namna mbili: kuna zinâ ya kumta'adi muungu na zinâ ya kuwata'adi waana Adamu na muungu pamoja. amma zinâ ya kumta'adi muungu ni kuzini na mwanamke, na yule mwanamke hana mume, wala yule mwanamme anayozini na mwanamke — hana mke, wote wawili hawana mtu. ile imekuwa ya kumta'adi muungu pekeyake. amma zinâ ya kuta'adi muungu pamoja na waana Adamu ni kuzini na mwanamke, na yule mwanamke ana mumewe, ile imekuwa ḥaqqi mbili — ya muungu na waana Adamu. ḥokûmu yake huḥokumiwa wenyi kuzini ote wawili, mwanamke na mwanamme, kwa sheri'a ya muungu. na sheri'a hii, iliyokuja katika qorâni, husema: „mwanamme na mwanamke wâjibu[7]) kupigwa watu wawili hao bakora[8]) mia kulla mtu, lakini illa ipatikane baina[9]) na mashâhidi watu wanne.“ na hao mashâhidi lâzima wawe waanawaume, tenna wawe

1) chebrechen. — 2) Unrecht tun. — 3) Grund. — 4) verboten. — 5) mwenyi 'ezi muungu. — 6) Ehebruch. — 7) Pflicht. — 8) Stockhiebe. — 9) Beweis.

waungwana, wasiwe watumwa, tenna wawe bâleghi, wasiwe vijana, tenna wawe na ʿaqili, wasiwe wana kichaa, tenna wawe wanaṣali, wasiwe walevi.

iwapo kama wamepatikana mashâhidi kama hao, wakishuhudia kama hivo — ndipo wanapopigwa hao wenyi kuzini kulla mtu bakora miamia, na isipopatikana mashâhidi na shuruṭi hizo, tulizozinena — bassi hawana lâzima ya kupigwa mwanamke wala mwanamme.

maneno hayo ya mtu aliyozini mwanamke na mwanamume kupata radda[1]) ya fimbo mia yameandikwa katika qorâni na vitabu vya sheriʿa, lakini katika mirima tangu zamani hayakufanyizika mambo hayo, illa mwanamume aliyokamatwa kwa ugoni[2]), hutozwa feḍḍa tangu reale thalathîn kutaka, ḥatta reale kumi na mbili kupata. na kama hana feḍḍa — hufanyizwa mtumwa.

na inchi nyingine za mrima, upande wa Mtangata, mtu akifumaniwa na mke wa mtu — hutozwa ñgombe watano na riale tano, ao riale khamso u khamsîn. feḍḍa hiyo huitwa feḍḍa ya ugoni.

na inchi nyingine tenna mwenyewe kufanya uḥaribifu[3]), akitwaa mke wa mwenzi wake — lazima hutozwa feḍḍa riale arbaʿ u ʿasherîn, ao watumwa wawili.

na iwapo ametwaa mke wa mkubwa wa mji máthali kama jumbe, hutozwa feḍḍa, kama anazo, na tenna hutolewa mji, akapelekwa maḥala pengine, asirudi katika mji, alipofanyiza uḥaribifu. lakini hutezamwa yule mtu, iwapo ana ndugu wengi, ndugu zake hawaqubali kutolewa. ao awapo mtu amemukhuṣṣi[4]) yeye jumbe, máthali kama ndugu yake ao jamaʿa[5]) yake, hutoa riale settini ao watumwa watano. hio ndio desturi ya zamani.

---

1) Strafe. — 2) Ehebruch. — 3) Verderbnis, Schlechtigkeit. — 4) eigentümlich sein. — 5) Familie.

na mtu akimpa mimba [1]) mtoto mwana mwari bikra [2]), hutozwa feḍḍa tangu rupia khamsini ḥatta settini ao záyidi. na baba yake yule mtoto mwanamke atakapo kumwoza yule mtu — atamwoza, asipotaka — hatozwi nguvu.

na zamani sana katika inchi za mrima mtu kumpa mtoto wa mtu mimba, hulana njama [3]) siku mbili ao tatu, ikesha njama, humtoza n̄gombe watano na kosa riale tano. kisha yule mke humwoza.

aiḍa iwapo mtumwa amezini na mke wa mungwana, hutolewa katika mji huuawa ao huuzwa.

iwapo mtu mwanamume amemkuta mwanamume mwenziwe nyumbani — anaongea na mkewe — lâzima atampiga, hana ḥokûmu. illa kama amemkuta amesha toka nje, hana rukhṣa kumpiga. iwapo atampiga — lâzima ataḥokumiwa.

na iwapo mtu amekwenda katika nyumba ya mwenziwe, billa ya mtu kumwona, lakini imeonekana fimbo yake ao kisu chake, naye amekataa — ya kama „mimi sikuzini na fulani“ — humwambia „kisu chako kimekwendaje katika nyumba ya fulani? na kama unakataa hukuzini, kula yamîni [4]).“ akikataa kula yamîni, hujua, ya kama amezini, humlazimisha feḍḍa kulipa, kama watakávopatana.

wa aiḍa huwa mwanamme amekaa kitako usiku, akimwona mwanamke kwa ule usiku, na pale alipomwona kiza — hapana taa, akithanni [5]) mkewe, akalala naye — ḥokûmu yake hakuzini. na ikiwa amempa mimba, akizaa mtoto — huwa wake. na huyu mtoto huitwa mtoto wa shubuha [6]). naye mtoto wa ḥalâli [7]), sababu hakuqusudia [8]) kuzini na yule mwanamke, alithanni,

1) Schwangerschaft. — 2) Jungfer. — 3) kufanya shauri. — 4) Eid. — 5) glauben. — 6) Aehnlichkeit. — 7) erlaubt. — 8) beabsichtigen.

kama ni ḥalâli yake. walakin khabari hiyo yaḥitaji [1]), iwe maḥala penyewe kiza, pasiwe na taa. pakiwa na taa, ao ikiwa mchana — ḥokûmu yake amezini.

---

khabari ya mali ya mtoto yatîma [2]).

aiḍa [3]) iwapo amekufa mtu, amekhálifu [4]) watoto wadogo — bassi wale watoto huitwa yatîma. na ikiwa yule babaye amekhálifu mali — watumwa na nyumba na shamba — lâzima ile mali, ikiwa yule babaye ana nduguye, huzuia ile mali, ḥatta akibáleghi yule mtoto, akampa mwenyewe.

na ile mali, ikiwa watumwa, huuza, akitwaa yeye kwa themani [5]), amma huuza kwa watu, walio jirani [6]) zake, akatwaa feḍḍa, akamwekea yule mtoto. na sababu ya kuza wale watumwa — ájili [7]) mtumwa si mali, maʿana roḥo [8]), na roḥo haina buddi [9]) inakufa, amma atakimbia.

bassi iwapo amekufa yule mtumwa, amma amekimbia, atapata żambi [10]) mwenyi kuweka, kwa maʿana anajua, ya kama mtumwa roḥo, lâzima kukimbia, tenna lâzima anakufa — bassi yafaʿa kuuza kumwekea feḍḍa yule mtoto, maʿana feḍḍa haifi.

wa amma shamba si lâzima kuuza, maʿana halifi shamba wala halikimbii. na nyumba każâlika, ikiwa ile nyumba nyenyewe ya mawe, nayo inaonekana itakaa siku nyingi, nayo haitaḥaribika [11]) — huwekwa ḥatta mwenyewe akiwa mtu mzima, ana ʿaqili kupewa nyumba yake.

na katika shamba ile na nyumba hii ikiwa inapatikana dughuli [12]) katika vitu hivo — lâzima kuwekwa

---

1) erfordern. — 2) Waise. — 3) ferner. — 4) hinterlassen. — 5) Wert. — 6) Nachbar. — 7) Grund. — 8) Seele. — 9) Ausweg. — 10) Sünde. — 11) verderbt werden. — 12) Einnahme.

zile feḍḍa zake za dughuli kuwekewa mwenyewe yule mtoto.

na ikiwa panatakwa chakula cha yule mtoto, ao nguo avae, ao anangua yule mtoto, anataka dawa, na dawa haipatikani illa kwa feḍḍa — wâjibu [1]) kutoa feḍḍa kununua vitu hivo, walakini hutolewa kwa ḥesabu [2]). wala haifai kabisa kula ḥaqqi [3]) ya mtoto yatîma, mwenyʿezimgu amekataza katika qorâni, akisema katika âya [4]): „msile mali ya watoto yatîma kwa kuthulumu.“ [5]) wako wengine husema — ya kama: „hii mali ya mtoto yatîma nayo iko mkononi mwangu — ntatwaa mimi, ntatumia, nani atajua?“ ile imekuwa uwizi, watu wote watajua. lâzima atafutwe mtu mwingine, asiokuwa mbaẓirifu [6]), aliye na âṣili ya mali, ao hana mali, lakini awe amîni [7]) sana.

---

1) Pflicht. — 2) Rechnung. — 3) Recht. — 4) Vers, Spruch des Korans. — 5) rauben. — 6) Verschwender. — 7) Vertrauensmann.

IV.

khabari za desturi za waṣiya[1]).

imejûzu[2]) waṣiya kuwa kitu maʿalûm[3]) kile kinachouṣiwa[4]). iwe yule mwenyi kuuṣi ana mali ya feḍḍa, ao ana watumwa, ao ana shamba, chochote alicho nacho — lakini kiwe mali — bassi imejûzu kuuṣi — kama: „namwuṣia fulani atwae qadri ya każa wa każa[5]).“

tenna imejûzu kile kitu, anachouṣi, iwe kitapatikana, isiwe hakipatikani.

tenna imejûzu kuuṣi kama kitu kilichoʿathimika[6]), walakini kitapatikana — kama „mnazi hauna nazi, lakini mnazi ukizaa — nazi na apawe fulani.“

tenna mwenyi kuuṣi aquṣudie[7]) kule kuuṣi.

tenna na huo waṣiya wake atakaouṣi — na auṣi thúluthi[8]) moja katika mali yake. na ikiwa anazidisha katika thúluthi moja, imekuwa makruhu[9]), tenna ḥarâmu[10]). maneno haya yameḥarimishwa[11]) kuzidisha katika ile thúluthi moja katika lile fungu la mawarithi[12]). hubaṭilika[13]) waṣiya wake bass, endapo akizidisha, sababu haifai kuwakirihisha[14]) wale mawarithi wake.

1) Testament. — 2) erlaubt sein. — 3) bestimmt. — 4) vermacht werden. — 5) ungefähr soundsoviel. — 6) erhöht sein, in der Ferne liegen. — 7) beabsichtigen. — 8) ein Drittel. — 9) widerwärtig. — 10) verboten. — 11) verboten werden. — 12) Erben. — 13) ungültig erklärt werden. — 14) Widerwillen erregen.

tenna imejûzu waṣii [1]) yule mwenyi kuuṣi — kile kitu atakachouṣi kiwe chake, isiwe mali ya mtu mwingine.

wa kaẓâlika imejûzu yule, atakayouṣi, awe islâmu, na tenna ampe islâmu mwenziwe dîni [2]) yao moja. isiwe yule anayompa dîni yake mbali, haifai waṣii wake.

tenna lâzima yule mwenyi kutoa ewe bâleghi [3]), asiwe kijana. na yule apewayo, akiwa bâleghi akiwa kijana, yote pia hufa'a.

tenna lâzima ewe na 'aqîli [4]) mwenyi kutoa, asiwe mwenda wazimu.

kaẓâlika imejûzu ewe mungwana, asiwe mtumwa, ájili [5]) mtumwa hana íẓini [6]) ya kutoa mali kumpa mtu mwingine, kwa sababu yeye mtumwa, ememilikiwa [7]), na alicho nacho kaẓâlika, haijûzu kutoa kumpa mtu.

tenna imejûzu mwenyi kuuṣi emeriḍi [8]) kwa ikhiyari [9]) yake kule kuuṣi, isiwe emeshurṭizwa [10]) kwa nguvu „toa mali yako, umpe fulani,“ hivyo haifai.

kaẓâlika imejûzu ewe amîni [11]) yule mwenyi kuuṣi, ewe 'ádili [12]) wa 'ibâda [13]), anamjua môla [14]) wake mwenye'ezimgu [15]) kwa kumwe'abûdu [16]), anamjua na mtume wake Muḥammadi — hapo inaṣiḥi [17]) kuuṣi.

wa kaẓâlika imejûzu kuuṣi kwa ndia [18]) ya muungu, kama kutoa mali anena „jengeni meskiti [19]) mali yangu,“ amma „toeni qádiri kaẓa wa kaẓa, mwape maskini za muungu,“ ao „mchimbe kisima, watu wányywe maji,“ ao „jengeni nyumba — qo'di [20]) yake ipelekwe meskitini,“ ao „jengeni nyumba, wakija wageni, watokayo mbali, walale katika nyumba, hawana qo'di.“

---

1) Testament. — 2) Religion. — 3) mündig. — 4) Verstand. — 5) Grund. — 6) Erlaubnis. — 7) beherrscht werden. — 8) einwilligen. — 9) Wille. — 10) gezwungen werden. — 11) vertrauenswürdig. — 12) gerecht. — 13) Anbetung Gottes. — 14) Herr, Gott. — 15) Gott der Allmächtige. — 16) anbeten. — 17) richtig sein. — 18) njia. — 19) Moschee. — 20) Miete.

inajûzu kuuṣi kwa njia ya ḥalâli [1]), kama hayo tuliyoyanena, haijûzu kuuṣi kwa njia ya ḥarâmu. imejûzu kuuṣi kwa mtu wa mbali, isiwe kuuṣi kwake — „nikifa, mali yangu mpeni hawara [2]) yangu.“ hio ndapo akauṣi kwa mwanamke wa nje — hubaṭilika waṣii wake.

na iwapo ameuṣi kwa mtoto wa ḥarâmu kwa mwanamke, aliyotembea naye, lakini akamwoa, na hapo ḥarâmu — haifai, kwa sababu mtoto wa ḥarâmu.

imejûzu katika waṣiya kukharijiwa [3]) mali yake, yaliyo mali ya ḥalâli, maʿana mali aliyofanya kazi, akapata, ao mali ya kurithi [4]), yasiwe mali ya kunyaŋganya kama mali ya yatîma [5]).

wala haijûzu kuuṣi kwa mtu, asiyokuwa na kitu, máthali kama mtoto hana íżini kuuṣi wala ya kuuza wala kununua, maʿana sheriʿa ya mtume wetu Muḥammadi — mtoto mdogo, asiyopata miaka khamstʿashara, hakufai kuuṣi kwake, kuuza kwake, wala kununua kwake. na iwapo ameuza kitu kwa mtu mwingine, amma ametoa kitu burre kumpa mtu mwingine, akitokea aliyo ndugu yake ao baba yake, akajua kama huyu ametoa kitu burre kumpa mtu fulani, ao kauza kitu kwa fulani, iwapo hakurithi beʿi ile, aliyouza yule mtoto, amma kile kitu alichotoa — hubaṭilisha babaye mtu, naye mwenyi kupewa lâzima kurejesha, kwa sababu kijana hana ʿaqili, ndio maʿana beʿi yake haifai, na ʿaṭiya [6]) yake haifai, bassi wa każâlika waṣii wake haifai.

wa każâlika wala haijûzu fanyiza waṣiya kuzidisha katika yule atakáyorithi — kunena „na azidi katika ḥaqqi yangu, ḥiṣṣa [7]) yake apite wenziwe,“ amma hayo haifai. na afanyapo hayo, imekuwa makruhu, watakirihika, waliobaqi katika mawarithi zake, kwa sababu

1) erlaubt. — 2) Geliebte. — 3) Verfügung treffen. — 4) erben. — 5) Waise. — 6) Geschenk. — 7) Sache, Anteil.

mawarithi sawasawa. ilikuwaje bassi yule mwingine kumzidisha, naye emerithi sawasawa na wenziwe, na ḥali yake na ḥali ya wenziwe sawasawa, amma hayo hayafai.

wa aiḍa mtu mwenyi kuandika waṣii katika mali yake anenapo „nikifa, mali yangu yote na apawe fulani,“ walakini yeye anayo mawarithi zake, naye hakunena — kama „mpeni nuṣṣu“ wala „robo‘,“ walakini ametaja kupawa mali yake, naye ana mawarithi zake, ikiwa hivo — hapati kitu yule mwenyi kuuṣiwa, kwa sababu ana mawarithi zake, imejuikana, ya kama huyu maiti[1]) aliyokufa amefanyiza ukhâini[2]), kuwazuilia mawarithi zake, wasipate kitu. illa anenapo „nifapo, katika mali yangu nimeuṣi, apewe fulani kwa ḥaddi[3]) ya sheri‘a,“ bassi anenapo hivo, hujulikana bora, kwa kuwa ḥaddi ya sheri‘a ni thúluthi moja. amma kwa hivo hupata, kwa sababu amesema neno la sheri‘a, na sheri‘a ni thúluthi katika mali yake.

na huyu mwenyi kuuṣi iwapo amemwuṣia mtu kupewa záyidi ya thúluthi ḥatta nuṣṣu ya mali — hupewa kwa desturi ya mila, lakini sheri‘a imeziwia. na ikiwa ameuṣi záyidi ya nuṣṣu, ḥatta kwa mila hukataza kupewa.

aiḍa ikiwa mtu amekufa, ameuṣi mali yake katika ḥaqqi ya thúluthi kupelekwa meskitini, na sehemu[4]) kupewa maskini, na sehemu kuchimbwa kisima — bassi ḥaqqi hiyo yote hutoka katika thúluthi moja, haizidishwi ba‘ada ya thúluthi moja. ileile thúluthi moja ndio itakayokasimiwa[5]), kidogo kitapelekwa meskitini, na kidogo kitachimbwa kisima, na gharama[6]) hizo zote hutoka katika thúluthi moja, hiyo ndiyo ṣaḥihi[7]). wala haizidishwi kitu chengine, ijapokuwa lile jengo la meskiti

1) Verstorbene. — 2) Verrat. — 3) Regel. — 4) Anteil. — 5) verteilt werden. — 6) Kosten. — 7) richtig.

na kile kisima kuchimbwa — na wale maskini kupawa hapatakuwa na kitu, kwa sababu mali zake ni haba — hutosha, kwa sababu ndio ḥaqqi yake aliyotoa, na sheri'a ndivo ilivomṣiḥia. na ikiwa itazidishwa kitu, waonapo ile kazi ni kubwa, na gharama ndogo, na wale mawarithi wakapendelea kutaka thawabu [1]), watatoa mawarithi wazidishe wafanyize ile shughli [2]), aliyouṣi yule maiti. walakin watafanyiza kwa khiyari yao [3]), si lâzima kule kuzidisha wale mawarithi. na iwapo wamekataa kuzidisha wale mawarithi — bassi hapana sharṭi. hiyo ndio desturi.

wa aiḍa mtu akiuṣi mali yake yote, yapelekwe meskitini, na jama'a zake wasipate kitu — amma maneno hayo hayasikizwi, kwa sababu amefanyiza ukhâîni kuwakhîni mawarithi zake. bassi hayo hakushika ndia ya sheri'a ya kunena „ḥaqqi yangu wasipate mawarithi zangu.“ amma hapo ḥatta mweny'ezimgu na mtumewe Muḥammadi hakuwa raḍi, kwa ma'ana emekhálifu [4]) sheri'a ya mtume. na sheri'a ya mtume lâzima, mtu akiwa na mtoto wake ao baba yake ao mtoto wa ndugu yake, ikiwa amekufa — lâzima kurithiwa.

wa aiḍa ikiwa mtu amekufa, naye amekhálifu mali, akauṣi mali yake, watwae mawarithi zake, naye akiwa anawiwa deni na watu — wa amma wale mawarithi lâzima kulipa ḥaqqi ya watu kwanza, ndipo warithi kilichobaqi katika ile mali. walakini sherṭi ile deni anayowiwa iwe na baṿana [5]), ionekane khaṭṭi [6]) aliyoandika kwa mkono wake, ao kaandika ile khaṭṭi kwa ḥakimu [7]), ipatikane na mashâhidi [8]) wa kumshuhudia, ya kama anawiwa — hapo lâzima kulipa wale mawarithi. na isipotokea mashâhidi wa kumshuhudia, lâzima yule

1) gottgefälliges Werk. — 2) Arbeit. — 3) aus eigenem Antrieb. — 4) widerstreben. — 5) Beweis. — 6) Schriftstück. — 7) Richter. — 8) Zeugen.

anayowia aape yamîni[1]), kiapo cha sheriʿa ya muungu. akesha apa kiapo, anenapo „saḥihi namwia“ — lâzima kupawa ḥaqqi yake. na asipoapa — hapati kitu. wala si lâzima kuapa wale mawarithi.

aida ikiwa mtu amekufa, naye emeusi kwa wasiya, ikiwa ana watumwa, ikiwa kumi ao ʿesherini wale watumwa, na katika watu hao ameusi yeye mtu moja ao wawili, wawe waungwana, maḥurri[2]), ikiwa kule kuusi kwake emeandika katika khaṭṭi „fulani na fulani na waandikiwe ḥurri“ — amma hapo lâzima watakuwa wangwana. na iwapo hakuwaḥi[3]) kuandika, walakin aliponena wapo mashâhidi wa kweli wa kushuhudia maneno yale aliyonena yule mtu aliyokufa, maʿana „fulani na fulani wawe wangwana“ — hapo lâzima watakuwa waungwana. na iwapo yule aliyokufa emewambia wale watumwa „nikifa mimi. na mwe ḥurri“ — bassi khiyari yote juu ya wale mawarithi.

na pale atakáponena kuwausia uḥurri, ikiwa wapo mashâhidi, yakhitajia kule kuusi kwake sherṭi ewe na ʿaqili, isiwe roho — huku inatoka — huku ananena „fulani na fulani na awe mungwana“ — amma hapo haijûzu wasiya wake, kwa sababu amenena maneno hapo aliponena hana ʿaqili, yu katika wazimu, na mwenyi wazimu hasikilizwi. illa iwapo amenena, na ʿaqili yake timamu[4]), na roho haijatoka, wala yale maraḍi[5]) hayakumtoa ʿaqili — hapo iwapo wapo mashâhidi, aliponena hivo ya wale kuwa waungwana — lâzima watakuwa waungwana.

wa amma iwapo amenena hayo amelewa, lâzima watakuwa waungwana, kwa sababu ulevi hauna hoja ya kunena „huyu hana ʿaqili,“ sababu yeye akanywa ule ulevi, anajua, ya kama ʿaqili yangu itapungua, naye ikiwa anakunywa maqṣudi, apunguze ʿaqili yake — bassi hii lâzima watakuwa waungwana.

1) Eid. — 2) Freie. — 3) können. — 4) vollkommen. — 5) Krankheit.

wa aiḍa kažâlika mtu mwenyi kuwa na watoto wawili ao watatu, naye hajafa, yuko mzima, akatoa mtumwa moja ao wawili, akampa mtoto wake aliyo yote, akamwambia „nnakupa ʿaṭiya, ḥatta nijapokufa mimi — wako“ — amma hao watumwa lâzima kumtumikia yule aliyopawa. na afapo mwenyi kutoa, hawaḥesabiwi wale watumwa, sababu emetoa mwenyewe kwa khiyari yake, ili kumpa mwanawe yule moja katika watoto wake, naye amempa ʿaṭiya, na ʿaṭiya hairudi.

illa iwapo ametoa hibba[1]) kumpa yule mtoto wake, akitokea moja anampenda sana katika watoto wake, naye anao watumwa, akimwambia mtumwa „nenda katumike kwa bana wako,“ akenda mtumwa kutumika, na yule bwana wake, alikompeleka yule mtumwa, hakumwambia — kama „mtumwa huyu nimekupa ʿaṭiya,“ amenena tu — ya kama „nimemleta kufanyiza kazi kwako,“ bassi endapo akifa yule mwenyi kutoa, lâzima yule mtumwa ataḥasibiwa. na mawarithi waliobaqi watamtaka, wamtie katika ḥesabu, kwa sababu yule mzee wao amemtoa hibba, ili kumpa mwanawe.

ni mfano wa kumwʿazima[2]), na mtu mwenyi kuʿazima kitu cha mtu, amma mwenyi kupewa amâna[3]) ya mtu, lâzima kurejeʿa kwa mwenyewe, na haya kažâlika atarejeʿa, arithiwe kama sheriʿa.

aiḍa na mtu mwenyi kufa akiwa ana mtumwa, na yule mtumwa ḥurri, iwapo ameuṣi katika waṣiya wake, yule ḥurri apawe kitu katika thúluthi ya mali yake — lâzima kupawa.

na iwapo mtu amekufa, amewacha mtumwa wake, bado hajamwandikia ḥurri, walakini ameuṣi „fulani aandikwe ḥurri, na ḥaqqi yake katika mali yangu apawe

---

1) Stunde, Weile. — 2) leihen. — 3) Pfand.

thúluthi moja," lâzima — akafa — kuandikiwa, naye kupawa thúluthi moja katika mali yake.

na iwapo hakuandika katika waṣii, kanena kwa mdomo tu bass — wana ikhiyari wale mawarithi kumwandikia ḥurri, na kumpa kile kilichonenekana. watakapo, watampa khaṭṭi ya uḥurri na mali watampa. amma iwapo hawakuriḍi kumpa mali, wakitaka kumwandikia khaṭṭi ya uḥurri, watamwandikia. na iwapo wamekataa yote mawili — kumwandikia khaṭṭi ya uḥurri na kumpa mali wamekataa — bassi si lâzima, kwa maʿana hakuandika yule maiti katika waṣii wake, ndipo alipokosa yule mtumwa, ájili hapana bayana ya kuandikiwa ḥurru na kupawa mali, ndipo alipokosa.

aiḍa mtu mwenyi kuuṣi — ya kama mimi sina mtoto, walakini anao mawarithi ndugu zake, na wale ndugu zake yuko moja ana mwanamke, na yule mwanamke ana mimba, akauṣi katika waṣiya wake akanena „nifapo — thúluthi ya mali yangu katika thúluthi moja, azaapo mtoto ndugu yangu kwa hii mimba, aliyo nayo huyu mkewe, na apawe mtoto thúluthi moja." lakini yakhitaji iwe mwezi wa sitta mimba. akifa huyu mwenyi kuuṣi, akazaliwa mtoto, lâzima kupawa thúluthi moja.

aiḍa mtu mwenyi kufa akauṣi katika thúluthi moja ya mali yake, akawambia mawarithi zake „nimewauṣia aqrabu [1]) zangu, maʿana ndugu zangu, wapewe thúluthi moja katika mali yangu" — bassi imekuwa ndugu zao wote katika aqrabu zao wale mawarithi zake lâzima kupawa, nao hupata wote sawasawa katika thúluthi moja.

aiḍa iwapo ameuṣi mtu „katika mali zangu, nikifa, thúluthi moja na wapawe jamaʿa zangu," akifa mwenyi kuuṣi, akazaliwa mtoto, na yale mali hajarithiwa bado,

1) Verwandte.

na sasa wanataka kurithi wale mawarithi — na yule mtoto atapata, kwa sababu yule aliyokufa amenena „ḥaqqi yangu, nikifa, na wapawe jamaʿa zangu,“ na yule mtoto ni jamaʿa yake, atapata naye. ni iwapo yule mtoto amepata, naye akafa yule mtoto, lâzima ile ḥaqqi, aliyopata yule mtoto, kurithi mawarithi zake, kwa sababu imekuwa ḥaqqi ya mtoto wao, si lâzima kurejeʿa kwa wale washirka wake.

ikiwa shamba ya mpunga ao ya mtama amelima mtu, umequrubia kuwiva ile riziqi — akifa mwenyi kulima, walakini zamani alipokufa emeusi „katika shamba hili kitakachopatikana katika thúluthi moja nimeusi kupewa fulani“ — lâzima kupawa yule mwenyi kuusiwa. walakini hutazama kile kilichopatikana, ikiwa inapata jisla[1]) tano — hutoka ḥaqqi ya muungu kupewa maskini, na ḥaqqi ya muungu pishi kumi kwa moja. lakini lâzima ipate jisla tano, ndipo inapotoka hivo. hiyo ni fáraḍi[2]), hutolewa kwetu sisi kwa mazehebbu[3]) yetu Wasuaḥeli aliyo mzima na afayo, akacha kitu. huḥasibiwa, ikipata jisla tano — hutoka ḥaqqi ya muungu maʿana mali ya zaka[4]) kwanza. ikesha toka ḥaqqi ya muungu, ndipo inapoḥasibiwa ile mali thúluthi moja, akapawa yule mwenyi kuusiwa. hio ndio desturi ya sheriʿa ya Wasuaḥeli.

na zaka hutoka vilevile mtu akilima, akipata jisla tano, analâzima kutoa zaka. na zaka zake pishi settîn kwa pishi moja kupewa maskini. na akichuma feḍḍa vilevile. akifanya kazi, ukatimia mwaka, akipata riale ʿesherîn mali yake, lâzima kutoa rupia, ndio zaka yake. vilevile hupewa maskini.

wa aiḍa ni kuwa mtu ana shamba, ao ana nyumba, ao ana mtumwa, ao ana feḍḍa, naye ana rafiqi yake

1) ein jisla = 60 pishi à 6 Pfund. — 2) göttliches Gebot. — 3) religiöse Sitten. — 4) Heiligung des Besitzes durch Almosengeben.

anampenda, ao mkewe nyumbani, ao mtu tu, lakini anataka kumpa, naye ana khofu, kile kitu anachotaka kumpa — isiwe nikifa, mawarithi zangu wakaja wakamtaʿarraḍi[1]) kwa sheriʿa bassi — huandika khaṭṭi. na áuwali ya khaṭṭi huandika: „aqarri ao iqrari ala nafsihi,“[2]) maʿana yake „nimeqirri nafsi yangu, nimetoa mtumwa kumpa fulani, nimempa ʿaṭiya ḥai[3]) yangu, na baʿada ya mauti[4]) hana mtu wa kumtaʿarriḍa kwa sheriʿa, nimempa ʿaṭiya.“ bassi ikiwa namna hiyo, akiwa ḥai yeye mwenyi kutoa, ijapokuwa yule aliyompa alikuwa rafiqi yake, khalafu wakigombana, akitaka ile ḥaqqi aliyotoa kwa yule mtu aliyompa — hana sheriʿa ya kupata, mâdâm[5]) kaandika khaṭṭi ya kuqirri nafsi yake — hapati kitu kwa neno, alilolinena mwenyewe nafsi yake. kaẓâlika na ijapokuwa amekufa, wakija mawarithi zake kutaka ile ḥaqqi, hawapati nao, ájili iko khaṭṭi ya kuqirri nafsi yake, ya kama ile khaṭṭi ametoa kumpa yule mtu, ndipo watakapokosa wale mawarithi. hio ndio desturi ya sheriʿa ya Wasuaḥeli.

mila ya Wasuaḥeli katika khabari ya waṣiya si wengi sana wanaofanya, sababu haba wenyi vitu. na anayefanya waṣiya, humwandikia mwenziwe waṣiya ao humwita mtu amtakayo, qabla hajafa, akamwagiza — ya kwamba: „mimi nikifa, katika mali yangu twaa thúluthi, ufanyize maziko yangu tangu sanda ḥatta khítima[6]) na karamu[7]) yangu, na kitakáchobaqi katika thúluthi, nimekupa wewe, na kitakáchosalia cha mawarithi yangu.“

---

1) sich in den Weg stellen, Hindernis bereiten. — 2) ich erkenne selbst an. — 3) bei meinen Lebzeiten. — 4) Tod. — 5) während, da. — 6) Koranlesung. — 7) Festessen, hier Leichenschmaus.

khabari ya urithi[1]).

warithi katika waanaume watu kumi ndio wanaworithi:

kwanza: mtoto wako mwanamme atakurithi.

na ya pili: mtoto wa mtoto wako mwanamume atakurithi, na mtoto wa mjukuo atakurithi, iwapo huna watoto wengine illa yeye.

tatu: baba yako.

nne: babuyo, mzaa babako, atakurithi. tenna babiye babuyo atakurithi.

kama hawapo hao, atakurithi tano: nduguyo, baba moja mama moja.

kama hayupo nduguyo, atakurithi sitta: mtoto wa nduguyo.

kama hawapo hao, atakurithi saba': babayo mdogo, aliyozaliwa na babayo, baba moja mama moja.

kama hayupo huyu atakurithi nane: mtoto wake yule baba mdogo yako, aliyozaliwa na babayo.

tisa': na akiwa mwanamke, hurithiwa na mumewe.

kumi: na akiwa ḥurri[2]), aliyoandikwa — hurithiwa na bana wake.

na waanawake wanarithi watu saba':

kwanza: mtoto wako mwanamke atakurithi.

pili: mjukuo, aliyozaliwa na mwanao mwanamume, akiwa mwanamke yule mjukuo, atakurithi.

tatu: mama yako, aliyokuzaa, atakurithi.

nne: bibiyo, aliyozaa mamako, atakurithi.

tano: nduguyo mwanamke, uliyozaliwa naye, baba moja mama moja, atakurithi.

sitta: na mkeo, kama amekufa mumewe, atarithi.

---

1) Erbschaft. — 2) Freigelassener.

saba‘: na ḥurri wako, uliyomwandikia, akifa yule ḥurri, atarithi bibi yake.

* * *

ukiwa na mtoto wako mwanamme pekeyake, nawe ukiwa na nduguyo, baba moja mama moja — yule nduguyo hapati kitu, illa atachukua mali yote yule mtoto wako, kwa sababu mtoto mwanamume.

na iwapo una mkeo, katika ile mali, atakáyorithi yule mtoto wako, kulla riale moja atatoa thumni [1]), ampe mkeo. hio ndio warithi wa mwanamke, atakáyopata kwa mumewe.

iwapo yule mume ana mtoto yoyote, akiwa mtoto mwanamke ao mwanamume, afapo yule mumewe — mwanamke hurithi thumni katika ḥaqqi ya mumewe, kulla riale atapata thumni. qádiri ya mali aliyoacha mumewe, ḥuḥesabiwa mwanzo wa feḍḍa, ḥatta nyumba huuzwa, ḥatta mashamba huuzwa, ḥatta watumwa huuzwa ao huthaminiwa [2]) kwa themani, na kulla kilichomo nyumbani, ikaḥesabiwa feḍḍa, na kulla riale hutoka themuni, akapewa yule mwanamke. kilichobaqi huchukua mtoto wako mwanamume. amma hio ndio desturi ya sheri‘a ya Wasuaḥeli.

na iwapo yule, aliyokufa, ameacha mamake ḥai [3]), naye ameacha mtoto wake mwanamume, huḥesabiwa mali vilevile kama tulivonena áuwali. ikesha julikana ile mali qadri każa wa każa [4]) — áuwali hutoka súdusi [5]), ma‘ana ḥaqqi ya mamake mwenyi kumzaa, riale sitta kwa moja, settini kwa kumi. kilichobaqi akarithi mtoto na mkewe. mkewe atachukua thumni, na baqi ya mali yote atachukua mtoto wake. amma hiyo ndiyo desturi ya sheri‘a ya Wasuaḥeli.

---

1) ein Achtel. — 2) abgeschätzt werden. — 3) lebend. — 4) ungefähr soundsoviel. — 5) ein Sechstel.

na iwapo yule maiti, aliyokufa, ana watoto wawili, mwanamume na mwanamke, na mamaye ḥai, na mkewe yupo — áuwali huḥesabiwa ile mali yake yote, ijuikane themani yake, kisha bassi áuwali hutoka súdusi, ndio ḥaqqi ya mamaye mtu yule aliyokufa. kilichobaqi huḥesabiwa, kulla riale hutoka thumni, akipewa mwanamke yule mkewe. na iliyobaqi katika mali — hurithi yule mtoto mwanamme na nduguye mwanamke. na kurithi kwao: mwanamme huchukua mafungu mawili, mwanamke fungu moja. amma hio ndio desturi ya sheri'a ya Wasuaḥeli.

walakin katika ḥaqqi hii kwanza, akesha twaa súdusi mamaye mtu — hutoka máhari[1]) ya mwanamke, kwa qádiri aliyomwolea, ikiwa riale thalathini ao khamsini ao záyidi.

na iwapo yule maiti, aliyokufa, hana mtoto, emewacha mama yake, emewacha na ndugu yake mwanamke, baba moja mama moja, emewacha na ndugu yake mwanamme, baba moja mama mbalimbali, emewacha na mkewe — yule mama yake atatwaa súdusi, ikesha — itoke máhari, apewe na mwanamke, kama qiâsi[2]) cha máhari yake aliyomwolea. khalafu watarithi yule nduguye mwanamke wa baba moja mama moja, na yule nduguye mwanamume wa baba moja mama zao mbalimbali. atarithi sawasawa na yule nduguye mwanamke. na áṣili kurithi sawasawa na yule nduguye mwanamke — sababu huyu nduguye, aliyokufa, wamezaliwa baba moja mama moja, na yule nduguye wa baba moja — si mama moja. kama alikuwa nduguye baba moja mama moja — asingalipata kurithi sawasawa na nduguye mwanamume, angalirithi fungu moja, na mawili angalipata mwanamme.

na yule mkewe, akesha pewa máhari yake, mâdâm

1) Morgengabe. — 2) Wert.

yule mwanamme aliyokufa hana mtoto — hupewa kulla riale robo‘, ndio ḥaqqi yake mwanamke, kwa sababu hana mtoto yule mwanamme. kama alikuwa na mtoto, angalipata thumni. amma hiyo ndio desturi ya sheri‘a ya Wasuaḥeli.

na iwapo yule maiti, aliyokufa, ameacha mtoto wa mwanawe mwanamume, na yule mjukuu akiwa mwanamke, emeacha na nduguye mwanamke, baba moja mama moja, emeacha na mama yake, emeacha na mkewe — hurithi watu hao wote. kwanza hutoka súdusi, akipewa mama yake, ikesha ikitoka máhari akipewa mkewe, kilichobaqi huḥasibiwa. nuṣṣu akatwaa nduguye yule mwanamke, baba moja mama moja, na nuṣṣu hutwaa yule mjukuwe mwanamke. kisha hupewa mkewe robo‘ yake. walakin hii robo‘ hutoka katika fungu la huyu mjukuu. yule nduguye huchukua nuṣṣu yake kâmili[1]), hatoi kitu. hio ndio desturi ya sheri‘a ya Wasuaḥeli.

na iwapo yule maiti, aliyokufa, emewacha mtoto wake mwanamke, emewacha na mjukuwe, mtoto wa mwanawe mwanamume, walakini huyu mjukuu mwanamke, emeacha na mamaye, emewacha na mkewe — huyu mamaye mtu hutwaa súdusi, kilichobaqi hutoka máhari, kilichobaqi tenna huḥesabiwa, nuṣṣu hutwaa mtoto wake mwanamke, na thumuni katika ile mali hutwaa mkewe. na kilichobaqi huchukua yule mjukuwe, mtoto wa mtoto wake mwanamme. amma hio ndio desturi ya sheri‘a ya Wasuaḥeli.

na iwapo yule maiti, aliyokufa, hana mtoto, wala hana ndugu wa baba moja, ana nduguye wa mama moja, ana na mkewe, ana na babaye mdogo — yule mwanamke hutwaa robo‘ katika ile mali, na yule babaye mdogo hutwaa nuṣṣ, na yule nduguye wa mama moja baba mbalimbali hupata kidogo naye. naye yafa‘a

1) völlig.

kupata kitu kidogo, khaṣṣa[1]) ikiwa huyu aliyokufa hana mtoto, wala hana nduguye wa baba moja mama moja, wala hana mjukuwe. hio ndio desturi ya sheri'a ya Wasuaḥeli.

na iwapo yule maiti, aliyokufa, mwanamke, naye ana mtoto mwanamume, ana na mamaye, ana na mumewe — hurithi watu watatu hao. áuwali hutoka súdusi, akachukua mamaye mtu. kilichobaqi atarithi mtoto wake mwanamume. na yule mumewe kulla riale atapata robo', walakin yule mwanamume lâzima kwanza atoe máhari ya mkewe, yachanganye katika mali, yarithiwe pamoja — ndipo atwae robo' yake mwanamume.

na iwapo yule mwanamke, aliyokufa, ana mtoto mwanamke, ana na mumewe, ana na mamaye — áuwali hutoa máhari yule mwanamme ya mkewe, ikichanganywa pamoja na mali, aliyoacha mkewe. hutoka súdusi, akatwaa mamaye mtu. kilichobaqi — nuṣṣu hutwaa yule mtoto mwanamke na nuṣṣu huchukua mumewe. na yule mwanamme asingalipata nuṣṣu — sababu yule mtoto mwanamke — ndipo akipata nuṣṣu mumewe. kama alikuwa mwanamme yule mtoto wake, angalipata robo' mumewe. hio ndio desturi ya sheri'a ya Wasuaḥeli.

na iwapo yule mwanamke, aliyokufa, emewacha mwanawe mwanamke, emewacha na nduguye mwanamume, emewacha na mamaye aliyomzaa, emewacha na mumewe — áuwali yule mwanamme atatoa máhari. ikesha, iḥasibiwe ile mali yote, atwae súdusi mamaye mtu, kilichobaqi nuṣṣu atarithi mtoto wake mwanamke, na robo' atachukua nduguye mwanamme, na robo' atachukua yule mumewe. amma hio ndio desturi ya sheri'a ya Wasuaḥeli.

na iwapo yule mwanamke aliyokufa, emewacha nduguye wa baba moja mama moja — mwanamke,

1) besonders.

emewacha na mtoto wa nduguye baba moja mama moja — mwanamume, emewacha na mamaye — yule mamaye huchukua súdusi yake, kilichobaqi atarithi nuṣṣu atatwaa yule nduguye, na nuṣṣu atatwaa yule mtoto wa nduguye. na iwapo ana mume, yule mumewe atatwaa roboᶜ, lakini lâzima kutoa máhari, na yule mtoto wa nduguye atatwaa roboᶜ, na yule nduguye wa mwanamke atatwaa nuṣṣu. amma hio ndio desturi ya sheriᶜa ya Wasuaḥeli.

na iwapo yule maiti, aliyokufa, mwanamke, hana mtoto, wala hana nduguye wa baba moja mama moja, wala hana mtoto wa nduguye baba moja mama moja, walakini yuko babaye mdogo pamoja na yule mumewe — nuṣṣu huchukua babaye mdogo, na nuṣṣu huchukua mumewe.

na iwâpo maiti, aliyokufa, mwanamke, naye anaye mtoto wake mwanamke, anaye na mamaye, aliyomzaa, anaye nduguye wa baba moja mwanamume, anaye na mumewe — warithi hao hurithi wote, walakini lâzima mwanamme kwanza hutoa máhari, khalafu huḥasibiwa mali yote. yule mamaye mtu atachukua sudus, na yule mtoto atachukua nuṣṣu, na yule nduguye atachukua roboᶜ, na yule mume atachukua roboᶜ. hio ndio desturi ya sheriᶜa ya Wasuaḥeli.

aiḍa ikiwa amekufa mwanamke, na yule mwanamke amewacha mume, amewacha na mtoto wake mwanamume, naye ana mali — huḥasibiwa ile mali mafungu manne, fungu moja atatwaa mwanamume yule mumewe, na mafungu matatu atachukua mtoto wake mwanamume.

na ikiwa ana watoto wawili, moja mwanamke na moja mwanamume, naye ana na mumewe, warithi wake: yule mwanamume atachukua fungu moja roboᶜ, na inabaqi — watarithi wale watoto wake wawili, mwanamume atarithi mafungu mawili, mwanamke atarithi fungu moja.

ikiwa hana mtoto, aliyomzaa, walakin anayo nduguye,

baba moja mama moja, amma ana mtoto wa nduguye, warithi wake: yule mwanamme hurithi nuṣṣu, na kilichobaqi watachukua wale mawarithi zake. hio ndio desturi ya sheriʿa.

na ikiwa amekufa mwanamke, amewacha nduguye mwanamke, amewacha na mtoto wa mwanawe mwanamume, amewacha na mumewe — sasa mawarithi wamekuwa watu watatu, mali yao hugawiwa mafungu ethinʿashara. mafungu matatu atachukua mwanamume, ndio roboʿ yake, na mafungu matatu atachukua nduguye mwanamke, ndio thúluthi yake, na nuṣṣu atachukua yule mtoto wa mwanawe. hio ndio desturi ya sheriʿa ya Wasuaḥeli.

na iwapo maiti, aliyokufa, mwanamke, emewacha mtoto wake mwanamume, amewacha na babaye mwenyi kumzaa, emewacha na mumewe — yule mume lâzima kutoa máhari kwanza, akisha toa máhari, hurithiwa yale mali, nuṣṣu huchukua mtoto wake mwanamme, na roboʿ huchukua mumewe, na roboʿ huchukua babaye mtu. amma hio ndio desturi ya sheriʿa ya Wasuaḥeli.

na iwapo yule maiti, aliyokufa, mwanamke, amekhálifu[1]) mali, naye ana mume, ana na nduguze waanawake, baba moja mama moja, ana na watoto wa nduguze waanawaume, na wale watoto waanaume — lâzima yule mumewe kutoa máhari, ikisha toa máhari, hurithiwa yale mali, nuṣṣu hutwaa nduguze waanawake, baba moja mama moja, na nuṣṣu hutwaa yule mumewe. amma hao watoto wa nduguze hawapati kitu, kwa sababu nuṣṣu mbili zote zimekwisha. na aliyowazuia wale watoto, ḥatta wakikosa — ni yule mume. kama angalikuwa hana mume, wangalirithi wale watoto pamoja na mama zao, walakini wamekosa sababu hio. ndio desturi ya sheriʿa ya Wasuaḥeli.

1) hinterlassen.

na iwapo maiti, aliyokufa, mwanamke, naye hana mtoto, wala hana ndugu, wala hana baba, wala hana mama, walakini yuko mtoto wa nduguye mwanamme — hurithi yule mtoto pamoja na mumewe, walakin mwanamme lâzima kutoa máhari. na iwapo hana mume, huchukua yule mtoto ile mali yote.

na iwapo maiti, aliyokufa, mwanamke, naye amekhálifu babaye aliyomzaa, ana na mwanawe mwanamke, naye hana mume — amma katika mali ile hugawana sawasawa, nuṣṣu huchukua babaye mtu, na nuṣṣu huchukua yule mtoto.

na iwapo yule maiti, aliyokufa, akiwa mwanamke ao mwanamme, amekhálifu nduguze wa baba moja mama moja, amekhálifu na baba yake mwenyi kumzaa — amma wale nduguze hawapati kitu, kwa sababu baba yake yuko. illa awapo yule maiti ana mkewe, lâzima yule mwanamke hupewa máhari. ikisha toka máhari, huḥasibiwa yale mali, kulla riale hupewa robo' mwanamke, na kilichobaqi hupewa nduguze. hio ndio desturi ya sheri'a ya Wasuaḥeli.

na iwapo yule maiti, aliyokufa, mwanamke, ana nduguze waanaume, ana na babaye mwenyi kumzaa, ana na mumewe — wale nduguze hawapati kitu, sababu baba yake yuko. bassi lâzima yule mwanamme kutoa máhari. akesha toa máhari, atapata robo' mwanamme, na iliyobaqi atachukua babaye mtu. hio ndio desturi ya sheri'a ya Wasuaḥeli.

na iwapo yule maiti, aliyokufa, hana babaye, wala hana mamaye, walakin anaye mtoto wa mtoto wake mwanamme, anaye na mumewe — hurithi sawasawa. yule mtoto atachukua nuṣṣu, na yule mumewe atachukua nuṣṣu, walakin lâzima yule mwanamume kutoa máhari, ndipo arithi.

iwapo yule maiti mwanamke, naye amewacha mali, ana mamaye, ana na babaye, walakin hana mtoto mwin-

gine, lakini nduguze anao, ana wake na waanaume — wale nduguze hawapati kitu, illa mamaye mtu atapata súdusi, mali yote atachukua babaye. ndio desturi ya sheri'a ya Wasuaḥeli.

na mwanamke akiwa amekufa, naye hana babaye, wala hana mamaye, wala hana nduguye wa baba moja mama moja, wala hana babaye mdogo, wala mtoto wa babaye mdogo, wala hana na babuye, aliyozaa babaye, wala hana babiye, aliyozaa mamaye, illa ana mumewe bassi — ḥaqqi yake, anapokufa, yote huchukua mumewe.

na iwapo maiti, aliyekufa, hana ndugu, wala hana mwana, wala hana babaye mdogo, wala hana mtoto wa babaye mdogo, wala hana mtoto wa nduguye babaye mdogo, wala hana mume, walakin yeye anaye mtumwa wake, lakini yule mtumwa amemwandikia ḥurru — atarithi yule ḥurru.

na iwapo yule, aliyokufa, ḥurri, naye hana mke, wala hana nduguye, baba moja mama moja, aliyo ḥurri mwenziwe, akiwa na ndugu yake, aliyo mtumwa, hakuandikiwa — hafai kumrithi, sababu mtumwa hamrithi mungwana, naye ḥurri vilevile kama mungwana. ndio desturi ya sheria' ya Wasuaḥeli.

na iwapo yule ḥurri anaye mtoto wake, walakin yule mtoto alikomzaa mtumwa, sababu amekwenda mwona mjakazi wa mtu. akamwoa, akazaa mtoto — bassi yule mtoto amekuwa mtumwa wa watu, na mtumwa hafai kumrithi mungwana.

walakin iwapo yule baba yake amekwenda mwona mwanamke, akamtaka kumwoa, na yule mwanamke ḥurri, ameandikiwa, akaoa ḥurri mwenziwe, akizaa mtoto — yule mtoto huwa mungwana, sababu mama yake ḥurri na babaye ḥurri, na áṣili ya ungwana ameipata. sasa iwapo hivo — wājib [1]) atarithi yule mtoto. walakini

1) Pflicht.

asiwe mtoto wa zina [1]), amekwenda mwona mwanamke baba yake, akazini naye billa kumwoa — mtoto huyu hamrithi.

na iwapo ḥurri akiwa amekufa, naye hana mtoto, wala hana ḥurri mwenziwe, aliyoandikiwa pamoja, wala áṣili ya bwana zake, waliomwandikia, hawako, afapo — mali yake yote huchukua mumewe. hio ndio desturi ya sheri'a ya Wasuaḥeli.

iwapo maiti, aliyokufa, hana udugu kabisa, imetafutwa — haikupatikana katika áṣili yao, hurithi mtu, aliyonyonya naye ziwa moja. na huyo huitwa ndugu — hurithi huyu.

asipokuwapo huyo — mali yake huenda bêt el-mali [2]), ma'ana katika nyumba ya ḥakîm [3]). ndipo anaporithi ḥakîm. na yule ḥakîm yaḥitajia awe dîni yao moja na yule ra'ia [4]) aliyokufa, kwa sababu, akipata ile mali, atafanyiza katika njia ya dîni yao — atafanyiza meskiti, atatoa ṣádaqa [5]). atatoa zaka [6]) kuwapa watu, atachimba visima, atawaona waana wa zuoni [7]), atawapa ndia ya khêri [8]). na yale atakáyotoa — yote ni khêri kwake yeye ḥakîm na yule aliyokufa, watapata thawabu.

mtu amekufa, amewacha mtoto mwanamume na mwanamke, amewacha na mke wake, na ras el-mali [9]) yake riale khamsini. na mke amemwoa máhari yake riale arba'ini. na maiti huyu amewata [10]) deni ya riale mia. sasa watoto wanataka kurithi katika riale khamsini, na mke anataka máhari yake na thumni yake, na mdeni anataka feḍḍa yake riale mia. wote wamekwenda

---

1) Ehebruch. — 2) Haus des Vermögens. — 3) Herrscher. — 4) Untertan. — 5) Opfer. — 6) Heiligung des Besitzes durch Almosengeben. — 7) Schüler, d. h. die den Koran Lernenden. — 8) Weg zum Guten. — 9) Vermögen, Kapital. — 10) acha.

kwa ḥakîm kupatanishwa. nani atakáyepata, nani atakáyekosa katika sheri'a?

kwanza mwanamke atapewa ḥaqqi yake ya máhari, ma'ana neno la lâzima juu ya mwanamke kupata. zitabaqi riale kumi, atapewa mdeni katika deni, anayomwia, riale mia. na wale watoto wataondoka mikono mitupu.

Göttingen, Druck der Univ.-Buchdruckerei von W. Fr. Kaestner.

DATE DUE

GAYLORD

PRINTED IN U. S. A.

Velten, Carl

GN658
V419x

Desturi za Wasuaheli

African Collection

African Collection

GN658
V419x

STACKS GN658.V419x
Desturi za Wasuaheli na khabari za dest
3 5282 00190 1845
Univers
African Colle